

19 APRILI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

---

MAJADILIANO YA BUNGE

---

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Tisa - Tarehe 19 Aprili, 2013

(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MAZINGIRA NA MUUNGANO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu, Mazingira na Muungano, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

19 APRILI, 2013

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE.PAULINE P. GEKUL (K.n.y.MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

19 APRILI, 2013

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 66

### Kumaliza Tatizo la Madawati

**MHE. SARA M. ALLY** aliuliza:-

Kuna uhaba mkubwa wa madawati katika shule za msingi hali inayochangia wanafunzi kutokufanya vizuri katika masomo hayo:-

Je, kwa nini Serikali haitoi kibali cha kuvuna miti ya kutosha na kutambua mafundi Seremala katika Halmashauri na kuwapa kazi ya kutengeneza madawati ili kumaliza tataizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally kama ifuatavyo. Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na madawati ya kutosha katika shule ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Hadi mwezi machi, 2013 shule za msingi na za Serikali zilikuwa zina mahitaji ya madawati 3,339,678; yaliyopo ni 2,029,310 na upungufu ni 1,310,675.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa fursa ya uvunaji wa miti ya asili na kupandwa kwa shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoa na utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule. Ili kudhibiti uvunaji holela Halmashauri zinatakiwa kufuata taratibu zilizowekwa za uvunaji misitu ikiwa ni pamoa kuomba vibali kutoka katika mamlaka husika katika Wilaya.

Aidha, kutekeleza miradi ya kijamii Serikali imekuwa inasilitiza kutoa kipaumbele kutumia mafundi wenye sifa wa maeneo husika ikiwa ni sehemu ya ajira na kuinua kipato cha wanajamii wa maeneo miradi inapotekelezwa.

19 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, katika juhudini za kumaliza tatizo la madawati nchini, Serikali imekuwa inapeleka fedha katika Halmashauri kwa ajili ya ununuzi na utengenezaji wa madawati.

Mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 3 zilipelekwa katika Halmashauri zote kwa ajili ya madawati ambapo Mkoa wa Mara ulipata shilingi milioni 197 na mwaka 2012/2013 shilingi bilioni 1 zilipelekwa katika Halmashauri zote kwa ajili ya madawati na Mkoa wa Mara ulipata milioni 68.

Aidha, Serikali itatumia shilingi bilioni 18.4 zilizotokana na fidia ya ununuzi wa rada kwa ajili ununuzi wa madawati kwa Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahimiza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutenga fedha katika mipango ya Bajeti kwa ajili ya miundombinu mbalimbali ya shule ikiwemo madawati na kuhakikisha fedha zinatolewa kwa ajili hiyo zinatumika ipasavyo. (*Makofii*)

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia uvunaji wa miti na usafirishaji wa magogo nje ya nchi kupitia bandari ya Dar es salaam. Kwa nini Serikali isisitishe usafirishaji wa magogo nje ya nchi hadi hapo wanafunzi wote watakapo jitoseleza kwa madawati?

La pili, kwa kuwa Serikali imekuja na mpango mpya wa kuhakikisha kila mwanafunzi anakaa kwenye dawati lake.

Je, ni mkakati gani umeandaliwa na Serikali ili kuhakikisha kila mwanafunzi anafaidika na mpango huo?

**SPIKA:** Waziri wa magogo simwoni lakini Naibu Waziri hebu jibu huko, ninaona ana wasiwasi kuzuia magogo ya wenzie, Mheshimiwa nani atajibu suala la magogo? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa magogo na magogo yapo ya aina mbili yale yanayopatikana kwa njia halali na yale ambayo yanayopatikana kwa njia ambayo siyo halali na hatua mbali mbali zinachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya msako na kuyakamata.

Serikali imepiga marufuku na ninaomba nirudie kuwa, tumepiga marufuku usafirishaji wa aina yoyote wa magogo kwenda nje ya nchi kwasababu tungependa bidhaa zote za maliasili kwanza ziwekewe thamani hapa nchini kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya sehemu nyingine.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa shule zetu zote za msingi na Serikali zina mahitaji makubwa ya madawati ili kutosheleza watoto wetu wote kukaa kwenye madawati kama ambavyo tunatarajia iwe.

Kwa sasa mkakati tulio nao ni kuhakikisha kwamba tunaboresha upatikanaji wa madawati na kama ambavyo nimetoa kwenye jibu la msingi mahitaji ya shule za msingi, lakini pia katika eneo la sekondari mahitaji ya madawati sasa hivi ni milioni moja laki sita na arobaini na nane elfu, mia nane hamsini nane yaliyopo sasa hivi ni milioni moja laki mbili thelathini na moja elfu, mia nne arobaini na tunao upungufu wa madawati laki nne na kumi na saba elfu mia nne kumi na nane.

Mheshimiwa Spika, kwa upungufu huu wa maeneo yote mawili na kwa kuwa tumetoa Mamlaka hizi kwa Serikali za Mitaa, kwa maana ya Halmashauri zote nchini ambazo zinamiliki shule hizi, zinao uwezo wa kuratibu vizuri fedha wanazojitengea kwenye Bajeti yao lakini ambazo sisi TAMISEMI huwa tunazipeleka kama nyongeza lakini pia kutumia Maliasili kwa wale ambaao wana misitu hiyo, kuvuna

19 APRILI, 2013

mbao kwa taratibu zilizopo na nilipokuwa ninatoa mchango katika Bajeti ya Waziri Mkuu nilieleza kuwa Kamati ya uvunaji ya misitu iko katika kila Halmashauri na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ni Mkuu wa Wilaya katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili halina matatizo na mkakati huu tukiusimamia wote kwa pamoja tunaweza kufanikiwa kuondoa tatizo la madawati nchini. (*Makofii*)

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Hivi karibuni Serikali ilifanya operasheni maalum katika Wilaya ya Tunduru kuititia Wizara ya Malliasili operesheni ambayo ilipelekeea uvunaji au ukamataji wa tani nyingi tu za mbao ambazo mpaka sasa zimelundikwa katika Ofisi ya Halmashauri na kwenye Ofisi ya Malliasili pale Wilayani.

Je, Serikali itachukua hatua mahsus sasa kutumia mbao zile zilizoko pale kwa ajili ya kupunguza angalau kidogo tatizo la madawati katika Halmashauri ya Tunduru?

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tumekuwa na utaratibu ambao ni endelevu kwamba shule au taasisi zinazohusika zinaruhusiwa kuomba vibali vya uvunaji wa mbao na hasa inapokuwa kwa ajili ya utengenezaji wa madawati, jambo ambalo kwanza tunalichukulia kama uongezaji wa thamani wa mbao na kwa ajili ya kuendeleza elimu hapa nchini. Ninaomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kuwa maombi hayo yatapewa kipaumbele. (*Makofii*)

**MHE. CHRITOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kuwa kuna upungufu mkubwa wa madawati na hili ni tatizo kwa shule zote Tanzania nzima.

Je, Waziri haoni sasa kuwa kuna haja ya kutoa agizo maalum kwa Halmashauri zote ziweze kutoa tenda ya kutengeneza madawati katika vyuo vyetu vya VETA kuliko kutoa tenda kwa watu binafsi ambao wanatengeneza madawati kwa bei kubwa zaidi?

19 APRILI, 2013

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli na kama nilivyoeleza kwenye swalii la msingi na namna ambavyo alikuwa amelihitaji Mheshimiwa Msafiri kuwatumia wajasiriamali kwenye eneo hilo.

Haya mambo yote ni maamuzi ya Halmashauri yenye na kwa sasa tunavyo Vyuo Vya Ufundii, ziko Halmashauri zina Vyuo Vya Ufundii, lakini pia tuna VETA katika kila Mkoa. Kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri yenye kutambua umuhimu wa au kupeleka VETA kutengeneza madawati yotekwa pamoja au kutumia wajasiriamali walioko katika Halmashauri ambaao wana uwezo tayari na walishasoma katika vyuo vya VETA ili watengeneze kwa gharama nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni mipango ya Halmashuri yenye. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaendelea na swalii linalofuata Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

Na. 67

### **Ukosefu wa Maji Safi**

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swalii langu nilikuwa ninaomba Bunge lako Tukufu kulipa taarifa kwamba kumetokea mafuriko makubwa sana Meatu na mpaka tunapoongea hivi zaidi ya nyumba kumi zimeanguka na watu wamepoteza makazi. Aidha zaidi ya nyumba karibu 100 ziko mbioni kuanguka kutokana na kuwa na unyevunyevu mwingu kwenye matofali.

19 APRILI, 2013

Nilikuwa ninaomba Serikali yote kwasababu iko hapa iweze kuliangalia hili kwa ajili ya kuweza kusaidia watu hawa ambaao wamepata matatizo. Baada ya kusema hayo ninaomba swali langu Namba 67 lijibewe.

**SPIKA:** Kabla hajajibu swali msije mkadhani huu ndiyo utaratibu, siyo utaratibu wakati wa Maswali na Majibu, hayo yanawezekana wakati wa hoja kama aliyosema. Kuna utaratibu mwininge.

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji safi na salama wakazi wa Kata za Mwabuzo, Bukundi, Mwanjolo, Mwamishali, Mwamanyima, Nkoma, Imalaseko na Vijiji vyake ambaao wamekuwa kwenye matatizo ya ukosefu wa maji safi na salama kwa matumizi yao na mifugo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulkwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana kuwa ipo changamoto ya upatikaji wa maji safi na salama ya uhakika kwa matumizi ya binadamu na mifugo katika Kata za Mwabuzo, Bukundi, Mwanjolo, Mwamishali, Mwamanyima, Nkoma, Imalaseko na Vijiji vyake. Mkakati wa Serikali wa kuzipatia maji safi na salama Kata hizo kama ifuatavyo:-

Katika bajeti ya mwaka 2011/2012 utekelezaji wa miradi ya maji umefanyika katika kijiji cha Mwang'umbi Kata ya Imalaseko ambapo mradi mkubwa wa maji ya bomba ulioanza kujengwa chini ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji na kugharimu kiasi cha shilingi milioni 297.4 ambaao unatarajia kukamilika mwezi mei, 2013 na utakuwa na uwezo wa kuhudumia wakazi wapatao 2,500.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 chini ya mpango wa progaramu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji, shughuli ya usanifu wa mradi mkubwa wa maji katika Kata ya Bukundi Kijiji cha Bukundi umeshafanyika na kukamilika. Shughuli za Ujenzi wa miundombinu zitaanza mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo shilingi milioni 560.9 zimeidhinishwa kwa kazi hiyo. Kata ya Mwanyahini na Kijiji cha Mwanyahina inapata maji kuitia mradi wa maji wa mjini Mwanhuizi.

Mheshimiwa Spika, kuitia fedha za mfuko wa kuchochlea Maendeleo ya Jimbo la Meatu, Kijiji cha Mwanyahina kitapelekewa maji kwa kuongeza vituo vya maji viwili. Mradi huo utagharimu kiasi cha shilingi milioni 9.4 pamoja na nguvu kazi za wakazi wa kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele cha utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mengine yaliyobaki kadiri fedha zitakayopatikana. (*Makofii*)

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri mimi nina maswali ya nyongeza. Nilitaka kuuliza Serikali ina mpango gani lakini katika majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema kuwa mfuko wa Jimbo ambao umetoa fedha milioni 9.4 kwa ajili ya kuwasaidia Kata na Kijiji cha Mwanyahina kupata maji.

Mimi nikataka kumwambia Mhesmiwa Waziri kuwa Mfuko wa Mbunge siyo Serikali. Mimi ninataka kujua Serikali ina mkakati gani sasa katika Kata hizi ambazo zina upungufu wa maji safi na salama kwa ajili ya wananchi wake?

Mheshimiwa Spika, wakati Watanzania wote zaidi ya milioni 44 wana matatizo ya maji, lakini kwa bahati mbaya sana katika mwaka wa fedha unaokuja Waziri wa mwenye dhamana ya Maji amejitengea zaidi ya bilioni 30 kupeleka maji kwenye Wilaya yake peke yake.....

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge usiharakishe kazi sisi hatujaona hicho unachokisema, uliza swali kuna Kanuni inayokukataza usiharakishe biashara hii. Sisi hatujaona, haya uliza vizuri swali lako la pili.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Swali la pili ni kwamba, wakati Watanzania wote zaidi ya milioni 40 wana matatizo ya maji zikiwemo Kata ambazo nimezitaja kwenye swali langu.

Je, mwaka wa fedha unaokuja badala ya bilioni 30 kupelekwa kwenye Wilaya moja, Serikali ina mpango gani sasa wa kuzimega fedha hizi ili ziweze kwenda na kwenye maeneo mengine ambako hakuna maji kama Meatu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza hizi hela zinazoitwa *Constituency Development Catalyst Fund* ni hela za Serikali. Hizi ni hela za Serikali *that is the bottom line*. Anachopewa Mbunge pale ni dhamana kwa sababu yeye ndiye Mwenyekiti wa Mfuko wa kuchocheara Maendeleo katika jimbo lile.

Hizi hela zikienda zinaenda kwenye Halmashauri, Mwenyekiti wake anakuwa ni Mbunge, Katibu wake ni Afisa Mipango, Madiwani wawili, Watendaji wa Kata wawili na mtu mmoja anayetoka katika *Non Governmental Organization* anakuwepo pale na wanafungua akaunti ambayo CAG akija pale anakuja kukagua. *My judgment* kwa niaba ya Waziri Mkuu ni kwamba kumtaja Mbunge hapa ni *Credit* kwake kwamba Mbunge huyu anatumia hela yake vizuri. Kwa maana ya dhamana hiyo anayoibeba kufanya kazi hii inayozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Opulukwa tumeiweka hapa kwa sababu tunatambua jithada zako tunafurahishwa na jithada za Mbunge kwamba ameziweka hizi hela katika huu mpango hapa. Hii inakwenda kwenye kitu kinachoitwa *Opportunity and Obstacles to*

*Development (O and OD)* wao kwa priorities zao wanaona kwamba ni hili. Mimi nataka nichukue nafasi hii kukupongeza kwamba ulikaa kwenye kikao ukaruhusu hizi hela ziende katika mpango huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, ni kwamba sisi hapa hatujiondoi katika mpango huu, hela zilizopangwa kwa ajili ya Halmashauri hii shilingi milioni 833.1 katika vijiji na Kata hizi ambazo Mheshimiwa Opulukwa anazungumzia hapa vijiji sita vimo humu ndani vimepangwa kwamba vitafanyiwa kazi hiyo.

Kwa hiyo mimi siwezi kubishana na Mheshimiwa Opulukwa, anatoka kwenye *centre* ya tatizo lenyewe, kwa hiyo atakuwa anafahamu. Lakini *it is my opinion* kwamba katika jambo hili sisi tutahakikisha kwamba tutasaidiana na wewe Mheshimiwa Upulukwa ili wananchi waweze kupata.

Mheshimiwa Spika, sasa hili swalii la pili linaloulizwa hapa najua ni suala la Bajeti na Bajeti inakuja hapa, ombi langu ni tumpitishie Waziri wa Maji Bajeti yake ili aweze kwenda kutekeleza hii miradi mingine inayozungumzwa. (*Makof!*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kutoa maelezo ya nyongeza ya majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, nalo inahusu bilioni thelathini ambazo hatuzifahamu mpaka sasa kama zimetengwa au hazijatengwa, lakini najua linaelekea wapi. Nalo linahusu Mradi wa Maji wa Mwanga – Same - Korogwe na Olkesmet. Mradi huo ulianzishwa wakati mimi nikiwa Waziri wa Maji, kutokana na matatizo makubwa sana ya maeneo ya Wilaya zote hizo pamoja na Mji wa Olkesmet wote mlifika huko mnajua.

Kwa hiyo, tuliomba fedha za *BADEA* tumepata na fedha zetu za Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji nazo zipo. Kwa hiyo, ni bahati nzuri tu kwamba Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe amekuja kuwa Waziri wa Maji

19 APRILI, 2013

katika mradi ambao mimi niliuanzisha. Lakini unahusu Wilaya yake hamna uhusiano wowote kati ya kuanzishwa huo mradi na yeye, ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, hili tatizo la maji ni la nchi nzima na hasa maeneo ya vijijini na kwa kuwa lengo la Millennia la Saba ni uendelezaji wa asili ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu hasa kwenye masuala ya maji ikiwa ni sehemu mojawapo.

Je, Serikali haioni busara ya kushirikisha jamii yote na hasa vijijini namna ya kuyavuna maji ya mvua kama inavyotokea Meatu sasa, kuyahifadhi, kuyatumia na kuyasimamia ili yaweze kutumika na viumbe hai pamoja na *seepage* iweze ikafanya kazi yake ili uumbaji wa asilia wa Mwenyezi Mungu uendelee na tatizo hili linaweza likawa ni shirikishi kwa kila Mtanzania badala ya kuiachia Serikali peke yake?

**SPIKA:** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kifupi, tumevuta sana hili swali na litaishia hapo sasa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, katika Ofisi ya Makamu wa Rais kuna mkakati wa kitaifa wa kuhifadhi vyanzo vyote vya maji nchini na katika mkakati huu tumeainisha vyanzo vyote Baraza la Hifadhi ya Mazingira limeshaibua vyanzo vyote muhimu vya maji na tunaendelea na mkakati wa kuelimisha wanafunzi na mkipitisha Bajeti yetu leo mkakati huo uko ndani ya Bajeti hiyo. Kwa hiyo, tutaanza taratibu za kuelimisha wananchi na kuwafundisha njia mbalimbali za kuhifadhi vyanzo vya maji. (*Makof*)

**SPIKA:** Tumetumia muda mwangi sana kwa swali moja naomba tuendelee kwa sababu tunakwenda kwa wakati. Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli.

19 APRILI, 2013

Na. 68

### **Mchango wa Asilimia Kumi kwa Mfuko wa Wanawake na Vijana**

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Serikali mara zote imekuwa ikiziagiza Halmashauri kuchangia Asilimia kumi ya Mapato yake kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana, lakini agizo hilo halitekelezwi na Halmashauri nyingi hapa nchini:-

Je, Serikali inawaambia nini Wanawake na Vijana ambao wanategemea mfuko huo ili waweze kupata mikopo ambayo itawakwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Serikali imekuwa ikiagiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana. Fedha hizi hutumika kwa utaratibu wa kuwakopesha wanawake na Vijana ambao wamejiunga katika vikundi au *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambazo Serikali imekuwa inakabiliana nazo ni hizi zifuatazo:-

(i) Halmashauri nyingi kutotekeleza ipasavyo agizo la Serikali la kutenga asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya Wanawake na Vijana;

(ii) Mwamko mdogo wa jamii kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali na *SACCOS*; na

19 APRIL, 2013

(iii) Wajasiriamali wengi kutorejesha mikopo na hivyo kukwamisha wengine kupata fursa ya kukopa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ina vikundi 27 vya wajasiriamali wanawake na kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2009/2010 vikundi hivi vyote vilipatiwa mikopo ya jumla ya shilingi milioni 19.9.

Aidha, kwa upande wa Vijana Halmashauri hii ina vikundi (11) vya vijana na *SACCOS* (2) ambapo kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 na mwaka 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ilitoa mikopo ya shilingi milioni 21.8 kwa vikundi vya vijana.

Marejesho ya fedha za mikopo ya wanawake kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 – 2009/2010 ni shilingi milioni 8.1 sawa na asilimia 41.1 ya mkopo uliotolewa. Kwa upande wa vikundi vya Vijana jumla ya shilingi milioni 5 zilirejeshwa sawa na asilimia 23 ya mkopo uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa agizo kwa Halmashauri zote kutekeleza agizo la Serikali la kutenga asilimia 10 kwa ajili ya wanawake na vijana. Aidha, Halmashauri zinaagizwa kuhamasisha vijana na wanawake ili waweze kujiunga na vikundi vya ujasiriamali na *SACCOS* ili waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Wabunge na Madiwani kuendelea kushirikiana na watendaji wa Halmashauri kuhakikisha kuwa vikundi vya Wanawake na Vijana vilivyochukua mikopo vinarejesha ili vikundi vingine viweze kukopesheka. (*Makofii*)

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Waziri kunipa *data* za Rufiji japokuwa sijaziomba. (*Makofii*)

19 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, katika jibu lake la Msingi Waziri anasema kwamba pesa zinakwenda lakini hazirejeshwi. Tatizo kubwa ni kwamba mikopo hii inapewa watu binafsi na pia inapewa watu kuititia Vyama vya kisiasa na siyo Wajasiriamali kama ambavyo inatakiwa.

Je, Waziri ana mkakati gani wa kuhakikisha pesa hizi zinarudi kwa sababu Mfuko hauruhusu waliokopeshwa kupelekwa Mahakamani, mkakati gani wa maksudi upo kwa ajili ya pesa hizi zirudi?

Katika Mkutano wa Kumi tumepitisha Mfuko wa Vijana, lakini tunaona Mfuko wa YWF tayari umeshashindwa kuleta tija.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba mfuko tulioipitisha hapa katika Mkutano wa Kumi unaleta tija kwa walengwa waliokusudiwa siyo kama mfuko huu ambao umeshashindwa? (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeelewa? Haya jibu tu ulivyoelewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi naona tuweke vizuri hili jambo ili tuweze kuelewana hapa, maelekezo yametolewa.

Mheshimiwa Jumanne Maghembe wakati Rais alipokuwa katika sherehe za Ushirika Duniani kule Kagera, alitoa maelekezo na kuagiza kwamba Halmashauri zote zihakikishe kwamba zinatenga fedha hizi.

Ninayo barua hapa ya Katibu Mkuu anayekumbushia kuhusu agizo la Serikali kwamba Halmashauri zote zihakikishe kwamba zinatenga fedha hiso.

Ninaomba sasa hivi nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri Mkuu kutamka hapa kwamba *we shall never leave any stone unturned* tumeziagiza Halmashauri zihakikishe kwamba asilimia tano ya fedha zinatengwa kwa ajili ya akina mama na asilimia tano zinatengwa kwa ajili ya wanaume. Sasa majibu ambayo yametolewa na Halmashauri wanasema ni kidogo.

**SPIKA:** Ni vijana bwana siyo wanaume wote, ni kwa vijana tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ni Wanawake na Vijana ndiyo hiyo hiyo. Sauti hapa ni msisitizo tu nakuomba uniwie radhi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii Halmashauri inayozungumzwa hapa, hela za ndani kwa sababu hiyo asilimia tano tunayoizungumza na asilimia tano nyingine ya akina mama na vijana hii hela wao katika *own source* waliingiza bilioni 3.1 katika hali ya kawaida na mahesabu ya kawaida tulitegemea kwamba Halmashauri ya Rufiji ingetenga shilingi milioni 311 lakini imetenga milioni 67 tu ambazo ni chini ya nusu, ni robo ndiyo imetengwa pale. Kwa hiyo hela hizi haziendi.

Mheshimiwa Spika, moja ni hilo kwamba hawajajiunga na *SACCOS* huwezi kusema tu jamani Rufiji chukueni hela hizi, nyumbani kwako wapi pale kwenye kichuguu, nyumbani kwako wapi, pale karibu na Msikiti, hapo chini kwenye mfereji ndipo nyumbani kwetu, hakuna mtu anatoa hela katika mazingira ya namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachoomba hapa watu wetu wafundishwe kwamba hela zitakwenda katika utaratibu wa kifedha kwa maana ya kuijunga na *SACCOS*. Ninamwomba Mheshimiwa Mchuchuli atuchukulie hili jambo tunalozungumza hapa, hatutoi tu hela hapa tunarusha tu hivi hivi, tunaweka utaratibu.

19 APRILI, 2013

Lakini tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba Halmashauri zinatenga hizi hela. Hata katika taarifa ya CAGimeonesha kwamba kuna Halmashauri ambazo hazikutenga hizi hela.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme mbele yako kwa niaba ya Waziri Mkuu tutazitaka Halmashauri zote zipeleke na kama hazikupeleka Mkurugenzi Mtendaji tutamkata hela zake za mfukoni na Afisa Mipango. (*Kicheko*)

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mbona hajibu maswali yangu? Hajajibu!

**SPIKA:** Tunaendelea, maswali ya nyongeza na majibu yawe mafupi maana yake tunakula muda hapa. Mheshimiwa Zaynab Vullu.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa, swali la msingi linaulizia habari ya Halmashauri ya Rufiji na kwa kuwa, wananchi wa Halmashauri ya Rufiji bila kujali itikadi zao wamejiunga katika vikundi nya SACCO\$ na VIKOBA mbalimbali kwa ajili ya kukopa ili kuendeshea miradi yao; na kwa kuwa, Halmashauri nyingine hazina uwezo wa kuweza kutoa mikopo kwa ajili ya wananchi wao.

Je, Serikali iko tayari kuongeza pesa kwa zile Halmashauri ambazo hazina uwezo wa kutosha ili waweze kukopesta wananchi wao. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, suala hapa siyo suala la kwamba Halmashauri moja inafanya vizuri. Kwa hiyo ipelekwe hela, sisi tunachosema tu ni kwamba Rufiji tunawapongeza kama wamejipanga hivi wanavyozungumza, hela nyingine ambazo zinakwenda pale kuacha hizi asilimia tano ambazo tunazzungumzia hapa, ni hela zile zinazotoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, ndizo zinazokwenda pale, nazo hizo ugonjwa wake ni huo huo tena.

Unakuta kwamba watu wanapokea hizi hela zinatakiwa ziwe katika *revolving fund* hawarejeshi pale. Matokeo yake ni kwamba ukimwambia Maendeleo ya Jamii apeleke hela nyingine pale hapeleki, lakini nataka nimthibitishie Mheshimiwa Zaynab Vullu kama anachotuambia hapa ni kweli na ndivyo tumeona lakini nimetoa *percentages* hapa nikaonesha kwamba ni jinsi gani hawarudishi Rufiji.

Mheshimiwa Spika, tutakwenda kushirikiana naye kwenye ule mfuko wa wanawake ambao unatoka Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ili tuone kama wanafanya vizuri tumshawishi Waziri mwenye dhamana aendelee kuisaidia Halmashauri ya Rufiji. Tunapenda kumpongeza kwa kazi nzuri anayoifanya kwa upande wa akina mama. (*Makof!*)

**SPIKA:** Kwa sasa ni maswali matatu tumezidi nusu haiwezekani, tunaingia Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina atauliza swali hilo.

Na. 69

#### **Utoroshaji wa Fedha za Umma**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Ripoti ya *Global Financial Integrity* (GFI-2008) ilionyesha kuwa kwa kipindi cha miaka 39 toka 1970- 2008

Tanzania ilipoteza kiasi cha shilingi Triliion 11.6 na kushika nafasi ya 13 kati ya nchi bora kwa utoroshaji wa fedha za Umma kwenda katika mabenki ya kidunia:-

- (a) Je, ni kina nani walitorosha fedha hizo hapa nchini?
- (b) Je, hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maswali yanayoulizwa na Mbunge yamo mionganoni mwa mambo ambayo yanafanyiwa kazi na Kamati Maalum ya Kitaifa Iliyoundwa na Serikali kufuatia Azimio la Bunge Na.9 la Mwezi Novemba, 2012. Azimio hilo la Bunge lilitokana na Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Zitto Kabwe iliyozungumzia suala hili analoliuliza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Azimio la Bunge linaitaka Serikali kutoa taarifa kamili Bungeni baada ya kulfanya kazi, tunaahidi pindi kazi hiyo itakapomalizika Serikali itatoa taarifa kamili kuhusiana na suala hilo. Nashukuru sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa ajili tu ya kuweka kumbukumbu sawa sawa, ni kwamba mimi ndiye nilikuwa mtu wa kwanza kuleta taarifa za tafiti wa utoroshaji wa fedha nje ya nchi kabla hata ya Mheshimiwa Zitto Kabwe na niliwasilisha hapa Bungeni.

Kwa hiyo rekodi ikae sawa sawa kwamba hii hoja si tu ya Zitto Kabwe, isipokuwa Muasisi wake ni mimi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza. Kwanza kwa taarifa nilizonazo ni kwamba Kamati hii iliyoundwa ya Kitaifa inashughulikia utoroshaji fedha zilizofichwa Uswiss peke yake. Sasa Naibu Waziri wa Fedha anithibitishie kama hii Kamati ita-cover pesa zote ambazo zimeteroshwa na kufichwa kwenye mabenki mbalimbali, kwa sababu taarifa nilizonazo mimi ambazo najua ni za uhakika ni kwamba inashughulikia fedha za Uswiss peke yake.

Katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo *Draft* ya kwanza ilitaja suala la utoroshaji wa fedha kuwa ni kigezo kikubwa ambacho kinasababisha nchi kukosa fedha, kwa sababu fedha nyingi zinatoroshwa na kwenda kufichwa, lakini *final draft* ilioletwa sasa hivi ya Mpango wa Maendeleo kipengele kile cha utoroshaji wa fedha nje ya nchi kimenyofolewa hakipo. Sasa nataka kujua sababu iliyopelekea kunyofolewa kwa kipengele cha utoroshaji wa fedha nje ya nchi ni nini katika Mpango wa Maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako nijibu swali la kwanza na swali la pili nitamwachia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumalizia.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kwa sababu kwanza kulikuwa kuna suala la uasisi,

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba hilo liache.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**

Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kuhusiana na je, hiyo Kamati itashughulikia masuala yote hasa lile lililokuwa limeibuliwa hapa Bungeni?

Mimi nina imani kuwa hiyo ndiyo iliyopelekea hiyo Kamati kuundwa na kwa vyovvote vile, bila shaka italfanyia kazi kama ilivyokuwa inatakiwa kwa sababu ahadi imetolewa na Serikali kuwa ripoti italetwa hapa Bungeni kwa ajili ya majibu ya suala hilo kama ni kweli lipo hivyo ama sivyo.

19 APRILI, 2013

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kumjibu Mheshimiwa Mpina, jibu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sina uhakika na hiyo *page* iliyonyofolewa kwenye Kitabu chake, lakini namwomba Mheshimiwa Mpina, tukutane na timu ya Wataalamu wa Mipango tukiwa na vitabu vyote viwili. Hicho kitabu cha awali kilichokuwa na maelezo hayo na hicho cha pili kilichonyofolewa, ili tuone kitu gani kimetokea.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, majibu ya Kamati hii yanayosubiriwa na Watanzania walio wengi na hususan Watanzania masikini. Sasa ni lini Kamati hii itamaliza kazi yake na kuleta majibu hapa Bungeni? Ahsante sana.

**SPIKA:** Kwanza, hawaelewi hata mnasema nini.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwashukuru Wabunge wote, wanaozungumzia suala hili na Wabunge wote ambao wamekutana na Kamati yangu kuhusiana na suala hili.

Suala hili, tuliahidi kwamba, tutaleta majibu kwenye Bunge hili; kwa kweli, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu, kwamba, kazi hii ni kazi ngumu kama alivyosema Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, ambaye pia tunamshukuru, alifika kwenye Kamati na akatujulisha kwamba, ni vizuri tutumie taarifa hizo za uchunguzi kupata taarifa kamili.

Tunakwenda, Kamati inafanya kazi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, atatoa taarifa hapa kuhusu shughuli za Kamati hiyo. Ninafikiri tusubiri wakati huo, ahsante sana. (*Makof!*)

19 APRILI, 2013

Na. 70

**Nyaraka za Kodi Kufanyiwa Tathmini  
Dar es Salaam**

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR** aliuliza:-

Wafanyabiashara wanaotumia Kituo cha Tunduma kupitishia bidhaa zao, hulazimika kukaa hapo kwa muda wa siku 10 – 15 kungojea nyaraka za kodi zifike kutoka Dar-es-Salaam. Hali hii, husababisha usumbufu, utumiaji wa njia za panya na mianya ya rushwa:-

- (a) Je, Serikali, haioni kuwa, mpango huo haunta tija kwa Serikali na Wafanyabiashara?
- (b) Je, mpango huo utaboreshwu, ili kupunguza muda wa kungojea na kuwa siku 1 – 2?
- (c) Je, ni jambo gani linalosababisha nyaraka zote zifanyiwe tathmini Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo Februari 2010, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), ilianzisha utaratibu wa utengenezaji wa Nyaraka za Forodha katika Kituo kimoja (*Centralised Customs Data Processing*) kilichopo Dar-es-Salaam, ambapo waingizaji bidhaa au mawakala wao katika vituo vyote nchini huwasilisha nyaraka za kuingizia bidhaa nchini kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, tangu utaratibu huu uanzishwe Serikali, imepata faida mbalimbali kama; kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za Forodha, kuwanianisha taratibu za uthaminishaji wa bidhaa zinazofanana katika mipaka yetu nchini, kutekeleza kwa vitendo dhamira ya *TRA* ya matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika shughuli zake na kupunguza muda wa kuondoa bidhaa katika maeneo ya Forodha, ambapo ni wastani wa siku 11 hivi sasa.

Aidha, kupitia mfumo huu, *TRA* imeboresha uwezo wa wafanyakazi kwa kuwaunganisha kiutendaji katika mfumo mmoja na kuleta uwazi katika utendaji kwa vile wafanyabiashara au mawakala wa forodha, hawana nafasi ya kuwasiliana moja kwa moja na Ofisa Forodha anayefanya kazi nyaraka zake. Hii pia, imepunguza uwezekano wa kuwepo vitendo nya rushwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuchelewa kwa mizigo katika Mpaka wa Tunduma, hakutokani na kutumika kwa mfumo huu. Tatizo liliopo Tunduma ni uwezo mdogo wa kituo cha Nakonde, upande wa Zambia, kupokea malori kadiri yanavyowasili kutokea upande wetu. Kituo hiki hakina eneo la maegesho, *Parking Yard*, hali inayosababisha malori yote yanayoingia Zambia, kuegeshwa upande wa Tanzania, wakati yakifanyiwa taratibu za kiforodha kwa upande wao.

Aidha, kwa upande wetu nyaraka za mizigo husika, hukabidhiwa madereva wa malori wasafiri nazo, ili wazikabidhi kwa Afisa Mfawidhi wa Mpaka husika hivyo, hakuna nyaraka zinazobaki nyuma wakati mizigo hiyo inaposafirishwa. Aidha, *TRA* inatarajia kujenga Kituo kimoja cha forodha (*One Stop Border Post*) katika mpaka huu, mpango unaotekeliza kwa pamoja na nchi zote mbili.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu WAziri, amekubali kwamba, mizigo inakaa kwa muda wa siku 11 katika Kituo cha Tunduma, maswali yangu ni mawili.

19 APRIL, 2013

Je, ni lini kituo hiki kitajengwa?

Je, kituo hiki kitapunguza muda wa ku-process document hapo Tunduma?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nisahihishe, siku 11 ndio muda ambao unatumika kutoa mizigo na mawakala au wenyewe mizigo yao kwa mfumo huu unaotumika sasahivi na TRA.

Kwa hiyo, pale Tunduma mzigo unaweza ukakaa muda wowote kufuatana na taratibu zinazofanyika upande wa Nakonde, Zambia. Lakini kituo hiki kitakapojengwa, ambapo si muda mrefu sana tunategemea kutokana na Bajeti yetu, basi kitarahisisha matatizo yote haya kumalizwa.

**SPIKA:** Inabidi nimpendelee Mheshimiwa Silinde, kwa sababu, ndio pale kwake.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mimi nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, katika moja ya jitihada tuliyoifanya kwa sababu, siku hizi ambazo Serikali, imegundua kwamba, pana msongamano mkubwa sana wa magari eneo la Tunduma; moja ya sababu, aliyoitao ni kwamba, kituo cha Forodha cha Tunduma ni kidogo kama ilivyo upande wa Nakonde.

Lakini moja ya jitihada tuliyoifanya ni kuhakikisha kwamba, wenzetu wa Nakonde, walikuwa wako tayari kuruhusu magari ama kituo chao cha forodha kufanya saa 24; tukazungumza na upande wa Serikali yetu, wakasema watakuwa tayari.

19 APRILI, 2013

Lakini mpaka sasa niilize Serikali, imefikia wapi kuja na hatua ya kuhakikisha eneo la Tunduma, magari yanaruhusiwa? Yaani katika Kituo cha Forodha cha Tunduma, wafanye kazi saa 24, ili kuweza kuruhusu magari yaende upande wa pili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwanza kwa juhudini ambazo anazifanya kuhakikisha kuwa tatizo hili linapungua.

Lakini nimhakikishie kuwa kwa kweli, kwa jinsi hali ilivyo sasahivi pale itabidi kwanza papanuliwe kabla haijaruhusiwa kazi kufanywa hivyo. Kwa sababu, jinsi ilivyo sasahivi ukiruhusu saa 24 ina maana yatakuwa mengi zaidi na patazidi kuwa pana matatizo. Tunajaribu kuangalia uwezekano wa ku...

*(Hapa, Waheshimiwa Wabunge, walizomea kwa sauti)*

**SPIKA:** Ni kwa nini mnapenda kuzomea watu? Tabia mbaya pia.

Mheshimiwa Waziri, endelea.

Kuzomea hakusaidii kitu chochote.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**  
Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo ambalo linafanyiwa kazi. Tumesikia maoni yenu na sisi wenyewe tumekuwa tukilifanya kazi tangu mwanzo na ndio maana tunasema tunajenga *One Stop Border Post* kwa sababu hiyo hiyo kuhakikisha kuwa, tunazidisha *efficiency* ya Kituo cha Tunduma katika kuhakikisha kuwa, mizigo inakuwa *cleared* haraka zaidi.

19 APRIL, 2013

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishieni kuwa Serikali, ni lazima isimamie hili kwa sababu, tunapata mapato zaidi tunapofanya kwa muda mwingu zaidi. Kwa hiyo, sisi tunalifahamu hilo, ahsanteni. (*Makofii*)

Na. 71

### **Wageni Wanaotelekeleza Watoto Kuwajibishwa**

**MHE. ANNA M. J. MALLAC** aliuliza:-

Baadhi ya Raia wa Kigeni wanaoingia nchini kwa shughuli mbalimbali huzaa na raia wenyeji na kisha hutetelekeza watoto bila kutoa msaada wowote:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kuwawajibisha wageni hao, ili kuokoa maisha ya watoto hao na kupunguza wimbi la watoto wa mitaani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anna Mary Stella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za malezi, matunzo na ulinzi wa watoto waliozaliwa nje ya ndoa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria hiyo, Kifungu cha 43, kinæeleza kuwa, mama wa mtoto aliyetelekezwa anawajibika kuwasilisha shauri la matunzo ya mtoto katika vyombo vya Sheria. Wizara yangu kama msimamizi na mtekelezaji mkuu wa Sheria hii, baada ya kupokea mashauri ya aina hiyo hufanya mawasiliano na Wakala wa Kimataifa wa huduma za jamii (*International Social Service*), ili kuweza kufanya uchunguzi na ufuatiliaji katika upande wa mlalamikiwa ambaye, ndiye anayedhaniwa kuwa baba wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchunguzi huo, inapothibitika bila shaka yoyote kuwa, mlalamikiwa ndiye baba halisi wa mtoto husika, taratibu za malezi, matunzo na ulinzi wa mtoto huyo hufanywa kwa kutumia Ofisi za Balozi za Nchi husika.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha haki za watoto walio katika mazingira hatarishi, hususan watoto waliotelekezwa, wanaonyanyaswa na kufanyiwa vitendo vya ukatili zinalindwa. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri na Wadau wa Maendeleo, imeanzisha programu ya ulinzi na usalama wa mtoto, ambapo mifumo ya ulinzi na usalama wa watoto umeimarishwa kwa kuundwa timu za ulinzi katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji/Mitaa. Hadi sasa mifumo ya ulinzi na usalama imeanzishwa katika Halmashauri za Hai, Magu, Kasulu, Temeke, Nyamagana, Illemela, Kinondoni, Ilala, Musoma na Bukoba. Timu hizo hujumuisha Wataalamu mbalimbali wanaohusika na ulinzi wa watoto, wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 programu ya ulinzi na usalama itasambazwa katika Halmashauri 25. Hivyo, kupitia programu hii, matukio ya unyanyasaji, utekelezaji na ukatili kwa watoto yatazuiwa na kushughulikiwa ipasavyo. (*Makof*)

**MHE. ANNA M. J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la kumwuliza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, nalenga wanawake wa Vijiji ambao wamezalishwa watoto na wageni walioingia nchini kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za ujenzi wa barabara ama uchimbaji wa madini, Wachina ama Waingereza. Wale watoto mpaka sasa hawana matunzo kwa sababu, wamezaa na wale wafanyakazi wao wa barabarani waliokuwa wakibeba zege au wale wanaowapikia wakati wanapochimba madini. Wanawake wale mpaka sasa wanahangaika na wale watoto weupe ambao kwa kweli, wanahitaji matunzo. (*Kicheko/Makof*)

19 APRIL, 2013

**SPIKA:** Swali, swali, swali.

**MHE. ANNA M. J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, wanashikishwa kipande cha muhindi wanakula na wamechakaa vibaya na Serikali yetu inaona, Afisa Maendeleo Jamii huko Wilayani wanaona.

Je, Serikali, ipo tayari kutoa elimu kwa wale akinamama Vijijini kwa sababu hawajui haki zao wazipate wapi, ili wale watoto watunzwe?

**WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba, yapo hayo matatizo ya akinamama wanazaa na watu ambao wanawaacha na watoto. Tumejitalidi, Serikali, kuelimisha kuhusu uzazi wa mpango. Ni vizuri sana kama hawana budi wafanye hilo jambo, watumie kinga na hizi kinga zinatolewa bure katika Hospitali zetu na katika Vituo vya Afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kupitia Bunge hili, nawashauri akinamama wote na sio wale waliokuwepo kwenye machimbo tu, tuzae kwa mpango.

Sisi pia wenyewe tunajua kwamba, tunatumia hiyo kwa hiyo, kama Wabunge, pia tuwahamasishe wanawake wenzetu tukiwa katika Mikutano yetu kwamba, uzazi wa mpango ni muhimu, ili tusiwe na watoto wengi ambao wanazurura tu. Ahsante sana. (*Makof/Kicheko*)

19 APRILI, 2013

Na. 72

## **Operesheni ya Wafugaji Haramu Kagera**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA** aliuliza:-

Mnamo mwezi Novemba, 2012, Mkoa wa Kagera uliendesha operesheni ya kuondoa wafugaji haramu ndani ya Hifadhi ya Burigi:-

(a) Je, ni wafugaji haramu wangapi walibainika katika operesheni hiyo?

(b) Je, Serikali, imewapa fidia gani wale walioharibiwa mashamba yao na mifugo, hususan Kata ya Lusahunga na Kaniha?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya heshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Mbunge wa Bihamarulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Wizara yangu mwezi Novemba, 2012 ilifanya doria maalum kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kagera, ikiwa ni pamoja na Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Taasisi ya Idara ya Uhamiaji, Taasisi ya *TAKUKURU* na *JWTZ*, ili kuwaondoa wafugaji haramu ndani ya Mkoa wa Kagera, hususan Wilaya ya Bihamarulo, Muleba, Karagwe na Ngara; Operesheni hii, ilipewa jina la *OMAKA – Okoa Mazingira Kagera*.

19 APRIL, 2013

Umuhimu wa operesheni hii ultokana na ukweli kwamba, kulikuwepo na uingizaji wa mifugo, hasa ng'ombe, shughuli za upasuaji wa mbao, uchomaji wa mkaa, shughuli za kilimo na uchimbaji wa madini isivyo halali ndani ya Hifadhi ya Misitu na Mapori ya Akiba ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, nimjibu sasa Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Swali lake, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika operesheni hiyo, wafugaji haramu wanne walikamatwa ndani ya Mapori ya Akiba ya Burigi, Biharamulo na Kimisi, wakiwa na jumla ya ng'ombe 466.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 na Kanuni ya Kifuta Jasho na Kifuta Machozi ya mwaka 2011, Serikali, haitoi kifuta jasho kwa wafugaji haramu na wavamizi wanaolima ndani ya maeneo ya Hifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mbassa, swali la nyongeza?

Mtanisamehe sitawapa nafasi ninyi wengine muda huu.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini kabla sijaauliza maswali hayo, niombe tu uwe ushauri wa bure kwamba, Mheshimiwa Waziri anapoletewa majibu kama haya, wayaangalie kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, katika jibu la msingi, Naibu Waziri, amekiri kwamba, kulikuwa na uingizwaji wa ng'ombe katika Pori la Akiba la Burigi. Wafugaji wengi wamenyanyasika, mifugo yao imepigwa risasi, wengine ng'ombe wao wamechukuliwa na zoezi hili, limegharimu zaidi ya milioni 400.

Je, Waziri yuko tayari kulieleza Bunge hili Tukufu kwamba, operesheni hii haikuwa na tija? Kwa sababu, kama ni milioni 400 zimetumika, wamekamatwa wafugaji haramu wanne ndani ya Wilaya nne; inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, kuna watu ambao wameishi maeneo hayo miaka nenda rudi na juzi katika swali la nyongeza nilitolea mfano wa Profesa Kulikoyela Kahigi, anakozaliwa; leo hii wananchi hawa wanaambiwa kwamba, wanaishi kwenye hifadhi.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kurudi kuangalia mipaka yake ya asili na kuwasikiliza wananchi, ili waishi kwa amani? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya heshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kutokana na changamoto ambazo tunazo katika mapori haya ya akiba, ikiwa ni pamoja na pori la Burigi, Biharamulo na Kimisi, ambalo mimi mwenyewe nililitembelea. Nilizungumza na na Mheshimiwa Mbasa wakati nafanya hiyo ziara.

Tutafanya utaratibu ambao tunaendelea kuufanya wa kuangalia upya mipaka, tuhakikisha kwamba, hakuna ugomi wa kimpaka. Mipaka inatathminiwa upya kati ya wananchi na mapori yetu, kwa sababu uhifadhi hauwezi kufanikiwa bila ushiriki wa kutosha wa wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, katika shughuli iliyofanyika ya kuhakikisha kwamba, wafugaji wale ambao walikuja wakaingia katika maeneo kadhaa na katika Wilaya nyangi, Mkoa wa Kagera, jitihada ya Serikali, ilikuwa sio tu kwa ajili, ya kukamata na kuwaondoa wale ng'ombe.

Tuna changamoto katika maeneo ya Burigi, katika maeneo ya Biharamulo. Katika maeneo ya Kimisi na baadhi ya mapori Kagera ambako tuna, sio tu wafugaji, lakini tuna tatizo kubwa sana la ujangili, ambalo linafanywa na watu wanaotoka ndani ya nchi na wengine wanaotoka nje ya nchi.

Tuna watu ambao kwa taarifa tulizonazo, wamejichimbia ndani ya yale mapori ya Serikali, kwa kutumia utaratibu unaofahamika na kwa kutumia utaratibu mwingine ambao haufahamiki. Tunaendeleza misako hii mchana na usiku kuhakikisha kwamba, tunatunza hifadhi yetu, tunahakikisha kwamba, watu wetu watakuwa salama.

Lakini kikubwa ni misitu yetu kwa ajili ya suala zima la ecosystem ni lazima iwe salama na hifadhi ya wanyamapori ambao wako katika tishio na hasa tembo ambao wanatishiwa na watu ambao wana nia mbaya ya kuwamaliza kwa sababu ya ubin afsi wao wa kujitajirisha wao wenyewe. Tutahakikisha kwamba, misako hii itaendelea usiku na mchana, iliyotangazwa na ambayo hajatangazwa.

## UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize. Kufuatana na Kanuni yetu, Kanuni ya 7(1), ya Kanuni za Bunge; imeweka uwepo wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao wanapatikana kwa kuchaguliwa na Wabunge. Aidha, Kanuni ya 7(2), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 11(1)(a), ya Kanuni za Bunge, imeweka utaratibu utakaofuatwa katika kufikia upatikanaji wa Wenyeviti wa Bunge kwamba, Kamati ya Uongozi itapendekeza majina ya Wabunge sita, ambayo yatawasilishwa Bungeni ili kupigiwa kura kutoka miongoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, jana terehe 18 Aprili 2013, Kamati ya Uongozi ilikutana pamoja na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ili kuyapata majina sita ya kuwasilisha Bungeni ili yapigiwe kura. Hata hivyo, baada ya kupitia Kanuni hizo, kwa pamoja walifikia uamuzi wa kupendekeza majina matatu, ili yaweze kuwasilishwa Bungeni na Bunge liombwe kuyapitisha kama yalivyokubaliwa na Kamati ya Uongozi.

Sababu zenyewe ni kwamba, hii kazi msidhani kila mtu anaitaka, kazi ya kukaa hapa watu hawakubali, hata hao wengine watatu wamebembelezwa tu. Siyo rahisi watu kusema na mimi nataka, na mimi nataka, siyo rahisi. Hivyo, hao watatu waliweza kukubali.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge letu lilikwishaweka utaratibu wa chaguzi na hasa pale wagombea wanapolingana na idadi inayotakiwa na vigezo vinavyohitajika, vikitekelezwa *conventionally*, kwamba wagombea hao wanapita bila kupingwa.

Kwa kuwa maamuzi ya Kamati ya Uongozi yalifanywa jana ya kuleta majina matatu, Bunge linatekeleza uamuzi huo wa makubaliano ya kuwapitisha Wabunge wafuatao kuwa Wenyeviti wa Bunge. Wabunge hao ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Mussa A. Zungu na Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib. (*Makofii*)

19 APRIL, 2013

Kuna wengine hapa walibembelezwa, hayo ndiyo majina tuliyonayo. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Mussa A. Zungu na Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib; kwa kuungana nasi hapa Mezani tufanye mambo yetu. (*Makofi*)

Kwa kifupi lazima niwaambie kwamba, kazi ya hapa Mezani siyo nyepesi, ni nzito anayetaka kujaribu aje, siku moja tu, halafu atuachie. Kwa hiyo, siyo nyepesi. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 18 Aprili 2013, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Klongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, aliomba Mwongozo wangu kuhusu kama uamuzi wa Naibu Spika kumpa Mheshimiwa Tundu A. Lissu adhabu ya kutoka nje ya ukumbi wa Bunge na kutohudhuria vikao vya Bunge kwa siku tano pamoja na Wabunge wengine watano ambao ni Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa na Mheshimiwa Highness S. Kiwia kama ni sahihi na siyo kukiuka Kanuni ya 72 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokumbuka tarehe 17 Aprili 2013, wakati majadiliano ya Bunge yakiendelea kuhusu hotuba ya bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora) na (Uratibu na Mahusiano), Mheshimiwa Job Ndugai ambaye ni Naibu Spika, aliamuru Mheshimiwa Tundu A. Lissu atolewe nje kwa kukiuka sharti la Kanuni ya 60(12) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013 wakati aking'ang'ania kupewa fursa ya kutoa Mwongozo na kutokana na kukaidi Mamlaka ya Spika kwa kuendelea kusimama wakati Kiti kilipompatia Mheshimiwa Susan Kiwanga fursa ya kusema. Aidha, Naibu Spika, aliwatoa nje Wabunge wengine kwa utovu wa nidhamu kwa kitendo cha kuwazuia Wapambe

19 APRILI, 2013

wa Bunge, kutekeleza amri waliyopewa na Kiti ya kumtoa nje Mheshimiwa Tundu A. Lissu na kusababisha fujo.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu na hasa Kanuni 2(2) na 5(1) ya Kanuni za Bunge, imempa mamlaka Spika, kufanya maamuzi pale ambapo hakuna utaratibu uliowekwa kwenye Kanuni. Aidha, uamuzi unaofanywa na Spika, ambao unaruhusu uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na ambao unaleta amani na utulivu Bungeni, ukishafanywa, unaingizwa kwenye Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa shughuli za Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kitendo kilichotokea tarehe 17 Aprili 2013, hakiwezi kupuuzwa kwa vile ni kitendo dhahiri cha kudhalilisha mamlaka ya Spika na kilikuwa kitendo cha utovu wa nidhamu wa hali ya juu na Watanzania wote walishuhudia na wanalaani kilichokwuwa kinaendelea ukumbini na kustahili kwa yejote aliyejewa anaongoza Bunge wakati ule angeweza kutoa uamuzi kama huo.

Sasa Mwongozo wangu kuhusu suala hili ni kama ifuatavyo:-

Ninatumia Kanuni ya 5(1) na Kanuni ya 2(2) inayompa mamlaka Spika kufanya maamuzi pale ambapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi kwamba uamuzi uliofanywa na Mheshimiwa Job Ndugai ambaye ni Naibu Spika wa kuwatoa nje Mheshimiwa Tundu A. Lissu, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa na Mheshimiwa Highness S. Kiwia na kubaki nje kwa kutokuhudhuria vikao vya Bunge vitano, ni halali na sasa utaingizwa kwenye Kitabu cha Maamuzi ya Spika ili Mbunge yejote atakayefanya vitendo kama hivi, apewe adhabu hii. Mwisho wa kunukuuu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walismama  
kuomba Mwongozo wa Spika)*

19 APRILI, 2013

**SPIKA:** Hakuna mahali wana-*challenge* uamuzi wa Spika, fuateni utaratibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 - Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; na Malengo na Kazi zillizopangwa kutekelezwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana kwa kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Napenda kuzihakikishia Kamati zote mbili kuwa, tutazingatia ushauri na miongozo iliyotolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Machi, 2013 aliyeokuwa Mbunge wa Chambani Pemba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, alifariki Dunia. Kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rai,s natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kwa msiba huo mkubwa uliotupata. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kutupatia faraja, amina. Aidha, wapo wananchi waliofariki Dunia katika maafa na ajali nchini, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wafiwa na kuwatachia afya njema wote waliojeruhiwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako limepokea taarifa

kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Mwelekeo wa Mwaka 2013/14. Napenda kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa jinsi walivyoweza kutoa maelezo kwa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya utekelezaji kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2012/2013 na malengo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais katika mwaka 2012/2013, imeendelea kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa ya kuratibu masuala ya muungano na ushirikiano wa sekta zisizo za muungano pamoja na usimamizi wa mazingira hapa nchini. Ofisi imetekeleza majukumu hayo kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano wa mwaka 2011-2016, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 119.

Mheshimiwa Spika, masuala ya muungano. Utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2012/2013. Mwaka huu 2013, Muungano wetu unatimiza miaka 49 na wananchi wanaendelea kupata fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli za kimaendeleo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuienzi historia yetu hatuna budi kuulinda na kuuendeleza katika njia na mfumo utakaokubalika na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Muungano kupitia Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2012/2013, iliahidi mambo kadhaa ambayo utekelezaji wake umeendana na maagizo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 kama yalivyoagizwa kwenye Ibara ya 184. Uhalsia wa utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa majengo na Taasisi za Muungano Tanzania Zanzibar ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa Taasisi za Muungano Zanzibar ili kuimarisha huduma. Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuhamasisha Wizara, Idara na Taasisi za Muungano kujenga au kufungua Ofisi zao Tanzania Zanzibar. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2013, ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu, Fumba, Zanzibar umekamiliaka na ujenzi wa Ofisi ya Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyopo Buyu unaendelea. Taasisi ya kusimamia Blashara za Nje Tanzania (*TanTrade*) imefungua Ofisi ya muda na kwa sasa inaendelea na mchakato wa kujenga Ofisi ya kudumu. Aidha, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imefungua Ofisi yake Kikwajuni; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imefungua Ofisi huko Kilimani; na Tume ya Sayansi na Teknolojia (*Commission for Science and Technology – COSTECH*) na Tume ya Nishati za Atomiki (*Tanzania Atomic Energy Commission - TAEC*) ofisi zao zipo Tunguu.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia masuala ya Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya Kamati, na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa. Ofisi imeendelea kuweka ratiba na kuratibu vikao vya masuala ya Muungano na vile vya ushirikiano wa kisekta, ili kuendeleza majadiliano na hatimaye kupata ufumbuzi wa vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na Kamati ya Pamoja SMT na SMZ. Kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Ofisi ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuondoa changamoto katika

utekelezaji wa masuala ya Muungano. Katika jitihada za kujadili na kuondoa changamoto za Muungano, vimefanyika vikao vitano nya Sekretarieti, kikao cha Makatibu Wakuu, kikao cha Mawaziri na kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Kikao cha pili cha Makatibu Wakuu, Mawaziri na kile cha Kamati ya Pamoja SMT/SMZ vinatarajiwa kufanyika ndani ya mwezi Aprili, 2013, na kukamilisha idadi ya vikao vilivyopangwa kwa mwaka huu wa fedha 2013/2013.

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo bado zinafanyiwa kazi kwa maagizo ya Kamati ya Pamoja katika kikao cha Januari, 2013 ni pamoja na:-

(i) SMT na SMZ kushirikiana kuanzia hatua ya awali ya mchakato wa upatikanaji wa Misaada na Mikopo ya kibajeti. Agizo hili linafanyiwa kazi kwa pamoja na Makamishna wa Sera za Fedha na Makamishna wa Fedha za Nje wa Wizara zinazoshughulika na mambo ya fedha kwa SMT na SMZ.

(ii) Kujulikana kwa Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki. Mawaziri wa Fedha SMT na SMZ wameshapitia nyaraka zenye taarifa hizo na kuona hali ilivyokuwa na kiwango cha fedha kilichohamishiwa Benki Kuu ya Tanzania.

(iii) Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Faida ya Benki Kuu. Maamuzi ya jinsi ya kugawana mapato yatokanayo na Faidaya Benki Kuu yatatolewa baada ya kukubaliana na suala la hisa za SMZ katika iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, kwa sasa mgao unaendelea kutolewa kwa asilimia 4.5 (4.5%).

(iv) Utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi asili. Wanasheria Wakuu wa SMT na SMZ wanaongoza Kamati ya Wataalam wa sekta za nishati wanaofanyakazi ya kuandaa utaratibu wa mapendekezo ya kubadilisha sheria zinazohusu utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia, ili SMZ iwe na fursa ya kuanza kuijandaa kwa kazi hiyo, katika misingi ya kisheria, sera na matayarisho ya kitaasisi.

(v) Uvubi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Baada ya kumaliza utata juu ya uendeshaji uvubi kwenye bahari kuu na mfumo wa kugawana mapato, liliojitokeza juu yake ni kuwa mamlaka ya Uvubi wa Bahari Kuu inashindwa kufanya kazi zake kikamilifu kutokana na kutopitishwa kwa Sheria inayosimamia mamlaka hiyo, na suala zima la Uvubi katika Bahari Kuu. Kamati ya pamoja ilio agizo kwa sekta husika upande wa SMZ kuharakisha kupitishwa kwa Sheria hiyo.

(vi) Usajili wa vyombo nya moto. Vikwazo nya kuingiza na kusajili vyombo nya moto kutoka upande mmoja wa Muungano kwenda mwengine vitaondoshwa kupitia kutungwa kwa sheria mpya ya usafiri wa Barabarani kwa upande wa SMT. Sheria hiyo inatarajiwa kuondosha vikwazo vilivyomo kwenye Sheria ya *The Road Traffic Act*, 1973, Sura ya 168, na Kanuni zake za mwaka 2001, Kanuni Nambari 17 na 18, Kanuni za Magari ya Kigeni za 1973 (*The Foreign Vehicle Rules of 1973*), *Traffic Ammendment Rules* za 1973, pamoja na Sheria ya Tozo kwa Magari ya Kigeni (*The Foreign Vehicles Charges Act*), Sura ya 84. Kwa upande wa SMZ marekebisho yatahusisha Sheria ya Usafiri Nambari 7 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Usajili na Leseni za Magari za mwaka 2007, kanuni ya 13.

Mheshimiwa Spika, kuratibu uboreshaji wa Sheria na Kanuni za fedha zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Authority - TRA*) na Bodi ya Mapato Zanzibar (*Zanzibar Revenue Body - ZRB*) kwa faida ya pande zote za Muungano. SMZ imeanza kupata gawio la Kodi ya Mapato ya Mshahara (*PAYE*), kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 gawio kwa SMZ ni shilingi bilioni 21. Kwa kuwa *PAYE* ni suala linalohusu mapato ya Muungano, Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ wamekubaliana kwamba, ushauri wa kisheria upatikane kutoka kwa Wanasheria Wakuu wa SMT na SMZ kuhusiana na urekebishi waji wa Sheria ya Kodi ya Mapato. Aidha, Mawaziri hao wamekubaliana pia kufanya tathmini ya kubaini idadi ya wafanyakazi na Kodi ya Mapato ya Mshahara (*Pay As You Earn - PAYE*) itokanayo na wafanyakazi

19 APRILI, 2013

waliopo Zanzibar na mishahara yao kulipwa Tanzania Bara na kwa wafanyakazi waliopo Tanzania Bara na mishahara yao kulipwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*) kwa mashirika yaliyosajiliwa Tanzania Bara na kufanya kazi Zanzibar na Mashirika yaliyosajiliwa Zanzibar na kufanya kazi Tanzania Bara, Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ walikubaliana kufanya tathmini kubaini mashirika na kodi zinazohusiana na mashirika hayo. Baada ya Wizara zinazoshughulika na mambo ya fedha kufanya kazi maagizo hayo, taarifa ya yaliyobainika italetwa katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ tarehe 28 Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, kuratibu uboreshaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za ajira kwa Taasisi za Muungano ili kuwa na uwiano. Ofisi imeratibu Kikao cha Kamati ya Kuboresha Sheria na Sera za Utumishi katika Taasisi za Muungano. Kamati kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Ajira ilianda mapendekezo ya mgao wa ajira katika Taasisi za Muungano. Mapendekezo hayo ya mgao wa ajira ambayo yatahusu kada ya wataalamu tu, yameridhiwa na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ mwezi Januari, 2013. Ofisi ya Waziri Mkuu SMT na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais SMZ zitasimamia utekelezaji wa makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya kijamii na kiuchumi inayotekelawa na pande zote mbili za Muungano. Ofisi imefanya ufuatilaji wa utekelezaji wa miradi ya kiuchumi, miundombinu na ya kijamii inayofadhiliwa na mashirika ya kimataifa na kutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, chini ya udhamini wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi hiyo ni *Tanzania Social Action Fund - TASAF, Marine and Coastal Environment Management Programme – MACEMP*, miradi ya kuimarisha huduma za kilimo na ufugaji ili kuongeza tija *Agricultural/Livestock Sector Development Programme - ASDP/ASDPL*, na miradi ya *Millenium Challenge Account*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mfuko wa Maendeleo

ya Jamii – *TASAF*. Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya *TASAF*, (*TASAF II*), umefanyika kuanzia 2005 – 2013. *TASAF II* imetekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Miradi iliyotekelawa na jamii katika ngazi ya kijiji, mtaa na shehia wakati wa *TASAF II* ni 12,250. Jumla ya fedha zilizotumika katika *TASAF II*/ni Dola za Marekani milioni 288.5. Kuanzia Julai, 2012 hadi Machi, 2013, jumla ya shilingi bilioni 1.184 zimetumika kutekeleza miradi ya *TASAF* kwa Zanzibar na shilingi bilioni 18.816 kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio makubwa ya *TASAF II* Serikali iliamua kutekeleza Awamu ya Tatu ya *TASAF* ambapo mpango wa kunusuru Kaya Maskini utatekelezwa. *TASAF II*/itakelezwa kwa miaka kumi yenye vipindi viwili vyta miaka mitano. Utekelezaji utafanyika kwenye Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara, Unguja na Pemba kwa madhumuni ya kuwesheha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Tanzania –*MACEMP*. Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani, ujulikanao kama “*The Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)*” ni mradi uliotekelawa kuanzia Desemba 2005 na kukamilika Februari 2013. Mradi huu ulitekelezwa katika Halmashauri zote 16 za Pwani ya Bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania Bara na Wilaya zote 10 kwa upande wa Zanzibar. Mradi huu ulisimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, ambapo kwa upande wa Tanzania Bara, usimamizi wake ni kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa upande wa Zanzibar. Katika Mwaka wa Fedha 2012/13, hadi kufikia mwezi Machi, 2013 jumla ya shilingi 2,518,729,600/= zilitumika kwa Tanzania Bara na shilingi 1,321,617,472/= kwa Zanzibar, ambapo fedha hizo zimetumika kutoa mafunzo kwa Kamati za Uvuvi na Viongozi wa Serikali, kununua vifaa vya TEHAMA na ujenzi wa bweni la Chuo cha Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta

ya Kilimo na Mifugo – *ASDP/ASDPL*. Programu hii ina sehemu kuu mbili, ambazo ni Programu ya Kuimarisha Huduma kwa Wakulima, na ya pili ni ya kuendeleza Sekta ya Mifugo ambapo Dola za Marekani 16,565,600 zilitengwa kwa Tanzania Bara na Dola za Marekani 4,058,700 kwa ajili ya Tanzania Zanzibar. Kwa upande wa Zanzibar, katika mwaka huu wa fedha, hadi kufikia mwezi Februari, 2013 kiasi cha shilingi 499,723,405/= zimeshatumika kati ya shilingi 819,806,515/= zilizotolewa kwa ajili ya kilimo, na shilingi 702,670,784/= zimetumika kati ya shilingi 1,306,895,302/= zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mifugo. Kwa upande wa Tanzania Bara kwa mwaka huu wa fedha hadi kufikia mwezi Machi, 2013, zimeshatolewa shilingi bilioni 41.7 kati ya shilingi bilioni 101.8 zilizoidhinishwa kwa ajili ya kilimo na shilingi 542,336,123/= zimetumika kati ya shilingi bilioni 1.5 zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Millenium Challenge Account (MCA)*. Mradi huu umeendelezwa utekelezaji wake kwa kuboresha miundombinu katika sekta ya usafirishaji hususan ujenzi wa barabara, miundombinu ya umeme na maji. Katika mwaka huu wa fedha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umeme na kuanganishwa umeme kwenye miundombinu mipya kwa Zanzibar umekamilika. Mradi huu wa umeme Zanzibar umegharimu dola za Marekani 50 milioni kati ya dola za Marekani 698 milioni zilizotolewa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi hiyo imebainika kuwa na mchango mkubwa katika jitihada za kuwapunguzia wananchi umaskini. Zaidi ya wananchi Laki nane (800,000) wamenufaika na utekelezaji wa miradi hii kwa upande wa Unguja na Pemba na wananchi wanaokadiriwa milioni 14 wamefaidika kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, miradi yote hiyo imebainika kuwa na mchango mkubwa katika jitihada za kuwapunguzia wananchi umaskini. Zaidi ya wananchi 800,000 wamefaidika na utekelezaji wa miradi hii kwa Unguja na Pemba na wananchi wanaokadiriwa milioni 14 wamefaidika kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kutoa elimu kwa umma. Katika

kuhakikisha kuwa Serikali inatoa elimu kwa umma ili kuwa na jamii yenyewe uelewa wa masuala ya Muungano, Ofisi ilianda Taarifa ya Mafanikio ya Awamu ya Nne ya Serikali pamoja na kuelimisha Umma kuititia luninga za *TBC*, *ITV* na *Star TV*. Pia, Ofisi imeandaa nakala elfu tano (5000) za jarida la Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, kuratibu masuala ya kukuza uchumi na marekebisho ya Katiba. Ofisi imefanya mapitio ya Katiba za Nchi za Trinidad na Tobago, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uingereza, Finland, Brazil, Ethiopia, Afrika Kusini, Canada, Marekani, Nigeria, Ujerumanu na India ambazo zinifuata mfumo wa Muungano/Shirikisho kwa lengo la kuona na kulinganisha mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga Sheria na mamlaka ya utoaji haki. Aidha, masuala ya mahusiano ya kifedha na uchangiaji wa gharama za uendeshaji wa masuala ya Muungano yameangaliwa. Maoni yamewasilishwa kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, ili kusaidia kukuza uchumi wetu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapokea misaada ya kibajeti kila mwaka. Misaada hiyo hugawiwa kwa asilimia 95.5 kwa Tanzania Bara na asilimia 4.5 kwa Tanzania Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013, SMZ imepokea shilingi 18,737,000,000/= gawio la misaada ya kibajeti (*General Budget Support - GBS*); shilingi 14,000,000,000/= gawio la Kodi ya Mapato itokanayo na mishahara ya wafanyakazi (*Pay As You Earn - PAYE*); na shilingi 1,244,000,000/= fedha za Mfuko wa Maendeleo kwa Majimbo ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano. Ofisi imeendelea kuratibu ushirikiano wa SMT na SMZ katika maeneo ya kubadilishana uzoefu, sera, sheria, utaalamu na watalamu kati ya Serikali mbili; kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na ziara za kikazi za mara kwa mara kati ya sekta zinazofanya shughuli zinazoshabihiana, pamoja na kujadili kuhusu changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Vikao hivi vya kisekta vimeongeza ushirikiano kati ya SMT na SMZ.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2013/2014

kwa Idara ya Muungano. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 hadi 2015. Uratibu wa shughuli za Muungano na kudumisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utafanywa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kulitekeleza hilo, Ofisi inapanga kuratibu vikao viwili (2) vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano, vikao viwili (2) vya Mawaziri wa SMT na SMZ, vikao viwili (2) vya Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ na vikao sita (6) vya Sekretarieti ya SMT na SMZ.

Mheshimiwa Spika, Ofisi itaendelea kuelimisha umma kuhusu Muungano kupitia redio, luninga, magazeti, majarida, vipeperushi, semina na maonesho ya kitaifa. Aidha, Ofisi itaendelea na jitihada ya kubuni mradi kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma ili kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Uratibu wa masuala ya kiuchumi, kijamii, na kisheria yaliyo ndani na nje ya Muungano utaendelezwa kwa manufaa ya nchi yetu. Wizara na Taasisi za Serikali zenyet kazi zinazoshabihiana SMT na SMZ zitahimizwa kukutana angalau mara mbili (2) kwa mwaka katika Vikao vya kisekta na katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, Ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya kazi na kujenga uwezo wa watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi sita (6) kuhusu masuala ya diplomasia, usuluhushi, uandikaji wa taarifa na uongozi bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha masuala ya Muungano, naomba sasa niwasilishe masuala ya Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015 na utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2012/2013. llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 hadi 2015, Ibara ya 194 (ukurasa 232-234)

inaelekeza Serikali kutekeleza mambo yaliyoorodheshwa hapa chini ili kuhakikisha hifadhi ya mazingira nchini inakuwa endelevu. Kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti hususan miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa vitongoji, mitaa, vijiji na kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, vituo vya afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Ofisi imepokea taarifa za upandaji miti za Mikoa 17 katika kipindi cha 2011/12, jumla ya miti 145,156,884 ilipandwa, kati ya hiyo, miti 108,171,349 imestawi ambayo ni sawa na asilimia 74.52 ya miti iliyopandwa. Aidha, napenda kuipongeza mikoa iliyowasilisha taarifa ya upandaji miti na nikumbushe Mikoa yote ihakikishe zoezi hili linakuwa endelevu na taarifa zinawasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta mwamko zaidi kwa wananchi, Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji kwa kupanda na kutunza miti ilianzishwa mwaka 2008. Tuzo hii imeshatolewa mara mbili mwaka 2010 na 2012 na kwa mara ya tatu itatolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni, 2014. Mikoa inahamasishwa kwa mara nyingine kushiriki katika shindano hilo.

(b) Serikali za vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge Sheria ndogo za hifadhi ya misitu. Serikali kupitia Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira (*Environmental Management Act - EMA – ISP*) imewezesha

Wizara za kisekta na Halmashauri za Wilaya na Manispaa kuhuisha masuala ya hifadhi ya mazingira katika mipango ya maendeleo na kuhimiza Wilaya na Manispaa kutunga Sheria ndogo za hifadhi ya misitu, tathmini ya mazingira na usafi wa mazingira. Baadhi ya Halmashauri zimetunga na zimeanza kutekeleza sheria hizo. Pamoja na halmashuri nilizozitaja mwaka wa jana, Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Biharamulo, Arusha na Tanga zimeanza kutumia Sheria ndogo katika kuainisha vyanzo nya maji na kuvitunza.

(c) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo nya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe. Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani kwa Kupitia Miradi mitano (5) ya hifadhi mazingira ambayo ni *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP); Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP-PWANI); Western Indian Ocean Marine Highway Programme (WIOMHP); Coastal and Marine Contamination Prevention Project (CMCPP); na Agulhas and Somali Current Large Marine Ecosystems (ASCLME)*.

Mafanikio katika kutekeleza miradi hii ni kuboreka kwa mazingira ya bahari na fukwe, vipato nya wananchi kuongezeka kupitia miradi 15 iliyotekelawa, elimu kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira imetolewa na kuwezesha uandaaaji wa Mipango Kazi ya usimamizi wa mazingira kwa Halmashauri na Wilaya 16. Aidha, faida nyingine ni kupatikana kwa taarifa za mifumo ikolojia ya ukanda wa Bahari ya Hindi zilizotumika kuandaa taarifa ya hali ya mazingira ya Pwani, na ramani zinazoonesha maeneo muhimu yanayohitaji kuhifadhiwa (*Sensitivity Mapping*), na kuandaa mpango wa dharura utakaosaidia katika usimamizi wa mazingira ya bahari.

Aidha, miradi inayohimiza kupanda mazao yanayohimili ukame na ufugaji nyuki katika mikoko imeibuliwa. Vile vile, maofisa wa Mamlaka ya Bandari, NEMC na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

(SUMATRA) wamejengewa uwezo katika kusimamia matukio ya dharura za uchafuzi baharini.

(d) Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa Mazingira. Kama niliviyolieze Bunge lako Tukufu mwaka wa jana, Ofisi kuitia Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira, imeiwezesha Wizara ya Nishati na Madini kuandaa Mpango wa Mazingira wa Sekta ya Nishati na Madini. Mpango huu umewezechesha sekta hii kuandaa hadidu za rejea kwa ajili ya mtaalam mwelekezi atakayepitia na kuandaa Sera ya Nishati Mbadala.

(e) Kupunguza ghamra za vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti. Serikali katika bajeti ya mwaka 2012/2013, iliondoa kodi ya ongezeko la thamani katika vifaa vya gesi. Hatua hii ya Serikali imechangia kupambana na uharibifu wa mazingira utokanao na matumizi ya kuni na mkaa hasa maeneo ya mjini. Kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vya nishati mbadala (upepo na jua) imepungua kwa asilimia kumi na nane hivyo kuchangia kupunguza ghamra za vifaa hivi kwa ujumla wake. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na wadau kama vile Wakala wa Nishati Vijijini imetekeleza miradi ya kufikisha huduma za nishati nafuu ikiwa ni pamoja na zile za nishati mbadala.

(f) Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Ofisi kwa kuitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira iliendelea kufanya ukaguzi wa viwanda, biashara na migodi ili shughuli hizo zisichafue mazingira na kusisitiza uzingatiaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na ufuatiliaji wake. Jumla ya taasisi 70 vikiwemo viwanda na taasisi nyingine zenye shughuli za uzalishaji kama; viwanda vya vyakula, saruji, mbaao, vyuma, karatasi, migodi ya dhahabu, mashamba ya chai, kahawa, vituo vya mafuta na hoteli zilizopo ufukweni mwa Bahari ya Hindi na Ziwa

Victoria, katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Iringa, Mbeya na Mtwara zilifanyiwa ukaguzi. Viwanda ambavyo vimeonekana kuchafua mazingira vilipewa muda wa kurekebisha mifumo ya mitambo ya kusafisha majitaka na baadhi ya viwanda vimeanza kufanya Ulaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*). Vilevile, faini ilitozwa kwa viwanda kumi na tatu (13) katika mikoa ya kanda ya ziwa, viwanda vitano (5) vya Dar es Salaam na kimoja (1) cha Mtwara. Viwanda hivyo, viliamriwa kulipa faini ya kati ya shilingi milioni 3 - milioni 10. Jumla shilingi milioni 110 zinatarajiwa kukusanywa kutokana na zoezi hili.

(g) Kutekeleza mradi wa vijiji vya mfano vya hifadhi ya Mazingira (*eco-villages*). Kama nilivyoliezea Bunge lako Tukufu mwaka jana, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa vijiji vya mfano (*eco-villages*) kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya wengine lengo la kuongeza uwezo wa jamii wa kupunguza na kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Kama nilivyoliezea Bunge lako Tukufu mwaka wa jana, mradi huu unatekelezwa katika Mkoa wa Dodoma katika kijiji cha Chololo; Mkoa wa Morogoro katika Tarafa ya Mgeta na Matombo katika vijiji vya Matalawe, Londo, Luale, Tawa, Konde, Milawilila na Kibungo Juu; na Pemba katika Shehia za Uwandani (Vitongoji "A" na "B"), Pujini, Fundo, Uvinje na Kokota. Vijiji hivi vinatekeleza miradi ya ubunifu ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na hifadhi endelevu ya maliasili. Kutokana na mafanikio ya mradi huu, Jumuia ya Ulaya imekubali kusaidia awamu ya pili ya mradi kwa ufadhili wa kiasi cha *Euro* milioni 8, sawa na takriban shilingi bilioni 16 kuanzia mwaka 2013.

Mheshimiwa spika, kwa mwaka 2012/2013, shughuli zilizofanyika katika kijiji cha Chololo ni pamoja na hifadhi ya ardhi na mbini bora za uzalishaji wa mazao ya kilimo ambapo uzalishaji wa zao la mtama uliongezeka kwa asilimia 137 kutoka kilo 215 hadi 510 kwa ekari; uwele uliongezeka kwa asilimia 105 kutoka kilo 200 hadi 410 kwa ekari; na uzalishaji wa alizeti uliongezeka kwa asilimia 252 kutoka kilo 77 hadi 271 kwa ekari. Pamoja na hayo, wafugaji wa ngombe 26 na wafugaji 28 wa mbuzi walipewa mafunzo kuhusu ufungaji

bora. Vile vile, mabwawa 11 ya kufugia samaki yalijengwa na mizinga ya kisasa 60 ya nyuki ilitengenezwa na kupewa wafugaji 60 waliopatiwa mafunzo ya ufgaj nyuki. Mafunzo yalitolewa pia kwa washiriki 40 kuhusu utengenezaji wa kisasa wa ngozi, kati yao 12 ni wanawake. Kwa upande wa upandaji miti, jumla ya miti 22,321 ilipandwa, ambapo asilimia 70 ilimea. Aidha, jumla ya majiko banifu 100 yalikamilika na mengine 1000 yako katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012/2013 shughuli zilizofanyika katika viji ya Pemba ni pamoja na utengenezaji wa majiko banifu, ambapo jumla ya majiko 307 yalikamilika; utengenezaji wa mashine za kutengeneza vitofali vya nishati ya kupikia, ambapo mashine 5 zilitengenezwa. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wananchi 1085; katika utengenezaji wa matofali kwa ajili ya ujenzi (30); matengenezo ya vifaa vya nishati mbadala, kama nishati ya jua (10); utunzaji wa vitalu vya miti (268); utengenezaji wa majiko banifu (105); na mbinu za kisasa za uzalishaji wa miti ya matunda na mboga mboga (672).

(h) Kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) katika miradi ya ujenzi. Serikali kuitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, imeendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba miradi ya ujenzi inafanyiwa TAM kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira. Miradi ya ujenzi iliyosajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa TAM kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 ni 78 na iliyopatiwa Hati ni 34. Miradi iliyobaki imerejeshwa kwa wahusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi, naomba sasa nieleze Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2012/2013 na malengo ya mwaka 2013/2014 kwa usimamizi na hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Programu yake *EMA-ISP*. Katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zilitkelezwa: *K u a n d a a*

Mwongozo wa Kuendesha Mfuko wa Mazingira; kuandaa Mwongozo wa Kusimamia Fedha za Mfuko wa Mazingira; kuendelea kuandaa utaratibu wa kuendesha Baraza la Rufaa za Mazingira; na kuendesha kikao kimoja cha Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Mazingira. Aidha, mafunzo ya uongozi yalitolewa kwa watumishi 15 wa Ofisi ya Makamu wa Rais yakijumuisha viongozi na maafisa wakuu, mwezi Septemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Programu yake kwa kuendelea kuandaa na kukamilisha Kanuni na Miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; kuwezesha Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Mazingira na Baraza la Rufaa za Mazingira kufanya kazi zake; kuanza kuendesha Mfuko wa Mazingira; kukamilisha Maandalizi ya Ripoti ya Pili ya Hali ya Mazingira; kutoa mafunzo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa Maafisa Mazingira na Kamati za Mazingira za Wilaya na kuwezesha kuendelea na utekelezaji wa shughuli za Kikundi cha Kisekta cha Mazingira (*Environmental Working Group*).

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Programu hii inatekelezwa na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Kwa hapa Tanzania, shughuli zilizotekelizwa ni ukamilishwaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji sita vya mfano ambavyo ni Nyange (Kibondo); Titye (Kasulu); Ilagala (Kigoma); Karema (Mpanda); Korongwe (Nkasi) na Kisumba (Sumbawanga). Mipango hii iliyoidhinishwa katika ngazi ya kanda na Wizara husika, inalenga kuboresha matumizi bora ya ardhi na kuhifadhi mazingira katika vijiji vya mfano.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba mazingira ya bonde hilo yanahifadhiwa, mradi umetoa kiasi cha shilingi milioni 120 kwa vikundi sita (6) vya wajasiriamali (*SACCO\$*) ambavyo kila kimoja kimepata shilingi milioni 20 za kusaidia wananchi kufanya shughuli mbadala za kiuchumi. Aidha, Mradi umenunua mizinga ya kisasa ya ufugaji wa nyuki na

imegawiwa kwa vikundi kumi na sita (16) kwa vijiji sita vya mfano. Sambamba na hilo, mradi ulinunua vifaa vya kuchakata asali vyenye thamani ya shilingi milioni 20. Katika mwaka 2012, vikundi hivi vilizalisha tani 3.5 za asali na viliwezeshwa kuuza katika maonesho ya Nane Nane Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mradi umeendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo ya bonde la Ziwa Tanganyika. Miundombinu hiyo ni ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika kijiji cha Muzi, Wilaya ya Sumbawanga, ujenzi wa hosteli ya wasichana katika shule ya sekondari ya Kasanga Wilaya ya Sumbawanga, ujenzi wa wodi ya wazazi katika kijiji cha Samazi Wilaya ya Sumbawanga, ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 102 katika Wilaya za Kigoma, Mpanda, Nkasi na Sumbawanga. Kati ya hizo, kilomita 24.4 zimeshakamilika na kilomita 77.6 zinaendelea kujengwa. Barabara hizi zinajengwa katika kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mradi upo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa kisima chenye kina cha mita 60 kwa ajili ya wachakata mafuta ya mawese katika kijiji cha Ilagala. Katika kipindi hicho mradi pia umetenga hekta 6,276.6 za misitu ya asili kwa ajili ya hifadhi chini ya mpango wa utekelezaji wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji sita vya mfano. Mradi umenunua boti nne za kisasa za doria ambazo zitatumika katika vituo vya doria kudhibiti uvuvi haramu na matukio ya ujangili katika Ziwa Tanganyika. Injini kwa ajili ya kukarabati meli ya utafiti katika kituo cha Utafiti wa Uvuvi (*Tanzania Fisheries Research Institute TAFRI*) Kigoma imenunuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Programu ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika itaendelea kuratibiwa, na kuhakikisha kwamba miradi iliyoanza kutekelezwa inakamilishwa. Aidha, miradi ya ujenzi wa mialo minne (4) katika maeneo ya Kibirizi-Kigoma Mjini, Mwakizega-Kigoma Vijijini, Ikola-Mpanda, na Kirando-Nkasi utafanyika, pamoa na ujenzi wa soko la kisasa la samaki na kukarabati

mtambo wa kuzalisha barafu (*ice plant*).

Mheshimiwa Spika, Programu ya Ushirikishwaji wa Wananchi katika Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira. Programu ya Ushirikishwaji wa Wananchi katika Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira inayotekelizwa na Mashirika sita (6) yasiyokuwa ya Kiserikali chini ya ufadhilli wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (*USAID*) iliratibiwa. Mashirika haya ni *World Wide Fund for Nature (WWF)*, *Jane Goodall Institute (JGI)*, *University of Rhodes Islands and Tanzania Coastal Management Partnership (URI/TCM)*; *University of Florida-Integrated Water Sanitation and Hygiene (iWASH)*; *United States Department of Interior-International Technical Assistance Programme (DOI-ITAP)*; *African Wildlife Foundation (AWF)*.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *Jane Goodall* imesaidia Jamii kuhifadhi Mazingira katika maeneo ya Gombe na Masito katika Wilaya za Kigoma na Mpanda katika nyanja zifuatazo:-

(i) Kuhifadhi eneo la kilomita za mraba 12,047, ambapo asilimia 63 za eneo hilo yaani kilomita za mraba 7,588 zimefunkwa na misitu ya miombo na kilomita za mraba 2,200 ni maeneo yaliyohifadhiwa;

(ii) Mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji sita (6) imekamilishwa na kuwezesha vijiji vyenye matumizi bora ya ardhi kufikia 49;

(iii) Viongozi 272 walipata mafunzo kuhusu uongozi bora;

(iv) Kaya 5,950 zilihamasishwa kutengeneza majiko banifu 6,150 katika vijiji 27, hii ni katika kudhibiti uvunaji holela wa misitu;

(v) Maandalizi ya Sheria ndogo za usimamizi wa mazingira katika Wilaya za Mpanda na Kigoma yalifanyika;

(vi) Ilihamasisha wakulima 79 kuanzisha

mashamba-msitu (*agro-forestry*) na kusambaza mizinga 200 ya kisasa kwa wakulima katika vijiji vitano (5) vinavyozunguka msitu wa Masito-Ugalla;

(vii) Wadau 55 walipewa mafunzo kuhusu uangalizi wa Misitu na matumizi ya teknolojia ya kufuatilia matukio ya moto katika misitu kwa njia za kompyuta na simu; na

(viii) *SACCOs* katika vijiji saba (7) zenye wanachama 1,124 zimeanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia taasisi ya *African Wildlife Foundation (AWF)*, jamii zinazoishi Kanda ya Kaskazini katika maeneo ya mfumo-ikolojia wa Tarangire-Manyara-Kilimanjaro-Natron zimehamasishwa kuhifadhi mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali katika shughuli zao za kiuchumi. Aldha, maabara ya kisasa ya teknolojia ya mawasiliano yenye Kompyuta 39 pamoja na mfumo wa tovuti katika Shule ya Bweni ya Manyara Ranch yenye wanafunzi 1000 wa jamii ya wafugaji imejengwa. Pia, Chinjio la kisasa liliojengwa katika eneo la Makuyuni (Ranchi ya Manyara) kwa ajili ya kuongeza ubora wa bidhaa za mifugo na hivyo kuongeza kipato kwa jamii ya wafugaji limekamilika. Hatua inayofuata ni kutafuta mwekezaji wa kuendesha chinjio hilo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji huo ulikwenda sambamba na kuandaa mwongozo wa kuendesha Vikundi vya Hifadhi za Wanyamapor (Wildlife Management Areas - WMA); kufanya tathmini ya wanyamapor ya kila mwezi katika Vikundi vya Wanyamapor vya Burunge, Ikona, Unduimet na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor ya Idodi na Pawaga, pamoja na kutoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa programu, mipango na miradi ya usimamizi wa mazingira, na mafunzo kwa wawakilishi 45 wa Vikundi vya Hifadhi za Wanyamapor kuhusu mikataba ya kibiashara na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Tanzania Integrated Water, Sanitation and Hygiene (iWASH)* ambao unafadhiliwa chini ya programu hii uliwezesha watu 66,000 kupata maji safi; kuhamasisha watu 85,000 kuhusu usafi binafsi na usafi

wa mazingira; ulijenga majengo 28 ya vyoo, njia rahisi na nafuu za kuchimba visima, na pampu rahisi za kusukuma maji, zillioneshwa kwa jamii; na wanafunzi 17 shahada za uzamili za rasilimali za maji katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam walifadhiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa *Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP)* shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kutafsiri katika lugha ya Kiswahili utaratibu wa kupata vibali vya kufuga viumbe wa baharini katika Wilaya ya Bagamoyo;

(ii) Kuandaa ramani ya maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa viumbe wa baharini katika Wilaya ya Pangani;

(iii) Tathmini ya haraka ya hatari ya kuathirika na mabadiliko ya tabianchi ilifanyika katika Wilaya ya Pangani; na

(iv) Elimu ya hifadhi ya mazingira katika shule tisa za maeneo ya Pwani ilitolewa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2013/2014, shughuli za miradi hii zitaendelea kuratibowi kwa kuzingatia mipango na mikakati iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai na Itifaki ya Nagoya. Katika kipindi cha 2012/2013, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai pamoja na Itifaki zake kwa kufanya shughuli za maandalizi ya Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Bioanuai kulingana na shabaha ishirini za Mpango Mkakati Mpya (2011 hadi 2020), na kuandaa msimamo wa nchi na taarifa ya kuridhia Itifaki ya Nagoya inayohusu kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali Asili za Kijenetiki (*Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and The Fair and Equitable Sharing of*

*Benefits Arising From Their Utilization).* Mapendekezo ya kuridhia itifaki hii yanatarajiwa kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu ndani ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Ofisi kwa kushirikiana na wadau itakamilisha Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Bioanuai chini ya ufadhilli wa Mfuko wa Mazingira Duniani (*Global Environment Facility – GEF*). Vile vile, elimu kwa wadau kuhusu faida za utekelezaji wa Itifaki hii itaendelea kutolewa ili kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa Itifaki katika utekelezaji wa Mkataba wa hifadhi ya Bioanuai.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena. Katika utekelezaji wa Itifaki hii, shughuli zifuatazo zimefanyika: Kuendesha mafunzo ya kitaalam ya siku tano (5) kuhusu taratibu za Kufanya Tathmini na Usimamizi Angalifu wa viumbe au mazao yatokanayo na Teknolojia ya Uhandisi Jeni (*Risk Assessment and Risk Management*) kwa wataalam takriban ishirini (20) kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu ya Arusha, Shirika la Viwango Tanzania, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani - Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni, *Plant Health Service* ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, *Tanzania Official Seed Certifying Institute (TOSCI)* na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Ofisi ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa Sita wa nchi wanachama wa Itifaki ya Cartagena uliofanyika Jijini Hyderabad, India mwezi Oktoba 2012. Katika mkutano huo suala la nchi wanachama kuharakisha kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur inayohusu uwajibikaji kisheria na fidia kwa athari zinazoweza kutokea katika mazingira kutokana na matumizi yasiyo salama ya bioteknolojia ya kisasa (*Nagoya-Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety*), lilisisitizwa. Kwa upande wa Tanzania utaratibu wa kuridhia Itifaki umeanza.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kukuza weledi

kwa wananchi, Kanuni za Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa za mwaka 2009 [*The Environmental Management (Biosafety Regulations, 2009)*] zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha wananchi wengi kuelewa maudhui ya kanuni hizi na kuweza kuzitekeleza ipasavyo kulingana na nafasi yao katika utekelezaji wake. Ofisi imeendesha warsha za mafunzo kwa Wanasheria na Waheshimiwa Mahakimu kuhusu utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya teknolojia ya uhandisi-jeni hapa nchini. Mafunzo ya pili yalikuwa mahsus kwa watendaji wa mipakani wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa kuhusu suala la usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Ofisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwezi Desemba, 2012 iliendesha mdahalo wa wazi kuhusu matumizi ya bioteknolojia ya kisasa hapa nchini uliohudhuriwa na vikundi vya wakulima, watafiti, wanahabari/vyombo vya habari, wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, wanaharakati wa mazingira, watu binafsi na wazalishaji wa bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Ofisi inatarajia kukamilisha shughuli za mradi huu kwa kuzipatia vitendea kazi [*Genetic Modified Organisms (GMOs) laboratory equipment*] maabara za Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni. Vifaa hivyo vitasaidia shughuli za utambuzi na ung'amuzi wa mazao au viumbe ambavyo vimefanyiwa mabadiliko kwa kutumia njia ya uhandisi - jeni. Aidha, Ofisi itahuisha shughuli za mradi huu katika majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara za kisekta kwa ajili ya kuziendeleza baada ya muda wa mradi huu kumalizika.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto. Chini ya Mkataba huu, Programu na shughuli za Mpango wa Kuhimili

Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2007 (*National Adaptation Plan of Action- NAPA*), Miradi ya kupunguza gesijoto duniani na Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ucaa kutokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) zimeteklezwa.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya tabianchi imeendelea kuwa agenda ya kudumu kwa Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa Mwaka wa Fedha 2012/13; elimu juu ya mabadiliko ya tabianchi ilitolewa kwa umma wa Watanzania kama ifuatavyo:-

(i) Vipindi 20 vya luninga, 10 vya redio vilirushwa hewani kupitia TBC, ITV na Star TV. Vile vile, makala 20 zilichapishwa katika magazeti;

(ii) Baraza kwa ufadhili wa Serikali ya Japan kupitia *UNDP* limefanikiwa kutengeneza vipeperushi 5000, vikombe 1000, kalamu 1000, *wheel covers* 500, fulana 200, kofia 200, na kuzigawa kwa maafisa watendaji wa Serikali na taasisi zisizo za Serikali katika Wilaya 12 zikiwemo Pangani, Rufiji, Mkuranga, Handeni na Kiteto. Lengo kubwa lilikuwa kutoa Elimu juu ya Mabadiliko ya Tabianchi na namna ya kuhimili. Aidha, Baraza limechapisha kalenda 1000, *diaries* 500 za mwaka 2013 na nakala 1000 za jarida la Baraza lenye mada kuhusu utunzaji wa mazingira;

(iii) Ofisi kupitia vyombo vya habari ilitoa taarifa kwa umma kuhusu ushiriki wa Tanzania na yaliyojiri katika Mkutano wa 18 wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika tarehe 27 Novemba hadi 8 Desemba 2012, Doha Qatar. Katika hatua nyengine, taarifa kuhusu hali ya Mazingira nchini ilitolewa siku ya Mazingira Afrika tarehe 3 Machi 2013;

(iv) Mkakati wa Elimu kwa Umma wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi unaoweka mbinu za kuboresha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi umeandaliwa;

(v) Elimu kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi imetolewa kwa Wakuu wa Idara na Maafisa Waandamizi wa Wilaya za Karatu, Siha, Magu, Maswa, Meatu, Bariadi, Morogoro Vijijini, Mvomero, Pangani, Rufiji, Mkuranga, Longido, Monduli, Kiteto, Handeni, Sumbawanga Vijijini, Sumbawanga mjini na Nkasi;

(vi) Mafunzo kuhusu hatua muhimu za kupitia kabla mradi haujasajiliwa (*project cycle*) na aina za miradi inayoweza kutambulika na kusajiliwa kama miradi ya kupunguza gesi joto, yametolewa kwa wizara na idara za Serikali pamoja na sekta binafsi;

(vii) Maofisa wa Jeshi la Polisi, wafanyakazi wa Halmashauri za Kibaha, Morogoro, Tanga, Dodoma, Iringa na Moshi, wamejengewa uwezo wa kujua majukumu yao kisheria kama watekelezaji wa Sheria ya Mazingira;

(viii) Viongozi wa Asasi Zisizo za Kiserikali zinazojihusisha na masuala ya mabadiliko ya tabianchi, pamoja na viongozi wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira walipata nafasi kushiriki katika mikutano ya Kimataifa ya kila mwaka ya nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi;

(ix) Warsha tatu (3) za kuelimisha Kamati za Mazingira na Maafisa wa mazingira wa Wilaya kuhusu mabadiliko ya tabianchi zilifanyika katika Wilaya za Igunga (Tabora), Misenyi (Kagera) na Mbanga (Ruvuma);

(x) Mafunzo kuhusu biashara ya hewa ukaa yalitolewa kwa Maafisa wa *TRA*, Wizara ya Fedha na Wakaguzi kupitia Kikosi kazi cha mapitio ya Kodi chini ya Wizara ya Fedha, mwezi Februari 2013;

(xi) Kupitia Jumuiya ya Wakulima Tanzania- (*Tanzania Farmers Association*) elimu ilitolewa kwa viongozi wa jumuiya za wakulima na wadau wengine wa kilimo; na

(xii) Uliandaliwa mwongozo wa kufikisha taarifa za

kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima na wafugaji kuitia kitabu chenye mfumo wa vibonzo na lugha rahisi kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango ya maendeleo ya kisekta, yafuatayo yametekelizwa:-

(i) Kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika MKUKUTA II ili kuziwezesha sekta zinazotekeliza mkakati huu kutekeleza masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanayohusiana na sekta husika;

(ii) Kukamilisha Mkakati wa MKUHUMI uliozinduliwa tarehe 20 Machi, 2013, kuchapishwa na kusambazwa kwa wadau;

(iii) Kukamilisha mkakati wa kitaifa wa mabadiliko ya tabianchi ambao umeelekeza kila sekta kutekeleza mikakati na mipango ya mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Uandaaji wa Mwongozo wa Kuhuisha Masuala ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika sera na mipango ya sekta za Serikali za Mitaa. Mwongozo huu unatoa hatua rahisi za kuziwezesha Sekta na Serikali za Mitaa kuhuisha masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango yao;

(v) Kuandaa na kusambaza makala za kisera zinazohusu umuhimu wa uhuishaji wa masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi na mazingira katika Sera na mipango ya maendeleo kwa sekta za kilimo, wanyamapori na makazi. Aidha, makala za kisera kwa sekta za Misitu, Maji, Nishati na Afya zilikamilishwa na kusambazwa kwa wadau; na

(vi) Kuandaa makala zinazoonyesha ushahidi wa athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa sekta muhimu za kiuchumi zikiwemo nishati, misitu, maji, afya, kilimo, rasilimali za ardhi na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, mbali na elimu kwa mabadiliko ya Tabianchi, elimu ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira imeendelea kutolewa kwa madhumuni ya kukinga mabadiliko ya Tabianchi. Hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Elimu ya hifadhi ya mazingira ilitolewa kuitia maadhisho ya Siku ya Wakulima (Nanenane) Mkoani Dodoma, Siku ya Ozoni Duniani tarehe 16 Septemba, 2012, Arusha na Siku ya Mazingira Afrika tarehe 3 Machi, 2013, Jijini Dar es Salaam. Katika maadhisho haya elimu ya mazingira ilitolewa kwa kutumia hotuba za viongozi, vipeperushi 6000 na machapisho ya mabango ya matangazo 20 yalitolewa na vikundi 15 vya sanaa, ngonjera na kwaya za shule vilishiriki;

(ii) Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Jiji la Dar es Salaam iliandaliwa na kuzinduliwa Desemba, 2012. Nakala 3000 za taarifa hiyo zimesambazwa kwa wadau na wataalam wa mazingira nchini;

(iii) Wataalam 25 wa mazingira kutoka wizara za kisekta na majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, na Tanga walipatiwa mafunzo ya kuanda taarifa za hali ya mazingira; na

(iv) Baraza limeanzisha tovuti ya taifa ya mazingira ambayo ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Makamu wa Rais mwezi Septemba 2012 Jijini Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Ofisi imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya mfano chini ya Programu ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Africa Adaptation Programme - AAP*) unaofadhiliwa na Serikali ya Japan kuitia Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Utekelezaji wa miradi hii umeendelea katika Wilaya za Igunga Mkoani Tabora katika kijiji cha Nanga, Igumbi, Majengo na Itunduru; Mbinga Mkoani Ruvuma katika kijiji cha Ng'ombo; Misenyi Mkoani Kagera katika vijiji vya Byeju, Mbale, Kanyigo, Kashaha, Bukwali na Kitobo; na Wilaya ya Kaskazini A huko Unguja, kijiji cha Nungwi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa katika

maeneo yote yaliyokaguliwa miradi hiyo imekamilika na wananchi wa maeneo husika kufarijika kupata huduma ya maji kuititia miradi hiyo. Napenda kuwapongeza viongozi na wananchi wa maeneo yote ya mradi kwa kuonesha moyo wa kujitolea wakati wa ujenzi wa miundombinu na ninatoa rai kuwa waendelee kuitunza na kuiboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliandaliwa na kuzinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal tarehe 21 Machi 2013. Mkakati huoa unatoa mwongozo wa hatua zinazotakiwa kuchukuliwa na sekta husika katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na pia unaweka misingi kuziwezesha sekta husika kuandaa mipango ya kisekta ya utekelezaji wake. Sekta zilizoitikia mpaka sasa ni Kilimo, chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambayo inaandaa mpango wake kwa ufadhili wa Benki ya Dunia na Shirika la Msaada wa Maendeleo la Uingereza (*DFID*), na Maji ambapo Wizara ya Maji inayoandaa mpango wake kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Serikali ya Denmark (*DANIDA*) kuptitia Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira-*EMA-ISP*.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika chini ya Uenyekiti wa Tanzania kuanzia tarehe 21 hadi 23 Machi, 2013 katika Hoteli ya New Africa, Dar es Salaam, ukijumuisha washiriki kutoka zaidi ya nchi 50. Napenda kuwapongeza viongozi na wananchi wa Jiji la Dar es Salaam kwa ukarimu na ushirikiano wao wakati wote wa mkutano huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu kuanza utekelezaji wa Miradi miwili ya Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Pwani za Dar es Salaam, Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar. Miradi hii ni: Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wenye thamani ya takriban Dola za Marekani 3,356,000 kutoka Mfuko wa Mazingira wa Nchi Maskini Duniani

utatekelezwa katika maeneo ya Bagamoyo, Rufiji, Pangani na Zanzibar; na mradi mwengine wenyewe thamani ya takriban Dola za Marekani 5,000,000 unaofadhiliwa na Bodi ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi utatekelezwa maeneo ya Pwani katika Mkoa wa Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa taratibu zote za maandalizi zimekamilika na utekelezaji umeanza.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali itaendelea kutekeleza Mkataba wa mabadiliko ya tabianchi na Itifaki ya Kyoto ikiwa ni pamoja na miradi nilioitaja hapo juu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi. Katika mwaka 2012/13, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi unaotakelezwa na nchi kumi ambazo ni Tanzania, Kenya, Afrika ya Kusini, Somalia, Madagaska, Msumbiji, Comoros, Mauritius, Reunion-(Ufaransa) na Shelia. Lengo la Mkataba huu ni kuimarisha udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu pamoja na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kuwa Mwenyekiti wa Mkataba huu tangu 2013 hadi 2014. Katika kipindi hiki Tanzania imeratibu maandalizi na kushiriki katika marekebisho ya Mkataba ili kuimarisha hifadhi ya mazingira ya bahari na ukanda wa pwani. Aidha, Ofisi imeshiriki katika maandalizi ya Itifaki ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani unaotokana na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Vilevile, Ofisi ilishiriki katika maandalizi ya Mpango Kazi mpya wa Mkataba kwa kipindi cha 2013-2017. Mpango huu unaainisha mipango endelevu ya hifadhi na usimamizi wa ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha ujao 2013/2014, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi ikiwa ni pamoja na kutekeleza mpango wake wa

miaka mitano. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na UNEP itaandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Ukanda wa Pwani na Bahari.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mazingira Duniani – *GEF*. Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi ya *GEF* ikiwa ni pamoja na miradi midogo. Katika kipindi cha mwaka 2012/13 miradi mitano (5) mikubwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 21.22 ilipata ufadhili kutoka *GEF*. Miradi hiyo ni *Conservation and Management of Kihansi Ecosystem, Enhancing Forest Conservation in Tanzania and Highest Priorities for Forest Biodiversity Conservation, Strengthening Implementation of Cartagena Protocol on Biosafety, Promotion of Renewable Energy Applications for Rural Lighting and Agro-Industrial Sector in Tanzania na Institutional Empowerment for Advancing SLM and Upscaling the Equitable Payment for Watershed Services in Ruvu and Zigi*. Aidha, miradi midogo 33 yenye thamani ya Dola za Marekani takriban Milioni 1.3 iliyopata ufadhili ipo katika Wilaya za Kilosa, Morogoro vijijini; Moshi vijijini, Same; Korogwe; Mbinga; Bagamoyo; Ilala; na Zanzibar. Miradi iliyopata ufadhili inaonekana.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014, jitihada za kupata fedha kutoka *GEF* zitaongezwa na kuendelea kushauri Asasi za Kiraia namna ya kuandaa miradi midogo kwa ajili ya kupata fedha kutoka *GEF* kuitia *UNDP* zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya aina hiyo, sambamba na kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ambayo imepata fedha za ufadhili.

Mheshimiwa Spika, Mtando wa Taarifa za Mazingira Afrika. Kama nilivyoleza Bunge lako Tukufu mwaka wa jana. Katika mwaka huu wa fedha, Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Jiji la Dar es Salaam ilikamilishwa na kuzinduliwa tarehe 17 Desemba, 2012. Taarifa hii imesambazwa kwa wadau kwa lengo la kutoa mwongozo wa kutayarisha taarifa kama hii kwa Majiji na Miji mingine hapa nchini. Mwaka wa Fedha 2013/14, Ofisi itaendelea kufanya warsha za wadau na itaendelea kusambaza taarifa hii kwa wadau kwa lengo la

kutoa mwongozo wa kutayarisha taarifa za namna hiyo na kutoa elimu kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Kila ifikapo tarehe 5 Juni kila mwaka maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani hufanyika. Maadhimisho haya Kimataifa mwaka huu yatafanyika nchini Mongolia na kwa hapa Tanzania yatafanyika Mkoani Rukwa. Kaulimbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu Kimataifa ni: Fikiri Kabla ya Kula – Hifadhi Mazingira (*Think. Eat. Save*). Kitaifa kaulimbiu yetu itakuwa: Hifadhi Mazingira: Zingatia Uzalishaji na matumizi Endelevu ya Chakula. Ujumbe huu unahimiza kuwajibika katika uzalishaji na matumizi ya chakula endelevu kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. Katika kuadhimisha siku hii shughuli mbalimbali zinazohusiana na hifadhi ya mazingira zitafanyika nchi nzima kwa kipindi cha wiki moja, kuanzia tarehe 1 Juni hadi siku ya kilele tarehe 5 Juni. Shughuli hizo ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi ya Mazingira kupitia vyombo vyaa habari.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Kumi na Nne wa Mawaziri wa Mazingira wa Nchi za Afrika-AMCEN. Katika kipindi cha 2012/2013 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 14 wa Mawaziri wa Mazingira wa Afrika (*African Ministerial Conference on Environment – AMCEN*) ambao hufanyika kila baada ya miaka miwili kujadili masuala ya mazingira Barani Afrika na jinsi ya kukabiliana na changamoto zake. Mkutano huo ulifanyika Arusha katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (A/CC) kuanzia tarehe 10 hadi 14 Septemba 2012. Pamoja na Mambo mengine Mkutano huu ulijadili :-

(i) Matokeo ya Mkutano wa Rio +20 uliofanyika Mjini Rio de Janeiro, Brazil mwezi Juni, 2012;

(ii) Masuala ya uchumi wa Kijani na utekelezaji wake; na

(iii) Uimarishaji wa mfumo wa utekelezaji wa Masuala ya Mazingira barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, jumla ya washiriki 350 kutoka Serikali za nchi zote za Afrika na baadhi ya taasisi za kitaifa na kimataifa zinazojishughulisha na masuala ya mazingira walihudhuria. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupertia Waziri mwenye dhamana ya mazingira ilivishwa taji la Rais wa Mawaziri wa Mazingira wa Afrika kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi 2013/2014. Napenda kuwashukuru kwa namna ya pekee viongozi na wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano wao uliofanikisha mkutano huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika *AMCEN* na kuwa Rais kwa kipindi cha miaka miwili, utaiwezesha nchi kunufaika na fursa za kuwa na mipango ya kukabiliana na changamoto za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Montreal kuhusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni Angani. Katika kipindi hiki Ofisi iliratibu Maadhisho ya Siku za Kimataifa na Kitaifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni iliyofanyika tarehe 16 Septemba, 2012 sambamba na Mkutano wa *AMCEN*. Katika maadhisho hayo, maonesho ya shughuli zinazohusu kulinda tabaka la Ozoni; njia bora za kuhudumia majokofu na viyoyozi; jinsi ya kutumia vitambuzi vya gesi; na kubadilisha teknolojia zinazotumia kemikali haribifu kwa tabaka la Ozoni kwa kemikali mbadala yakiwa na nia ya kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulinda Tabaka la Ozoni. Aidha, Sekretarieti ya Mkataba (*Ozone Secretariat*) ikishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais waliandaa Mkutano Maalumu wa kuelezea mafanikio ya Mkataba wa Montreal na faida zake za kulinda Tabaka la Ozoni na kukabili/kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi. Mkutano huo ulikuwa wa kuadhimisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwa Mkataba wa Montreal.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Ozoni ikiwa ni pamoja na kazi zifuatazo: kutoa taarifa za utekelezaji wa Mkataba kwenye Sekretarieti ya Mkataba, kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa

Mkataba huu, kuendesha mafunzo kwa wakaguzi wa Mazingira kuhusu majukumu yao katika utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni) za mwaka 2007; kutekeleza Mpango wa kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya *Hydrochlorofluorocarbons - HCFCs* nchini, kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba; Kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba katika Sekretarieti ya Mkataba; kuendelea kutoa mafunzo ya Mafundi Mchundo wa majokofu na viyoyozi kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo na ubadilishaji wa teknolojia za mitambo ya kupozea inayotumia gesi haribifu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa muda mrefu (Mkataba wa Stockholm). Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Mpango wa Taifa wa Mkataba wa Stockhom uliendelea kutekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu uelewa wa athari za kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira, kufanya tathmini na kusimamia maeneo yaliyochafuliwa na kemikali hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Mkataba wa Stockholm kwa kutekeleza yafuatayo: kuimarisha uratibu na kukuza uelewa kuhusu athari za kemikali mpya; kukusanya takwimu za kemikali mpya zilizoongezwa kwenye Mkataba na kuititia upya Mpango wa kufanya tathmini ya uwezo wa kuainisha vipaumbele vya kusimamia kemikali husika.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mkataba kuhusu Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu baina ya Nchi na Nchi (Mkataba wa Basel) na Mkataba Unaouzia Uingizaji wa Taka za Sumu Barani Afrika (Mkataba wa Bamako). Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Basel na ule wa Bamako. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, kulifanywa ukusanyaji wa taarifa za usimamizi wa taka sumu na taka za kawaida katika bandari za Dar es Salaam na Tanga; Rasimu ya mpango wa usimamizi wa taka

hatarishi na za sumu zinazosimamiwa na mkataba huu pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa usafirishaji wa Baharini [*(International Maritime Organization - IMO)*] katika bandari hizo imeandaliwa; Warsha tatu (3) za mafunzo kuhusu usimamizi bora wa taka hatarishi na za sumu zilifanyika katika Jiji la Tanga na Dar es Salaam. Jumla ya wadau tisini (90) walishiriki mafunzo hayo. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/14, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mifuko ya plastiki. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi iliendelea kusimamia na kufuatilia Agizo la Serikali la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji, uuzaaji na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni thelathini iliyoanza kutumika tarehe 1 Oktoba, 2006. Katika kutekeleza hatua hiyo, Ofisi imewasiliana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata muafaka wa utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika kutekeleza azma hii ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, ofisi kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kufuatilia na kukamilisha hatua muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa agizo hilo la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. Zoezi hili litafanywa kwa hadhari kubwa ili kuepusha migogoro ya kisheria, na athari za kiuchumi na kijamii zitazotokana na katazo la matumizi ya bidhaa za plastiki nchini.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Sasa ni mwaka wa nane (8), tangu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ianze kutekelezwa. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ni mionganoni mwa wadau muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria hii. Katika mwaka wa fedha 2012/13 Baraza liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii kwa kuzingatia Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Mpango Mkakati wa Baraza (*NEMC Strategic Plan 2010-2014*), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo

wa Miaka Mitano, MKUKUTA II, maelekezo ya viongozi wakuu wa kitaifa, miongozo, nyaraka na mikakati mingine ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lilitkeleza Sheria ya Mazingira kwa kusimamisha ujenzi uliokiuka sheria katika maeneo ya mikondo ya mito na mikoko jijini Dar es Salaam. Kazi hii ilitekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Manispaa ya Kinondoni, na Jeshi la Polisi. Utekelezaji wa hatua hii ulipelekea nyumba 17 kubomolewa na kurudisha mkondo wa Mto Mbezi katika hali yake ya kawaida. Ubomoaji wa nyumba katika viwanja namba 2019 na 2020 zilizopo Mbezi Beach haujafanyika kutokana na wamiliki wa nyumba hizo kufungua kesi Mahakama Kuu, katika kitengo cha Ardhi. Aidha, mipaka ya kiwanja namba 2002 kilichopo Kawe Beach itarekebishwa na Idara ya Upimaji na Ramani ili kuondoa Mipaka ya Kiwanja hicho ndani ya Mkondo wa Mto.

Mheshimiwa Spika, mashimo ya mchanga yaliyotokana na uchimbaji holela katika eneo la Wazo Mivumoni, Dar es Salaam, yalifukiwa. Waliopatwa na hatia ya uchimbaji wa mashimo hayo walitozwa faini kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira. Ili kudhibiti uchimbaji huo, wananchi wa maeneo hayo wameunda ulinzi shirikishi dhidi ya uvamizi wa aina hiyo usitokee tena. Shughuli za uchimbaji mchanga katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mito, ni changamoto kubwa inayohitaji hatua za haraka, kwa Serikali za Mitaa kusimamia na kutoa miongozo ya maeneo ya kuchimbwa mchanga, na namna ya kufanya shughuli za uchimbaji. Hatua hizi zitafanya uchimbaji mchanga uwe endelevu na bila kusababisha athari kubwa kimazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2012/2013, Baraza lilianza utekelezaji wa Kanuni za Tozo (*Fees and Charges Regulations*) katika nchi nzima. Baraza liliendelea kutoa elimu na kuhamasisha umma kuhusu masuala ya ada na tozo za mazingira nchini. Pia, katika kipindi hicho, Jeshi la Polisi kwa

kushirikiana na Baraza limeanzisha Kikosi cha Polisi Mazingira (*Environmental Police Unit*) na kimeanza kazi. Jumla ya Askari Polisi 64 wameteuliwa nchi nzima kushughulikia masuala ya mazingira. Polisi hao wanashirikiana na Baraza katika kusimamia uzingatiaji wa sheria ya mazingira kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Baraza kwa kushirikiana na wadau litaendelea kufanya ukaguzi wa mazingira kubaini uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika vyanzo vya uchafuzi katika kanda nne (4) za katи (Dodoma, Singida na Manyara), Magharibi (Tabora, Shinyanga na Kigoma), Kusini (Lindi, Mtwara na Ruvuma) na Kanda ya Pwani yenye mikoa ya Pwani, Morogoro na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kasi ya utafiti wa kimazingira wa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa gesi asili itaongezwa nchini ili kuhakikisha kwamba shughuli hizi zinafanyika kwa kutumia Njia Bora (*Best Available Practices*) na Teknolojia za Kisasa (*Best Available Technologies*) zinazozingatia hifadhi ya mazingira katika maeneo ambayo shughuli hizi zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Jumla ya miradi ya maendeleo 554 ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa TAM mwaka huu wa fedha 2012/2013. Katika kipindi hicho, taarifa za TAM za miradi 239 zilifanyiwa mapitio (*reviews*) na wahusika kupewa maagizo ya maboresho kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya kutoa au kutotoa Hati za TAM (*EIA Certificates*). Aidha, miradi 207 ilipata Hati za TAM baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa Kanuni za TAM. Maombi 192 ya wataalam na makampuni 37 yalipokelewa kwa ajili ya kusajiliwa kufanya TAM na Ukaguzi wa Mazingira. Kati ya maombi haya, wataalam 166 na makampuni 27 ya kitaalam yamesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa Fedha 2013/2014, mapitio ya taarifa za TAM na usajili wa wataalam yataendelea kufanywa, Ukaguzi wa Mazingira na miradi ya maendeleo utafanyika ili kuhakikisha kuwa, miradi hiyo inatekeleza matakwa yaliyoainishwa kwenye Hati za TAM na Mipango ya Hifadhi ya Mazingira (*Environmental*

*Management Plans).* Baraza pia, litaendelea kuwajengea uwezo wadau kuhusu masuala ya TAM ili kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo zinakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza litaendelea kuboresha mifumo ya mawasiliano kati yake na wadau wa mazingira, ikiwa ni pamoja na Tovuti ya Baraza, Tovuti ya Mazingira ya Taifa na mfumo wa kuandaa taarifa za kijigrafia na mazingira (*Geographical Information System - G/S*); pamoja na kuhamasisha matumizi ya mitandao hii, Baraza litaendelea kukusanya taarifa na kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira kwa kuzingatia haki, wajibu na majukumu ya wadau katika hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Mazingira na Utafiti. Baraza liliendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira (*National Environmental Research Agenda - NERA*) na kuwajengea uwezo Maafisa Mazingira katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili waweze kuainisha maeneo muhimu yanayohitaji utafiti wa mazingira. Maafisa Mazingira 31 wa Wilaya, manispaa na mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara walishiriki. Aidha, maandalizi ya rasimu ya mpango wa utafiti wa Mazingira wa Baraza ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa NERA yanaendelea; na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2013.

Mheshimiwa Spika, Baraza liliendelea kukusanya taarifa za hali ya mifumo ikolojia ya milima ili kutengeneza mipango ya usimamizi wa mazingira katika maeneo yaliyoathirika zaidi (*hotspots*). Zoezi hilo limekamilika katika kanda zote saba (7) za kiikolojia nchini. Taarifa hizi zimeanza kufanyiwa uchambuzi na ripoti kamili inatarajiwa kupatikana katika Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kumalizika kwa mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bonde la Kihansi kuititia Benki ya Dunia mwezi Juni, 2011, kwa sasa, shughuli zilizobaki zinatekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), ambalo linaendelea kutumia rasilimali ya maji kuzalisha umeme.

Aidha, zoezi la kurejesha vyura wanaotunzwa nchini Marekani linaendelea hatua kwa hatua. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2013 vyura wapatao 4,430 walikuwa wamerejeshwa katika makazi yao ya asili katika Bonde la Kihansi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza litaendelea kukusanya taarifa kuhusu hifadhi ya mazingira; kuendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira (NERA) kwa kuainisha maeneo yanayohitaji kipaumbele cha utafiti, na kuwezesha utekelezaji wa mpango kamilifu wa usimamizi wa rasilimali za pwani ya bahari katika ngazi za Wilaya na Vijiji; kukusanya taarifa za hali ya mazingira katika maeneo ya pwani na milima pamoja na kuratibu utekelezaji wa mpango wa kuhifadhi mazingira ya bonde la Kihansi.

Mheshimiwa Spika, uratibu wa Miradi ya Kusimamila na Kuhifadhi Mazingira. Katika hotuba ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2012/2013, nilieleza kuwa Baraza linatekeleza programu ya uondoshaji wa viuatilifu chakavu nchini (*African Stockpile Programme – ASP*). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa zoezi la kukusanya shehena ya viuatilifu chakavu linaendelea vizuri na litakamilika mwezi Mei 31, 2013. Hadi sasa programu imefanikiwa kuondosha mlundikano wa viuatilifu chakavu ambapo takribani tani 630 katika vituo 135 pamoja na udongo tani 415 uliokuwa katika kituo kikuu cha Morogoro vimekusanywa na kusafirishwa kuititia bandari ya Dar es Salaam kwenda kuteketezwa nchini Uingereza na Poland.

Mheshimiwa Spika, Programu hii haikuweza kukamilika mwezi Desemba, 2012 kama ilivyokusudiwa awali kutokana na zoezi la kufungasha viuatilifu chakavu kuwa gumu na hivyo kuchukua muda mrefu, na kuathiri ratiba za meli zilizopangwa kusafirisha shehena hiyo. Baada ya kazi hii kukamilika nchi yetu itaingizwa kwenye orodha ya nchi salama duniani kutokana na kuondosha viuatilifu hivyo chakavu vyenye athari kwa mazingira na afya ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kuititia ufadhili wa Shirika la Mpango

wa Mazingira la Umoja wa Mataifa (*United Nation Environment Programme - UNEP*), Baraza lilifanya yafuatayo:

(i) Kupitia sheria za kisekta kubaini vipengele vinavyohusu mazingira na kuandaa mtaala wa mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira, pamoja na kuandaa mwongozo wa mafunzo kwa ngazi ya Serikali za Mitaa kuhusu uandaaji wa kanuni ndogo na mpango wa kudhibiti usafi wa mito ya Dar es Salaam;

(ii) Ilitayarishwa taarifa ya hali ya uzalishaji na matumizi endelevu ya rasilimali, na rasimu ya Mwongozo wa Uzalishaji na Matumizi Endelevu ya Rasilimali ambao utatumika katika mfumo wa elimu na wadau wengine; na

(iii) Kutambulika na kuwekwa alama za mipaka ya hifadhi ya Mto Mlalakua jijini Dar es Salaam. Kazi hii iliwezekana kupitia ufadhili wa Shirika la Misaada ya Kiufundi na Maendeleo la Ujeruman (GIZ).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza litaendelea kukamilisha mpango wa kuhifadhi mipaka ya mito nchini na kukamilisha uwekaji wa alama za mto Mlalakua jijini Dar es Salaam. Aidha, Baraza litaimarisha huduma ya G/S katika usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika uratibu wa masuala ya Muungano katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, pamoja na kutekeleza uhifadhi na usimamizi wa mazingira, Ofisi ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Pamoja na jitihada zinazofanywa kutoa elimu kwa umma wa Watanzania juu ya masuala ya Muungano, na yale ya utunzaji na hifadhi ya mazingira, bado kunaonekana kuwepo kwa uelewa usiotosha kwenye mambo hayo, na kwamba gharama za utoaji wa elimu kipitia vyombo vyaya habari zimepanda sana;

(ii) Ufinyu wa bajeti unaosababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa;

(iii) Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati; na

(iv) Mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa katika hifadhi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi ya Makamu wa Rais inajipanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea na juhudzi za kuelimisha Umma kuititia radio, televisheni, magazeti, machapisho mbalimbali, maadhimisho na maonyesho ya kitaifa kuhusu masuala ya Muungano, na Utunzaji na hifadhi ya Mazingira. Kasi itaongezwa katika kuratibu vikao vingi zaidi vya majadiliano ya pamoja, ya kutafuta ufumbuzi wa vikwazo vya utekelezaji wa mambo ya Muungano. Aidha, kwa upande wa Mazingira, jitihada itafanywa katika kuhamasisha Halmashuri za Wilaya, Miji na Vijiji (Serikali za Mitaa) kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo, na kuhimiza utekelezaji wake;

(ii) Katika kukabiliana na uhaba wa fedha, Ofisi inakusudia kuishirikisha kikamilifu Sekta Binafsi na vyuo vya elimu ya juu, pamoja na kuandaa miradi itakayovutia wahisani kuchangia katika utekelezaji wa Mipango kazi ya kila mwaka, kwa mambo ya Muungano, na kutunza na kuhifadhi mazingira;

(iii) Kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa mafunzo na vifaa kwa Waratibu wa Mazingira wa sekta mbalimbali na Maafisa Mazingira wa Serikali za Mitaa; na

(iv) Baraza kutekeleza mpango wake wa kupata mapato kutoka vyanzo vingine, ikiwemo tozo pamoja na kuibua miradi mipya katika kukabiliana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi imeendelea kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hiki watumishi ishirini na sita (26) walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi yanayohusiana na taaluma zao ili kuongeza ujuzi. Ofisi imeajiri watumishi wapya kumi na saba (17) wa kada tofauti kwa lengo la kuongeza nguvukazi ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, taarifa za watumishi wa Ofisi zimepitwa na kuboreshwa kwa kutumia mfumo wa taarifa za kiutumishi (*Human Capital Management Information System – HCMIS*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi imetua elimu kwa watumishi 227 kuhusu UKIMWI na kuwahimiza kujitokeza kupima afya zao kwa hiari. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kuwaelimisha wafanyakazi wote hususan, kuititia semina moja iliyoendeshwa kwa wafanyakazi 227 wa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu athari za rushwa mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ililendelea ushirikishwaji wa watumishi katika maamuzi na mipango ya Ofisi kuititia vikao viwili (2) vya Baraza la Wafanyakazi. Aidha, Ofisi imeimarisha mshikamano, ushirikiano na mahusiano kati ya watumishi wake na watumishi wa Ofisi nyingine za Serikali kwa kushiriki kikamilifu katika michezo ya SHIMIWI.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki Mazingira ya utendaji kazi yameboreshwa kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya Ofisi. Aidha, Ofisi imeendelea kusimamia ukamilishwaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi itaendelea kuratibu utoaji wa elimu ya UKIMWI kwa watumishi na kuendelea kuwashawishi kupima afya zao kwa hiari na kuwapatia huduma zinazostahili wanaojitokeza na kuthibitika

kuwa na VVU. Ofisi itaendelea kusimamia na kuendeleza maadili ya Utumishi wa Umma na kuwashirikisha watumishi katika maamuzi na mipango ya Ofisi kuititia mabaraza ya wafanyakazi. Ofisi pia itawawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo kulingana na taaluma na majukumu yao ya kazi na inatarajia kuajiri watumishi wapya 30 wa kada husika ili kuongeza nguvu-kazi. Kumbukumbu za watumishi zitaendelea kuboreshwa kutumia mfumo wa taarifa za kiutumishi (*Human Capital Management Information System - HCMS*) na tathmini ya upimaji utendaji kazi wa watumishi itafanya kupitia mfumo wa wazi wa upimaji utendaji kazi (*Open Performance Review and Appraisal System - OPRAS*).

Mheshimiwa Spika, ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuhakikisha kuwa vitendea kazi vinapatikana na ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais awamu ya pili Luthuli, Dar es Salaam unakamilika na kuwekewa samani. Aidha, Ofisi itawawezesha watumishi kupata stahili, haki zao na kushiriki katika maadhisho mbalimbali ya kitaifa pamoja na michezo ya SHIMIWI.

Mheshimiwa Spika, utawala na Utumishi katika Baraza (*NEMC*). Ili kuongeza ufanisi wa kazi na tija Baraza limejaza nafasi 30 za ajira mpya za Maafisa Mazingira na kuwezesha watumishi 17 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu [14 shahada za uzamili na watatu (3) shahada za uzamivu] na watumishi 13 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, kumefunguliwa ofisi mpya ya kanda huko Mtwara ili kusogea huduma kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na kufanya jumla ya ofisi za kanda zinazofanya kazi kuwa nne (4).

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza litaendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mazingira (2004); malengo yatakayotiliwa umuhimu ni kuendelea kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja; kujenga uelewa wa watumishi wa Baraza kuhusu Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma. Aidha, Baraza litaendelea kufanya ukaguzi wa ndani wa miradi na shughuli zake na kuandaa taarifa; kuimarisha mfumo wazi

wa upimaji utendaji kazi (*OPRAS*), kuboresha Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kusimamia utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makusanyo ya fedha, Baraza litabuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza kasi na kiwango cha ukusanyaji wa tozo nchini kwa kuzingatia Kanuni za Tozo (*Fees and Charges Regulations - 2008*); kutathmini utekelezaji wa Mpango Mkakati wake na Mpango Kazi wa 2013/2014; kuendelea kubuni miradi mipya itakayosaidia katika usimamizi wa mazingira; kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka mzima kwa mahitaji na kufanya ununuzi; na kusimamia matumizi ya fedha na mali, na kuandaa taarifa husika. Aidha, Baraza litaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu yake na kuongeza vitendea kazi; na kuendeleza mafunzo stahili kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi wa kazi na tija.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru waliotusaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mohammed Gharib Bilal kwa uongozi wake makini uliotuwezesha kufanikisha kazi zetu. Shukrani pia ziwaendee Mawaziri wenzangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga, (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano wao thabiti ambao umeniwezesha kuwasilisha hoja hii. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu, Bwana Sazi Bundara Salula; Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Ngosi Charlestino Mwihana; Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Mhandisi Bonaventure Thobias Baya; Wakuu wa Idara na Vitengo na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na *NEMC* kwa juhudii zao na utendaji katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana

na Washirika wa Maendeleo. Napenda kuzitaja baadhi ya Nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo Ofisi imefanya nayo kazi kwa karibu kama ifuatavyo: Serikali ya Norway, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Serikali ya Marekani, Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), Shirika la Mpango wa Mazingira la Umoja wa Mataifa (*UNEP*). Taasisi nyingine za kimataifa ambazo ni Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*), Mfuko wa Mazingira Duniani (*GEF*), Benki ya Dunia, *International Development Agency (IDA)*, Shirika la Maendeleo la Canada (*CIDA*), Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*), *Crop Life International (CLI)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Shirika la Misaada ya Kiufundi na Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*) na Asasi Zisizo za Kiserikali (*AZISE*).

Aidha, napenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo waendelee kushirikiana nasi katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini na juhudzi za kuboresha maisha ya kila Mtanzania bila kuathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2013/2014. Ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kama ifuatavyo:-

**(a) Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 5,699,642,000/= fedha za Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za Mishahara ya watumishi shilingi 852,486,000/= na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi 4,847,156,000/=.

**(b) Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu,

liidhinishe makadirio ya matumizi ya shilingi 55,682,428,000/= kwa Fungu hili. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi 42,710,545,000 fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 12,971,883,000/= fedha za Matumizi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 1,980,404,000/= mishahara ya watumishi, shilingi 32,627,535,000/= mgao wa kibajeti kwenda SMZ, shilingi 3,164,303,000/= ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na shilingi 4,938,303,000/= fedha za Matumizi Mengineyo kwa Idara na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha fedha za ndani shilingi 3,700,000,000/= na fedha za nje shilingi 9,271,883,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha utekelezaji wa kazi zetu kwa mwaka 2012/2013 na kuwasilisha maombi ya mwaka wa fedha 2013/2014 naomba sasa kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Wizara hii. Bahati mbaya sana, hii Wizara itatuchukulia muda kwa hotuba nyingi sana. Maana kuna Mwenyekiti wa Kamati, halafu kuna Mwenyekiti wa Mazingira, halafu kuna na Msemaji wa Kambi ya Upinzani (Muungano), halafu kuna Msemaji Kambi ya Upinzani (Mazingira). Kwa hiyo, kuna hotuba hapa na zinakula muda kwelikweli, lakini nitatoa maamuzi baada ya wote kusoma, nisiwapotzee muda wao. Msemaji kutoka kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa majukumu

ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31- Ofisi ya Makamu Wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata muda wa kutosha wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Samia S. Hassan (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano akishirikiana na Naibu waziri Mheshimiwa Charles M.Kitwanga. Katika maelezo yake, Pamoja na mambo mengine, Waziri alieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, yapo maagizo na maoni yaliyotolewa na Kamati. Napenda kuliari fu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, yapo maagizo na maoni yaliyotolewa na Kamati. Napenda kuliari fu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ionyeshe dhamira ya dhati ya kushughulikia suala la Muungano kama suala nyeti ili matatizo yaliyopo yapate ufumbuzi. Serikali katika kushughulikia matatizo ya Muungano iliunda Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ambapo hoja 13 za masuala ya Muungano zimejadiliwa na hoja tisa zimepatiwa ufumbuzi.

(ii) Utolewe ufanuzi kwa nini Serikali ya Muungano wa Tazania hajatoa maoni kuhusu mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Ikiwa ni pamoja na kufunguliwa akaunti ya Fedha ya pamoja kwa mujibu wa

Ibara 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali katika kuzitafutia ufumbuzi hoja za fedha, Mawaziri wa Fedha wa pande mbili za Muungano walikutana tarehe 10 Januari, 2013 kujadili masuala ya fedha likiwemo suala la mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekwishakamilisha kupitia mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha na kupata maoni ya Serikali. Ripoti imeshajadiliwa katika ngazi ya Wizara na sasa iko tayari kujadiliwa katika Baraza la Mawaziri.

(iii) Elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano izidi kutolewa ili kuwaelimisha wananchi masuala ya Muungano. Ofisi imeendelea kuelimisha umma kupitia *TBC, ITV, na Star TV*. Pamoja na hili illiandaa taarifa ya mafanikio ya awamu ya nne ya Serikali kwa lengo la kuelimisha umma na iko katika matayarisho ya kuchapisha majarida na kuandaa makala za magazeti kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi.

(iv) Utolewe ufanuzi kwa nini Wafanyabiashara waishio Zanzibar wanatozwa kodi mara mbili ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kumaliza tatizo hili Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ wamekubaliana kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ifanye tathmini (*Import-Export valuation Data base*) ili kubaini faida na upungufu wake na kuwasilisha ripoti kwa Mawaziri wa Fedha wa pande zote mbili baada ya Mkutano wa Bunge la Bajeti wa Mwaka 2013/2014. Aidha, wamekubalina kuwa utaratibu huu unaotumika kwa sasa utumike kwa hiki kipindi cha mpito.

(v) Mgawanyo wa mapato yanayotokana na misaada kutoka nchi za nje bado ni kero hasa kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Serikali itoe ufanuzi kuhusu jambo hili. Kumekuwa na tatizo la ushirikiano linalojitokeza katika hatua za awali na utayarishaji wa Bajeti ya Taifa na utafutaji wa misaada ya kibajeti kwa washirika wa maendeleo. Suala hili limefanyiwa kazi na kukubaliana kwamba Makamishna wa Sera za Fedha, pamoja na Makamishna wa Fedha za nje wa Wizara zinazoshughulikia masuala ya Fedha SMT na SMZ waandae mapendekezo ya utaratibu utakaoshirikisha pande

zote mbili kwenye mchakato mzima wa upatikanaji wa Misaada na Mikopo ya kibajeti. Mapendekezo ya mfumo huu yamepangwa kujadiliwa na Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ katika mwaka huu wa Fedha 2012/2013.

(vi) Pamoja na kuongeza juhudini katika kutoa elimu ya kuhusu Muungano, ni vyema mipango ikafanyika ili kuangalia namna ambayo somo kuhusu Muungano linaweza kufundishwa kuanzia Shule za Msingi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisimmo imepitia mitaala na mihtasari ya masomo yanayofundishwa kuanzia Elimu ya Msingi na kubaini kuwa maudhui juu ya masuala ya Muungano yanayojitokeza katika masomo ya Uraia, Historia na Jiografia. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wanapitia sera, sheria, mitaala na mihtasari ya Elimu kuhuisha maeneo muhimu yakiwemo masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano imekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti. Pamoja na utekelezaji wa majukumu yake Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano imekuwa ikikabiliwa na ufinyu wa bajeti kiasi cha ofisi kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa. Changamoto hii ni ya muda mrefu hivyo Kamati inashauri bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano iongezwe.

Mheshimiwa Spika, uelewa mdogo kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Hali iliyopo hivi sasa inaonyesha kuwa kizazi kilichopo hakina uelewa wa kutosha kuhusu masuala yanayohusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Kufuatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kama yalivyowasilishwa kwa kila Fungu, yafuatayo ni maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais Fungu 26. Ofisi

binafsi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, iliidhinishiwa kiasi cha Sh. 4,653,309,000. Kiasi hiki kinajumuisha Sh.654,153,000 fedha za mishahara na Sh. 3,999,156,000 fedha za matumizi mengineyo. Kamati inaipongeza Ofisi hii kwa kumwezesha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza jukumu lake la msingi la kumsaidia na kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Kamati inashauri kwamba Ili kumwezesha Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake ipasavyo akiwa Zanzibar ni vyema kukawa na fedha zinazotengwa kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais kwa upande wa Zanzibar, kuliko kutegemea fedha zinazotengwa kwa ajili ya Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais upande wa Bara. Lengo ni kurahisisha ufanisi wa utendaji kazi kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa upande wa Muungano imekuwa ikihusika na kuratibu mambo ya Muungano na ushirikiano kwa mambo yasiyo ya Muungano. Katika mwaka wa Fedha 2012/2013, Ofisi hii iliidhinishiwa kiasi cha sh. 52,965,482,000. Kiasi hiki mgawanyo wake ni Sh.1,941,818,000, Bajeti ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Sh.32,625,766,000 Mgao wa kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Sh.3,716,883,000 Fedha za ruzuku kwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Sh.4,410,073,000 Bajeti ya matumizi mengineyo na Sh. 10,270,942,000 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa uratibu mzuri wanaoufanya katika masuala ya Muungano, hususan katika kushughulikia hoja tisa kati ya 13 za Muungano zilizowasilishwa katika vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo, Kamati inaona kwamba bado iko haja ya kuongeza nguvu zaidi katika kushughulikia masuala ya Muungano kwa lengo la

kuboresha Muungano wa Nchi yetu. Hivyo basi Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Ni vyema Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ikazishughulikia kero nne za muungano zilizobaki kwa umakini na uharaka ili kufikia mwaka 2014 kero hizo ziwe zimepatiwa ufumbuzi.

(ii) Aidha, Kamati inashauri kwamba ni vyema ikapata mrejesho wa vikao vinavolenga kutatua hoja/keru za Muungano wanavyokaa viongozi na wataalam wa pande zote mbili za muungano ili kuweza kujiridhisha na mambo yanayojiri katika vikao hivyo, lengo ni kuipa fursa Kamati kutoa ushauri pale inapobidi.

(iii) Elimu itolewe zaidi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha Muungano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa historia ya Muungano, maendeleo yake, changamoto na jinsi kero za Muungano zinavyotatuliwa kwa wakati. Aidha, Kamati inashauri kuwa ili kufikisha elimu kwa wananchi wa ngazi zote, vyombo vyta habari kama redio vitumike sanjari na runinga (TV). Vilevile majarida na machapisho mbalimbali ni vyema yakatumika kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala ya Muungano. Hata hivyo, kamati inapendekeza kwamba ni vema upangwe mkakati maalumu wa kwenda vijiji zaidi ili kuwafikia wananchi wa ngazi zote.

(iv) Utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayotokana na fedha zinazotoka kwa wafadhili ni vyema ukaangaliwa upya kwa Serikali zote mbili yaani SMZ na SMT. Kamati inashauri kwamba, Serikali itolee uamuzi mapendekezo ya Tume ya pamoja ya fedha yaliyowasilishwa Serikalini tangu 2006 na kuwasilishwa tena 2010 kuhusu utaratibu wa mgao wa fedha kwa Serikali zote mbili.

(v) Utaratibu wa mgawanyo wa raslimali kuangaliwa upya kati ya Serikali zote mbili, hili ni katika suala la mafuta na gesi. Kamati inashauri kwamba Serikali zote mbili

zikutane kwa lengo la kufanya utafiti ili kuangalia maeneo ambayo yanakinzana ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

(vi) Wabunge wanaotoka Zanzibar wapewe nafasi ya kushiriki katika kujadili fedha za miradi zinazotoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuititia *TASAF* kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwani Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya Wabunge wa maeneo hayo hawashirikishwi katika miradi ya maendeleo inayotekelizwa kuititia mfuko wa *TASAF* katika maeneo/Majimbo yao. (*Makofii*)

(vii) Wananchi waelimishwe na kushirikishwa kuhusu mambo ya muungano na yasiyo ya muungano.

(viii) Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Tunguu Zanzibar ni vyema ukamilishwe mapema iwezekanavyo na maeneo ambayo mkandarasi hajayakamilisha au amejenga chini ya kiwango kinachotakiwa yafanyiwe uchunguzi wa kina na kurekebishwa kabla ya makabidhiano.

(ix) Ofisi ya makamu wa Rais itengeneze mfumo mzuri wa kuajiri wataalamu wazoefu, wenye weledi wa hali ya juu wa kumshauri Makamu wa Rais kuhusu masuala ya Muungano ili kuiwezesha ofisi kushughulikia kero za muungano kwa haraka zaidi kwa lengo la kudumisha muungano wa nchi yetu.

(x) Malalamiko ya wafanyabiashara waishio Zanzibar kutozwa kodi mara mbili yafanyiwe kazi. Kumekuwepo na tatizo kubwa la wafanyabiashara waishio Zanzibar kutozwa kodi ya mapato mara mbili wanapotoa bidhaa zilizokwishalipiwa ushuru Zanzibar pindi wanapofika Tanzania Bara wanalazimika kulipia tena. Tatizo hili limesharipotiwa mara kadhaa hata katika taarifa ya Kamati ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 bila kupatiwa ufumbuzi. Kamati inashauri tena kwa msisitizo kwamba suala hili lishughulikiwe kikamilifu mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014, katika Mwaka

19 APRIL, 2013

wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ili kutekeleza majukumu yake inaomba fedha kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26 - Makamu wa Rais: jumla ya kiasi cha Sh.5,699,642,000 kinaombwa, kiasi hiki mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo: Sh. 4,847,156,000 ni kwa matumizi mengineyo na Sh.852,486,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Jumla ya kiasi cha Sh. 55,682,428,000 kinaombwa, Kiasi hiki mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo: Sh 40,730,141,000 ni kwa matumizi mengineyo, na Sh. 1,980,404,000 ni mishahara na Sh. 12,971,883,000 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Naibu Waziri Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala ya sheria, utawala na sekta nyingine mbalimbali ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mwenyekiti, Mheshimiwa William M. Ngeleja - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mheshimiwa

19 APRILI, 2013

Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Jason S. Rweikiza, Mheshimiwa Nyambari C.M. Nyangwine na Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Theonest Ruhilabake, ndugu Haika Mtui na Matamus Fungo, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante nitamwita msemaji wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu eneo la Mazingira, Mheshimiwa Ester Bulaya. Mwanamazingira huyo. (*Makofii*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ambayo imesomwa hatuna.

**SPIKA:** Haya, ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 116(11), Toleo la Mwaka 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira (Fungu 31), kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niweke wazi kwamba, katika Fungu 31, Kamati haikupitisha kifungu kidogo cha 5001 kwa ajili ya Idara ya Mazingira kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, hii haizuii Bunge lako Tukufu kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, na makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge (2013) Kifungu namba 6(8) na 7 (1) kuwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na kuchambua Bajeti ya Ofisi hii; kusimamia na kuishauri kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 04/04/2013 Kamati ilikutana katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pamoja na wataalam wake, na kupokea Taarifa ya Ofisi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti hiyo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipata fursa ya kujadili:-

(i) Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi kwa Mwaka wa

Fedha wa 2012/2013 na malengo yanayoombewa fedha kwa Mwaka wa 2013/2014;

(ii) Muhtasari wa kazi zilizotekelawa na Idara ya Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014;

(iii) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2012/2013; na

(iv) Mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa majadiliano ya Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa 2012/2013, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo mbalimbali kwa Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati japokuwa kuna maeneo ambayo Serikali hajayatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi hii hasa kwa Idara ya Mazingira na *NEMC* kwa miaka miwili mfululizo (2011/2012; 2012/2013), bado Serikali imeedendelea kutenga fedha kidogo ambapo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 jumla ya shilingi 5,184,372,000/= ikiwa ni pungufu kwa asilimia 3.5 ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Shilingi 5,372,218,000/=. Katika hali halisi fedha hizi hazitoshelezi mahitaji ya msingi katika kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na suala hili, kwani inaonekana wazi kwamba, Serikali haijalipa kipaumbele suala la Mazingira wakati inajulikana wazi kwamba, hakuna maendeleo endelevu yoyote yanaweza kupatikana nchini hivi sasa bila kuwa na uhifadhi bora wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, aidha, mipango mingi inayopangwa na Serikali haiwezi kufanikiwa iwapo mazingira yatakuwa yameharibika. Mipango mizuri kama ya Kilimo Kwanza, umeme unaotokana na maji na kadhalika haiwezi kufanikiwa kama mazingira hayako salama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu huu, kubwa zaidi ni pale ambapo Serikali inatenga pesa kidogo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni ya pili kwa umuhimu baada ya Ofisi ya Rais. Fedha kidogo zinazotengwa haziwiani na kazi za Idara hii, umuhimu wa sekta yenyewe, lakini pia na uzito wa Ofisi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bajeti hiyo finyu, Serikali imeonesha uwezo mdogo katika kusimamia Kanuni ya matumizi ya mifuko ya plastiki na kuhakikisha inatekelezwa kama ilivyo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni dhahiri kwamba mazingira yameendelea kuchafuliwa kwa kuzagaa ovyo kwa mifuko hii katika miji yetu ikiwa ni pamoja na maeneo ya fukwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutimiza ahadi yake ya kupiga marufuku kabisa (*total ban*) matumizi ya mifuko laini ya plastiki ili kulinda mazingira na afya za wananchi kutokana na madhara yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kama nchi ndogo ya Rwanda imefanikiwa kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko ya plastiki, kwa nini Tanzania tunashindwa? Kamati haipendi kuamini kuwa, jambo hili linashindikana kwa kuwa wenye mamlaka ya kupiga marufuku wana maslahi katika viwanda na biashara ya mifuko ya plastiki. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia na kuyafanya kazi maoni yanayotolewa na Kamati hii ili kazi ya kutunza na kuhifadhi mazingira ifanikiwe kwa faida ya vizazi nya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2012/2013. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ilikadiria kukusanya jumla ya Sh. 11,002,000/= kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo uuzaaji wa nyaraka za zabuni. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2013, Ofisi ilikuwa imekusanya jumla ya Sh. 5,930,000/=, sawa na asilimia 54 ya makadirio yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31 iliihdinishiwa Sh. 43,938,540,000/=, ambapo kati ya hizo mishahara ilikuwa sh. 1,941,818,000/= na sh. 41,996,722,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiasi hicho kinajumuisha sh. 32,625,766,000/= kwa ajili ya mgao wa kibajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na fedha za ruzuku za *NEMC* sh. 3,716,883,000/. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2013, Ofisi ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya sh. 40,152,699,021/= kwa ajili matumizi ya kawaida sawa na asilimia 97.5 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya sh. 41,996,722,000/=.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, ziliidhinishwa jumla ya Sh. 10,270,942,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo; kati ya fedha hizo sh. 4,500,000,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na Sh. 5,770,492,000/= zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2013 jumla ya Sh. 1,672,000,000/= tu ambazo ni fedha za ndani zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, hali hii kwa mara nyingine, inadhihirisha kilio cha Kamati kuhusu Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwani mpaka mwezi Machi 2013, ikiwa ni miezi tisa toka mwaka wa

fedha 2012/2013 uanze, hakuna fedha yoyote kutoka kwa wadau wa maendeleo imetolewa. Utiegemezi huu kwa wahisani unasababisha miradi mingi ya maendeleo kutotekelzeaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali, kuacha kutegemea sana misaada toka nje na badala yake ianze kujenga uwezo wake wa ndani, kwa kuwa imedhihirika kwamba, misaada ya wafadhili haina uhakika wa kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio na changamoto cilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kukabiliwa na ufinyu wa bajeti, bado imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa elimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa umma kuitia warsha, maadhimisho, maonesho na njia mbalimbali;

(ii) Kuendelea kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira chini ya ufadhili wa *DANIDA* na *CANADA CIDA*. Kwa kipindi hiki Ofisi imeweza kuandaa mwongozo wa kuendesha Mfuko wa Mazingira, mwongozo wa kusimamia fedha za Mfuko wa Mazingira na kuandaa utaratibu wa kuendesha Baraza la Usuluhishi la Mazingira;

(iii) Kuratibu na kutekeleza Mikataba minne (4) ya Kimataifa ya Mazingira ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ambapo mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI uliandaliwa na kuzinduliwa tarehe 20 Machi, 2013 na Mkakati wa Kitaifa wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi uliandaliwa na kuzinduliwa tarehe 21 Machi, 2013;

(iv) Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ambapo Baraza (*NEMC*) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi limeanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira na

kimeshaanza kufanya kazi kikiwa na Askari Polisi 64 walioteuliwa nchi nzima;

(v) Kuendelea kuratibu, kusimamia na kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa kufanya kaguzi katika viwanda na shughuli za uzalishaji zaidi ya 70 na kubomoa ujenzi uliokiuka Sheria katika maeneo ya mikondo ya mito na mikoko Jijini Dar es Salaam; na

(vi) Kuendelea kusajili wataalam wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*TAM*) na ukaguzi wa Mazingira na kukagua miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa inatekeleza matakwa yalioanishwa kwenye hati za *TAM* ambapo wataalam 166 na makampuni 27 ya kitaalam yamesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto; kama ilivyoolezwa hapo awali, pamoja na mafanikio yaliyopatikana ufinyu wa bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa inayosababisha kutotekelizwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, changamoto nyingine ambazo zimeendelea kuikabili Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni pamoja na:-

(a) Uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira;

(b) Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira kwa wakati; na

(c) Mwitikio mdogo wa Serikali za Mitaa katika hifadhi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuihimiza Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuweka, kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia fedha kidogo wanayopata katika bajeti, lakini pia kwa fedha inayotokana na miradi mbalimbali ambayo huiandika;

(ii) kuboresha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa mafunzo na vifaa kwa waratibu wa mazingira wa sekta mbalimbali na maafisa mazingira wa Serikali za Mitaa; na

(iii) Kuendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa kuhuisha masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2013/2014, Kamati ilijulishwa kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yamezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mkakati wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II) na maoni na mapendekezo ya Bunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa zimegawanywa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Ofisi na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). Hivyo basi, fedha kiasi cha sh. 55,682,428,000/= katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, zinaombwa kwa ajili ya Fungu 31. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida sh. 42,710,545,000/= na fedha za matumizi ya maendeleo sh. 12,971,883,000/=.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha matumizi ya kawaida kinajumuisha fedha za mgao wa asilimia 4.5 ya bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sh. 32,627,535,000/=, hivyo Idara ya Mazingira imetengewa kiasi cha sh. 5,184,372,000/= ambazo zinajumuisha sh. 3,164,303,000/= za fedha za ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*).

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa fedha za

maendeleo, jumla ya sh. 12,971,883,000/= zimetengwa ambazo zinajumuisha fedha za ndani sh. 3,700,000,000/= na fedha za nje sh. 9,271,883,000/= .

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii na kupitia Kifungu kwa Kifungu. Japokuwa Kamati haikuridhishwa na kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira; naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili maombi hayo yenye jumla ya sh. 55,682,428,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuujadili kwa kina Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira; Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, Kamati imesikitishwa sana na bajeti ndogo ambayo imeendelea kutengwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa miaka miwili mfululizo (2012/2013- 2013/2014), licha ya Kamati kushauri mara zote kuhusu Idara ya Mazingira kuongezewa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira hasa katika sekta za kilimo, misitu, mifugo, nishati, maji na kadhalika, inasikitisha kuona kwamba Serikali yetu bado haijatoa kipaumbele katika suala la mazingira. Ni ukweli usiofichika kwamba, ili kuwa na maendeleo endelevu lazima uhifadhi wa mazingira upewe kipaumbele. Hii itawezekana endapo tu Serikali itatambua umuhimu huu na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa mwaka ujao wa fedha 2013/2014, Idara ya Mazingira imetengewa jumla ya sh. 5,184,372,000/= zinazojumuisha fedha za ruzuku kwa Baraza (*NEMC*) sh. 3,164,303,000. Bajeti hii ni ndogo kwa Idara na Baraza lake kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa kwa kuzingatia kwamba,

hawana vitendea kazi vya kutosha kama vile magari ambayo ni muhimu kwa ajili ya kaguzi hasa katika maeneo ya viwanda na migodi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, bajeti hii ni ndogo sana kulinganisha na gharama kubwa zinazotumika katika kulinda maeneo ya fukwe na kingo za mito hususan pale ambapo inahusisha kuboma majengo yaliyojengwa katika maeneo hayo kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inapendekeza kwamba, kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Fungu 31, hujumuisha mgao wa kibajeti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa chini ya Fungu 31 ni pesa nyingi kulinganisha na zinazobaki kwa ajili ya Idara ya Mazingira, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ione umuhimu wa kuipatia Idara ya Mazingira na Baraza lake Fungu la pekee ili kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira kijulikane wazi.

Mheshimiwa Spika, moja ya maoni ya Kamati hii kwa Ofisi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ilikuwa ni Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kamati ilitoa ushauri huu kwa kuzingatia kwamba mara nyingi fedha za nje huwa hazitolewi kwa wakati na hivyo kukwamisha miradi mingi. Ni jambo la kusikitisha kuwa, pamoja na ushauri wa Kamati, kwa mwaka ujao wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga fedha za ndani sh. 3,700,000,000/= tu ukilinganisha na fedha za nje sh. 9,272,883,000/= ambazo ni sawa na asilimia 71 ya fedha zote.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha za ndani zilizotengwa, sh. 3,200,000,000/= zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli na Tunguu na ujenzi wa jengo la Baraza (NEMC) zimetengwa sh. 500,000,000/= tu ndio zimetengwa kwa ajili ya miradi sita inayojumuisha miradi ya

mabadiliko ya tabia nchi. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za ndani ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa ya Idara ya Mazingira ni uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya mazingira hasa Sheria ya Mazingira namba 20 ya Mwaka 2004. Sheria hii inasema wazi kwamba, itakuwa ni makosa kufanya shughuli zifuatazo bila kupata kibali cha Waziri mwenye dhamana ya mazingira:-

- (i) Kujenga jengo au umbile lolote kwenye fukwe za bahari, ziwa, ukingo wa mto au bwawa;
- (ii) Kufukua/kutoboa fukwe na kingo za mito;
- (iii) Kuchepusha au kuzuia mito; na
- (iv) Kufanya shughuli za kudumu za kibinadamu, ujenzi wa nyumba ndani ya mita 60 kutoka baharini au kwenye kingo za mito ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha ulinzi wa mazingira na utunzaji wa bahari au kingo za mito.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kuhusu kuwepo kwa ujenzi usiofuata Sheria katika maeneo ya fukwe na kingo za mito. Hali hii inasababishwa na wananchi aidha, kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ya Mazingira ama kukaidi Sheria hiyo. Ujenzi huu hasa katika kingo za mito unaathiri mazingira ya asili ya mito ikiwa ni pamoa na kupindisha mikondo ya mito. Hali hii ni ya hatari kwani imekuwa ikisababisha mafuriko kwa pande ambazo mito imemelekezwa na hivyo kuharibu mazingira;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba, nyumba zote zilizojengwa kinyume cha Sheria katika kingo za mito na fukwe za bahari zibomolewe na kurudisha mito iliyoathirika katika hali yake ya asili ili kuondoa athari kubwa za kimazingira zinazoweza kutokea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, aidha, pale ambapo imebainika kwamba waliojenga katika maeneo tuliyoyataja kwa kupewa vibali kama vile hati na kadhalika kinyume cha Sheria, waliohusika na vitendo hivi nya kifisadi nya kutoa vibali au hati wakamatwe na kufikishwa katika vyombo nya Sheria. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni dhahiri kwamba, wananchi wengi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faida zake hususan wakati huu ambapo kuna changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, athari mbalimbali zimeendelea kutokea kutokana na uharibifu wa mazingira. Vitendo nya kuharibu vyanzo nya maji, ukataji ovyo wa misitu na utupaji ovyo wa taka, ni vitendo vinavyofanyika kwa kiasi kikubwa kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira miongoni mwa wananchi;

Mheshimiwa Spika, pamoja na mahitaji makubwa ya elimu ya Mazingira kwa umma, Idara ya Mazingira kutokana na kutokuwa na pesa ya kutosha, imetenga jumla ya sh. 6,000,000/= tu kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi nya kutolea elimu na kuendesha programu ya elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, kiasi hiki hakiwezi kutosheleza kabisa mahitaji ya kuiwezesha Idara ya Mazingira kuendesha programu ya elimu kwa umma itakayoleta mafanikio. Kamati inashauri Serikali kutambua umuhimu wa elimu hii na kuongeza bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mnamo Oktoba 2006, Serikali ilitoa agizo la kupiga marufuku uingizaji, utengenezaji, uuzaaji na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya mikroni thelathini (30). Aidha, Serikali iliahidi kuchukua hatua ya kupiga marufuku kabisa matumizi ya mifuko laini ya plastiki ili kulinda mazingira. Hata hivyo, ni dhahiri kabisa agizo hilo

halijatekelezeka kwani mazingira yetu yameendelea kuchafuliwa na mifuko hiyo hususan maeneo ya mijini na kwenye fukwe za bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza agizo lake na kuisimamia kanuni ya Kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki mapema iwezekanavyo ili kuondoa tatizo hili sugu la uchafuzi wa mazingira ambalo linaitia aibu nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sanjari na hilo, ni pendekeso la Kamati kwamba, Serikali isimamie usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji taka ovyo. Vile vile elimu ya utunzaji/usafi wa mazingira iwekwe kwenye mitaala katika shule za misingi ili kuwajengea wanafunzi utamaduni wa kuwa na mazingira safi na yaliyohifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali za Mitaa zimeendelea kuwa na mwitikio mdogo katika hifadhi na utunzaji wa mazingira, Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kufuatilia utungaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo za Hifadhi ya misitu, Hifadhi ya Vyanzo vya Maji, Tathmini ya Mazingira na Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza Halmashauri zilizoanza kutunga na kutekeleza Sheria Ndogo hizo na kutoa msisitizo kwa Halmashauri nyingine kuiga mfano huo. Halmashauri zilizotunga Sheria Ndogo zinazohusu mazingira ni Manispaa ya Moshi, Jiji la Mwanza, Halmashauri za Wilaya ya Njombe, Babati, Singida Vijijini, Iramba, Bahi, Mbeya Vijijini na Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mgongano wa kimamlaka katika baadhi ya sekta na Idara ya Mazingira. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo ambayo huhifadhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kama vile maeneo ya hifadhi za misitu, fukwe na vyanzo vya maji. Hata hivyo, bado mamlaka nyingine za Halmashauri na Wizara kwa kutumia Sheria zao zinaendelea kutoa vibali kwa

ajili ya shughuli mbalimbali kama vile ujenzi kandokando ya mito na fukwe za bahari.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kwamba kwa kuwa Mamlaka hizi zote zipo chini ya Serikali moja, zishirikiane kwa pamoja kuondoa migongano ya matumizi ya ardhi inayoendelea kukua kwa kasi nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi limeendelea kuleta athari nydingi ikiwa ni pamoja na ukame na mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini na duniani kote. Kamati inashauri Serikali kuendelea kukuza weledi kuhusu tatizo hili na jinsi ya kukabiliana nalo kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha upandaji miti na kuzuia kilimo kisichofuata utaratibu katika miinuko kinachosababisha maporomoko ya ardhi na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ianzishwe ili itoe mwongozo kwa Serikali, Taasisi na Mashirika mbalimbali kuhusu uhuishaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira ambacho tayari kimeanza kazi. Kamati inaamini kabisa kwamba ushirikiano wa kitengo hiki na Baraza (*NEMC*), utafanikisha shughuli za ukaguzi hasa wa viwanda na hatimaye kukamata wahalifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Naibu Waziri, Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga; Ndugu Sazi M. Salula, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wataalam wote wa Ofisi hii na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kwa ushirikiano, ushauri na utaalalm wao ambaa umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa busara, ushirikiano na kujituma kwao bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti inayoombwa na hivyo kufanikisha Taarifa hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mwenyekiti; Mheshimiwa Abdulkarim E. Hassan Shah, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mjumbe; Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mjumbe; Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mjumbe; Mheshimiwa Muhamad Amour Chomboh, Mjumbe; Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mjumbe na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mjumbe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mjumbe; Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mjumbe; Mheshimiwa John John Mnyika, Mjumbe; Mheshimiwa Salim Hassan Turky, Mjumbe; Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mjumbe; Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mjumbe; Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyr, Mjumbe; Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mjumbe na Mheshimiwa Waride Bakar Jabu, Mjumbe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Theonest Ruhilabake, Makatibu wa Kamati Ndugu Grace Bidya na Evelyn Shibandiko wakisaidiwa na Ndugu Lukindo Adrian Choholo kwa kuratibu shughuli za Kamati kwa ufasaha na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa

naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi wa Makamu wa Rais, Mazingira kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa kuzingatia kwamba, hoja kubwa ya Kamati ni ufinyu wa bajeti usiotosheleza utekelezaji wa malengo katika Idara ya Mazingira kwa miaka mitatu mfululizo (2011/2012- 2013/2014) na kwa kuwa jambo hili sasa linashughulikiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MHE. TUNDU A. LISSU - MSEM AJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO):** Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013, naomba kutoa maoni kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani Ofisi ya Makamu Rais, Muungano, Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu juu ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Machi mwaka huu Mheshimiwa Waziri aliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Taarifa hii imekiru kuwa “uelewa mdogo wa umma kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano.”

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Taarifa hii, hali inaonesha kuwa kizazi kilichopo hivi sasa kinaonekana hakina uelewa wa kutosha wa masuala ya Muungano.” Taarifa inaongeza kwamba “changamoto nyingine ni masuala ya Muungano kuonekana ya kisiasa zaidi na hivyo watu wengi kutokuwa na mwamko wa kupenda kuyaelewa zaidi.”

Mheshimiwa Spika, kauli hizi zinathibitisha kwamba, baada ya miaka arobaini na tisa ya uhai wake, Muungano huu umebakni mali ya viongozi wa Chama Tawala na kundi la watu wachache wanaonufaika nao.

Mheshimiwa Spika, kama baada ya karibu ya nusu karne tangu kuzaliwa kwake bado kuna uelewa mdogo wa umma juu yake; kama baada ya karibu miongo mitano ya uhai wake, Serikali inakiri kwamba, kizazi cha sasa hakina uelewa wa kutosha wa Muungano na kama baada ya Awamu Nne za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Awamu Saba za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, bado Watanzania wengi wa pande zote mbili za Muungano wanauona ni wa kisiasa zaidi na hawana mwamko wa kupenda kuuelewa, huu ni uthibitisho mwengine kwamba, Muungano huu haujawahi kuwa wa wananchi, bali ni ndoa ya watawala na wachache wengine wanaofaidika na ndoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Ofisi hii mwaka jana, tuliliambia Bunge lako Tukufu kwamba, licha ya kauli za mara kwa mara za watawala kuhusu kuelimisha umma juu ya Muungano, historia halisi ya Muungano wetu haifahamiki kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, katika Maoni hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kwamba, Serikali iweke wazi nyaraka mbalimbali zinazohusu historia ya Muungano wetu na mapito yake ili Watanzania waelewe masuala yote yaliyotokea yanayouhusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kuwa, kutolewa hadharani kwa nyaraka hizo kutasaidia kuweka sawa picha inayoelekea kuwa ya upande mmoja inayotokana na nyaraka za kijasusi na za kidiplomasia za Mataifa ya Magharibi kama vile Marekani na Uingereza zinazoonesha jinsi ambavyo Serikali za Mataifa hayo zilihusika katika kuzaliwa kwa Muungano.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yetu juu ya kuanikwa kwa nyaraka mbalimbali zinazohusu Muungano na historia yake halisi yalipuuzwa na Serikali hii sikivu. Badala yake, Serikali hii imeendeleza propaganda zake juu ya jinsi Muungano huu ulivyo mfano wa kuigwa katika Bara la Afrika, licha ya kutokuwepo nchi yoyote ya Kiafrika iliyouiga mfano

huu! Matokeo yake ni kwamba hata baada ya karibu miaka hamsini Watanzania wengi bado hawafahamu ilikuwaje kukawa na Muungano wa aina hii, yapata siku mia moja tu baada ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, aidha, wengi hawafahamu kilichowasibu baadhi ya viongozi waandamizi katika Baraza la Mapinduzi la kwanza la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ambao walipotea katika uso wa dunia katika mazingira ya kutatanisha.

Mheshimiwa Spika, pia wala watu wengi hawafahamu ilikuwaje Mambo ya Muungano yaliyokubaliwa katika Hati za Muungano yaliongezeka kutoka 11 yaliyokubaliwa na Marais Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume hadi kufikia 22 yaliyoko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya sasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Watanzania wengi hajajui chanzo cha kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisiasa kulikomng'oa Rais wa Zanzibar Aboud Jumbe madarakani mwaka 1984 au madai ya Kundila 55 kuhusu kuanzishwa kwa Serikali ya Tanganyika mwaka 1993, au chanzo cha upinzani mkubwa wa Wazanzibari kwa Muungano ambao kwa muda mrefu umevikwa vazi la kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya aina hii, haiwezi kuwa ajabu kwa wananchi wa Tanzania kuwa na uelewa mdogo wa Muungano au kuuona Muungano kama wa kisiasa zaidi, yaani wa kiuongo uongo na usiokuwa na maslahi yoyote kwa wananchi wa kawaida wa nchi ya Zanzibar na wa iliyokuwa nchi ya Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, katika maoni yetu ya mwaka jana tulielezea kwa kirefu historia ya ukiukwaji wa Hati za Muungano za mwaka 1964 ambao ulianza tangu miaka ya mwanzo ya Muungano na ambao umeendelea kwa kipindi chote cha maisha yake. Ukiukwaji huu sasa umekuwa ni sehemu ya utamaduni wa kisiasa wa nchi yetu. Mfano mzuri

wa utamaduni huu wa ukiukwaji wa Katiba katika masuala ya Muungano ni utaratibu wa kutatua migogoro inayohusu tafsiri ya masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Muungano, chombo chenye mamlaka ya kuamua juu ya jambo lolote linalohusu tafsiri ya Katiba linalobishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni Mahakama Maalum ya Katiba iliyoundwa chini ya Ibara ya 125 ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wajumbe wa Mahakama Maalum haijatajwa lakini ibara ya 127(1) inatamka kwamba, wajumbe wake nusu ya jumla ya wajumbe wote watakaoteuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na nusu nydingine watateuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ibara ya 128(2) ya Katiba, akidi ya kikao cha Mahakama hiyo ni wajumbe; na kila suala linalohitaji uamuzi litaamuliwa kwa kufuata kauli ya theluthi mbili ya wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar. (Ibara ya 128(3) na kwa mujibu wa ibara ya 126(3), uamuzi wa Mahakama Maalum ya Katiba utakuwa ndio wa mwisho (na) hakutakuwa na haki ya kukata rufaa popote.

Mheshimiwa Spika, licha ya Katiba ya Muungano kuweka utaratibu huu wa kutatua migogoro ya tafsiri ya Katiba kuhusu masuala ya Muungano, Mahakama Maalum ya Katiba haijawahi kuitishwa kusikiliza migogoro mingi kuhusu tafsiri ya Katiba kuhusu masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, jaribio pekee la kukiitisha chombo hiki cha kikatiba kutatua migogoro hiyo lilizimwa mwaka 1984 wakati aliyekuwa Rais wa Zanzibar Aboud Jumbe, Waziri Kiongozi Ramadhani Haji Faki na Mwanasheria Mkuu Bashir Kwaw Swanzy walipong'olewa madarakani kwa kile kilichoitwa kuchafuka kwa hali ya hewa ya kisasa, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Profesa Issa Shivji

katika kitabu chake *Pan Africanism or Pragmatism? Lessons of Tanganyika and Zanzibar Union*, Rais Jumbe akisaidiwa na Mwanasheria Mkuu wake Kwaw Swanzy aliandaa 'Kesi Iliyonayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Tanganyika.'

Mheshimiwa Spika, Waraka huo wenye kurasa zaidi ya 100 ulihoji, pamoja na mambo mengine, mfumo wa Muungano wa Serikali mbili kwa madai kwamba Hati za Muungano zilikuwa zimeweka utaratibu wa mfumo wa Muungano wa shirikisho lenye muundo wa Serikali Tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovypote vile, utaratibu wa kuitisha Mahakama Maalum ya Katiba ulikuwa ndio utaratibu pekee wa kutatta mgogoro wa tafsiri ya Katiba na Rais Jumbe alikuwa sahihi kikatiba kudai Mahakama hiyo iitishwe. Badala ya kufuata utaratibu wa kikatiba, Jumbe aligeuziwa kibao na kulazimishwa kujiuzulu kwa madai ya kutaka kushtaki Mahakamani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano!

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo, mjadala juu ya Hati ya Kuzaliwa ya Muungano kama Jumbe alivyoziita Hati za Muungano wakati akijitetea mbele ya Kikao Maalum cha Halmashauri Kuu ya CCM, imekuwa, kwa maneno ya Jumbe, ni dhambi.

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo, migogoro katika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu tafsiri ya masuala ya Muungano imeacha kutaja Hati za Muungano, badala yake migogoro hiyo imefichwa ndani ya lugha ya kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kinachoitwa kero za Muungano kiuhalisia ni migogoro juu ya tafsiri ya masuala mbalimbali ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hii inadhihirishwa na Hoja za Muungano zilizojadiliwa katika vikao mbalimbali vilivyofanywa kati ya Serikali zote mbili kati ya Oktoba, 2012 na Machi, 2013:-

- (i) Hisa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki;
- (ii) Usajili wa vyombo vyaa moto;
- (iii) Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili;
- (iv) Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha;
- (v) Mgawanyo wa mapato;
- (vi) Ushiriki wa Zanzibar katika taasisi za nje;
- (vii) Utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi asili;
- (viii) Ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano;
- (ix) Uvubi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu;
- (x) Ongezeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO*; na
- (xi) Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hoja hizi ni ongezeko la gharama za umeme kati ya *TANESCO* na *ZECO* pekee ambayo haina uhusiano wowote na masuala ya Muungano. Kwa upande mwingine, hisa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha na mgawanyo wa mapato yana uhusiano wa moja kwa moja na mikopo na biashara za nchi za nje, kodi ya mapato na ushuru wa forodha, mambo yanayohusiana na sarafu na fedha yaliyoko katika orodha ya Mambo ya Muungano ambayo ni Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, aidha, ushiriki wa Zanzibar katika taasisi za nje na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni masuala yenye uhusiano wa moja kwa moja na mambo ya nchi za nje kwenye orodha ya Mambo ya Muungano. Vile vile, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili yanahusiana na maliasili ya mafuta na gesi asilia katika orodha ya Mambo ya Muungano; wakati uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu yanahusiana moja kwa moja na Katiba ya Tanzania inayotangaza sehemu ya bahari inayopakana na Tanzania kuwa ni sehemu ya eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hoja ya ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano iko katika utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenye orodha ya Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kero hizi za Muungano zimekuwepo kwa miaka mingi na zimelalamikiwa mara kwa mara na Wazanzibari. Kwa mujibu wa Katiba ya Muungano, kero hizi zinazohusu tafsiri ya masuala ya Muungano zilizotakiwa kuamuliwa na Mahakama Maalum ya Katiba. Hata hivyo, kama anavyosema Profesa Shivji katika *Pan Africanism or Pragmatism*, pengine Mahakama hiyo haikupaswa kufanya kazi, ndio maana hajjawahi kuundwa!

Mheshimiwa Spika, badala ya kutatua matatizo ya Muungano kwa njia zilizowekwa Kikatiba, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimeanzisha taratibu za kirasimu zilizoko nje kabisa ya mfumo wa Kikatiba wa Muungano. Ndio maana Taarifa ya Utekelezaji Bajeti Mwaka wa Fedha 2012/2013: Kipindi cha tarehe 1 Julai hadi 31 Desemba, 2012, iliyowasilishwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, tarehe 23 Januari mwaka huu inaelezea uratibu wa vikao vitatu vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, iliyoundwa mwaka 2006 ili

kushughulikia changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, vile vile, vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mawaziri wa Serikali hizo vilivyokaa kati ya tarehe 20 Desemba, 2012 na 13 Januari 2013 vilikutana kujadili Hoja za Muungano. Haihitaji misisitizo kusema kwamba, vikao hivyo vyote, pamoja na manufaa yake kama yapo, havitambuliwi Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli mbele ya Bunge hili Tukufu ni kwa nini Serikali hii ya CCM imejenga utamaduni wa kutumia vyombo visivyotambuliwa na Katiba ya nchi yetu kushughulikia matatizo au migogoro ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieze Bunge kulikuwa na sababu gani ya kuanzisha utaratibu wa Mahakama Maalum ya Katiba kwa ajili ya kutatua migogoro ya Muungano kama utaratibu huo haukupaswa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ikiri mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba, taratibu zake za kirasimu zimeshindwa kutatua Kero za Muungano kwa sababu kero hizo haziwezi kutatuliwa bila kufanyika kwa mabadiliko makubwa ya mfumo na muundo wa Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieze Bunge hili Tukufu kama ni kweli au sio kweli kwamba Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, 1984, sasa yameongeza Kero za Muungano kwa kuhoji kama Tanzania bado ni nchi moja au la; kama kila ya nchi hizi ina mipaka na eneo lake la Bahari Kuu au la; kama tuna wakuu wa nchi wawili au la; kama tuna Amiri Jeshi wawili au la na kama masuala ya ulinzi na usalama bado ni masuala ya Muungano au la. Kwa kifupi, Serikali iwaeleze Watanzania

ukweli wote kama bado kuna haja na sababu ya kuendelea na Muungano huu licha ya kero zake kuongezeka badala ya kupungua!

Mheshimiwa Spika, hata mchakato wa Katiba Mpya unaonesha jinsi ambavyo Muungano wetu umekuwa wa mashaka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezungumzia mara nydingi na kwa kirefu ushawishi na uwakilishi mkubwa wa Zanzibar na Wazanzibari katika hatua mbalimbali za mchakato wa Katiba Mpya hata kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano ya Tanzania Bara na hakuna sababu ya kuyarudia hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mwongozo Kuhusu Muundo, Utaratibu wa kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka za Serikali za Mitaa), ulioandaliliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na ambao umelalamikiwa sana na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, unathhibitisha kwamba kuna *double standards* katika utaratibu wa kuunda Mabaraza hayo kwa Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wakati ambapo kuna hatua mbili katika kuwapata wajumbe wa Mabaraza hayo kwa Tanzania Bara, kwa upande wa Zanzibar kuna hatua moja tu. Kwa hiyo, wakati wajumbe wa Tanzania Bara wamechaguliwa na wananchi katika vijiji na mitaa na baadae kuchujwa (na kuchakachuliwa) kwenye Kamati za Maendeleo za Kata (*WDC*) ambazo kwa sehemu kubwa chini ya CCM, wajumbe wa Zanzibar wamechaguliwa moja kwa moja katika ngazi ya shehia na hakuna mchujo au uchakachuaji wowote uliofanywa na chombo kingine baada ya kura ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, wakati kwa upande wa Tanzania Bara mikutano ya uchaguzi katika ngazi ya vijiji na mitaa imeendeshwa na Wenyevitii wa Vijiji na Mitaa na Makatibu wake kuwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa ambao wengi wao ni wana-CCM, kwa upande wa Zanzibar

mikutano ya uchaguzi ya Sheria imechagua Wenyevit na Makatibu wake kutoka miongan mwa wananchi waliohuduria mukutano.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni wa kibaguzi kwa maana halisi ya neno kubagua kama linavyotafsiriwa katika ibara ya 13(5) ya Katiba ya Muungano. Hii ni kwa sababu utaratibu huu umetimiza haja au haki ya kuchagua wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya mbalimbali kwa kuzingatia uteifa wao, mahali wanapotokea kwa namna ambayo watu wa Tanzania Bara wamefanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa Zanzibar wametendewa tofauti au wamepewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nydingine tena Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Tume ya Mabadiliko ya Katiba kufuta matokeo ya uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya amba unaonekana wazi kuwa wa kibaguzi na kuweka utaratibu mpya utakaohakikisha kwamba kuna haki sawa kwa watu wote wanaotaka kuchaguliwa kuwa wajumbe wa Mabaraza hayo bila kujali ni Wazanzibari au Watanganyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kukataa kufanya hivyo sio tu ni kuharibu mchakato wa Katiba Mpya kwa nchi yetu bali pia ni kuthibitisha kwamba Muungano wetu ni kiini macho tu kinachotumika kulinda maslahi ya watu wachache walioshikilia nafasi za utawala katika nchi yetu. Huko sio kuuimarisha Muungano, bali ni kuubomoa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka unaokwisha, kati ya shilingi bilioni 40.152 za matumizi ya kawaida zilizopokelewa na kutumiwa katika Fungu 31, shilingi bilioni 1.244 zilitolewa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Fedha hizi ni wastani wa takriban shilingi milioni 25 kwa kila moja ya Majimbo 50 ya Uchaguzi yaliyoko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, inaelekea, hata hivyo, kwamba kumekuwa na madai ya kuwahusisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama wajumbe wa kudumu wa Kamati za Maendeleo za Majimbo husika ili kuweza kujua matumizi ya fedha za mipango ya maendeleo ya Jimbo." Hii ni kwa mujibu wa Kauli ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Kuhusu Utekelezaji wa Masuala ya Muungano, iliyotolewa hapa Dodoma mwezi Januari mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Kauli ya Waziri, kumekuwa na hoja kwamba Wawakilishi wa Viti Maalum Baraza la Wawakilishi Zanzibar nao waalikwe katika kupanga matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo. Kwa maeleo ya Waziri, katika kurekebisha hali ya utata ilijojiteza kwenye Majimbo ya Zanzibar, SMZ imeamua kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kufanya hoja hii kupatiwa ufumbuzi. Kwa heshima zote kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ufumbuzi huu unazua maswali yanayohusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu, kwa ufumbuzi huu, sasa kila Jimbo la Uchaguzi la Zanzibar litakuwa linapatiwa mafungu mawili ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wakati Majimbo ya Tanzania Bara yakipata fungu moja. Majimbo madogo na yenye idadi ndogo ya watu, sasa yatapata fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vile vile kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wakati Majimbo makubwa na yenye idadi kubwa ya watu ya Tanzania Bara yatapata fedha za Mfuko kutoka chanzo kimoja tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu kama ni halali kwa fedha za umma kuendelea kuiruzuku (*subsidize*) Mifuko ya Maendeleo ya Majimbo ya Zanzibar wakati sasa itakuwa inapata fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kero za Muungano sio mali binafsi ya Wazanzibari na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pekee. Hata Watanganyika wanakerwa na ubaguzi unaoendeshwa dhidi yao Zanzibar. Mfano mzuri ni katika suala la umiliki wa ardhi ambapo Watanganyika wanaoishi na kufanya kazi Zanzibar hawaruhuswi kumiliki ardhi Zanzibar, wakati Wazanzibari wanaoishi na kufanya kazi Tanzania Bara wana haki kamili ya kumiliki ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, kitakwimu idadi ya watu wanaonyimwa haki hiyo ni ndogo sana, jambo hilli linaacha ladha mbaya katika mahusiano ya Watanganyika na Wazanzibari kwa sababu inaonekana kwa wengi kuwa, Wazanzibari wanapendeleta wakati Watanganyika wanabaguliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili kuhusu suala hilli.

Mheshimiwa Spika, kero ya pili inahusu uwakilishi katika vyombo vya Jamhuri ya Muungano. Wakati, kama tulivyoona, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na wawakilishi wa Zanzibar hata katika Bunge hili Tukufu mara nyingi wamelalamikia kutokuwakilishwa Wazanzibari katika taasisi za Muungano, Watanganyika wanalalamikia uwakilishi usio na uwiano wa Wabunge wa Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, wakati katika Bunge la sasa, Mbunge mmoja wa Tanzania Bara kwa wastani anawakilisha watu laki moja na elfu hamsini na saba, Mbunge mmoja wa kutoka Zanzibar kwa wastani anawakilisha watu elfu kumi na sita.

Mheshimiwa Spika, Uwakilishi usio na uwiano katika Bunge kati ya Wabunge wa Zanzibar na wa Tanganyika ulianza tangu miaka ya mwanzo ya Muungano. Kwa mfano, katika Bunge la kwanza baada ya Muungano kati ya Wabunge 204, kulikuwa na Wazanzibari 55 au takriban asilimia

27 ya Wabunge wote. Katika Bunge la sasa karibu nusu karne baadaye, kuna Wazanzibari 83 kati ya Wabunge 357 au asilimia 23 ya Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimewahi kusema ndani ya Bunge hili, idadi ya Wabunge wanaotoka Zanzibar iliongezwa kama njia ya kisiasa ya kuzima upinzani kutoka kwa ukiukwaji mkubwa wa Hati za Muungano ambaa ulianza mara tu baada ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ndio maana katika Bunge la mwaka 1965 ambapo idadi ya Wazanzibari iliongezeka kwa kiasi kikubwa, ni kipindi hicho hicho ambacho Zanzibar ilipoteza mamlaka yake katika masuala ya fedha na sarafu na hisa zake katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ambazo inazilalamikia hadi leo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa jambo hili ni Kauli ya Waziri ya Januari mwaka huu inayoonesha jinsi ambavyo hoja ya Wazanzibari kutaka kujua kiwango cha hisa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Bodi hiyo liliyoyjibwa: "Katika Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika tarehe 14 Januari 2013 imeelezwa kwamba, Mawaziri wa Fedha wa SMT na SMZ wamepatiwa nyaraka maalum zenye taarifa za siri na wamekubaliana kujadili suala hili mwezi Februari, 2013 baada ya kuzipitia nyaraka hizo."

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine, sio tu kwamba, Wazanzibari hawajui ni kiasi gani cha fedha zao zilichukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kufuatia kuvunjwa kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, bali pia hawana uhakika watarudishiwa lini!

Mheshimiwa Spika, kipindi cha idadi ya Wazanzibari kuongezeka katika Bunge hili kilikuwa kipindi hicho hicho ambapo Zanzibar ilipoteza mamlaka yake katika masuala ya maliasili ya mafuta na gesi asilia ambayo miaka zaidi ya arobaini baadaye imekuwa ndio donda ndugu kubwa katika siasa za Muungano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama ambavyo wanafunzi wa historia ya Muungano wameonesha, wakati mambo haya yanatokea hakukuwa na mjadala wala upinzani wowote wa maana kutoka kwa Wazanzibari waliokuwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kilichokwuwa muhimu kwa Wabunge hao kilikuwa kile ambacho Mwanasheria Mkuu wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar Wolfgang Dourado aliwahi kukisema akimnukuu Sheikh Abeid Karume: "Msiwe na wasi wasi, sisi tuna haki ya kuwakilishwa katika Bunge lao lakini wao hawana haki ya kuwa kwenye Baraza letu la Mapinduzi"!

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumesema mara nyingi katika Bunge hili, uwakilishi huu usio na uwiano sasa umeingizwa katika mchakato wa Katiba Mpya ambapo Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, inaeleza wazi kwamba idadi ya Wazanzibari katika Bunge Maalum haitapungua theluthi moja. Hawa watajadili na kuamua masuala ya Katiba yanayohusu Mambo ya Muungano ambayo wana haki nayo, lakini watajadili na kuamua masuala ya katiba yanayohusu mambo yasiyokuwa ya Muungano ya Tanganyika ambayo hawana haki nayo!

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya maoni haya.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru familia yangu; mke wangu mpenzi Alicia Bosensera na mapacha wetu Agostino Lissu na Edward Bulali kwa kuendelea kuvumilia upweke unaotokana na *Daddy* kuwa mbali muda mwingu kwa sababu ya majukumu mazito ya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, pia, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Singida Mashariki kwa imani na nguvu wanayonipa kila siku kwa kuendeleza msimamo wetu thabiti wa kukataa kunyanyaswa, kunyonywa na kupuuzwa na *Ndaa ya Njou!*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Nawaomba waendelee kutuunga mkono na kututia nguvu katika siku ngumu na za majaribu makubwa zinazokua!

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu leo ni siku ya wenzetu kuswali, ningesema tuongeze dakika baada ya saa saba lakini haiwezekani.

Waheshimiwa Wabunge, tumepata tatizo katika Hoja hii; kuna sehemu ya Muungano na kuna sehemu ya Mazingira. Kwa hiyo, wasemaji kila eneo wamekuwa wawili wawili. Kwa hiyo, sasa hivi msemaji mmoja wa Kambi ya Upinzani itabidi awasilishe hotuba yake baadaye.

Tulipofanya hesabu na tukisema tuache hivi hivi basi watawasilisha, sana sana mtoa hoja atakuja kujibu hoja kwa saa lake moja kwa haya yaliyozungumzwa na Kamati pamoja na Taarifa ya Upinzani. Lakini hakuna Mbunge atakayepata nafasi ya kuzungumza. Kwa hiyo, tulifikiri kwamba, kama tukikubaliana badala ya kumaliza saa mbili kasarobo, tumalize saa mbili na nusu tunaweza tukafanya yote vizuri. Sasa naomba Waziri wa Nchi pale atoe hoja, tuanze kikao saa kumi na moja na tumalize saa mbili na nusu.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni za Bunge, chini ya Kanuni ya 153 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013.

KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) Bunge linakutana hadi saa saba mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(4) Bunge huendelea kukaa mpaka saa moja na dakika arobaini na tano usiku ambapo Spika husitisha shughuli za kuahirisha hadi tarehe ya siku nyingine inayofuata.

NA KWA KUWA katika mjadala unaoendelea sasa wa Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano muda wa michango ya Wabunge ni mfupi sana.

NA KWA KUWA hoja hiyo ya Ofisi ya Makamu wa Rais ili ihitimishwe vizuri, inabidi kuongeza idadi ya wachangiaji kwa maana ya kuongeza muda wa Wabunge kuchangia.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Bajeti, Kanuni ya 28(4) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Bunge litaendelea kukaa hadi saa moja na dakika arobaini na tano usiku ambapo Spika atasitisha shughuli na kuahirisha Bunge hadi kesho yake, itenguliwe na badala yake Bunge liendelee kukaa hadi saa mbili na nusu usiku ili kuweshesha Bunge kujadili na kuitisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sasa hivi nisitishe shughuli za Bunge wanaokwenda kuswali wakaswali, halafu turudi saa kumi na moja, Msemaji wa Kambi ya Upinzani

aliyebaki kuhusu mambo ya Mazingira ataendelea wakati huo. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 6.40 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge, Wasemaji Wakuu katika Wizara hii watatu walikuwa wamekwishamaliza, tukabaki na mmoja, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Mheshimiwa Halima Mdee, askari wa akiba!

**MHE. HALIMA J. MDEE (K.n.y. MHE. MCH. PETER S. MSIGWA- MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kuhusu Mazingira Mheshimiwa Peter Simon Msigwa, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2012/2013. Maelezo haya yanatolewa chini ya Kanuni 99(9)ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2013).

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za kisera, kisheria na kikanuni katika utekelezaji wake katika suala zima la mazingira, lazima Serikali ikubali kuwa pamoja na jitihada zake, imeshindwa kudhibiti kasi ya vitendo vya uharibifu wa mazingira kwa kuwa watu waliopewa mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sera, sheria na mipango ya Taifa kwenye suala la mazingira, wamekua wa kwanza kushindwa kutimiza wajibu wao. Pia Serikali imeshindwa kuwawajibisha watendaji wake, ndio maana tunasema Serikali ya CCM imeshindwa kudhibiti na kusimamia kikamilifu suala la mazingira ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yawezekana kabisa Serikali imeshindwa kusimamia sheria zilizopo, hasa Sheria ya

Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009, kwa kuwa baadhi ya watendaji wake wana maslahi kwenye baadhi ya sekta zinazoongoza kwa uchafuzi na uharibifu wa mazingira ama kwa kuwa Sheria zilizotungwa hazitekelezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilitunga na kupitisha Sheria Na 12 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira. Pamoja na sheria hizi kuwa na vifungu vinavyotaka mchafuzi wa mazingira akamatwe na kutozwa faini ya Shilingi milioni moja, au kwenda jela mwaka mmoja, bado zinaonekana kupuuuzwa. Hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu iliyoridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kuhusu utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 (*Environment Management Act, 2004*) kama inavyojulikana kama *EMA* pamoja na Kanuni zilizotungwa kwa utekelezaji wa *EMA* lakini kanuni hizo hakuna anayezifuata ama kutilia maanani. Ndiyo maana tatizo la uharibifu wa mazingira linaendelea kukua kila kukicha na waliopewa mamlaka ya kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinafuatwa hawaonekani wakichukua hatua zozote madhubuti katika kukabiliana na hali hiyo .

Mheshimiwa Spika, kwa manufaa ya Bunge hili nitaorodhesha baadhi ya maeneo muhimu ya kanuni hizo ambazo zikifuatwa kikamilifu na kila mmoja wetu zinaweza kuwa sehemu ya suluhisho la kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kuonesha ufanisi katika kuyatunza na kuyalinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kanuni ya tahadhari, inataka kwamba pale ambapo kuna hatari kubwa ya uharibifu ambaao hauwezi kurekebishwa kutokea, ukosefu wa uthibitisho wa kisayansi usizue au kudhoofisha uchukuaji wa hatua za tahadhari ili kuhifadhi mazingira hayo kwenye eneo husika;

(b) Madhara makubwa yazuiliwe au kupunguzwa kuita mipango ya pamoja na uratibishaji, mfungamano/ ushirikiano na juhudzi za pamoja zinazochukulia mazingira yote katika ujumla wake;

(c) Kanuni ya mchafuzi kulipa gharama, ambayo inataka kuwa mtu ye yeyote anayesababisha madhara makubwa kwenye mazingira kulipa kikamilifu gharama za kijamii na za kimazingira za kuepusha, kupunguza / au kurekebisha athari hizo;

(d) Kanuni ya ushiriki wa umma, inayotaka uhusishaji wa watu katika uandaaji wa sera, mipango na michakato ya menejimenti ya mazingira;

(e) Ufikiaji wa taarifa za kimazingira, zinazowezesha wananchi kufanya uchunguzi binafsi ulio makini na unaoboresha utendaji katika shughuli za uzalishaji wa viwandani na Serikalini kwa ujumla wake;

(f) Ufikiaji wa haki, ambao unawapa watu binafsi, umma na vikundi mbalimbali fursa ya kulinda haki zao za ushiriki na kipinga maamuzi yasiyozingatia maslahi yao;

(g) Uzalishaji wa taka upunguzwe, pale inapowezekana taka lazima kwa kuzingatia kipaumbele zitumike tena, zizungushwe, zipatikane tena na ziondolewe kwa usalama kwa namna ambayo haitaleta athari kubwa au kama hii haiwezekani kuepukwa, kwa hali ambayo ina uwezekano mdogo wa kuleta athari kubwa;

(h) Kanuni ya usawa katika mwingiliano wa vizazi, ambayo inataka matumizi ya maliasili isiyorudishika yafanyike kwa uangalifu mkubwa, kwa kuzingatia matokeo yake kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo, viweze kupata fursa ya kutumia maliasili hiyo; na

(i) Kanuni ya matumizi endelevu, ambayo

inataka maliasili inayorudishika na mfumo ekolojia vitumike tu kwa namna ambayo ni endelevu na isiyoathiri uwezo wao wa kuendelea kuishi au kumea kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni zote za menejimenti ya mazingira zilizotajwa hapo juu ni za manufaa sana kwa ulinzi, uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa mazingira yetu kama kila mmoja wetu atazifuata kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeona wazi kuwa, kanuni hizi hazifuatwi kikamilifu. Hii inatokana na wale ambao tumewapa jukumu la kusimamia utekelezaji wa kanuni hizi kutokutimiza wajibu wake ama kutokana na uzembe au rushwa iliyokithiri kwenye mfumo wa Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya nishati na mazingira; Nishati ya mkaa na kuni ni nishati ambazo hutumiwa kwa kiwango kikubwa zaidi kama chanzo kikuu cha nishati kwa Watanzania katika shughuli zao za kila siku. Ni wazi kuwa nishati hii imekuwa ikiharibu mazingira kwa kiasi kikubwa na hatimaye kuwekewa vikwazo na mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uharibifu huo upo kwa sababu Serikali ya CCM haitambui umuhimu na mchango wa nishati hizi katika ukuaji wa uchumi. Ukosefu wa mipango na mikakati makini ya kutafuta nishati mbadala ndio imekuwa kiini cha uharibifu wa mazingira unaofanywa kutokana na uzalishaji na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, takribani zaidi ya tani milioni moja ya mkaa hutumiwa kwa mwaka hapa nchini huku Dar es Salaam pekee ikitumia zaidi ya asilimia 50% ya mkaa wote unaozalishwa na kutumika hapa nchini. Magunia zaidi ya elfu ishirini na nane (28,000) yenye kilo kati ya 60 hadi 80 huingizwa Dar es Salaam kila siku.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kuwa, Dar es Salaam pekee huingiza wastani wa zaidi ya magunia milioni 10.2 kwa mwaka. Kiasi hiki kinaifanya Tanzania kushika nafasi ya nne

na kuwa mionganoni mwa nchi kumi duniani zinazoongoza kuzalisha mkaa kwa wingi kuliko nchi zote ambapo Tanzania pekee inazalisha asilimia 3% ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa Tanzania hutumia zaidi ya tani 2,650 za mkaa kila siku.

Mheshimiwa Spika, ili kuzalisha tani moja ya mkaa kwa njia ya jadi kama inavyofanyika hapa nchini, zaidi ya tani 10 hadi 12 za miti au kuni huhitajika. Hii ina maana kuwa kuzalisha magunia 15 huhitajika tani 10 hadi 12 za miti au kuni hivyo kuhitaji ekari 846 za miti kila siku ili kuvunwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya mkaa kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, matumizi ya mkaa tangu mwaka 1960 yamekuwa yakiongezeka kila siku. Itambulike kuwa eneo la misitu Tanzania ni kilomita za mraba 344,326 sawa na asilimia 38.9% ya ardhi yote.

Mheshimiwa Spika, wakati familia za Watanzania zaidi ya laki tatu (300,000) waishio vijjini huishi kwa kutegemea uzalishaji wa mkaa kama msingi wao wa kujipatia kipato. Hii ina maana kwamba shughuli za uzalishaji wa mkaa imeajiri na kutunza familia nyingi zaidi kuliko shughuli zingine za kiuchumi vijjini. Shughuli za uzalishaji wa mkaa imeajiri watu wa kada anuai katika mchakato wake mzima wa kuanzia uzalishaji hadi utumiaji.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji hutoa ajira kubwa mionganoni mwa Watanzania walio wengi. Watu kama wakataji miti, watengenezaji, wapakiaji, wapakuaji, wenye magari, pikipiki, baiskeli, stoo, wauzaji wa jumla, rejareja wote kwa pamoja husukuma gurudumu la maisha yao kwa njia ya kujipatia kipato kwa kutumia mkaa.

Mheshimiwa Spika, Watanzania zaidi ya asilimia 90% hutumia nishati ya kuni na mkaa; asilimia 2% hutumia nishati itokanayo na umeme; asilimia 8% hutumia nishati zitokanazo na mafuta. Tafiti zinaonesha kuwa mchango wa matumizi

ya mkaa kwenye sekta ya ajira na uchumi ni takribani dola za Kimarekani milioni mia sita na hamsini kwa mwaka. Hii ni sawa na zaidi ya shilingi trillioni moja, sawa na zaidi ya asilimia 8% ya bajeti ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, licha ya mchango wa mkaa kuingiza zaidi ya dola milioni mia sita na hamsini kwa mwaka na kuajiri mamiloni ya Watanzania hususani waishio vijijini na mijini, ni wazi kuwa sekta hii imeachwa bila mikakati na sheria unganifu. Ni sekta ambayo kimsingi kwa mtupo wa jicho la haraka utaona ni sekta ndogo, inayoharibu mazingira, inayopaswa kutokomezwa wakati ni sekta muhimu kwa ukuaji wa pato la Taifa ikiwa tu Serikali itakuwa na nia ya dhati ya kuiwekea mipango endelevu ili iwe ni sekta endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003 utashangaa kuona kuwa mkaa ya mawe ambayo hutumiwa chini ya asilimia 1% imepewa mkazo mkubwa kama nishati ya kibashara, wakati mkaa na kuni imetajwa kama nishati inayoongoza kwa matumizi bila kuwekewa mkazo wa kimkakati wa makusudi wa kuifanya iwe endelevu. Ni sekta inayopingwa na wadau wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hakuna anayepinga kuwa ukataji hovyo wa miti uharibu mazingira. Hoja ya msingi ni kuifanya sekta hii iwe ni sekta endelevu. Katika Mpango Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umaskini awamu ya pili ya mwaka 2010 hakuna mkakati wowote wa kuifanya sekta ya mkaa na kuni kuwa endelevu zaidi ya kutajwa tu katika lengo namba mbili.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa utupu wa akili hutoa utupu wa fikra, hadi sasa hakuna dhana, wazo, mkakati au malengo ambayo yanaweza kugeuza uzalishaji na utumiaji wa mkaa kuwa wa kisasa na endelevu. Badala ya kuiwekea vikwazo ni vyema Serikali ije na mpango kwa kuwawezesha wataalam wetu wa ndani watakaoweza kuigeuza sekta hii kuwa endelevu na ya kisasa na yenye kutumia majiko ya kisasa, kiasi kwamba itakuwa ikipunguza gesi ya ukaa ili kutokuwa na athari katika mfumo wa mzima wa mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa mkaa ni Brazil ambayo huzalisha asilimia 11% ya mkaa wote unaozalishwa duniani. Kwenye miaka ya 1990 asilimia 60.3% ya uzalishaji wa mkaa Brazil ulifanywa kutoka kwenye uvunwaji wa misitu ya asili, baadaye mkakati wa makusudi ulifanywa ili mkaa uzalishwe kutoka katika misitu ya kupandwa.

Mheshimiwa Spika, ingawa matumizi ya mkaa Brazil ni kwa ajili ya viwanda vya kufua chuma, jambo la msingi ni kwamba uvunaji wa mkaa kwa misitu ya asili ilipungua kwa asilimia 82% kati ya mwaka 1989 hadi 1996. Makampuni makubwa yalipewa jukumu la kupanda miti, kuzalisha na kusambaza mkaa kwa ajili ya kuifanya iwe endelevu. Hapa nchini upo uwezekano kabisa wa kuboresha ubora wa mkaa kwa kuwajengea uwezo wazalishaji na kuifanya kuwa sekta rasmi huku tukiendelea kuboresha mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafi na uchafuzi wa mazingira; kama kuna jambo ambalo linatishia usafi wa mazingira ni pamoja na ukosekanaji wa vyoo na kutapaka kwa vinyesi hapa nchini. Ingawa wengi wanaweza kudhani kwamba ni suala dogo, lakini tafiti mbalimbali zimeonesha jinsi hali na mazingira ya ukosekanaji wa vyoo ilivyo katika hali ya kutisha. Takribani asilimia 14% ya Watanzania wote hawana vyoo, hii ni sawa na Watanzania milioni 6.3.

Mheshimiwa Spika, pia asilimia 73% vya watanzania wote wana vyoo visivyo na ubora unaotakiwa kwa viwango vya Kimataifa. Ni asilimia 13% tu ya Watanzania wote ndio wenye vyoo vyenye kukubalika kwa ubora kulingana na viwango vinavyokubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, zipo Taasisi mbalimbali za Serikali na Zisizo za Serikali hapa nchini ambazo hazina vyoo kabisa au zinakabiliwa na upungufu wa vyoo. Tafiti zinaonesha kuwa ni asilimia 11% tu ya shule zote Tanzania nzima ndizo zenye vyoo vinavyokidhi viwango vya vyoo kulingana vigezo vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwenye vituo vingi vya mabasi sehemu mbalimbali kumekuwa hakuna vyoo kabisa au havina au havitoshelezi mahitaji wa watumiaji. Vile vile wasafiri wanaosafiri katika njia kuu wamekuwa wakijisaidia pembezoni mwa vichaka vilivyoko kwenye barabara kuu kutokana na ukosekanaji wa vyoo kwa watumiaji wa barabara kuu. Ni wazi hili ni tatizo kubwa katika kutishia uharibifu wa mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa vyoo kwa Watanzania takribani milioni 6.3 imesababisha uchafu unaotoka kwa wanadamu hao kuwa na bakteria mbalimbali ambazo pengine husafirishwa katika vyano vya maji, mapito ya maji, visima, mabomba kwa njia mbalimbali za usafirishaji kama vile upepo, maji, mvua, mmomonyoko wa udongo, na kadhalika. Hali hii huweza kusababisha kiasi kikubwa cha maji yaliyoko juu na chini ya ardhi kuweza kuchafuliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM inapozungumzia maisha bora kwa kila Mtanzania, inapaswa kuweka mkazo katika mambo ya msingi kama haya. Ikiwa leo ni miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru takribani Watanzania milioni 6.3 sawa na asilimia 14% hawana mahali pa kuhifadhi vinyesi vyao; asilimia 73% wana vyoo visivyo na ubora unaohatarisha mazingira na afya zao ni jambo la hatari sana.

Mheshimiwa Spika, leo hii magonjwa ya milipuko kama kipindupindu na kuhara yana kiwango kikubwa katika kusambaa na kuenea. Magonjwa ya kuharisha yanashika nafasi kati ya pili hadi tatu kwa kusababisha vifo wa watoto chini ya umri wa miaka mitano hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, takribani watu 26,500 hufariki kila mwaka kutoka na magonjwa ya kuhara; kati yao watoto chini ya miaka mitano ni takribani 18,500. Tafiti zinaonesha kuwa ukosefu wa vyoo huchangia vifo vya watoto na watu wazima kutokana na magonjwa kama vile minyoo, trakoma na mengineyo ya milipuko.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia usafi wa vyoo

ina uhusiano mkubwa katika kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa pato la Taifa. Tafiti zinaonesha kuwa, takribani shilingi bilioni 301 hupotea kila mwaka kutokana na uchafuzi unaotokana na ukosekanaji wa vyoo na hasa kutokana na madhara ambayo yanababishwa na hali hiyo hasa magonjwa. Wakati Serikali ikipalililia msamiati wa sungura mdogo yapo mamilioni ya fedha yanayopotea kutokana na Serikali kushindwa kuleta maisha bora kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa hata kauli ya Waziri, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe imejaa utupu usio na matendo kwa kukataza wasafiri njiani wasichimbe dawa. Je, anataka wachimbie dawa wapi wakati Serikali ya CCM imeshindwa kuweka miundombinu itakayoondoa kudharaulika na kushusha utu wa wanawake, wasichana na mama zetu?

Mheshimiwa Spika, hatuna maana kuwa, tunataka wasafiri waendelee kuchafua mazingira, bali Serikali iache kauli za kufurahisha jukwaa na masikio ya Watanzania ila iwe na utendaji utakaoleta tija na kuondoaa kero na uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya maazimio ya mukutano wa e *Thekwini* uliofanyika Durban, Afrika Kusini ulizitaka nchi wanachama kulipa nguvu na msukumo suala la usafi wa vyoo na maji kama ajenda muhimu Afrika. Kwamba, Serikali ya nchi husika itenye asilimia 0.5% ya pato la Taifa katika uwekezaji wa upatikanaji wa vyoo bora. Hivi sasa hakuna jitihada za makusudi zinazowekwa na Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kupoteza asilimia 1% ya *GDP* kutokana na ukosekanaji wa vyoo bora, Serikali inawekeza chini ya asilimia 0.1%. Hii ina maana kuwa, jitihada za ujenzi wa vyoo bora kwa wananchi siyo kipaumbele kwa Serikali ya CCM. Hii inadhihirishwa pia katika taasisi mbalimbali za Serikali hususani shule ambapo ni asilimia 11% ya shule zote nchini ndizo zenye vyoo vinavyokidhi vigezo vyta Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu ya kina, kuna mkakati gani wa kukabiliana na hali hii ya ukosefu wa vyoo hapa nchini mwetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa mazingira katika Mlima Kilimanjaro na athari zake kwa Taifa; Mlima Kilimanjaro ni urithi wa dunia unaoteketea kutokana na uharibifu wa mazingira unaochangiwa na shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi hiyo muhimu katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa wataalam wa mazingira wamethibitisha kwamba, barafu katika Mlima Kilimanjaro imepungua kwa asilimia 82 ya theluji yote iliyopo tangu mwaka 1912 na kwa asilimia 52 ya theluji iliyopo sasa tangu mwaka 1962.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imechangiwa na vitendo vya kupungua kwa uoto wa asili hasa ukanda wa misitu ya asili ya mlima huo, ambao umekuwa ukiliingizia Taifa mapato makubwa kutokana na utalii unaofanywa kila mwaka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa zaidi ya mito 20 na vyanzo vya maji vipatavyo 70 vilivyoukuwa vikitiririsha maji yake kutoka ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (K/NAPA) katika Wilaya za Rombo, Hai na Moshi Vijijini, vimekauka na kusababisha upatikanaji mdogo wa maji. Lakini hoja ni je, nani atamfunga paka kengele? Kama wanaopaswa kutekeleza maagizo mbalimbali ya utunzaji wa Mlima Kilimanjaro ndio wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo hivyo vinavyouweka Mkoa wa Kilimanjaro katika mikoa inayokabiliwa na uharibifu wa mazingira kwa kiwango cha juu kabisa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana Serikali ikawa imefanya jitihada za kuzuia uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro, lakini kasi ya ongezeko wa uharibifu wa mazingira ni dalili kuwa utekelezaji wa sera, sheria

na kanuni za mazingira una upungufu na ni lazima Serikali ifanye uchambuzi wa tatizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu ya kina kuna mkakati gani madhubuti wa kukabiliana na hali hii na hasa ikizingatiwa kuwa theluji inaendelea kwisha na kama hatutachukua hatua madhubuti tunakwenda kuathiri chanzo muhimu cha utalii na mapato kwa uchumi wa Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utunzaji wa mazingira katika Maziwa Makuu nchini; Ni wazi kuwa asilimia kubwa ya Watanzania waishio katika Maziwa Makuu nchini wanaendesha shughuli zao maeneo hayo. Kwa mfano, Ziwa Victoria lililopo Kanda ya Ziwa ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vyta maendeleo ya nchi yetu, na hata nchi nyingine kama vile Uganda, Rwanda, Burundi, Kenya na Misri inayopata huduma ya maji ya Mto Nile unaoanzia kwenye Ziwa hili la kwanza kwa ukubwa barani Afrika na la pili kwa ukubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kumekuwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira unaosababishwa na shughuli za binadamu, umechangia kwa kiwango kikubwa kupungua kwa samaki ndani ya Ziwa Victoria lenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba zaidi ya 68,100. Kutokana na kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira, utafiti wa kitaalam unathibitisha kwamba samaki wamepungua kutoka kati ya tani 400,000 na 500,000 hadi tani 243,564 kwa mwaka 2010, ikilinganishwa na miaka kadhaa iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, kuanza kupungua kwa samaki ndani ya Ziwa Victoria lenye kina cha wastani wa mita 40 (futi 130) na mwambao wa urefu wa mita 4,828 (maili 3,000), kunatokana na Serikali ya Tanzania inayomiliki eneo kubwa la ziwa hili, kuonekana kuzembea katika kutoa elimu kwa raia wake kuhusu athari za uchafuzi wa mazingira pamoja na kushindwa kudhibiti na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lazima tufike mahali Serikali itimiza wajibu wake wa kulinda mali na rasilimali za Taifa hizi zinazoharibiwa kutokana na kukosekana kwa mpango endelevu wa kuwainua wananchi kiuchumi, ili kujikimu na gharama za maisha zinazopanda kila siku.

Mheshimiwa Spika, ingawa Serikali yetu imeanzisha miradi ya kijamii, takribani 126, kupitia chombo chake cha Hifadhi ya Mazingira Ziwa Victoria (*LVEMP II*). Lakini, miradi hiyo inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (*WB*), chini ya maridhiano ya utekelezaji wa *MoU* isimamiwe vizuri, iweze kusaidia kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuwa sasa tunataka utekelezaji tu na sio maneno ya kila siku ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka miradi hii isimamiwe kikamilifu na kwa watendaji wale watakaoshindwa kuvisimamia na kuongoza miradi hii wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma ili kuweza kuyalinda mazingira yetu na rasilimali za Taifa letu kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa Fukwe za Bahari; Serikali ilitunga Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Sheria ya Mipango Miji Na. 7 ya mwaka 2008 kwa lengo la kulinda ardhi na mazingira ya nchi yakiwemo maeneo ya fukwe za Bahari. Athari za mabadiliko ya Tabianchi zinaendelea kujidhihirisha katika maeneo mbalimbali hapa nchini yaliyomo katika ukanda wa Pwani ikiwemo Dar es Salaam, Bagamoyo, Pangani, Kilwa na ukanda wote wa Bahari Kuu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uharibifu wa maeneo ya fukwe za bahari na kulinda mazingira ya maeneo husika kwa vizazi vijavyo, tunashauri Serikali sasa itenye rasmi fidia kwa ajili ya wale wote waliojenga maeneo ya fukwe, kwa kuwa kuna viwanja vilivyopimwa na kugawiwa waendelezaji miaka ya 1950 kabla ya baadhi ya sheria kutungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahusika walimilikishwa na mamlaka halali, maendelezo ya viwanja hivyo na kwa kuwa athari za maendelezo ya maeneo hayo yaliyo katika fukwe za bahari zimeendelea kushika kasi, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Wizara ya Mazingira kuhakikisha kuwa Serikali kuititia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaandaa mpango wa fidia ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayotokea katika maeneo hayo ya fukwe za bahari. Halikadhalika kuwabomolea wale wote waliojenga baada ya sheria hizi kutungwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta tathmini ya athari za mazingira Bungeni kama ambavyo ilivyoahidi katika moja ya ripoti za utekelezaji wake, ili Wabunge waweze kushauri na kuchukua hatua stahiki hata ikibidi kubadilisha sheria zetu kuhusiana na matumizi rafiki, bora na sahihi ya fukwe zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inayo ushahidi kuwa baadhi ya watendaji wa Serikali wamekua kikwazo katika kutekeleza Sheria ya Mazingira nchini, kwa kutumia madaraka na mamlaka yao vibaya. Kitendo cha baadhi ya watendaji wa Serikali ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Bwana Patrick Rutabanzibwa kumwekeea dhamana Ndugu Robert Mugishwagwe pamoja na kuwakingia kifua wamiliki wa viwanja namba 1040, 1041, 2000 na 2002 vilivyotakiwa kuvunjwa kwa mujibu na matumizi bora ya ardhi hususan maeneo ya fukwe za bahari kama ilivyoainishwa na Sheria ya Ardhi ya 1999 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inayoelekeza kuwa upana wa mita 60 ya eneo la ufukwe linaachwa wazi kwa ajili ya matumizi ya umma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Wizara ya Mazingira kwa kushirikiana na Baraza la Mazingira la Taifa (NEMC) kuvunja kingo hizo, vijiko vikubwa aina ya Katapila

vilianza kufukua mto na kujaza udongo katika maeneo hayo na kuendelea na ujenzi na kudharau maagizo ya Wizara husika ya Mazingira na *NEMC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza na la kujiuliza, ni kitendo cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Bwana Rutabanzibwa kwenda kumuwekea dhamana Bwana Mugishwagwe kwa kigezo kuwa anamfahamu kama jamaa yake, wakati yeye akiwa na maslahi kwa kuwa ni Mtendaji Mwandamizi wa Wizara ya Ardhi ambayo inahusika kutoa vibali vya umiliki na uendelezaji wa ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo ambapo tunaamini kuwa Watendaji wa Serikali wanafanya ufisadi mkubwa kwa kutoa hati za umiliki wa ardhi kinyume na Sheria kwa kuwa licha ya kuwa Mugishwagwe amevunja Sheria lakini Katibu Mkuu Rutabanzibwa aliiagiza *NEMC* kumlipa fidia Mugishwagwe ambaye ni wazi alivunja Sheria. Nashangaa hotuba ya Seriali haioneshi hivyo wakati sisi tunajaribu kuwatetea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, matukio kama hayo yamezidi kufumbiwa macho na Serikali, ambayo licha ya kuwa na vyombo husika vinavyosimamia utunzaji wa mazingira kwa faida ya Taifa zima, mwingiliano wa Wizara kisekta unakwamisha jitihada hizo na ndio maana watendaji wa Serikali wanapata mwanya wa kukiuka sheria za nchi hii ambazo zipo wazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu ya kina ni hatua gani serikali itachukua dhidi ya Maafisa wake Waandamizi ambao wanashiriki katika kuhujumu mapambano ya kulinda na kuhifadhi mazingira yetu kwa kuanzia na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa *Bauxite* katika Wilaya ya Same; katika hotuba yetu ya bajeti ya 2012/2013, tulihoji kuhusiana na suala la uchimbaji wa *Bauxite* katika Wilaya ya Same na uchafuzi mkubwa wa mazingira

19 APRILI, 2013

ambao unasababishwa na uchimbaji wa madini hayo na Waziri aliahidi kwamba atalifuatilia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, *NEMCmnamo* tarehe 27 Juni, 2012 waliandika barua ya kuikataza kampuni ya *Willy Enterprises Limited* kutokuendelea na uchimbaji wa madini ya *Bauxite* katika Mlima Shengena yenye kumbukumbu namba *NEMC/366/1/Vol. 10/17*, ila bado uchimbaji huo uliendelea kufanywa na kampuni hiyo bila kuzingatia amri hiyo ya *NEMC* na bila kufuata sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu ya Serikali ni kwanini kampuni hii ya *Willy Enterprises Limited* inapuuza maagizo ya vyombo halali vyta Serikali na inaachwa na inaendelea kufanya shughuli zake kinyume na sheria hapa nchini? Je, ni dalili za kushindwa kwa Serikali ya CCM? Ni lini uchafizi huu wa mazingira utadhibitiwa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimwia Wabunge kama tulivyosema, bahati mbaya Wizara hii tutachangia watu wachache sana, tutaanza na Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Chombo, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Mheshimiwa Omar Rashid Nundu. Halafu watafuata Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Riziki Omar.

Kama Mheshimiwa Tauhida yupo, aanze.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia Wizara ya Muungano. Nitachangia mambo matatu kama muda utaniruhusu; elimu juu ya suala la Muungano, kero za Muungano na elimu ya juu katika suala zima la Muungano.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kusema yote nimpe

hongera Waziri kwa hotuba yake nzuri, ya kistaarabu, kiungwana na kuonesha mfano kwamba, yeze kweli ni Mтанzania halisi. Naishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa uelewa wao na Mawaziri hawa waliochaguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, muda unakwenda, nina dakika kidogo, lakini nimwombe Waziri asije akapoteza muda wala wakati kujibu hizi hotuba zilizoletwa na Kambi ya Upinzani, hana atakachowea kukijibu yeze na wala hastahili kukijibu. Yeze ni mama yetu, sisi ni watoto, tukipata muda na kama ataturuhusu tutawajibu. Jibu hoja za wananchi walioituloeta hapa, jibu mama masuala mazima yanayohusu Tanzania na faida za Watanzania, usije ukasimama ukajibu haya, haya tunaweza kuyajibu sisi akina Tauhida, waambie watufuate kwa wakati wao tuwajibu, hapa ni mahali pa kuleta faida kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala zima la elimu kwa wananchi, limezungumzwa sana lakini kweli fedha katika suala la Muungano ili kutoa elimu halipo, hususani sasa Watanzania wengi hivi ni vijana, wanahitaji kupewa elimu ya kutosha kuhusu suala zima la Muungano.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimestaabisha kuna hotuba moja hapa ya Kambi ya Upinzani, mwenzangu kijana kama mimi alizungumza kwamba hawaelewii wala hawafahamu jambo usilolielewa na kulifahamu tafuta wanadolielewa uliulizie ili upate kulielewa. Maana limekuwa ni jambo la kichekesho Mbunge tena wa Jimbo, umeingia mpaka hapa Bungeni huelewii suala la Muungano, una faida gani wewe kuwepo humu ndani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kweli tunajitahidi kutii maagizo yako, lakini yanakuwa magumu, tuseme kwa maneno mafupi uzalendo unashindikana. Kwa sababu vijana kama sisi na vijana wenzetu wanazungumza maneno kama yale kweli tutajitahidi lakini ni magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kijana aliyekaa pale anasema

hana uelewa juu ya suala la Muungano, umefuata nini, umefuata ngoma au mdundiko? Basi kama umechoka tafuta nyumba japo ya jirani ukapumzike, inaonekana hii ngoma uliifuata huijui inatokea wapi na tena ngoma yenewe mbwa kachoka! Sasa hiyo hasara iliyoje! Maana unataka kutoka hujui uende wapi, nyumba ya mtaa wa kwenu umeisahau! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimwambie Waziri kwamba, Zanzibar sasa hivi vijana wanahitaji zaidi elimu kuhusu suala la Muungano. Suala zima la Muungano, wananchi wa Zanzibar waeleweshwe na wafahamishwe, faida ya kuwepo Muungano, nini kinapatikana ndani ya Muungano. Mambo yanayofanyika ndani ya Serikali hii ni mazuri, makubwa na mengi, lakini inaonekana dhahiri kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya suala zima la elimu ni kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimwombee Waziri, Fedha aliyoidhinishiwa iongezwe ili apate nafasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya suala zima la Muungano. Sisi Chama chetu, vijana hatuna woga wala hatusiti kuuliza suala lolote linalohusu nchi, linalohusu maslahi ya vijana na wananchi wa Tanzania, tukipata muda, viongozi wetu tunawaauliza. Vijana wenzangu mliopo Vyama vingine mwulize pia, msione woga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ilifika wakati sisi tumekaa tunawaauliza mpaka Viongozi wetu, tukawaambia tuleteeni Mheshimiwa Kingunge, tuleteeni Mheshimiwa fulani tukawaauliza mpaka tukajua mustakabali wa nchi hii unaendeleaje, sasa ninyi mnafika wakati mmekaa kama Bibi Harusi anayemsubiri bwana, samahani!

Mheshimiwa Spika, kero za Muungano ziko nyingi, lakini hizi kero tunaona Waziri amejitahidi kuzielezea, kati ya mambo aliyoyaelezea...

**SPIKA:** Mheshimiwa Galos naomba simama, nimewita Mheshimiwa Halima.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mhehsimiwa Spika, nafuta hilo neno.

**SPIKA:** Mheshimiwa Galos naomba ukae kidogo, Mheshimiwa Halima nimekuita.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka tu unipe Mwongozo wako kuhusiana na Kanuni ya 68(7) kwa sababu naona zinatumika lugha za kuudhi hapa kitu ambacho ulitoa maelekezo kabisa kwamba tuongee kwenye hoja, kama una *criticize, criticize* kwenye hoja. Sasa kama tunaanza mipasho hapa wakati tumewekana sawa sidhani kama itasaidia mjadala. Kwa hiyo, naomba tu kiti chako kielekeze watu ambao wanakwenda kinyumenyume, tuweze kwenda vizuri ili tuweze kuokoa huu muda ambao ni mdogo sana kwa ajili ya kujadili hili suala. (*Makof!*)

**SPIKA:** Sawa, naomba kila mmoja ajitahidi, Mheshimiwa Galos endelea!

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba muda wangu ulindwe.

Mheshimiwa Spika, neno utupu limetupandisha jazba, lipo kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani. Kero za Muungano zipo nydingi, lakini tunaona kila siku zinatatuliwa. Kwa hiyo, namwomba Waziri, kwa sababu kero zipo nydingi, mambo yapo mengi, kuna vitu vipewe vipaumbele ndani ya Serikali yetu, ambavyo hivyo ndiyo vinawasumbua Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, naamini sana kwamba, haya mambo yanafanyika kwa sababu umetoa majibu leo, zaidi ya kero 13 tayari zimeshatatuliwa na nyininge ziko mezani bado mnaendelea kuzifanyia kazi. Namwomba Waziri anipe majibu hili suala la *TRA*, kodi ambayo Wabunge waliotoka

Zanzibar awe wa Chama chochote, iwe CCM ama *CUF* akisimama kero kubwa ni suala zima la ulipaji ushuru *TRA* mara mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la bandarini, Zanzibar *TRA* wanalipa wakija hapa wanalipa, Waziri akija hapa naomba majibu, hivi suala hili pingamizi yake kubwa iko wapi? Pingamizi ni Wizara ya Fedha na kama ni Wizara ya Fedha tipe majibu ni Wizara ya Fedha Tanzania Bara, Wizara ya Fedha Tanzania Zanzibar au ni *TRA* kuna matatizo?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kati ya kero za Muungano, hii ni kero ambayo Wazanzibari inawasumbua kwa miaka mingi. Toka sisi hatujaingia Bungeni mpaka leo tumefika Bungeni, *Hansard*zingine zinaonesha kwamba suala hili limezungumzwa si mara moja, si mara mbili, si mara tatu.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimenifanya na mimi kuwa na uchungu hata Rais Jakaya hapendi kusikia kero za Muungano. Kwa kukuthibitishia hili kwamba Rais Jakaya hapendi kusikia kero za Muungano, alimwambia Waziri Mkuu, akamwambia na wakati ule kuna Waziri Kiongozi Zanzibar, mkutane japo mnywe kahawa kwa sababu hiki kitu kinachoitwa kero za Muungano hapendi hataki kukisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Rais wa nchi hakitaki, kwa nini au kuna watu gani wanaozuia haya mambo yasitatuliwe? Maana naamini sana hata Rais wetu Shein hapendi, lakini kuna watu wanazuia. Sasa Waziri atakapokuja hapa, katika mambo atakayokuja kuzungumza naomba hili leo alipatie majibu tatizo liko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mashaka mara huyapeleka *TRA*, mara huchukua mashaka yangu

nikayapeleka Wizara ya Fedha. Nikifika Wizara ya Fedha nashindwa kutoa uamuzi, inawezekana tunapiga kelele Wizara ya Fedha, lakini pengine tatizo liko Zanzibar, pengine liko tatizo Tanzania Bara. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri ndiye anasimamia Muungano namwomba atakapokuja mahali hapa leo hili alitolee majibu. Mawaziri wapo hapa, Waziri Mkuu yupo hapa Bungeni, tunaomba hili militatue.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote yaliyopo, juzi mwenzangu mmoja alisimama akataka kuongelea *TASAF* muda ukamwishia. Miradi mingi ipo kwa wananchi, yapo masuala ya *TASAF*, masuala ya *TASAF*, leo Mbunge Mzanzibari hashirikishwi, Watanzania Bara wanaingia ndani ya Halmashauri zao, wanasililiza, wanatoa hoja kuhusu wananchi wao. Sasa Mbunge wa Zanzibar anatolea wapi na ile miradi ya kijamii, ya wananchi inawahu. Waziri atakapokuja hapa kati ya majibu atakayokuja kutoa na hili alichukue atupe majibu.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Galos hiyo ni kengele ya pili!

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mohamed Chomboh, simwoni, Mheshimiwa Riziki Omar Juma.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia hii nafasi. Naomba nianze mchango wangu, kwanza nijielekeze kwenye Idara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ndiyo Serikali ambayo tunaitegemea. Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ukiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, na mara zote Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na ndivyo ilivyo, hii inatajwa kama ni Idara ya Muungano, jambo ambalo linatudhoofisha sana. Kwa sababu, haiwezekani Muungano ukawekwa kama Idara katika Ofisi ya Makamu wa Rais, jambo ambalo linatupa hata ufinyu wa bajeti, inatengewa kama kiidara kidogo ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ni jambo la msingi sana, na hili nimelisemea siyo mara ya kwanza wala ya pili. Haiwezekani jambo kubwa kama hili likapewa kijiidara. Haiwezekani! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu ni Idara, hata bajeti inayotengewa ina udhaifu. Kwanza, naomba niseme, kwa mfano, mwaka 2011/2012 bajeti ambayo imetengwa ni bajeti ambayo inachanganywa pamoja na matumizi ya Serikali ya Zanzibar, inapelekwa huko Shilingi bilioni 31.1. Lakini mgawo huo wote unakwenda huko, Idara ya Muungano inabakishiwa Shilingi milioni 680 tu kwa ajili ya matumizi ya Idara hiyo ya Muungano. Mwaka 2012, zilitengwa Shilingi bilioni 33 zikapelekwa huko Shilingi milioni 675 ndiyo zilizobaki kwamba ni mgawo wa matumizi ya shughuli za Idara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Muungano una matatizo mengi. Kero zake ni nyangi sana. Mheshimiwa Waziri, ametwambia anahitaji nyenzo, anahitaji fedha za kutosha ili kuweza kufanya Vikao vya *SMT* na *SMZ* na vikao vya Mawaziri ili kutatua kero za Muungano. Hatima yake, fedha anayotengewa au anayogawiwa ni ndogo sana ambayo haitoshelezi. Vikao hivi kama vitafanyika, basi kwa mara moja nadhani wanatumia Shilingi milioni 120 kama sikosei. Sasa kwa Shilingi milioni 675 ambazo anatengewa, anaweza kufanya vikao vingapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukiiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ametoa, inatuonyesha vikao ambavyo vimefanyika na vile ambavyo havikuweza kufanyika. Je, tatizo la kero hizi litaondoka? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kila siku tutakuja hapa tukiimba kero za Muungano, kero za Muungano. Inaonekana hakuna nia thabiti, hakuna nia madhubuti ya kutatua kero hizi. Hofu yangu kubwa ni kwamba, tunaelekea kwenye muundo wa Katiba Mpya, lakini hatuwezi kuvunja Muungano.

Kwa hiyo, hata huo Muungano tutakaouunda mwininge tutaendelea na kero hizi hizi. Kero zitaendelea kuwepo milele kwa sababu hatuna nia ya dhati ya kutatua kero hizi. Tusingetenga bajeti ndogo, tusingeweka Idara tu katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Ni afadhali mambo mengine yanaonekana kupewa umuhimu. Afrika Mashariki imepewa Wizara, lakini Muungano umepewa Idara. Tunajidhalilisha, tunajidhoofisha sisi wenyewe? Haiwezekani! Ni jambo la kujidhoofisha. Ni lazima turudi nyuma tuangalie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, halafu tuangalie, Wizara zote zina Mawaziri. Idara ya Muungano, tunasema Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa nini hakuna Waziri wa Muungano? Kwa nini asiwekewe Wizara yake maalum akapewa mafungu yake akaweza kufanya kazi? Hiyo taaluma itawafikiaje wananchi bila ya fedha? Taaluma tunayotaka kuwaelimisha wananchi, kuna wananchi kweli hawaelewi Muungano. Vizazi vyetu vya leo havielewi umuhimu wake wala maana yake. Wanahitaji taaluma kubwa. Hata sisi Wabunge wenyewe tuna upungufu. Kwa hiyo, tunahitaji taaluma ya kutosha. Mheshimiwa Waziri, namwombea avezeshwe vizuri ili aweze kufanya wajibu wake ipasavyo na malalamiko haya yaondoke.

Mheshimiwa Spika, upungufu ambao upo umeanza zamani. Kwanza nije kwenye Katiba sasa. Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kifungu cha 133, kuna Mahakama ya Katiba kwanza ambayo ilipaswa iundwe au iwepo ili iweze kushughulikia mambo au matatizo yatakayojitokeza baina

ya Serikali hizi mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Mahakama hii hadi leo tangu mwaka 1977 ilipoamrisha Katiba hiyo, hakuna kilichofanyika. Leo, tumefikia hapa, kila siku kila anayesimama analalamikia kero za Muungano. Tungekuwa na hatima yake basi. Tunaunda Kamati, tunaunda Tume, tunaunda nini sijui, kutatua kero za Muungano. Ingekuweko hii Mahakama tukawapeleka watu wawili hawa Muungano na Zanzibar, basi kero hizi zingetatuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu akaunti ya pamoja ya fedha, hadi leo imeshindikana kuwekwa Mfuko Mkuu huu wa hazina. Tunafanyaje kazi? Fedha hizi ambazo zitatumika kwa ajili ya mambo yanayohusiana na Muungano, tumekaa kimya hadi leo hakuna Mfuko huu wa hazina ambao umeundwa. Hiyo akaunti ya pamoja ya fedha haiku! Tunaendelea kuzungumzia kero, hadi lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi mambo yanavyoonekana, siku moja mwaka 1994 Mheshimiwa Msekwa alipokuwa Spika wa Bunge, alitoa *paper yake* kule Tanga akiwa na Semina, inayoitwa “*State of Union*” tarehe 25 na 27 Februari, 1994, alisema: “Kwa jinsi mambo yanavyoonekana, inaonekana Zanzibar kama ni *Invited Guest* katika Muungano.”

Kwa hiyo, maneno hayo yanathibitishwa na hivi mambo yanavyokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, Muungano ni kitu kizuri, Muungano ni jambo kubwa, hatuna jinsi, hatuna namna, hatuwezi tena kuuvunja Muungano huu. Lakini kama kuna nia thabiti, basi Muungano huu uangaliwe kwa kina, tuurekebishe, tuuboresha. Hata hiyo Katiba nyngine ikija tutakwenda kufanya vituko hivi hivi, ikiwa mambo haya hayakurekebishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Chuo kule wanaita Taasisi ya Sayansi ya Bahari Buyu; haina pesa, ujenzi wa Chuo kile umesimama, hakuna fedha. Sasa hivi sidhani kama

kumetengewa fedha yakutosha, Mheshimiwa Waziri amesema hapa. Ni muhimu sana kile Chuo, naomba kitengewe fedha za kutosha ili kiweze kufanya mambo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Naomba Mamlaka hii ipatiwe fedha yakutosha, watoe taaluma yakutosha. Wananchi wetu hawaelewi umuhimu wa vitambulisho hivi, wala hawaelewi ni nini. Utakuja kukuta kwamba, watu hawakujandikisha kutaka vitambulisho hivi, jambo ambalo ni haki yao ya Kikatiba. Naomba sana jambo hilo tulizingatie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nije kwenye mazingira. Mheshimiwa Waziri, aliposoma hotuba yake, amesema kwamba, kwa mwaka tunapanda miti kama milioni 145.

Sisi Watanzania tuko zaidi ya milioni 40. Ina maana kwa mwaka mtu hawezi kupanda hata mti mmoja. Bado tatizo la mazingira litaendelea kuwa gumu mno kama Serikali haikusimamia mkakati madhubuti wa upandaji wa miti, nchi itaendelea kututoka bila kuyajali mazingira.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Msabaha watagawana dakika zao.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naona kijana mwenzangu Tauhida amechangia kwenye Muungano, mimi nitajikita kwenye mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba nilikwenda Jeshini na wakaniongezea baadhi ya vitu, na vitu ambavyo wameniongezea ni kwamba, natakiwa kuwa hodari na jasiri kwa nchi yangu na kuwa wazi na kukemea watu ambao wanavunja Sheria bila kujali nyadhifa zao, na watu ambao wanafanya Viongozi wenzao washindwe kutekeleza majukumu yao kwa sababu yao. Hili, viongozi wenzangu,

Wabunge wenzangu, kama kweli tunataka kuboresha mazingira yetu, kama kweli tunataka nchi yetu iendelee, ni lazima vitendo hivi tuvikemee bila kuoneana haya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 wakati nachangia Wizara ya Ardhi, nilipongeza na nitaendelea kupongeza kwa jitihada ambazo Wizara ya Ardhi na Mazingira, ilionyesha katika kubomoa nyumba ambazo zimejengwa katika fukwe zetu na kuzuia mikondo ya maji. Matokeo yake, moja ya athari ambazo tulizioni ni yale mafuriko ambayo yalitokea mwaka 2011 *Kawe Beach*. Serikali iliingia gharama na kujenga upya daraja na kulipa fidia kwa wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwamba siku hizi kumekuwa na utamaduni wa watu ambao wanakiuka taratibu makusudi, eti kwa kutumia kigezo cha kwenda kuweka zuio Mahakamani. Hili, kama Wabunge, kama Viongozi, hatuwezi kufumbia macho watu wa namna hiyo ambao wanafanya makusudi kuifanya Serikali ishindwe kutimiza wajibu wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, *NEMC* mwaka 2012, kama kumbukumbu zangu ziko sawa, waliweza kuvunja nyumba maeneo ya *Mbezi Beach* huko na nyumba za wananchi wa kawaida na kulikuwa na zuio Mahakamani, lakini nyumba zile zilivunjwa. Lakini vilevile Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, ambaye ninamwamini na ana uwezo sana, na yeye hakutaka kabisa kukubali watu ambao wanatumia Mahakama kwa ajili ya kufanya Serikali, ishindwe kutimiza wajibu wake. Naye alivunja nyumba, huku vilevile kukiwa na zuio Mahakamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa nikiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 58 anasema: "*Ubomoaji wa nyumba katika viwanja namba 2019, 2020, zilizopo Mbezi Beach, haujafanyika kutokana na wamiliki wa nyumba hizi kuwa na kesi Mahakamani.*" Hii ni double standard na hatuwezi kulivumilia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini nina ripoti hapa ya Taarifa ya Uchunguzi wa Mgogoro wa Ardhi wa Mazingira katika

Eneo la *Kawe Beach*. Ripoti hii ni Wizara mbili, ya Maliasili na Wizara ya Ardhi. Tena kipindi hicho akiwa Baba yangu namheshimu sana, *Comred Chiligati*, na waliweka wazi matatizo na hivi viwanja vikiwepo.

Tena wengine waliambiwa kabisa, hawapaswi kujenga, wakadharau Serikali, wakajenga. Serikali imekuwa ikiwafuata ikiwaambia waache kujenga, wakaendelea kujenga. Wengine ni Viongozi tuko nao humu humu. Kwa nini mnafanya Viongozi wenzenu washindwe kutimiza wajibu wao? Mbaya zaidi tena ni Viongozi wa Kiimani! Kwa nini mnashindwa kufanya Viongozi wenzenu washindwe kutimiza wajibu wao? Hili ni jambo ambalo haliwezi kukubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niwaambie, na nimwombe Mheshimiwa anayehusika na suala la Mazingira, una uwezo wa kubobomoa hizi nyumba. Nawe unashimamia Sheria yako na hawa watu wamekiuka Sheria. Hakuna haja ya kuogopa! Hakuna haja ya kuogopa na wala hakuna kuingilia mhimili mwингine kwa sababu na wewe una sheria zako ambazo zimekiukwa, kama ambavyo kuna wengine ambavyo walivunja nyumba na kesi ziko Mahakamani. Wewe unashindwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha! Tunaambiwa Kiongozi ni mfuasi, lazima tuongoze kwa mfano. Kama wenzako wanakwambia unakiuka taratibu na unaendelea, hatuwezi kuruhusu nguvu za fedha kushindwa kuwezesha dola kufanya kazi yake! Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi niwaambie tu Wabunge wenzangu, tunaweza kufanya hivi kwa pamoja mkinzunga mkono. Bunge letu Tukufu, tunaweza kuazimia Manispaa ya Kinondoni na Wizara – *NEMC*, kuhakikisha inakwenda kuvunja nyumba hizo ambazo zimebakia ambazo athari yake ni kubwa.

Athari yake ni kwa kuhakikisha wananchi wa kawaida, mafuriko yanapotokea wanapata taabu, Serikali, inaingia gharama.

Mheshimiwa Spika, hili haliwezekani! Wabunge wenzangu, naomba kutoa hoja, tuazimie *NEMC* na Manispaa ya Kinondoni, iende ikavunje hizo nyumba ndani ya wiki moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Hoja inayoingilia uhalali wa vyombo vingine, siyo hoja. (*Kicheko*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivi, Viongozi wetu hawa ambao wamewekwa kwa ridhaa ya wananchi, watashindwa kufanya kazi yao. Haiwezekani sisi Viongozi wachache kutumia nafasi zetu eti kufanya Viongozi wengine washindwe kufanya kazi zao. Haiwezekani! Huu ni ushauri tu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, hatukatazwi Viongozi kuwa na mali, hatukatazwi Viongozi kumiliki ardhi, lakini tufuate taratibu. Mtu una viwanja saba, nane, kumi, mpaka uende kuzuia mkondo wa mto! Kwa nini tunafanya hivi? Kwa nini tunawafanya Viongozi wenzetu washindwe kufanya kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama tulivyoeleza kwenye Kamati kwamba Wizara ya Mazingira inapaswa kuongezewa bajeti, ili hata hiki chombo tunachokisema, *NEMC* kifanye kazi yake. Sasa hivi *NEMC* hawana Ofisi, wanafanya kazi yao kwenye ma-*Container*. Nami nawapongeza kwa sababu wanashindana na mijitu yenye fedha na huku wako kwenye ma-*container*. Wana-risk maisha, wanafanya kazi na wanafuatwa sana na watu ambao wamezoea kutoa rushwa na hawafanyi hivyo, bado wanasisimamia misimamo yao kwa kuhakikisha sheria inafuatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa *NEMC* imetengewa Shilingi bilioni tatu na milioni kadhaa, lakini fedha hizo zote zinakwenda kwenye ujenzi wa Ofisi. Inabaki Shilingi milioni 500. Hii Shilingi milioni 500 ni miradi sita. Sasa tunaona hivi kweli wataweza kupambana na hawa watu ambao wanakiuka taratibu kwa makusudi? (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria muda wa  
Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Grace Kiwelu dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha, dakika tano.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami niungane na Mchangaiji aliyemaliza kusema kwamba, bajeti ya Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ni kidogo, tunahitaji iongezwe kwa sababu ina kazi kubwa sana ya kuelimisha wananchi kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, Iakini suala la pili naomba niongelee Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro, umeingia katika Maajabu Saba ya Dunia.

Ningependa Wizara iniambie: Je, kuna fungu lolote limetengwa kwa ajili ya kuuendeleza mlima huu kwa sababu umeharibika sana kwa mazingira. Wananchi wamekata miti, wamechoma misitu na kusababisha Mlima ule, theluji yake kuanza kuyeyuka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, imeonyeshwa kabisa kwamba theluji ile imeendelea kuyeyuka, Asilimia 82 sasa ya theluji imeyeyuka. Hii imesababisha kupata tatizo la maji katika Mkoa wa Kilimanjaro; maeneo yale yote yanayozungukwa na Mlima Kilimanjaro, Wilaya ya Rombo, Moshi Vijijini hata Moshi Mjini kumekuwa na tatizo kubwa sana la maji. Ningependa Wizara iniambie, imejandaa kiasi gani kuunusuru mlima ule? Mlima ule ni chanzo kikubwa sana cha fedha katika kuingiza mapato katika nchi yetu. Kwa hiyo, ningependa kujua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine la tatu ni kuhusu zoezi la upandaji miti. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 20 naomba kunukuu, amesema: "Jumla ya miti 145,156,884 ilipandwa, lakini katika ya hiyo, miti 108,171,349 ndiyo iliyostawi." Hii inamaanisha kuna miti zaidi ya 36,000 ambayo haikuota.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Wizara, hali ya hewa imebadilika katika Mikoa yetu. Ile siku ya kupanda miti duniani au Kitaifa ya tarehe 1 Aprili, ningeomba tuachane nayo, ili tuendane na hali ya hewa ya ile Mikoa kwa sababu, tukifanya hivyo ninaamini miti tulioipanda inaweza ikastawi na tutapunguza gharama za hii miti tunayopanda halafu haioti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ningependa kuongelea ni kwamba Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake ukurasa wa 58 ambalo hili amelisema Mheshimiwa Ester Bulaya; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili. Tulitembelea eneo hili ambalo Taarifa hii ninayoisoma hapa ni tofauti na hali tulioikuta eneo la tukio.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda na Kamati, tulitembelea eneo lile ambalo tumekuta watu wamejenga ndani ya mikoko, wamekata mikoko wakaleta vifusi, wamefukia na vifusi wakawenza kutengeneza viwanja wakajenga. Hivyo viwanja Namba 2020 na 2019 ambacho amekisema Mheshimiwa Ester Bulaya, cha kushangaza hakina *Offer*, wala hakina hati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza mtu huyu kwa kutumia kiburi cha fedha na kwa kuwarubuni Watendaji wakashindwa kusimamia Sheria mtu huyu aliweza kujenga bila kuchukuliwa hatua yoyote.

Tunachoomba, tunaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama wanataka kurudisha imani kwa wananchi wa Tanzania wasimamie haki kwa sababu wananchi wa eneo lile wamekata tamaa. Waliobomolewa wanajiuliza, kwanini sisi tumebomolewa na wengine wameachwa?

Kwa hiyo, niiombe sana Wizara ya Ardhi pamoja na Mazingira wahakikishe hatua kali zinachukuliwa na kwa wale wote waliohusika kutoa maeneo haya wachukuliwe hatua. Tukiachilia hivi bila kuchukua hatua, tunalipeleka Taifa letu mahali pabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, amesema Mheshimiwa Ester, mimi nilibahatika kutembelea eneo hilo la Daraja la Mto Mbezi mwaka 2012 nikiwa kwenye Kamati ya Miundombinu. Tuliona madhara makubwa yaliyosababishwa na mafuriko yale na yalisababishwa na mjenzi aliyejenga kwa kuzuia mkondo wa mto yale maji ili yasibomoe nyumba yake na ndiyo ikasababisha daraja lile kubomoka na kuliingizia Taifa gharama kubwa ya kujenga daraja lile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe kuitia Mawaziri wanaohusika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa  
Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Msabaha, dakika tano. Unapiga dakika tatu, halafu mbili.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nichukue fursa hii kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais na napenda kushauri Ofisi hii ya Makamu wa Rais yale mazuri yaliyosemwa na Kambi ya Upinzani wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, tuangalie, kuna kero nyingi za Muungano. Hizi kero za siyo tu za Wazanzibari, nao hata Wazanzibari nao wana kero za huku Tanzania Bara. Leo hii nimeshudia, nimeangalia, nimesikiliza, najua suala la ulinzi na usalama ni suala la Muungano, lakini leo hii nasikia chenji ya rada haiuhusu Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, sasa kweli Wazanzibari watasema vipi? Si hizo kero zitazidi kuwa ni za kudumu? Kwa sababu suala la ulinzi ni suala la Muungano. Kuna vitu ambavyo viko

katika Wizara za Muungano na kuna vitu ambavyo vinahusu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hata suala la bandari Wazanzibari kwa kweli ni wavumulivu, lakini sasa ule uvumilivu wao tena unaondoka. Leo mtu amepitisha godoro pale bandarini unamwambia mtu alipie. Leo hii tumeshuhudia Wabunge wa Zanzibar tunakuja hapa tunashindwa kuleta magari yetu hapa tunakodisha taxi kwa ushuru uliokuwa pale. Hata ile gari yako ukiifikisha pale kuna pesa ambazo unatozwa na pesa zile mpaka wewe urudishe gari kupeleka Zanzibar ndiyo urejeshewe pesa zako. Ukitazama, hizi ndizo kero za Muungano. Sasa kila siku tunalalamika kero hizi zitaondoka lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na lingine nilikuwa nashauri Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wanakaa vikao vyao vya hizi kero za Muungano, naomba kabisa watoe taarifa kwa Wazanzibari kupitia vyombo vya Zanzibar, *radio*, *magazeti*, *television* na mahali popote ili wananchi wapate kufuatilia hizi kero na wazitambue na wazipime ziko vipi na wakitaka waendelee nao na wakitaka wakatae.

Mheshimiwa Spika, mengine ni kuhusu suala la *TASAF*. Kwa kweli Wabunge nasema kabisa Ofisi ya Makamu wa Rais, sisi Wabunge tumekaa kama watoto yatima hatujui tuelekee wapi.

Tukiangalia miradi ya *TASAF* wanashirikishwa Wawakilishi, na kuna baadhi ya Wabunge watachaguliwa labda kuingia mle ndani labda kuwa ni Wajumbe. Lakini wakishaletewa zile barua, hawajui kinachoendelea kule kwenye miradi ya *TASAF*na sisi tunahitaji kusimamia ile miradi ya *TASAF* tukiwa kama Wabunge. Kwa sababu sisi kama Wabunge tukiangalia zile pesa za Jimbo hatushirikishwi kwenye pesa za Jimbo wala hatukai kwenye Kamati ile ya pesa za Jimbo, hatujui kinachoamuliwa mle ndani, kwa Wabunge wa Viti Maalum. Ukiangalia Wabunge wa Viti Maalum pia kwenye Baraza la Madiwani hatuingii. Kwa hiyo, sasa sisi Wabunge tupo tupo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hili suala namna ya kuliweka na hii Ofisi ya Makamu wa Rais iangalie namna ya kuiweka. Hata Wabunge wa Viti Maalum wengi hawana Ofisi kule Zanzibar. Hili pia liangaliwe kwa sababu Wawakilishi hawa wameshadai pesa zao za Majimbo na sisi hizi pesa zetu angalau Wabunge tuwe tuna Ofisi zetu kule Zanzibar.

Hii miradi ya *TASAF*ikija kule Zanzibar na sisi Wabunge tushirikishwe kwa ukamilifu kupitia Vyama vyote bila kubagua Chama. Tuingie mle wanaotoka Pemba, wanaotoka Unguja, wanaotoka wapi na sisi tukae mle tuwe na maamuzi yetu tuangalie zile pesa kweli zinakwenda kwenye mambo ya miradi au zinaliwa na watu wachache? Hizi kero ndiyo zitaondoka.

Mheshimiwa Spika, niingie kwanza kwenye suala lingine la mazingira. Kumekuwa na tatizo, nami katika Bunge liliopita pia nilizungumza kuhusu suala hili la ukataji miti kufanya kama alama za barabarani. Hii imekuwa ni kero na isitoshe mpaka magari yanapata ajali kwa ajili ya zile alama, watu wakashaweka zile alama za barabarani basi hawaondoi. Kwa hiyo, magari mengine yanapata ajali kutokana na yale magogo ambayo yanawekwa barabarani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa  
Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Haya, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Chomboh. Mheshimiwa Muhammad Chombo yupo!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba yetu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na Mazingira kwa sababu mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya Mazingira.

Wajumbe waliotangulia Mheshimiwa Bulaya na Mheshimiwa Grace, walieleza vizuri tuliyoyaona na ukweli waliyoyasema ndivyo ilivyo hasa. Ni jambo la kisikitisha sana kwamba kati ya hawa amba wanavunja sheria tuliyopanga au iliyopitishwa na Bunge hili wanaivunja kwa mikono yao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kisikitisha sana. Hili jambo nafikiri ni la kuchukua hatua ipasavyo. Lakini pia chombo chetu cha *NEMC* kwa kweli hatukitendei haki, kwa kiwango cha fedha kilichopewa na majukumu waliyopewa.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua, wanaofanya mambo haya ni watu amba wana nguvu na uwezo wa kifedha. Sasa kama na wao wanakwenda kupambana na watu amba wana nguvu ya kifedha, hawana hata jinsi ya kufuatialia iwe ni kwa usafiri, iwe ni kwa mawasiliano, ni wanyonge tu, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ilizingatie jambo hili, Wizara hii ya Mazingira waipe uwezo wa kifedha ili wafanye kazi zao vile ambavyo sisi na Watanzania wote wangependa iwe hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama mapendekezo yetu yalivyo, Wizara au Ofisi ya Makamu wa Rais, kuna Idara mbili; ya Muungano na ya Mazingira, tungeomba pia wakati wa bajeti yake basi fedha zile zitengwe kwa kila mmoja awe na fungu lake. Siyo linakuja kwa mfuko mmoja, inaleta *confusion* baadaye wakati ya kuyajadili na kuweza kuyazingatia.

Mheshimiwa Spika, unaona kwamba ni fungu kubwa la fedha liko katika Ofisi ya Makamu wa Rais lakini mgawanyo wake unakuwa unaleta mashaka, utakuta Wizara ya mazingira haina kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naingia kwenye Muungano. Kati ya watu amba wameuona Muungano ukiundwa, mimi mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu mpaka leo nipo, lakini pia naupenda uendelee na nisingependa nife ikiwa hakuna Muungano. Napenda uendelee na vizazi vyote viliivyo, bado muungano uwepo.

Mheshimiwa Spika, najua na naelewa kwamba Muungano wetu una matatizo na kwa sababu ni Muungano ulioundwa na binadamu hauwezi kukosa matatizo, hiyo ni kitu cha kawaida. Kwa umri wake sasa una miaka karibu 50. Huu ni Muungano! Wewe binadamu uliyembwa na Mwenyezi Mungu ukishafika miaka 50, basi kuna vitu vinaanza kukupotea. Hiyo ni dhahiri, unabadijika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa haiwezekani pia Muungano ukawa ni vile vile tu, haiwezekani! Kwa hiyo, ni lazima Muungano ufumuliwe, utengenezwe uwe ni Muungano ambao unapendeza kwa kizazi kilichopo sasa hivi. Hiyo mimi nakubali, sina wasiwasi. Lakini cha msingi kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu sana kwamba jambo hili linatoka kwamba na mimi naomba niwepo angalau nitoe mchango wangu. Lakini namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia na kukubali kuja na rasimu au kuja na mchakato wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo peke yake ambalo litatusaidia Watanzania tuliouwepo na walioko sasa hivi na watakao kuja, tukaamua tukashauriana na mwisho tukapata muungano ambao una maslahi yetu sote kama ni Watanzania.

Kwa hiyo basi, ni vizuri sana kila mmoja ashiriki kwa nafasi yake na atoe mchango wake, tusianze kuanza kususia kwamba mimi nimo, mimi simo, hilo siyo jambo zuri. Yale ambayo tunakubaliana na *inshaallah* tutakubaliana kwa sababu Muungano ni kitu kizuri, kila jambo liwekwe katika Katiba. Kwa sababu sasa hivi kinachogomba, mambo mengi sana ni maamuzi ambayo yamekuja juu juu tu kwa vikao, havikuwekwa kwenye Katiba. Lakini likiwa liko ndani ya Katiba, bila shaka litatekelezwa kwa mujibu wa Katiba iliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, nawasihi Watanzania wenzangu wa Bara na Visiwani tuwajibike na sasa hivi ni wakati mzuri kabisa wa kutoa mchango wetu na kila mmoja mawazo yake, na kila mmoja mapendekezo yake na baadaye tupate Katiba ambayo itatuongoza katika Muungano wetu wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawasihi tena wale waliokuwa na nia ya kutaka kujitoa katika Muungano huu au katika mchakato huu wa Katiba, waache mawazo hayo wanasihiike roho zao na tuungane pamoja.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni la watu wote ili baadaye tusije tukafika hapa tukaanza, mimi sikuwepo, mimi sikuchangia, haitakuwa inaleta maana. Tukaeni kama ndugu moja, kama Watanzania tuchague tunafanya nini na tunapendekeza lipi ili tuweze kupata Katiba mpya kwa maslahi ya Tanzania na Watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa leo mimi naishia hapa, natoa nafasi kwa wenzangu. Ahsante. (*Makofii*)

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya mita 60 kutoka ufukwe imepitwa na wakati na inafaa irekebishwe kwa sababu fukwe ulimwenguni kote hujengwa karibu sana na bahari ili kuona madhari ya ufukwe kama kivutio kwa watalii.

Aidha, sura za fukwe za bahari zimejengwa kwa mtindo huo na majengo ya Hotel na watu binafsi yamejengwa kwa kibali cha mamlaka kama vile *permit* za ujenzi. Kikubwa hapa ni kusisitiza "*Management*" ya mazingira pamoja na "*treatment*" ya majitaka. Ukitaka kutekeleza sheria hii, utavunja majengo mengi pamoja na nyumba ya Rais Mstaifu, Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa. Kwa upande wa *Coco Beach*, kituo hiki ni maalum na msaada mkubwa

kwa kutoa fursa kwa vijana kuburudika angalau mara moja kwa wiki badala ya kujihusisha na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, amri hii ya mita 60 imekuwa chanzo cha kero katika bonde la Simiyu. Miaka yote wananchi wanatumia maji ya mto Simiyu kwa ajili ya maji ya kunywa na pia maji ya mifugo. Amri hii inakataza binadamu kusogelea mto kwa shughuli yoyote ya kibinadamu. Matokeo ya utekelezaji wa sheria hii, ni rushwa shilingi 150 kwa kila ng'ombe na shilingi 100 kwa kuoga. Maoni yangu ni kufundisha watu kutunza zile fukwe kwa kupanda 'Ngobi majani', miwa na mianzi. *This is Environment Management* na siyo kuacha mazingira yajimalize.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kuachia mazingira "*conservation*" ni potofu zaidi kwa fukwe za Dar es Salaam zinazoharibiwa na mawimbi kwa sababu ya tabianchi (*climate change*).

Mfano mzuri ni ufukwe wa "*Ocean Road*" ambao unakula ufukwe wote, unakula barabara na nyumba ya Balozi wa Uingereza itaanguka kama hatua za haraka hazitachukuliwa. Kwa kutumia dhana ya "*conservation*" inafanya Serikali isisitize zaidi kutunza "*conservation*" na siyo "*management*". Nashauri fedha iwekezwe ili kupambana na tabianchi. Uwekezaji huu unaweza kufanywa na wawekezaji wa fukwe hizi pamoja na Serikali. Tukiacha tu na tukiwakataza wawekezaji kupambana na uharibifu huu wa mawimbi, fukwe zetu zitarudi na hata nyumba zilizojengwa katika umbali wa mita 60 zitafikiwa na kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuruhusu uwekezaji katika fukwe hizi, ni vizuri basi sheria ya mita 60 ikafutwa kwani imepitwa na wakati.

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Spika, kutohana na mabadiiiko ya haraka ya teknolojia ya habari na utangazaji na pia kutohana na kushuka kwa bei ya vifaa vya TEHAMA, imesababisha kuongezeka kwa matumizi ya vifaa hivyo lakini pia imeongeza kwa kiasi

kikubwa kuwa na vifaa chakavu nya TEHAMA. Vifaa hivyo vimekuwa vikitupwa maeneo mbalimbali hapa nchini. Vifaa hivi vina baadhi ya madini ambayo yanaweza kuhatarisha mazingira yetu. Njia mbalimbali zinatumika ulimwenguni ili kupambana na vifaa chakavu nya TEHAMA. Njia hizi ni kama vile Sera, Sheria, mitambo ya kuangamiza vifaa hivyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania bado hatuna Sera au Sheria mahsus ambayo inasimamia eneo hili. Ninaelewa Sheria ya *NEMC* inasimamia kidogo jambo hili. Miezi miwili (2) iliyopita Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. G. Bilal alielekeza Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia kuandaa Sera itakayosimamia jambo hili.

Kwa hiyo, ninachukua fursa hii kuwaomba wadau wote tushirikiane ili tuweze kukamilisha jambo hili. Kwa upande wa Wizara yetu suala hili linasimamiwa na *TCRA*. Kwa hiyo, ninaomba tushirikiane kwenye kufanikisha jambo hili muhimu sana kwa nchi yetu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, suala la mabadiliko ya tabianchi, ni jambo geni kwa Watanzania walio wengi. Ingawa elimu imetolewa kuititia Luninga na Redio, bado jitihada zinahitajika hasa kwa Watanzania waishio vijijini na hata mijini kupewa elimu zaidi kuhusu mabadiliko hayo ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoombwa kwa ajili ya Idara ya Mazingira na *NEMC*, Sh. 5,184,372,00/= bado ni kidogo sana. Ni kweli kwamba maendeleo hayawezi kuwa endelevu endapo suala la utunzaji wa mazingira halitapewa kipaumbele.

Hivyo basi, ni kwa nini suala la utunzaji wa mazingira halijapewa kipaumbele na hivyo kutengewa fungu la fedha linaloridhisha? Serikali itenye fungu la kutosha kwa ajili ya Idara hii ya Mazingira na *NEMC*, ili udhibiti na utunzaji wa mazingira uweze kuwa endelevu na utoaji wa elimu unaowalenga hata wale waishio pembezoni.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Baraza la Mazingira (*NEMC*) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi limeanzisha Kitengo cha Polisi wa Mazingira. Je, kitengo hiki cha Polisi wa Mazingira kinafanyaje shughuli zake na wapi?

Mheshimiwa Spika, ujenzi usiofuata Sheria katika maeneo ya fukwe na kingo za mito hapa nchini umekomaa. Hivi sasa kuna ujenzi wa makazi unaoendelea kuelekea Mlima Meru, Mkoani Arusha. Ili kuhifadhi mazingira na msitu wa asili uliopo katika Mlima Meru Wilayani Arumeru – Arusha, ongezeko la wanaoishi karibu na Mlima Meru lidhibitiwe ili kuhifadhi mazingira badala ya kuacha ujenzi unaopelekea kukata miti/msitu wa asili hovyo na kuharibu vyanzo vya maji. Sheria iwekwe kuzuia ujenzi kupanuka kuelekea Mlimani Meru na badala yake ujenzi uendelee kuelekea maeneo ya bondeni yaani Ngaresero, Usa – River, Makumira, Leganga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, aidha, ujenzi holela uliofanywa katika fukwe zetu na kingo za mito, ujenzi huo ubomolewe ili kuhifadhi na kutunza fukwe zetu ambazo zipo kwa ajili ya Watanzania wote na watalii wa nje na ndani pia.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya na kwa kuleta hotuba nzuri ndani ya Bunge lako Tukufu. Pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia katika kuboresha hutuba hii.

Mheshimiwa Spika, upandaji miti; nchi yetu imeendelea kuhamasisha upandaji miti katika sehemu mbalimbali ya nchi yetu. Hata hivyo, juhudzi za Serikali katika kuhamasisha upandaji miti sio za uhakika kwani tumekuwa na siku ya upandaji miti duniani na baada ya hapo tunalala usingizi. Ninapendekeza na kushauri Serikali yaani ofisi ya Makamu wa Rais (*Muungano na Mazingira*) ikae pamoja na Wizara ya TAMISEMI waweke mpango mkakati wa muda mfupi na mrefu wa kupanda miti. Serikali ni moja, lazima

Wizara zote hizi mbili zitusaidie na ziache kupigana chenga kwani Taifa linaangamia.

Chini ya utaratibu huu, TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano Na Mazingira) iwe na Idara katika kila Halmashauri inayoshughulikia Mazingira, waajiriwe Maafisa katika kila kijiji na Kata kwa ajili ya Mazingira. Maafisa Vijiji na Kata wa Mazingira mojawapo ya majukumu yao iwe ni kusimamia upandaji na ukataji miti katika maeneo yao. Pia itengwe bajeti kwa ajili ya kuotesha vitalu vya miti mbalimbali kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchomaji moto bado ni tatizo kubwa linaloharibu kwa kiwango kikubwa mazingira ya nchi yetu. Uchomaji moto huharibu miti, nyasi na viumbi hai hivyo kuleteleza mmomonyoko wa ardhi. Pamoja na kuwepo Sheria ya kutochoma moto, lakini bado Sheria hizi hazijasimamiwa vizuri. Wakiajiriwa Maafisa Mazingira Vijiji watasaidia kusimamia kwa karibu uchomaji moto katika vijiji vyote nchini.

Mshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya maji; Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi ni aina gani ya miti ni rafiki wa maji na waelezwe inapatikana wapi karibu na maeneo yao. Pia elimu itolewe kuhusu miti isiyofaa kupandwa katika vyanzo vya maji kama mikaratusi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi kandokando ya fukwe za Bahari, Ziwa na Mito; kwa sasa imekuwa tabia ya kawaida watu kujenga kandokando ya Mito, Ziwa na Bahari bila kuchuliwa hatua yoyote. Serikali ifanye kazi zake kwa kusimamia Sheria za Mazingira kwa kukamata, kuvunja nyumba na kuchukua hatua mahsusii haraka iwezekanavyo. Watanzania tunataka tuelezwe ni lini zoezi la kubomoa nyumba hizo litaanza na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchomaji mkaa; hakuna ubishi kuwa uchomaji mkaa unaathiri sana mazingira lakini pamoja na athari hizo ni wazi kabisa kuwa matumizi ya mkaa kwa ajili ya kupikia ndiyo njia pekee inayotumiwa na watu

wa kipato cha chini waishio mijini na vijijini. Kwa kuwa matumizi ya umeme ni karibia asilimia mbili tu (2%), ya Watanzania wote hivyo basi kuna umuhimu Serikali kuwa na mpango kabambe wa kupanda miti kwa ajili ya kuivuna na kuchoma mikaa kwa ajili ya biashara. Hili linawezekana kwa sababu ardhii tunayo ya kutosha kwa ajili ya kupanda miti. Pia Serikali inaweza kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa, Taasisi binafsi, *NGOs* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongoza kwa mfano; nashauri kila Kiongozi kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkao hadi Taifa awe na shamba la miti kuanzi ekari moja na kuendelea. Shamba hili linaweza kuwa shamba la miti ya mbao, mkaa, matunda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono bajeti ya Waziri wa Mazingira na Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dokta Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayofanya juu ya ufuutilaji wa mazingira na masuala yanayotuunganisha kama Watanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uharibifu unaotokana na mifugo, ipo haja ya kuwa na mjadala wa kitaifa juu ya ufumbuzi wa malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, vyoo shulenii, kweli ni tatizo lakini Serikali imeshafanya jitihada ya kuzitambua shule pamoja na mahitaji yake, mfano SWASH. Kinachotakiwa ni kuendeleza juhudii hizo kwa kutenga pesa za kutosha ili kufanikisha mradi huo.

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro ya kidini, pande zote mbili za Tanzania ziendelee kulifanyia kazi kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, suala la "*Environmental Impact Assessment*" (*EIA*), kuna ucheleweshaji mkubwa unaolalamikiwa na baadhi ya wawekezaji juu ya kucheleweshwa vibali. Nashauri Wizara iwezeshe kupatikana wataalam na kuridhia vibali kutoka katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara hii ni ndogo ukilinganisha na masuala yanayotakiwa kushughulikiwa.

**MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu kutoka kwenye Wizara hizo hapo juu ya mambo yafuatayo:-

- (i) Ni lini Serikali itatekeleza wajibu wa kuondoa tazizo sugu linalolalamikiwa sana na Watanzania wengi kutoka Zanzibar juu ya tofauti za kodi zinazojitokeza pindi Mtanzania anapotoa mzigo kutoka Pemba kuja Dar es Salaam au Tanga?
- (ii) Lini magari kutoka Zanzibar yatapata nafasi ya kutembea Tanzania Bara bila kubughudhiwa?
- (iii) Serikali imeweka utaratibu gani kwa maana ya asilimia inazopata vijiji kutokana na mgao wa mapato yatokanayo na hewaukaa (*carbon*)?
- (iv) Kwa nini Serikali inaendelea kutoa Leseni/Vibali kwa wafanyabiashara wa mkaa?
- (v) Kwa nini Serikali haitoi motisha kwa wananchi wanaofanya vizuri katika utunzaji wa mazingira?

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, naanza na mazingira. Tunatambua wazi jitihada zote zinazofanya na Serikali kuhakikisha mazingira yanatunzwa.

Suala la mazingira ni nyeti ambalo lisipozingatiwa huleta athari katika nchi kama majanga, magonjwa na hata vifo.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira Serikali imejikita kuongelea utekelezaji wa miradi tu ambayo inaleta "*Positive Impact*" katika jamii lakini kwa upande mwingine Serikali hajajikita kwa undani juu ya uharibifu wa mazingira katika jamii ambayo huleta "*Negative Impact*" katika jamii.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kuna uharibifu unaofanywa aidha na viwanda karibu na makazi ya watu mijini na kuleta madhara kwa binadamu, pia uchafu wa sura ya miji. Pia kuna uharibifu wa mazingira unaotokana na binadamu kama kukata miti hovyo, kuchoma misitu na kusababisha jangwa na kuharibu vyanzo vya maji. Kuna uharibifu wa mazingira unaosababishwa na wanyama ambaao huharibu udongo kwa kuleta mmomonyoko, kuchafua mito na barabara. Serikali hajaeleza imeandaa mazingira gani ya kukabiliana na uharibifu huu ambaao unaleta mabadiliko ya hali ya hewa, yanayochangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabianchi na kusababisha kukosekana kwa mvua na kuua vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi kama viwanda, machimbo ya madini, Serikali itoe elimu sana kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa sehemu hizo hasa machimbo ambaao husafisha dhahabu kwa kutumia (*mercury*) katika mito ambapo wananchi wanakunywa maji hayo, hii ni hatari kwa afya zao.

Wakati wa kuhitimisha hoja, namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anifafanulie Serikali imechukua hatua gani ya kulinda afya za binadamu kwa hawa wanaochimba dhahabu, wanasafishia dhahabu kwenye Mito ambayo ipo karibu na makazi ya watu kwa kutumia *mercury*? Kwa mfano, Katavi Wilaya ya Mpanda ambapo wanachimba dhahabu na kusafishia katika Mto Mpanda uliopo mjini karibu na makazi ya watu ambaao wanatumia maji hayo kwa kupikia na kunywa. Naomba majibu kama kuna athari kwa watumiaji waelewe na Serikali imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, wafugaji watengewe maeneo ya kufugia mifugo yao kwa kufuata sheria ya mipaka yao na watakapokiuka na kufugia maeneo tofauti kama barabaran na kusababisha uharibifu wa barabara, Serikali iwawajibishe kwa kulipa faini na fedha hizo ziwekewe utaratibu wa matengenezo ya barabara ambazo zimekuwa zikiharibiwa na wafugaji holela.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri.

Mheshimiwa Spika, hali ya Misitu ya Tabora ni mbaya. Tunaomba msaada wa kutoa elimu kwa wananchi waache kukata miti na kuharibu misitu yetu.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, *adaptation to climate change*. Sote tumeshuhudia matukio mbalimbali yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi kama ukame, mafuriko, mvua zisizoaminika na kadhalika. Je, Serikali inakabiliana vipi na ubomokaji wa madaraja, barabara pamoja na shule zetu nydingi? Kwa sababu mabadiliko ya tabianchi hayatabiriki, naishauri Serikali ijitahidi kujenga miundombinu imara hasa ya barabara, umeme, madaraja na shule kama njia mojawapo ya *"adaptation to climate change"* kwa upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kufunika mitaro inayopita katikati ya miji itokayo viwandani ili kuzuia harufu mbaya na gesi chafu zitokazo kwenye uchafu wa viwandani. Mitaro hii mingine ina upana mdogo kama mita moja hadi mbili hivyo ni rahisi kufunika kwa juu na kuacha uchafu upite kwa chini. Mfano mmoja ni ule unaopita *Alfa High School* kule Mikocheni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pia madampo yanayoanzishwa katikati ya miji ni aibu tupu kwa nchi yetu kwa mfano lile dampo lilitopo Kirumba jirani na Sokoni. Serikali itafute eneo la mbali na mji kwa ajili ya dampo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye tathmini ya mradi wa *MACEMP* kwani kwa sasa uvuvi wa kutumia mabomu ndio unazidi kuongezeka kutohana na wavuvi kuchomewa nyavu zao.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ni mtambuka. Bila kuwepo mazingira kulinda mazingira tujue hakuna kilimo, utalii, maliasili na maisha.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengewa Wizara ya Mazingira halifanani na hali halisi ya mazingira nchini. Hivyo, naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuongeza fedha katika bajeti ya Wizara ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya Serikali kwa masuala yafuatayo:-

(i) Uharibifu wa mazingira unaofanywa katika Milima ya Uluguru Morogoro kwa kujenga majumba/hoteli, nani ametoa kibali na kwa nini Serikali imekaa kimya?

(ii) Uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu pembezoni mwa bahari hasa fukwe za Kawe, wapo baadhi ya viongozi wana viwanja na nyumba karibu na bahari kwa kukata mikoko na kufukia mto na kusababisha mafuriko na madhara kwa wananchi.

Naishauri Serikali ilete taarifa ya uharibifu uliofanywa katika eneo lote la fukwe na hatua na sababu zinazokwamisha.

(iii) Nataka Serikali ilete taarifa ya mmiliki wa baa ya *Coco Beach* na uhalali wa umiliki wake kwa kuwa anafanya maendelezo kwa kukaidi maagizo ya Serikali.

(iv) Serikali ilete taarifa ya maeneo yote yenye uharibifu wa mazingira na utatuzi uliochukuliwa.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii na nawapongeza Mawaziri wa Wizara hii kwa mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Spika, suala la kutunza Mazingira tumekuwa tunalitamka tu bila kuweka mikakati ya kiutendaji. Tumesema hifadhi ya vyanzo vya maji, mbona hili limewekwa kwenye sheria. Sawa, iweje wananchi wanalima vinyugu ndani ya mita 60; iweje mahoteli makubwa yamejengwa ndani ya mita 60 kandokando ya Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na kadhalika, sasa nani ni msimamizi wa sheria hii?

Mheshimiwa Spika, tuangalie tena kanuni za sheria hii kama hazitekelezeki, basi wahusika waifanye mapitio ili kama kuna dosari ifanyiwe marekebisho. Tume na mkakati wenye bajeti ya kutunza vyanzo vya maji kwenye Mito, Maziwa, Mabwawa na fukwe za Bahari.

Mheshimiwa Spika, tuwe na mkakati wenye bajeti na kupanda miti kila panapowezekana kuoteshwe miti.

Tuveke mkakati wenye bajeti wa kufanya usafi katika maeneo ya makazi, barabara, ofisini na maeneo ya shule na kadhalika. Mji wa Moshi unaweza kuwa mfano wa kuigwa kwa usafi, sasa kwa nini miji mingine isifanye hivyo. Tuzuie kabisa matumizi ya *plastic* kwa kubebaa bidhaa madukani, sokoni na mahotelini kama walivyoweza nchini Rwanda, sasa Tanzania tumeshindwa nini? Mji wetu na barabara zimezagaa ovyo na uchafu wa ma-*plastic* (vifungashio).

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa matakwa ya kisheria na kisera yaani elekeza kuwa miradi yote mikubwa ya maendeleo ya nchi yetu inatakiwa ifanyiwe tathimini ya athari ya mazingira (*TAM*) kabla mradi haujaanza ili Serikali ijiridhishe na athari za mazingira zinazoweza kujitokeza, zinadhilitwa vipi na kama zikijitokeza wakati wa mradi zinarekebishwa vipi na wataalam wakijiridhisha kwa mujibu wa sheria na kanuni na taratibu zote zinafuatwa, basi Waziri mwenye dhamana anatoa kibali (*Certificate EAI*).

Mheshimiwa Spika, lakini sheria haikomi hapo, inahitaji wakati mradi unaendelea kuwe kunafanyika ukaguzi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa, miradi hiyo inatekeleza matakwa yalioainishwa kwenye Hati za *TAM* na mipango ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, aya ya 37 ukurasa 27 imeonesha miradi ya ujenzi ilioorodhesawa kwa ajili ya kufanyiwa *TAM* mwaka 2012/2013 ni 78 na 34 ndio ilipatiwa Hati. Lakini pia aya 87 ukurasa 60 na 61 imeeleza miradi ya maendeleo 554 ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa *TAM* mwaka 2012/2013, ni miradi 239 ilifanyiwa mapitio ili ama wapewe au kutopata hati za *TAM*.

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu kama walishafanya ukaguzi wa tathimini ya Mazingira katika miradi ya maendeleo inayoendelea ambayo mingine inakamilishwa mwezi Juni. Kwa mfano, miradi ya barabara ya Songea - Namtumbo na Songea - Mbinga kwani miradi hii imekuwa ikipasua mawe kwa Baruti zinazosababisha mawe kuruka hadi katika nyumba na mashamba ya wanavijiji vinavyozunguka Milima waliyokuwa wanapasua mawe, hivyo kusababisha uchafuzi wa mazingira katika mashamba na visima vya maji asili vilivyoingia vumbi ya mawe yaliyokua yanalipuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kama *NEMC* haijakwenda kufanya ukaguzi wa athari za mazingira uliojitokeza katika Vijiji vya Utwango na Chengena, Wilayani Namtumbo, lakini pia ukaguzi ufanywe Kijiji cha Lumecha walipokua wanachimba mchanga wa kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isimamie hili na kuelekeza kurejesha au kusafisha yale maeneo yaliyoathirika kabla Kampuni hizo hazijamaliza kazi yake yawe yametimiza takwa hili la kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mradi wa uchimbaji Makaa ya Mawe, Mbinga. Lakini kumekuwa na kituo cha

kumwaga mavumbi ya Makaa ya Mawe katika moja ya Kijiji katika njia ya kutokea Amani, Makoro kwenda Manda. Hapo kimekuwa kituo cha kushusha chini mavumbi hayo na kuyapakia tena katika malori yanayosafirisha ambapo ni ndani ya kijiji na karibu na nyumba wanazoishi watu.

Mheshimiwa Spika, naomba *NEMC* wakakague athari za Mazingira zinavyojitokeza pale na wachukue hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano, wananchi wengi wa nchi hii wanajivuna kuwa Watanzania na Utanzania umeletwa na Muungano wa nchi zetu mbili. Zanzibar na Tanganyika kabla ya Muungano hakukuwa na nchi au Taifa lililoitwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Muungano una faida kubwa kwetu Watanzania na kama zitaorodheshwa faida na hasara za Muungano naamini orodha ya faida itakuwa ni ndefu kuliko ya hasara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero; ijapokuwa kama nilivyoeleza hapo juu kwamba, Muungano una faida nydingi, lakini pia zipo kero ndani ya Muungano huu, jambo la msingi ni kuwa na dhamira ya dhati ya kutafuta ufumbuzi wa kero hizo. Zipo kero ambazo ufumbuzi wake utapatikana kwenye Katiba mpya ambayo itategemea maoni yaliyotolewa na Watanzania, lakini mengine ni ya kiutendaji ambayo haya hitaji Katiba mpya yanahitaji utashi na dhamira thabiti ya kuyafanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hivyo ushauri wangu kwa Serikali zetu kuhusu haya matatizo ya kiutendaji na yanayohitaji marekebisho tu ya kisheria yatafutiwa ufumbuzi katika mwaka huu wa fedha, aidha, uandaliwe utaratibu unaoeleweka ili kila zinapojitokeza kero za Muungano zifanyiwe kazi mara moja kabla hazijaleta athari na mivutano isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kitasaidia ni kujenga uelewa wa wananchi juu ya mambo ambayo yamejadiliwa na kupatiwa ufumbuzi na yale ambayo yanaendelea kujadiliwa katika vikao vya Kamati ya pamoja na SMT na SMZ. Uwazi ni jambo la msingi, bila ya uwazi maadui wa Muungano wanapata nafasi kueleza ya kwao ambayo hayana ukweli wowote.

Mheshimiwa Spika, mfano baadhi ya watu walikuwa wakiwaeleza wananchi kule Zanzibar kwamba mapato yanayokusanya na *TRA* Zanzibar yanaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Muungano na Zanzibar kutokupata chochote wakati ukweli ni kwamba, fedha zote zinazokusanya na taasisi hiyo upande wa Zanzibar zinapelekwa katika Mfuko wa Hazina wa Zanzibar na kutumika kule Zanzibar. Bahati mbaya sana suala hili halikukanushwa, hivyo kubakia katika vichwa vya watu kama ilivyoelezwa. Hivyo elimu kwa umma ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza kuhusu ufunguaji wa *Account* ya pamoja *joint financial account* kama inavyotakiwa Kikatiba, Wizara za Fedha zote mbili ziache ajizi juu ya jambo hili kwani ni la muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato wa kuandaa Katiba Mpya; Tume ya Mabadiliko ya Katiba imepewa mamlaka ya kisheria kuandaa mwongozo wa kuundwa Mabaraza ya Katiba katika ngazi za Serikali za Mitaa na Wilaya kule Zanzibar uchaguzi wa wajumbe katika mabaraza hayo umekwenda vizuri ingawa yapo maeneo ambayo zilifanyika fujo za hapa na pale na kubidi uchaguzi kutofanyika au kufanyika siku nyingine tofauti na ilivyopangwa awali.

Kwa yale maeneo hasa Unguja yenyeye wana-CCM wengi, wana-CCM wamechaguliwa kwa kura nydingi kuwa wajumbe na maeneo ya Pemba ambayo *CUF* ni wengi wajumbe wengi wametokea Chama cha *CUF*na hiyo ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, wenzetu wa CHADEMA wasilalamike kuwa wamekosa nafasi za ujumbe katika

Mabaraza hayo na wakubali tu kuwa wamezidiwa kwa idadi na wana-CCM ambao ndio wapiga kura.

La msingi ni kwamba, wote waliochaguliwa hawaendi kuwakilisha Vyama vyao, kazi hii ya kupitia rasimu ya Katiba inataka uadilifu mkubwa ili maoni ya Watanzania wote (*regardless of their political affiliation*) yafanyiwe kazi vizuri ili ipatikane katiba iliyo bora kama matumaini ya walio wengi hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nitachangia katika mambo yafuatayo:-

- (i) Uharibifu wa Mazingira katika Mlima Kilimanjaro;
- (ii) Ufuatiliaji na ukaguzi wa majengo hasa maghorofa mjini;
- (iii) Uchafu katika miji yetu; na
- (iv) Ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mlima Kilimanjaro umetajwa na kuingizwa katika maajabu saba ya dunia.

Hata hivyo, yapo mambo ambayo kama hatua hazitachukuliwa haraka mlima wetu, utapoteza sifa zake.

Mheshimiwa Spika, theluji Mlimani inapungua sababu kubwa ni uvunaji wa misitu unaozunguka Mlima ambao unapeleka hewa ya unyevu Mlimani. Serikali inapaswa kuongeza juhudui au kubuni mbinu za kupambana na uvunaji huu vinginevyo theluji yote itamalizika.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kwamba, baadhi ya wanasiasa na viongozi ndani ya Serikali kuanzia Serikali za Mitaa wanatuhumiwa kwa uhalifu huu.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni kila Mji na hasa Majiji yetu kumejitokeza ujenzi wa magorofa na nyumba nyingi za kisasa. Hata hivyo, inatia shaka kama kweli ujenzi huu unapata kibali cha Idara ya Mazingira. Ushahidi ni ghorofa ambalo limeanguka Dar es Salaam siku za karibuni, mitaro ya maji machafu kufumuka kwa kuja na vinyesi kumwagika barabarani.

Mheshimiwa Spika, Mji yetu mingi haina maeneo rasmi ya kutupia taka na magari ya taka yenyewe ni taka kwa kuwa ni mabovu na yanamwaga takataka barabarani. Katika karne ya sasa hatuwezi kuendelea kuvumilia hali kwa hali hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kwamba sheria zitazamwe ili kila kaya ijiwekee utaratibu wa kuhifadhi taka zake. Magari yanayozoa taka yakaguliwe ili yale mabovu yaondolewe barabarani. Lakini maeneo yanayotupia taka yaainishwe na utaratibu ufanyike ili taka ziweze kutumika kwa faida kama mbolea kutengeneza matofali na kadhalika. Vyoo nya kaya zikaguliwe mara kwa mara na Maofisa Afya ili kudhibiti wale wanaomwaga vinyesi barabarani na katika vyanzo nya maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri Serikali isiidharau Idara ya Mazingira kwani bajeti yake ni ndogo sana na huenda ndiyo inayozuia ukaguzi na ufuatilaji kufanyika. Serikali lazima ione umuhimu wa kuongeza fedha, vitendea kazi kama magari na watumishi ili kufanya idara hii kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, taarifa za upandaji miti zinazotolewa katika Mikoa na Wilaya katika nchi yetu siyo taarifa sahihi, naomba kufahamishwa ni chombo gani kinahakiki taarifa hizo kama ni za kweli.

Mheshimiwa Spika, ingelikuwa taarifa hizo za upandaji miti kila mwaka zingekuwa ni za kweli, basi nchi yetu ingekuwa haina tatizo tena la Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie kwa dhati uharibifu wa Mazingira uliopo katika Ziwa Rukwa. Naomba pia Serikali iangalie namna ya kudhibiti uharibu wa Mazingira katika Ziwa Rukwa, karibu Ziwa lote limezingirwa na mifugo jambo ambalo ni hatari na litaweza kusababisha Ziwa hilo kukauka.

Mheshimiwa Spika, sheria ya kudhibiti uharibifu wa mazingira haisimamiwi sawasawa na Serikali na matokeo yake watu wanaendelea na uharibifu wa mazingira siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, kuna uharibifu wa Mazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kupitia Wizara itoe fedha kwa Halmashauri na kuanzisha bustani za miche ya miti na kugawa kwa wananchi. Kwa sasa ni wimbo usio na korasi bila beti na usio na mwisho.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishakataza mifuko ya Rambo, lakini utekelezaji wa agizo hilo haujatoa majawabu, bado mifuko ya rambo imeendelea kuwa ndio chanzo cha vyombo vyaya kubebaa bidhaa zinazonunuliwa sokoni.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Wilaya walio wengi hawawezi kusimamia agizo la Makamu wa Rais la kulinda mazingira ama kwa kutojua umuhimu wa kutunza mazingira au kwa kuwaogopa wananchi ambaao sasa hawaogopi na kutii sheria.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, wawajibike.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara hii ni finyu sana kulingana na majukumu mazito na muhimu iliyonayo, ningependekeza Wizara iongeze Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafi na uchafuzi wa mazingira; katika maeneo mengi sana kumekuwepo na usimamizi hafifu sana wa kusimamia utekelezaji wa sheria hii. Mazingira mengi sana yamechafuliwa kwa kutokuwa na vyoo, vinyesi kutapakaa ovyo.

Mheshimiwa Spika, tushukuru Wizara ya Uchukuzi kwa amri yao ilyotolewa kuhusu kuchimba dawa abiria wanaosafiri.

Hilo pia lilikuwa eneo kubwa sana, wasafiri wanaposafiri huchafua maeneo mengi sana ikiwa ni pamoa na kutupa uchafu ovyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna baadhi ya kaya hazina vyoo na wafanyabiashara wa baa na stoo za bia kutokuwa na eneo la kujisaidia wateja wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utunzaji wa mazingira katika vyanzo vya maji; hakuna kabisa usimamizi mzuri wa kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia vyanzo hivyo na kusababisha wananchi kuendeleza kilimo katika vyanzo hivyo, ujenzi holela karibu na vyanzo, kulisha mifugo na kadhalika.

Hii pengine inatokana na ufinyu wa bajeti, pia nashauri elimu ya mazingira itolewe, inawezekana wananchi wanafanya yote hayo bila kuwa na ufahamu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya mazingira; niipongeze Serikali kwa kampeni za mara kwa mara kuhusu kupanda miti kwenye maeneo yalijotengwa.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali ihakikishe inasimamia, maeneo mengi sana miti inapandwa, lakini si yote inayokua, mingi inakuwa kutokana na kutokuwa na mpango mzuri wa usimamizi. Pamoa na kuwa na mkakati mzuri wa kampeni ya kupanda miti na iwepo mikakati ya usimamizi wa miti hiyo inayopandwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, Muundo wa Serikali mbili. 26 Aprili, 2013 Muungano utahitimmo miaka 49 tokea uasisiwe, takribani miaka 50. Ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na duniani kama alivyosema Jaji Mkuu wa Kenya Willy Mutunga hivi karibuni alipohutubia kongamano la Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam. Ni njia sahihi kuelekea shirikisho la Afrika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali zote mbili ziendelee kudumisha Muungano huu kwa mfumo uliopo wa Serikali mbili kutokana na uwiano uliopo ili Zanzibar isijione inamezwa (Serikali moja) au inakandamizwa chini ya mfumo wa Serikali tatu. Kero za Muungano ziendelee kuainishwa na kushughulikiwa kimya kimya huku Muungano ukisonga mbele kufikia miaka mia moja.

Mheshimiwa Spika, Muungano wa Senegal na Gambia haukuweza kudumu kwa sababu walikimbilia haraka mfumo wa Serikali moja (*overnight*). Vurugu na kutoaminiana kukavunja Muungano huo katika muda mfupi, ukafa. Pia nchi za kiarabu hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti wachochezi, aidha, naishauri Serikali ya JMT na SMZ kuwadhibiti wale wote wanaoleta chokochoko za Muungano kwa nia ya kuuvunja Muungano. Wapo wenyewe nia njema ya kuainisha upungufu au kinachoitwa kero, lakini wapo wanaotumia kisingizio cha kero kutaka kuvunja Muungano. Hawa wa mwisho wadhibitiwe haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Muungano, suala la udini, na suala la ukabila, yote matatu yawe kipaumbele, kwenye *agenda* ya Serikali zote mbili kuwadhibiti wanaochochea kuvunjika kwa amani na utulivu kwa kutumia masuala haya matatu. Watu hawa wajengewe *Siberia* maalumu watakapofichwa na kutengwa na jamii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna masuala ya utawala bora na haki za binaadamu, lakini hata Mataifa yanayotutaka tuzingatie haya zina *Quantanamo bay* zao kuwadhibiti wale wanaotishia uhai wa Mataifa yao.

Aidha, nchi ya China ina mfumo mzuri unaowadhibiti wale wote wanaoleta chokochoko kama hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali tatu, aidha, sikubaliani na hoja ya Serikali tatu. Hizo ni mbinu za kudhoofisha na hatimaye kuvunja Muungano. Ukubwa wa Tanganyika na udogo wa Zanzibar hauwezi kuweka uwiano mzuri wa kuweka msingi wa mfumo wa Serikali tatu.

Katika mfumo wa Serikali tatu ni dhahiri kuwa, Zanzibar kila mara itajikuta ikionewa/kulalamika na hivyo kero nyingi zaidi za Muungano kuzaliwa kulivyo ilivyo sasa chini ya mfumo wa Serikali mbili. Aidha, mfumo wa Serikali moja ndiyo mbaya zaidi utavunja Muungano siku ya pili yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudui kubwa zinazofanywa na Serikali katika kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali juu ya wananchi wanaoharibu mazingira hasa kwa kujenga nyumba katika maeneo yaliyokatazwa hasa kwenye fukwe za bahari na vyanzo vya maji, kwamba Serikali isipochukua hatua za makusudi kusimamia uvunjifu wa Sheria, Taifa hili litaangamia na kupoteza sura ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lazima Serikali iangalie ni juu ya kupunguza idadi ya mifugo mingi ambayo inaharibu mazingira ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima itoe maamuzi magumu juu ya kuangalia upya wa Sheria ya Mifugo kuzuru nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza mifugo ambayo kwa kiasi kikubwa inaharibu mazingira kwa kusababisha ufyejaji mkubwa wa misitu unaofanywa na jamii ya wafugaji, lakini ili

mifugo ipunguzwe, Serikali ianzishe Kodi ya Mifugo itakayosaidia kupunguza mifugo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Serikali kuwachukulia hatua kali wananchi wa Wilaya ya Mpanda wanaoishi katika Kata ya Katuma na Kata ya Mpanda Ndogo katika Kijiji cha Bugwe, watolewe katika maeneo ya vyanzo vya mito vilivyo vingi katika eneo hili. Ili kunusuru mazingira, tunaiomba Serikali ihakikishe wale wote waliopeleka mifugo katika maeneo haya, watolewe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni umuhimu wa kupanda miti. Ni muhimu sana kukawa na Sheria itakayotungwa kwa ajili ya kuhakikisha kila mwananchi anapanda miti.

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa na sheria, nchi hii itakuwa jangwa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi yake kwa mwaka 2013/2014 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi kubwa sana la uvunaji misitu nchini kiasi ambacho hatua stahiki zisipochukuliwa, nchi itabaki jangwa. Matumizi makubwa ni kwa ajili ya nishati za kupikia kwa maana ya kuni na mkaa. Ili kuondokana na tatizo hili, Serikali iweke mkazo katika matumizi ya nishati mbadala kwa maana ya gesi, *blogas* na umeme. Tunayo fursa kubwa sana ya kubadilisha matumizi ya mkaa kwa kutumia makaa ya mawe kutengeneza *briquettes* ambazo ni gharama nafuu na itaokoa matumizi mabaya ya misitu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi katika Mikoa ya Kusini, kwa maana ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani wananchi wanafanya kilimo cha kuhamahama. Hii inatokana na mbinu za asili kubadilisha mashamba kila msimu. Utaratibu huu unatugharimu sana kutokana na misitu

miti kupotea kutokana na kukatwa au uchomaji moto. Naishauri Serikali kuweka jitihada za makusudi kuelimisha wananchi matumizi ya viatilifu na namna ya kushiriki kilimo bora chenyenye ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zimenufaika na *carbon credits*, sijaona jitihada zozote za Serikali kuvuna mapato haya. Elimu ya kutosha itolewe ili wananchi wengi zaidi wanufaika badala ya kuziachia taasisi binafsi.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa hewa unapata madhara makubwa sana kutokana na uzalishwaji wa hewa ukaa za viwanda, magari na mitambo mingine. Serikali iweke mpango madhubuti kuthibiti *emission control* kwa kiwango kinachokubalika.

Mheshimiwa Spika, uvuvi wa kutumia mabomu umekithiri sana katika ukanda wa Pwani yote ya nchi yetu. Hili ni jambo la hatari sana, kwani linaharibu mazalia ya samaki, kuhatarisha mazingira ya bahari na viumbe wengine. Hatua kali zichukuliwe sambamba na elimu kwa wavuvi.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbolea za kemikali yaangaliwe upya, kwani yanachangia sana uharibifu wa mazingira na kuua viumbe wengine wa majini. Baada ya mvua kunyesha, mabaki yote husombwa na kuingia katika mito, maziwa na bahari. Pamoja na kuhitaji kuendeleza kilimo, ni heri pia tukaangalia umuhimu wa ustawi wa viumbe wengine wa majini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Waziri wa Mazingira pamoja na Waziri wa Maji wafike Bonde la Eyasi katika Halmashauri ya Karatu wapate kuona uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji. Ni muhimu sana kwa afya ya wakazi wa Bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Waziri wa Mazingira pamoja na Waziri wa Nishati na Madini wafike katika Halmashauri ya Karatu na waone uharibifu wa mazingira katika machimbo ya dhahabu ya *Murus-Endabash Gold Mining* na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa kuchukua hatua haraka, hilo ni janga kwa jamii hiyo.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo chanzo kikubwa cha kupata maisha kwa wananchi wengi hususan wanaoishi vijiji. Bahati mbaya katika utumiaji wa mbolea za chumvi chumvi wananchi hao wengi wao hawana utaalamu. Matokeo yake ardhi, kutokana na matumizi mabaya ya mbolea imekufa kiasi ambacho bila ya kutumia mbolea hakuna uzalishaji wa mazao katika ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, katika kukabili tatizo hilo la utumiaji wa mbolea za chumvi chumvi kiholela, inabidi wapatikane Mabwana Shamba wengi wapelekwe kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kero za Muungano, kinachokwamisha kero nzito kutotatuliwa ni Kamati zinazokutana kutatua kero hizo, hazipo kisheria, bali ni vyombo viro kwa matakwa ya wakubwa. Ipo haja kiwepo chombo cha kisheria kutatua kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Ahsante.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ni jambo jema sana kutunza mazingira, lakini kuna tatizo kubwa sana ambalo ni gumu sana kutekelezwa kama taratibu hazifuatwi na wala utendaji wa wahusika hawafuatilii, na hawatekelezi yale yanayoagizwa.

- (1) Kupanda miti hakujatiliwa mkazo.
- (2) Kulinda vyanzo vya maji hakujatiliwa mkazo wa kutosha na hakuna elimu ya kutosha ya kutunza mazingira. Hivyo basi, ni vyema elimu ya kutosha ikatolewa, ukizingatia

watu wamezidi. Maeneo mengi watu waliopo ni zaidi ya vyanzo nya maji. Hivyo kuna umuhimu sana Serikali kusaidia wananchi kwa kuwapatia maji ili vyanzo hivyo vilindwe na kwa maana hiyo uoto utaongezeka, utapata maji ya kutosha na hivyo kusaidia miti kustawi na hivyo kubadilisha hali ya hewa na hata kupata mvua.

(3) Mheshimiwa Spika, kuzuia watu wasikate miti ni suala jema sana, lakini ni ngumu kutekelezeka kwa sababu watu wengi zaidi ya asilimia 80 wanatumia kuni au mkaa. Serikali inaposema miti isikatwe, watu hawa wataishije? Ni ngumu sana kuzuia kukata miti bila nishati mbadala. Kama kweli Serikali inataka miti isikatwe, basi suala la umeme na gesi liliwe mkazo na lipewe uzito wa kutosha. Naamini hili likitekelezwa, tutakuwa tumeondoa tatizo la kukata miti. Bila hivyo, miti itakatwa tu.

(4) Mheshimiwa Spika, kuhusu Tabia nchi, nashauri Serikali itangazie Watanzania na kuelimisha watu kuwa majira yamebadilika, hivyo watu waweze kulima kwa wakati, maana majira yamebadilika mno, matokeo yake watu mwaka huu itakuwa njaa, maana mvua wamepishana nayo.

Hivyo, ni vyema mikakati ya kutosha ifanyike ya makusudi kuhakikisha kuwa wakulima wote wanajulishwa na wanapata vipeperushi, magazeti, TV na redio zifanye kampeni ya kuelimisha ili watu wapande mazao yao kulingana na muda wa mvua. Idara ya Hali ya Hewa ifanye kazi yake kwa makini na hata kufanya stadi za kutosha ili wakitabiri hali ya hewa na iwe hivyo.

**MHE. HAMADI ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa masikitiko makubwa kwamba kuna mambo mengi ambayo tangu tumeungana hadi leo Serikali bado imekuwa ikituambia mazungumzo, vikao, majadiliano, bado yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, mimi naona kwamba kuhusu jambo la kuyapatia ufumbuzi yale mambo ambayo ni ya msingi na ambayo ni kero kubwa hasa kwa Wazanzibari, mfano:-

- (1) Akaunti ya Pamoja Kati ya SMT na SMZ;
- (2) Mgawano wa Mapato;
- (3) Ushuru kwa Bidhaa zitokazo Zanzibari;
- (4) Uwiano kwa Watumishi; na
- (5) Uwiano wa Mabalozi nchi za nje na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka, Wizara inayohusika na Muungano ambayo ndiyo yenyewe jukumu la kuitisha na kusimamia vikao hivyo, inalazimika kufanya vikao viwili tu ili kujadili kero hizi. Vikao viwili havitoshi kwa umuhimu wa mambo yenye!

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia kwakuwa mambo haya ni muhimu sana na kwa kuwa kinachokwamisha vikao ni tatizo la bajeti ndogo kwa Wizara husika, ni vyema sasa Wizara ikaongezewa bajeti yake kwa mwaka huu ili vikao viongezeke na tuweze kupata muafaka juu ya matatizo haya ya msingi na ya siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa sasa wa kwamba Wizara hii inatumika kama bomba tu la kuitisha fedha zote zinazokwenda Zanzibar, hili linaonekana kama fedha za Wizara ni nyingi, lakini siyo kweli. Mfano:-

(1) Mwaka 2012 Fedha iliyopita katika Wizara ni Sh. 31,103,453,500/= kati ya hizo zilizopita katika bomba hili kwenda Zanzibar ni Sh. 30,423,054,500/= na Idara ilibakiwa na Sh. 860,000,000/= tu.

(2) Mwaka 2013 fedha iliyopitia hapa Wizarani ni Sh. 33,301,101,000/= na zilizokwenda Zanzibar ni Sh. 32,625,766,000/= na Idara ilibakiwa na Sh. 675,000,000/= tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na takwimu hiyo, lakini kikao kimoja kinagharimu Sh. 120,000,000/=, hivyo kufanya vikao hivi muhimu kuzorota. Kwa mwaka huu kuna ongezeko

dogo sana ambalo pia halitaweza kusaidia kufanyika vikao zaidi ya hivyo vya sasa. Naomba Serikali iongeze bajeti katika eneo hili ili kutoa fursa ya kuweza kufanya vikao zaidi ili kuweza kumaliza kero hizi za siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Akaunti ya Pamoja; Katiba ya mwaka 1977 ambayo ndiyo tunayoitumia hivi sasa, katika kifungu 133 imesema wazi kwamba pawepo na Akaunti ya Pamoja kati ya SMT na SMZ. Lakini hadi leo bado Serikali inaendelea kuvunja Katiba kwa kutotekeliza hili pamoja na Zanzibar kwamba imeshawasilisha mapendekezo yake, lakini kwa kuwa hakuna nia njema kwa SMT juu ya jambo hili, hadi leo miaka 46 sasa bado jambo hili linasuasua.

Mheshimiwa Spika, ieleweke pia kwamba kutofanyika kwa Akaunti ya Pamoja kunainyima Zanzibar haki zake, maana ile asilimia 11.5 ya *share* iliyotokana na iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki kama haki ya Zanzibar, ilikwenda Hazina na ndiyo iliyotumiwa kuanzisha *BOT*.

Hivyo basi, kwakuwa kodi, ushuru wa bidhaa na mapato yote yanayoingia pale *BOT*, Zanzibar inakosa fursa ya kuelewa kinachopatikana baada ya matumizi, lakini kwakuwa SMT haina nia njema kwa Zanzibar, bado haijataka na haiko tayari kulimaliza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Balozi za nje; tunazo balozi 31 Tanzania nchi za nje, lakini Wazanzibari ni wanne tu. Kama hili halitoshi, hata wafanyakazi katika Balozi hizo na ambao ni vijana watokao Tanzania, kwa vijana wa Kizanzibari ni kwa baadhi tu ya Balozi chache na idadi yao ni kama vile kikombe cha babu; ni mmoja tu wa dawa na sio zaidi ya watatu kwa baadhi ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, hili halishangazi, maana hata katika ile *Management team* ya Wizara inayoongozwa na Waziri na Naibu Waziri pia ina *Directors* 18 lakini pia Wazanzibari ni wawili, Naibu Waziri kwa nafasi yake na kwakuwa Zanzibar wana Ofisi yao, ndiyo maana wameona albu, wamempa Mzanzibari nafasi hiyo, yupo pale Bwana Simai Kombo Haji.

Mheshimiwa Spika, Mzanzibari anaposafirisha gari huku Bara kwa kazi zake na baadaye arudi na gari lake, analazimika aweke *bond*, lakini mgeni toka Uganda, Kenya, Ruanda, Burundi na kadhalika huyu hupewa kibali cha hadi miezi mitatu na hata zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili ni lingine kati ya mambo yanayomdhalilisha Mzanzibari katika Muungano wetu huu.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo undugu wa damu kweli!

Mheshimiwa Spika, Ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza, kwanini Bajeti ya Wizara ya Muungano ipo finyu sana? *Why?*

Mheshimiwa Spika, mfano, bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa Sh. 31,103,453,500/=, zilizopelekwa Zanzibar ni Sh. 30,423,054,500/= na kubakiza Shilingi milioni 680 kwa Idara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya bajeti kwa Idara ni Sh. 33,301,101,000/=, kati ya hizo zilizopelekwa Zanzibar ni Sh. 32,625,766/= na kuacha Shilingi milioni 675 tu kwa Idara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 bajeti ya Idara ya Muungano ni Sh. 747,710,000/= *OC* na Mishahara. Fedha hizi hazitoshii kabisa kwa Idara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwanini Idara hii haina mradi wa kuelimisha? Idara ina mpango gani wa kutafuta fedha za kutolea elimu ya Muungano? Kwanini Tume ya Mipango hajatoa kibali cha Idara ya Muungano kuruhusiwa kupewa fedha za kuelimisha?

Mheshimiwa Spika, je, maelekezo na ushauri wa *JFC*, kwanini unachelewa? Ili ijulikane *Formula* ya mgao wa Serikali zote mbili.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ajenda ya mazingira inakuwa kila siku na umuhimu wake kuongezeka sana.

Mazingira sasa ndiyo maisha, maana yake ni kwamba binadamu ambaye ndiye mtawala wa viumbe vyote analo jukumu kubwa la kuhakikisha siyo tu uhai wake, lakini pia uhai wa viumbe vyote na kwa ujumla uumbaji wote ikiwemo mimea pia.

Mheshimiwa Spika, nimeziona kazi zilizofanywa na Ofisi ya Mazingira katika sehemu mbalimbali za nchi. Ni kazi njema na zinatafaa sana, zisambae nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa vile gharama ya Vijiji vya Mfano vya Hifadhi ya Mazingira (*eco villages*) sasa umepewa fedha, basi naiomba Wizara ihusishe pia Tarafa za Namswea Kigonsera na Hagati Wilayani Mbanga, Jimbo la Mbanga Magharibi. Mradi huu uhusishe vijiji vyote katika Kata hizo.

Mheshimiwa Spika, wananchi katika maeneo hayo ni wakulima. Miti inakatwa na pia kilimo cha milimani kinafanyika sana. Bila shaka katika misitu ya Tarafa ya Namswea na Kigonsera Vijiji kama Kuanda, Ntunduwao, Ukombozi, Amani, Mahoro, Litumbandyosi, Kuigili, Kihindi inafaa sana kwa kuanzisha ufugaji wa nyuki, hivyo mizinga inahitajika.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya milimani kama Maguu, Langiro, Litembo, Mkumbi, Mfangamao, Kitumbilumo, Ngina wanacho kilimo cha Ngolo ambacho kinahifadhi maji. Kilimo hiki kinapaswa kupewa nguvu na naiomba Wizara itume wataalam wake ili waone njia bora zaidi ya kukiboresha na kukifanya endelevu kwa hali ya sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Mbanga iwemo pia katika miradi mbalimbali kama programu ya ushirikishwaji wananchi katika usimamizi wa hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Makaa ya Mawe Ngale, mradi huu ni wa uchimbaji wa makaa ya mawe kwa

ajili ya kuzalisha umeme na kuuza. Pia mradi umeanza na mkaa umesafirishwa kwa malori toka eneo la mradi Ntunduwao kwenda amani Makoro na Ndembii (Nyasa). Magari haya yanababishi vumbi sana kwa wananchi wanaoishi kando ya barabara ya Kitai – Lituhi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile mradi ni muhimu kwa Taifa, naiomba Wizara kufanya tathmini juu ya madhara ya vumbi na shughuli nydingine za mradi ili kuona namna ya kuondoa athari hizo. Vumbi kwa mfano suluhisho lake ni kujenga barabara ya lami. Hivyo, Serikali na mwekezaji wanawenza kushauriwa ipasavyo ili kuchukua hatua za kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutembelea mradi huu pia kutawapa nafasi ya kuangalia maeneo mengine ya kimazingira na kushauri Serikali, wananchi na wawekezaji ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwa nini Serikali isiimarishe upandaji wa miti ya asili ili kulinda mazingira? Hili lipewe kipaumbele kulinda miti na uoto wa asili kama Mto Mara amba mazingira yake yameharibika kwa kiasi kikubwa na kusababisha mafuriko makubwa kama yanayoendelea sasa na kusababisha mbuzi 1,000 na ng'ombe zaidi ya 600 na mtu mmoja kufariki Wilayani Serengeti.

Pia kuna mimea iliyozuka, magugu pori ambayo yameenea eneo hilo la Ukanda wa Mto Mara, Wilaya ya Butiama, Bunda, Serengeti na yameanza kuvamia Hifadhi ya Taifa ya Serengeti!

Nashauri Serikali ichukue Mto Mara kwa ajili ya kuimarishe na kulinda mazingira. Pia Mto Mara kuna miti mizuri ambayo haipatikani sehemu nydingine nchini na kuna nyati, maji, viboko na mamba; hivyo, Serikali itayariske sheria ili Ofisi

ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii washirikiane katika hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Mazingira ya Vitongoji, Vijiji na Kata ziimashirwe na kuundwa katika maeneo ambayo Kamati hizi hazipo.

Mheshimiwa Spika, “e”- Waste Management ni vizuri elimu hii ifundishwe kwa kina na utupaji taka wake usimamiwe kwa vile ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu yafuatayo:-

(i) Kwa nini Maafisa Mazingira hawapo katika Wilaya? Ni vizuri Maafisa hawa kwa taaluma zao waajiriwe kwa makusudi.

(ii) Je, Serikali ina mpango gani ili kudhibiti magugu maji katika Ziwa Victoria na pia kuzuia mafuriko katika Mto Mara?

(iii) Serikali inalinda vipi Mazingira ya Hifadhi za Taifa ikiwemo ya Serengeti?

(iv) Je, utupaji taka katika hoteli zilizo mbugani unasimamiwa vipi ili kudhibiti na kulinda mazingira?

(v) Serikali inadhibiti vipi meli ambazo zinatupa taka katika Bahari iliyo kwenye mipaka ya nchi zetu na taka nyiningine ni za sumu?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Ghalib Billal, Makamu wa Rais, kwa kazi kubwa anayofanya. Nawapongeza Mawaziri wote katika Ofisi yake; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga na Mheshimiwa Charles Kitwanga, kwa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kero za Muungano zimeongezeka sana ndani ya Bunge hili. Kasi ya

kutatua kero hizo hairidhishi na kuonekana kuwa Serikali ya Muungano haiko *serious* kutatua kero hizo. Naomba na nasisitiza Serikali ifanye maamuziju ya kero hizo; kwa mfano, suala la mafuta na gesi , suala la magari ya Zanzibar yanapoletwa Tanzania Bara pamoja na bidhaa nyingine iliyokwisha lipiwa kodi Zanzibar. Vilevile suala la kujunga na IOC.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kuna jitihada zinaendelea za kudhibiti na utunzaji mzuri wa mazingira, bado jitihada zaidi zinatakiwa kufanyika. Suala la ukataji miti hovyo bado ni tatizo hasa maeneo ambayo wanakaa Wananchi wenye utamaduni wa kukata miti hovyo kwa sababu ya kuhamahama hasa wanaotoka Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita na Simiyu. Nashauri ifanyike Kampeni Maalum ya kutoa Elimu kwa Wananchi wa Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walio wengi wanatumia kuni kama nishati kwa maisha yao. Ingawa suala la nishati mbadala limezungumzwa sana, lakini bado matokeo ya jitihada za matumizi ya nishati hazijaonekana.

Mheshimiwa Spika, *contradiction* iliyopo ni kuwa gharama za umeme zipo juu; hivyo, Wananchi walio wengi pamoja na wenye uwezo, wanalazimika kutumia mkaa kwa matumizi ya nyumbani ya kila siku, kama tupo *serious* gharama za umeme hazina budi kuteremshwa. Aidha, jitihada zaidi zifanywe za kuhakikisha miti mingi inapandwa kwa kutumia vizuri Siku ya Upandaji Miti.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pesa inayotolewa kwa Wizara hii haiwezi kupambana na changamoto kubwa sana za uharibifu wa Mazingira hapa nchini. Nchi zote Duniani, suala la mazingira limepewa uzito mkubwa sana na wanatenga fedha za ndani za kutosha kutunza mazingira na kupambana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kilio cha Wananchi kila kona kuhusu tatizo la maji, Mito imekauka, mabwawa yamekauka *pressure* ya maji hata kwenye mabomba inapungua kila leo, ni kutokana na kuharibiwa kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanalima hadi milimani kwenye vyanzo vya maji, miaka yote wanalima jirani kabisa na vyanzo vya maji vya karibu na Mito, hawafuatiliwi na sheria ichukue mkondo wake. Leo hata kilimo chetu hakina uhakika kutokana na mvua kuwa chache na hata misimu ya mvua imebadilika.

Mheshimiwa Spika, kilio cha miti inayokatwa kona zote kwa ajili ya mbaao, mkaa, kuni na magogo pasipo kupandwa miti hakijasikika. Tatizo la uchomaji wa mkaa Serikali imeshindwa kulishughulikia kabisa. Misitu inateketea kwa uchomaji wa mkaa na Serikali inajua vizuri, asilimia 80 ya watu wanaokaa mijini wanatumia mkaa.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kushindwa kuwa na uhakika wa nishati mbadala hapa nchini kwa matumizi ya nyumbani ni hatari sana. Leo ni zaidi ya miaka kumi tangu tuanze kusikia suala la makaa ya mawe kuwepo ndani ya nchi yetu tena kwa wingi. Kwa nini makaa ya mawe hayatumiki?

Mheshimiwa Spika, umeme ni ghali, gesi ghali, mafuta ya taa ni ghali na watu lazima wapike wale.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe majibu ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa kwa viwanda vinavyokwepa kutumia umeme kwa uzalishaji na badala yake wanatumia magogo na kuni zaidi ya tani kumi kwa siku wakati hawana shamba la miti? Kiwanda cha nguo cha Morogoro cha Mheshimiwa Mbunge furani humu ndani kinatumia magogo kwa miaka yote na Serikali inalijua hilo; kwa nini hakifungwi? Naomba jibu. Kiwanda cha *A to Z* cha kutengeneza *net* kilichopo Arusha kinatumia magogo na Serikali inajua imetulia.

Mheshimiwa Spika, Serikali na nchi yoyote lazima viendeshwe kwa sheria, suala la watu wenye uwezo kulelewa wavunje sheria za nchi kwa sababu wana pesa nydingi halikubaliki hata kidogo. Wale wote waliovunja sheria za nchi na kujenga maeneo yaliyokatazwa na sheria, nyumba zao zivunjwe.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya ufukweni mwa bahari ni ya Watanzania wote kuyatumia kwa kuburudika, kustarehe na kupumzisha akili. Serikali imeyauza maeneo yote ta Fukwe za Bahari ya Hindi upande wa Dar es Salaam, watu wamejenga hadi kwenye kingo za bahari.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleze Bunge ni kwa nini Watanzania wanatozwa pesa na wamiliki wa maeneo ya ufukweni pale wanapotaka kutembelea fukwe hizo; hata kama unataka kupiga picha baharini unatakiwa kulipia kwanza ndipo uruhusiwe?

Mheshimiwa Spika, ni haki gani aliyonayo mfanyakishara kutosa fedha kwa Watanzania kuangalia maeneo au mandhari ya bahari iliyo ndani ya nchi yao?

Mheshimiwa Spika, Viongozi wakubwa na wengine ni Wabunge, ndiyo waliomilikisha na kujimilikisha maeneo ya fukwe. Wengine wameshindwa kuyaendeleza yamekuwa vichaka na Serikali inayaona. Je, Serikali imekosa meno?

Mheshimiwa Spika, mifuko ya nailoni imeongezeka na kuwa kero kila kona. Mwaka 2007 Serikali iliweka *size* ya mifuko inayotakiwa kutumika na kuongeza ushuru wa *material* za kutengeneza mifuko na hata kwenye mifuko yenye; leo lile agizo limefia wapi au ndiyo Serikali imewekwa kwenye viganja vyta wafanyabiashara?

Mheshimiwa Spika, tukifanya suala la Mazingira ni siasa, nchi itakuwa jangwa. Serikali iwajibike kikamilifu na hakuna aliye juu ya sheria.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Nchi, Muungano - Mheshimiwa Samia Sululu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa - Waziri wa Nchi, Mazingira, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye lengo kuleta ufanisi bora kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, mazingira ya nchi yetu yameharibu na kukausha vyanzo vya maji kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kuwepo kwa miti aina ya mikaratusi inayofyonza maji kwa kiasi kikubwa, kulima kwenye vyanzo vya maji na kuchungia mifugo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kutoa kauli ya utawala kwamba; miti aina ya mikaratusi ivunwe na kupanda miti mbadala ambayo haina athari; kuagiza Halmashauri zote nchini kuainisha vyanzo vya maji na kupiga marufuku Wananchi wasilime wala kuchungia mifugo maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa upandaji miti wa kila mwaka ni mzuri sana, bali bado hakuna usimamizi madhubuti kwa Serikali ili siku hiyo kila kaya kutekeleza mpango huu kwa kupanda idadi ya miti iliyotangazwa na Serikali kwa lengo la kurutubisha nchi yetu na kuondoa ukame wa mvua. Vilevile agizo hili la kupanda miti liwe endelevu kwa kipindi chote hasa masika.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, bado kuna tatizo la Wananchi kuchoma mkaa au kukata kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Hili tatizo ni kubwa sana, kwani bado hakuna nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani hususan vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuziagiza Halmashauri nchi nzima kutoa elimu ya nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kwani nishati ninazoelezwa na Serikali, Wananchi hawajui na hata namna ya kuzipata nishati hizo, hivyo ni muhimu sana kutoa elimu kwa wananchi ili waache kuchoma mkaa na kukata kuni kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana la matumizi mabaya ya mifuko ya lambo. Matatizo haya yanatokana na watumiaji kutupa ovyo na kusababisha mazingira kuwa machafu. Vilevile madhara mengine ya mifuko hii ya lambo ni kwenye mifugo inapokula hufa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshindwa kudhibiti utupaji wa mifuko ya lambo, ni bora kupiga marufuku viwanda kutokutengeneza mifuko ya lambo tena, watengeneze mifuko mbadala ili kuondoa kutapakaa kwa mifuko ya lambo nchini kote na pia kuinusuru mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa la ukusanyaji wa takataka majumbani kwani hakuna utaratibu mzuri wa Halmashauri zetu kukusanya; hivyo, Serikali iangalie upya kila Halmashauri utaratibu madhubuti uwekwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Migogoro yote inayohusu Muungano inatokana na kutokuelewa hasa nini tafsiri ya Muungano, hasa kwa upande wa Tanzania Bara, kwa Wananchi walio wengi kutokuelewa Muungano. Tena bahati mbaya sana wengine ni Wabunge, tena Viongozi wa Upizani, kwa kutoa kauli kuwa Wazanzibari hawapaswi kuingia katika Bunge la Katiba!

Mheshimiwa Spika, Muungano ni wa nchi mbili; Zanzibar ikaamua jina lake libakie na Watanganyika wakaamua mambo yao wakayaingiza kwenye Muungano. Mzanzibari ana haki katika Jamhuri ya Muungano na pia ana haki za Zanzibar, lakini Mtanzania ana haki katika Jamhuri ya Muungano tu, hana haki katika Tanganyika maana haipo.

Leo imefikia hadi kwenye Bunge la Tisa kuna Mbunge wa Kanda ya Ziwa alihoji kwa nini Geita kuna watu milioni moja na kidogo, inawakilishwa na Wabunge watatu, lakini Zanzibar ina watu milioni moja na kidogo pia inawakilishwa na Wabunge hamsini. Hii yote inatokana na watu wetu kutokuuelewa Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *Article of Union* ni mambo 11 yale ya mwanzo, Bandari ilikuwa ni sehemu ya

Muongano, lakini Bandari zote zaidi ya 13 za Bara haziendeshwi Kimuongano na hakuna gawio lolote katika Bandari za Dar es Salaam kwenda Zanzibar.

Bahati nzuri kuna mabadiliko ya Katiba sasa, tutapata ufumbuzi wa masuala yote yaliyokuwa hayaendesheki Kimuongano yatatolewa ikiwemo mafuta na gesi.

**MHE. CECELIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, changamoto za Muungano zimeelezwa kuendelea kuongezeka, hakuna jitihada za kuzitolea maamuzi kwa kuangalia unufaika wa nchi mbili kwa maana ya Bara na Visiwani. Hata hivyo, mchakato wa upatikanaji wa misaada na mikopo ya bajeti kwa SMT na SMZ unafanyiwa kazi na wataalam (hii ni kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 7). Ni ukweli kuwa utegemezi wa bajeti, siku zote umekuwa ni kikwazo kwa maendeleo ya nchi yetu.

Tanzania ni nchi yenyeye rasilimali nyingi sana, ni lazima tufike mahali Serikali iache dhana ya utegemezi na iongeze na kusimamia kwa dhati mapato ya nchi kwa kudhibiti matumizi mabovu ya fedha zinazopatikana, ikiwa ni pamoja na kuangalia vipaumbele vichache vyta kimaendeleo ili kuwa na ufanisi uliokusudiwa wa kuwalettea Wananchi maendeleo sahihi kulingana na mahitaji yao na kwa wakati. Hata hivyo, ni wakati sasa wa kutatua masuala haya kwa mujibu wa Katiba, yaani Mahakama ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaeleza kuwa mgawanyo wa mapato yatokanayo na faida ya Benki Kuu yatatolewa. Hata hivyo, ni wakati mwafaka sasa wa mgawanyo huo kuangalia idadi ya watu kwa pande zote za Muungano, kwa maana ya Tanzania Bara yenyeye idadi kubwa ya watu na Tanzania Zanzibar yenyeye idadi ndogo ya watu. Hili haliwezi kukwepeka, ni vyema lizingatiwe na Wananchi waelezwe kwa uwazi ili kuondoa manung'uniko yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Muungano inaeleza kuwa masuala ya Muungano yenyeye changamoto yatatatuliwa na Mahakama Maalum ya Kikatiba. Hata hivyo,

mpaka leo Mahakama hii haijawahi kuitwa na kufanyia kazi changamoto hizo. Serikali itueleze ni lini sasa Mahakama hii Maalum itaitishwa na kuyafanya kazi ili kuondoa kiitwacho kero za Muungano. Tunaitaka Serikali itoe majibu ya kina kuhusu hili la Mahakama Maalum.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yenye Mazingira mazuri na ya kupendeza. Hata hivyo, Serikali na Wananchi wake bado hatuthamini na kuyatambua haya, kwani bado Mazingira hayatiliwi mkazo na Serikali kwa kutenga bajeti ya kutosha katika suala la Mazingira na pia Wananchi wenyewe hawatambui umuhimu wa suala la Mazingira na athari yake katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya nchini zimekuwa na tatizo la kutoliona suala hili la Mazingira ni muhimu. Kwa kuwa mamlaka hizo ndizo zenye Wananchi; hivyo, ni wakati sasa Halmashauri za Wilaya kuwa na mikakati inayoendana na bajeti zao ili kwa pamoja na Serikali Kuu kutoa elimu ya Mazingira kwa Wananchi na athari zake.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wa Wizara zote mbili zilizo chini ya Ofisi hii, kwa utendaji wao wa kazi hususan kazi zenye changamoto kubwa hasa katika kipindi hiki.

Ofisi ya Waziri anayeshughulikia Muungano, ina changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa Muungano wetu hauyumbishwi na Wanasiasa uchwara, wanaoupinga Muungano wetu kwa maslahi yao binafsi. Ofisi ya Waziri anayeshughulikia Mazingira nayo ina changamoto kubwa ya kuhakikisha Mazingira yetu yako salama.

Mheshimiwa Spika, sina shaka juu ya Muungano wetu ambao umedumu karibu nusu karne tangu ulipoasisiwa na Waasisi wa Muungano huu; yaani Mzee Nyerere na Mzee Karume. Ni ukweli usiopingika kuwa, Muungano huu umekuwa ni mfano wa kuiga katika Bara la Afrika na hata Dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa hizo zote zilizopelekea Muungano wetu uwe thabiti na mfano wa kuigwa, bado kuna kero ndogondogo ambazo bado zinahitaji kutatuliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Baraza la Mitihani la Taifa lilianzishwa kwa mujibu wa kutahini Wanafunzi wa Tanzania (Tanganyika na Zanzibar), ingawa Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Chini siyo suala la Muungano. Ni dhahiri kuwa kumekuwepo na malalamiko hasa upande wa Zanzibar kuhusu Baraza hili; hivyo, napendekeza kuwa Zanzibar pawepo pia chombo kama hiki, yaani Baraza la Mitihani la Zanzibar (BAMIZA), kikiwa na jukumu la kutunga, kutahini na kusahihisha mitihani yote ya Zanzibar toka elimu ya awali, msingi, sekondari, hata ngazi za stashahada. Baraza la Mtihani la Taifa (BAMITA), lipewe jukumu la kutunga, kutahini na kusahihisha mitihani yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utoaji ushuru katika pande zote mbili haqidhishi. Inavyoonekana hii ni kero kwani bidhaa zinazoingizwa Zanzibar zinatozwa ushuru kidogo na pindi zikiletwa Tanzania Bara zinatozwa ushuru wa ziada. Hivyo, ili kuondoa kero hii naishauri Wizara hii ishirikiane na TRA (Wizara ya Fedha) ili kuona ni namna gani ya kuondoa kero hii na hasa lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa pande zote mbili zinaridhika na mfumo huu wa utoaji wa ushuru.

Mheshimiwa Spika, changamoto nytingine ambayo ni kero ya Muungano ni mgawanyo wa mapato yanayotokana na misaada kutoka nchi za nje. Sehemu ya pili ya Muungano hasa Zanzibar inalalamikiwa suala hili; hivyo, naishauri Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa kushirikiana na Waziri wa Wizara husika, wahakikishe kuwa wanashughulikia suala hili na kuhakikisha kuwa linapatiwa ufumbuzi. Serikali ihusishe Wizara ya Fedha na Wizara ya Mambo ya Nchi ya Nje kwa pamoja zishughulikie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanaitwa Mambo ya Muungano na Mambo yasiyo ya Muungano. Hili suala la rasilimali, napendekeza liwe la Muungano ili kuleta

umoja na mshikamano katika nchi. Hivyo, masuala ya gesi, mafuta, uvuvi, madini, hifadhi na kadhalika, viwe ni vitu vya Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajibu maswali yafuatayo:-

(i) Je, anafahamu wazi kuwa uchafuzi wa Mazingira ya Mto Tigite Mkoani Mara, Wilayani Tarime, katika Mgodi wa *North Mara* Nyamongo bado ni kero kubwa kwa Wananchi wa Tarime?

(ii) Je, watu walioathirika kutokana na maji hayo machafu watalipwa lini fidia?

(iii) Je, hadi sasa Serikali imechukua jukumu gani kuhakikisha kuwa Wananchi wa Nyamongo wanapata maji safi na salama?

(iv) Je, Serikali ilichukua hatua gani za kinidhamu dhidi ya Mgodi wa *North Mara*?

(v) Je, mazingira wanayoishi watu wa Vijiji vya Nyamwaga, Nyakunguru, Genkuru, Nyangoto na vingine vyote vinavyozunguka mgodi yanawakilisha nini katika Wizara hii?

(vi) Baraza la Mazingira la Taifa (*NEMC*) limelishughulikiae suala la Mto Tigite hadi sasa?

Mheshimiwa Spika, Mto Mara uliopo Mkoani Mara ni tegemeo kubwa sana katika Wilaya za Tarime, Serengeti, Ranya, Musoma na Butiama. Mto huu unatishiwa na magugu pamoja na tope toka Ziwa Victoria. Mto huu umevamia Vijiji vya Nkerege (Tarime) na kumeza vijiji vingi katika Wilaya ya Butiama. Hata hivyo, wafugaji na wavuvi wamekosa riziki kutoka Mto huu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajibu maswali yafuatayo:-

- (i) Je, Wizara inasema nini juu ya hili?
- (ii) Je, *NEMC* wamelishughulikia vipi suala hili?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu sahihi. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri. Nakupa dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**  
Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nitajaribu kujibu maswali mengi hasa yanayohusu mazingira kwanza kwa kuelezea chanzo hasa kwa nini tunaharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, mazingira yanaharibika kwa sababu binadamu anataka kupata maendeleo. Binadamu anataka kupata maendeleo kwa kufanya shughuli mbalimbali katika eneo alilopo, ndiyo sababu Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ikalitambua hilo na ikatoa ufanuzi wapi binadamu wanakaa. Binadamu wanakaa katika Mitaa, binadamu wanakaa katika Vijiji. Kwa namna hiyo basi, mpangilio wa uongozi na utawala katika nchi yetu ukaweka Halmashauri za Miji na ukaweka Halmashauri za Wilaya kwa Sheria Na. 7 na Sheria Na. 8 zilizoanzisha Halmashauri hizi mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, sasa katika Sheria hizo kuna mambo au kuna vifungurasi vinavyoelekeza ni namna gani Halmashauri zetu zinaweza zikatunza mazingira haya. Ukiangalia katika kifungu Na. 148(1) cha Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 kinaelekeza ni namna gani Halmashauri zetu za Wilaya zinaweza zikatunga Sheria ndogo ndogo ambazo zitatusaidia katika kudhibiti uharibifu wa mazingira pamoja na Sheria ndogo ndogo nyininge.

Kwa hiyo, kama sisi Waheshimiwa Wabunge ambaa ni Wajumbe wa Halmashauri hizi katika Mabaraza ya

Halmashauri hizi tutasimamia vizuri, basi tutakuwa tumepongua sana suala la uharibifu wa mazingira kwa sababu mazingira yanaharibiwa na wakaazi huko chini kabisa katika vijiji yetu na Mitaa yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Sheria ya Mazingira ukiantgalia kifungu cha 114 mpaka 132 vinatoa maelekezo namna ya kuzuia na kudhibiti uharibifu wa mazingira. Sasa ni vyema wote kwa pamoja tukalielewa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufanuzi huo niende moja kwa moja katika hoja ambazo Wabunge wengi wamezungumzia. Hoja ya kwanza ni ya upandaji miti na uharibifu wa mazingira, wengi wamezungumzia na wasemaji wa mwisho wamezungumzia ikiwemo na pamoja na mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hiyo hiyo niliyosema ya watu kujitafutia maendeleo wanakata miti, wanatengeneza mkaa ili wajipatie kitu chochote.

Sasa ni wajibu wetu kuwa na mipango mkakati katika kila eneo ili kuhakikisha kwamba utafutaji wa maendeleo unakuwa na mpangilio ulio sahihi. Ni kwa namna gani basi tutafanya hivyo. Cha kwanza ni lazima tuiwekee mikakati pamoja na Serikali kwa kuititia Wakala wa Kuhifadhi Misitu, ina mpango mkakati wa upandaji wa miti na lakin na sisi tumetoa maelekezo ya kwamba tuweze kupanda miti ya kutosha angalau miti 1,500,000 kwa mwaka. Sasa tusimamie hilo wote kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba uoto wa asili unatunzwa. Hii ipo katika Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira wa Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006 ambao Waheshimiwa Wabunge wengi tunaufahamu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nitalizingumzia ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni hii sheria yetu na hizi mita 60 katika mito, maziwa na bahari. Wengi wanasema Sheria hii imepitwa na wakati na wananchi wanazuiwa kufanya shughuli zao za kibiashara katika maeneo.

Kwanza, niseme kwamba wananchi hawazuiwi. Nia hasa ya sheria hii ya mita 60 ni kutoa nafasi kwa raia wote kuweza kuwa na uwezo wa kufikia bahari, kufikia mito, kufikia maziwa yetu tuliyonayo. Sasa kama katika mita 60 hizi kutakuwa na mtu amejenga na anaendeleza shughuli zake maana yake ni kwamba raia mwininge ambaye angependa kwenda *beach* hataweza kufika kule.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao wameshauri kwamba Sheria hii imepitwa na wakati, tuliangalie kwa namna hiyo. Lakini haitukatazi, kama tunaona hii sheria kweli imepitwa na wakati, hatutaki tena kwenda kuogelea, watu wajenge mpaka baharini, basi iletwe hapa na Serikali ipo itasikiliza ione namna ya kubadilisha hii sheria. Lakini nia yake kubwa ni kuwawezesha wananchi wote waweze kuwa na nafasi ya kufikia kwenye bahari.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala la Usimamizi wa Sheria. Wizara inaweka sera, inaweka sheria na inatunga kanuni. Halafu kanuni hizi na sheria hizi zinazipa mamlaka mbalimbali zilizo karibu kabisa na wananchi kuweza kusimamia, na usimamizi unafanyika. Mmetuona tukishughulika tukienda katika sehemu mbalimbali, kwenye mahoteli na viwanda, lakini sote kwa pamoja tutafanya kazi kama Watanzania wenye nia ya kuhifadhi mazingira yetu, tuatekeleza wajibu wetu kupitia kwenye Halmashauri zetu, kupitia kwenye Vijiji vyetu na Kata zetu, nina uhakika kabisa tutawenza kudhibiti na kuhakikisha kwamba mazingira yetu tunayalinda.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tutakaporudi baada ya Bunge hili, tuhamasishe na tuelewe kwamba tuna wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira yetu. Shughuli zetu za kujiletea maendeleo zisiwe ndiyo chanzo cha kutufanya sisi tuharibu mazingira yetu na maendeleo yetu sijui tena tutayafanyaje. Kama tutakuwa na mazingira mabaya, basi maendeleo yetu na yenye yatakuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kengele imeshalia, nitoe tu pole kwa wananchi wa Jimbo la Misungwi, kwa mafuriko makubwa yaliyowapata pamoja na ajali kubwa iliyotokea na kuleta hasara kubwa sana, pamoja na kuumiza watoto wa Shule ya Sekondari Kasololo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), dakika 25.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na majanga ya mafuriko, Simiyu na kandokando ya mto Mara kwa sababu mafuriko hayo yamesabibisha upotevu wa watu. Kwani kuna vifo vimetokea, lakini vilevile kuna mali zimepotea kama vile mifugo; mbuzi na vitu vingine. Kwa hiyo, natoa pole sana.

Baada ya kusema hayo, naomba nijibu moja kwa moja hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nami niungane na Naibu Waziri kujibu hizi hoja. Naanza na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi na Maliasili pamoja na Mazingira.

Hoja ya kwanza inasema, Serikali itenye fedha za kutosha, hoja hii imejadiliwa kwa kina na nadhani Serikali imeshalisikia hilo na sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tutaendelea kufuatilia.

Hoja ya pili, vilevile iongeze bajeti, tunapokea ushauri. Hoja ya tatu, Serikali itekeleze agizo lake la kusimamia kanuni za kudhibiti matumizi ya mifuko ya *plastic*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuarifu Bunge lako Tukufu kwamba suala hili tumeshalfanyia kazi kwa kina. Tulikuwa na Mikutano na Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Mazingira pamoja na Maliasili. Tulijaribu kuleta mifuko mizito ya *plastic* kutoka Dubai na tukaipeleka kwenye viwango *TBS*, ambapo wao walikubali kwamba inaweza ikafanyiwa *recycling*. Lakini tulipopeleka kwenye Kamati ya

Mazingira, walikataa na kwamba hili suala halikubaliki, nadhani mlisikia kwenye vyombo vya habari. Lakini siyo hivyo tu, tulikuwa na Mikutano miwili na Wakuu wa Mikoa, nao wame-raise concern kwamba hawalikubali.

Kwa hiyo, sisi tukaenda hatua zaidi, kwa sababu wale wenye viwanda hivi vya mifuko ya *plastic*, wamepeewa kuendeleza kwa sheria. Hivyo, inabidi tufuate sheria na ilibidi niwasiliane na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naye anafanyia kazi, na amewapa wataalam. Vilevile tutawasiliana na Mwanasheria Mkuu ili aweze kutupa maelekezo ambayo yatatusaidia tusije tukagongana na sheria za nchi hii. Kwa hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais inalifanyia kazi kwa nguvu sana suala hili na wote tunajua kweli mifuko ya *plastic* inachangia uchafuzi mkubwa, lakini katika utekelezaji lazima pia tuwe makini ili tusikiuke taratibu na sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, suala linalofuatia, Serikali ihamishe usafi. Naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, suala la usafi ninyi ni mashahidi, mmeshaona tukihangaika na tumeshaanza kutekeleza na tumeshafanya Semina na Wakuu wa Mikoa kuhusu Sheria ya Mazingira inavyotakiwa kutekelezwa kwenye Halmashauri na sasa hivi Wakuu wa Mikoa napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa kazi nzuri walioanza kuifanya.

Hata ninyi Waheshimiwa Wabunge mkitoka Dar es Salaam kuja Dodoma, mnakuta kuna Mikoa imeshaanza kufanyiwa usafi. Kwa mfano, Mkoa wa Morogoro, wameshaanza kusafisha, Mkoa wa Pwani wamesafisha, sehemu zilizobaki ni chache sana, hata Dar es Salaam wamesafisha.

Naomba kwa wale watakaokuwa Dar es Salaam terehe 26 naomba mshiriki, kuna *NGO* imeamua kufagia *Bagamoyo Road*, kutoka *Surrender Bridge* mpaka kwenda kwenye mpaka wa Dar es Salaam na Pwani. Tumeshawasaidia vifaa na *NEMC* itasimamia kwa bidii sana. Kwa hiyo, hili suala linafanyiwa mkakati kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja anayekwenda kwenye Jimbo lake, tusaidiane kwa sababu Tanzania ni yetu sote na tupo hapo wote kusaidiana kulinda mazingira salama. Kwa hiyo, naomba sana tunapokwenda kwenye Majimbo yetu, tusaidiane kwenye Halmashauri zetu kuhakikisha usafi unatekelezwa.

Suala lingine, ni kuhusu sera ya mabadiliko ya tabia nchi, kwamba ianzishwe. Ni kweli kwa sababu ni kitu muhimu sana sasa hivi, na ni *topic* ambayo ni ya kwanza kabisa kimataifa. Lakini Ofisi ya Makamu wa Rais tayari inayo mikakati ya mabadiliko ya tabia nchi. Mkakati huu umeshaandaliwa.

Kipaumbele kilichopo sasa hivi ni utekelezaji wa mkakati huu ambao unaelezea hatua mbalimbali za kuchukuliwa. Siyo hivyo tu, Ofisi inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997, ambapo masuala ya mabadiliko ya tabia nchi yatazingatiwa. Hizo zilikuwa hoja za Kamati.

Hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani, hoja ya kwanza inasema ukosefu wa mipango na mikakati ya kutafuta nishati mbadala. Tumekuwa hatufanyi, hatuna mpango wowote na kwa kweli lugha iliyotumika siyo nzuri sana na inaibua hisia za watu; lakini mimi kama Mwakilishi wa Serikali, ni jalala napokea, lakini napenda kusema tu, mnyonge mnyonge, lakini haki yake mumpe.

Mheshimiwa Spika, tumefanya mambo mengi hapa ili kusaidia mkakati huu wa kupata miti ya kutosha kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa. Kama unavyojuu, Serikali hajakataza kwa sababu tunajua nishati pekee tunayoitumia nchini mwetu ni kuni na mkaa. Lakini tunachosema, tutumie njia ambazo zinatufanya tutumie kuni na mkaa kidogo.

Mkakati mwengine, upo makakati wa Kitaifa wa upandaji miti. Kuna tuzo ya Rais ya Upandaji Miti, imetolewa mwaka 2010 na imetolewa mwaka 2012 na itatolewa tena mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, naomba Mikoa yote na Majimbo mjiunge kwenye tuzo hii ya upandaji miti inayotolewa na Mheshimiwa Rais ili tuweze kupanda miti mingi sana kwenye Majimbo yetu na hatimaye Mikoa na nchi nzima. Hiyo tuzo ni kitu muhimu sana. Hiyo yote, tumeanzisha mashindano ili kuhamasisha watu, kaya mbalimbali, Halimashauri, na sehemu zote za Serikali tunahimiza tushiriki. Kwa sababu tumeshaona kwamba, miti inayopandwa ni kidogo sana, lakini tunaohitaji miti ni sisi wote, pamoja na sisi tuliomo humu ndani.

Kwa hiyo, wote tushirikiane, tuhakikishe angalau kila mmoja kwa mwaka apande mti mmoja. Lakini siyo hilo tu, tayari tumeshawasiliana na Wizara ya Elimu, kuna mtaala ambao uko mashulenii utakaoshughulikia kuwafundisha watoto upandaji wa miti. Tuna tuzo ya Makamu wa Rais ambayo inaanza mwaka huu na itaanzia shule ambayo mwaka jana, wakati wa tuzo ya Mheshimiwa Rais ilipata zawadi, Shule ya Kameu Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara.

Kwa hiyo, Wiki ya Mazingira Duniani ambayo inaanza tarehe 1 Juni mpaka kilele chake tarehe 5, Makamu wa Rais atakwenda kule kuwapa zawadi, kwa sababu hawa walipanda miti mingi sana iliyosababisha kuwe na mawingu mengi au ukungu ambao wanavuna na wanapata maji ya kutumia pale shulenii. Kwa hiyo, hii ni *initiative* moja nzuri sana katika Wilaya ya Babati.

Vilevile, Taasisi mbalimbali kama vile *TECH, TATEDO* na *MIGESADO* zimeshiriki katika kufanya usafi. Hii *MIGESADO* ni Taasisi ya Mazingira iliyoko Dodoma, wameshiriki katika kufanya utafiti juu ya nishati mbadala na *technology* sahihi zinazolenga kupunguza mahitaji ya kuni na mkaa. Utafiti huu umeongeza matumizi ya majiko bunifu na matumizi ya majiko ya gesi yatokanayo na kinyesi cha ng'ombe (*bio-gas*) katika Mikoa ya Dodoma na Tanga.

Kwa hiyo, bado tunaendelea lakini yejote mwenye mawazo mazuri tunayakaribisha ili Ofisi ya Makamu wa Rais iweze kuyatekeleza.

Hoja nyingine ilikuwa, Serikali ije na mkakati na mpango unaoweza kugeuza uzalishaji wa utumiaji wa Mkaa kuwa wa kisasa na endelevu; tayari Ofisi ya Makamu wa Rais imeshaanza kutekeleza mambo haya. Haya mambo siyo ya Serikali ya Tanzania tu, kuna Mikataba ya Kimataifa inayozingatia suala hili.

Kwa hiyo, Serikali ina mkakati wa Kitaifa wa kuhifadhi ardhi na upandaji miti, pamoja na mambo mengine. Mkakati huu unahimiza Halmashauri zote na kila kaya, Taasisi mbalimbali na viwanda vinavyotumia kuni, mkaa kama chanzo cha nishati, kuanzisha mashamba ya kupanda miti.

Kwa kweli, tunategemea kwamba hata kama mtu binafsi unatumia miti na mkaa, basi tuwe na utaratibu wa kupanda miti kwenye mashamba yetu. Kuna kilimo bora cha *agro-forest*, yaani kilimo cha mseto ambacho ni kilimo kinachokubalika, ambacho mtu unaweza ukachanganya mazao ya kawaida, mahindi pamoja na miti au kunde na kadhalika.

Kwa hiyo, mazao haya tukifanya hiki kilimo cha mseto kitasaidia sana kuwa na miti ya kutosha katika mashamba yetu. Kwa hiyo, kila mmoja atavuna miti kwenye shamba lake na siyo kwenye hifadhi.

Suala lingine, kuna mkakati gani wa kukabiliana na uharibifu wa mazingira katika Mlima wa Kilimanjaro. Ni kweli, mlima wa Kilimanjaro kwa Tanzania ni kitu muhimu sana, kwa sababu kwanza ni mlima mrefu sana duniani na unajulikana, lakini siyo hivyo tu, unavutia watalii wengi sana. Kwa hiyo ni *source* kubwa sana ya *income*. Sisi wote kwa pamoja hasa Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa wa Kilimanjaro, ninaomba tusaidiane.

Kilimanjaro Mkuu wa Mkoa ameanzisha mpango mzuri sana, ingawa ulikuwa unalalamikiwa na watu wengi sana, pamoja na Wabunge walioko humu ndani, yeye ameanzisha mkakati kwamba, hakuna ruhusa kukata mti bila kuomba ruhusa ya Halmashauri. Ukikata, hata kama ni usiku wa saa

sita, taarifa inakwenda kwa Mkuu wa Mkoa na mtu yule anashikwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe ni shahidi, alishanionyesha watu ambao wameshikwa wakati nilipokwenda kuzindua *campaign* ya kutafuta pesa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya Mkoa, lakini hususan Mlima wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, Mkuu wa Mkoa nampongeza, anafanya kazi nzuri sana, lakini sisi tumpe ushirikiano wa kutosha ili *campaign* hii iweze kuwa endelevu.

Vilevile, tuna mradi unaitwa *COMPACT* kule Kilimanjaro, Ofisi ya Makamu wa Rais imepeleka pesa kule na Ofisi hii iko kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Ni pesa zinazotumika kuhifadhi Kilimanjaro na Mlima Kilimanjaro.

Vilevile, mwaka 2012 siku ya Mazingira Duniani, Rais alikwenda kufunga sherehe zile, lakini Kanisa la KKT nitumie nafasi hii kulishukuru kwa sababu walitoa ahadi kwa Mheshimiwa Rais kwamba, wao wakati wa kutoa Kipaimara Kanisani, watahakikisha kila mtoto kwenye familia yao, lazima wapande kwanza miti kumi ndipo apate Kipaimara.

Kwa hiyo, nina waomba madhehebu mengine ya *Roman Catholic*, Waislamu na madhehebu mengine, hata Wapagani, kwa sababu wote tunatumia kuni, hivyo wote kwa pamoja tuijiwekee mikakati, tusaidiane na Halmashauri ili tupande miti ya kutosha.

Suala lingine ni miradi ya hifadhi ya mazingira katika maziwa makuu. Maziwa Makuu tunayo matatu. Ziwa Victoria, Lake Tanganyika na Lake Nyasa. Niwambie wenzangu wa Kambi ya Upinzani wameibua tu Ziwa moja Victoria, lakini Tanzania ina maziwa makuu matatu kama hamjui. Kwa hiyo, *Lake Victoria* iko chini ya mradi wa *LAVEMP* ambao ni mradi wa kimataifa, *Lake Victoria Environmental Management Program* na mradi unasaidia vijiji vilivyoko jirani na *Lake Victoria*, wanawafundisha uvuvi ulio salama lakini pia wanawafundisha kilimo bora. Pia mradi huu unahuishisha *Inter University Council* ya *East Africa* kusimamia *project* mbalimbali kuhakikisha tunahifadhi Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, kwenye *Lake Tanganyika* kuna kitu kinaitwa *Lake Tanganyika Authority*, ambayo iko katika Burundi, DRC Congo, Zambia na Tanzania. Mimi ni Mwenyekiti wa *Lake Tanganyika Authority* na kule tumefanya vitu vizuri tu, mashahidi ni Wabunge wote walioko humu ndani wanotoka kando kando ya *Lake Tanganyika*. Kuna pesa nyingi zimepelekwa kule, lakini kila nchi mwanachama ni lazima kwa mwaka achangie Dola za Marekani 303,900.

Kwa hiyo, katika hii *Lake Tanganyika* kuna hela za Tanzania ambazo tunachangia na Ofisi ya Makamu wa Rais kwenye bajeti yetu, tuna bajeti ya kuchangia *Lake Tanganyika Authority*. Kwa hiyo, nchi zote zinazoshiriki kwenye *Lake Tanganyika Authority*, wanachangia.

Mheshimiwa Spika, *Lake Nyasa* pia nalo tuna mkakati, kikwazo kikubwa kilikuwa ni mpaka, lakini tumeona tuachane na mpaka kwa sababu *project write-up* ilikuwa imeandikwa kutunza vyanzo maji. Sasa vyanzo vya maji vya *Lake Nyasa* vyote viko kwenye Milima ya Umatengo. Ni mbali kabisa na mpaka.

Kwa hiyo, tumeona tuandike *write -up* nyingine inayohusisha utunzaji wa vyanzo vya maji na tuachane na suala la mpaka kwa sababu tumeona suala la mpaka, ni lazima tukubaliane na Malawi ndipo mradi tuanzishe. Kwa sasa hivi litakuwa gumu sana, kwa sababu ni suala la kitaifa, kwa hiyo, ni ngumu.

Kwa hiyo, tumeona huu mradi sasa tuhamishe, tuzingatie tu vyanzo vya maji ambavyo viko kwenye Milima ya Umatengo. Kwa hiyo, maziwa yote matatu haya, Ofisi ya Makamu wa Rais inayazingatia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilihusu kudhibiti uharibifu wa mazingira katika maeneo ya fukwe za bahari, kulinda na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi; suala hili tumeanza kulitekeleza. Mwaka 2012 wakati wa hotuba yangu ya bajeti, tulisema tutashirikiana na Waziri wa Maliasili kuzunguka fukwe zote kuanzia Tanga, mpaka Mtwara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumeshaanza kufanya kazi hii, Dar es Salaam pale, mmeshaona, tumebomoa hizo nyumba ingawa kuna changamoto. Katika kila jema lazima changamoto zitokee na tunaendelea kuzifanya kazi. Lakini vile vile tumeshafika Mtwara, Lindi na tunaendelea na maeneo mengine, hivyo suala hili limezingatiwa.

Katika kutekeleza hili, kwa sababu ni suala zito sana la kubomoa nyumba ya mtu, na hasa tulibomoa nyumba zile zilizokuwa zimeziba ile mito Ndumbwi na kule kawe. Lakini tuliomba Kikosi cha Polisi cha Mazingira, tumeshapata na katika hotuba tumeshasema tuna Askari mpaka kwenye ngazi za Kata kwa ajili ya kusaidia hizi shughuli ngumu ngumu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho ya Kambi ya Upinzani, walisema Serikali iwachukulie hatua Watendaji wa Serikali wanaotumia madaraka yao kuzuia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira hasa katika kuwaondoa wananchi waliojenga nyumba ndani ya mita 60 ya eneo la fukwe za bahari ambazo zimezuiliwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nikushukuru kwa kuingilia kati ile hoja iliyotolewa, maana ile hoja ilikuwa inaingilia muhimili mwingine, na sisi siyo kwamba hatutaki kuboa, lakini suala liko Mahakamani, ni lazima tufuate sheria na taratibu za Mahakama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hizi hoja, naomba na mimi niungane na Naibu Waziri kuelezea sheria hizi za Mazingira, nikianza na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004, Tangazo la Serikali namba 193, sehemu ya pili kufungu 4(1), ambacho kinasema: "Kila mtu anayeishi Tanzania, atakuwa na haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya." Kila mtu!

Kifungu 4(2) kinasema: "Haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya itahusisha haki kwa kila raia kutumia *element* za Umma, au sehemu muhimu mbambali za mazingira kwa madhumuni ya burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na uchumi."

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie. Kifungu cha 4(2) kinasema: "Haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya, itahusisha kila raia kutumia *element* za umma, au sehemu muhimu mbalimbali za mazingira kwa dhumuni la burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na uchumi."

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kutokana na vifungu nilivyosoma hapo juu, mtu ye yote anayeharibu mazingira kwa kuchafua hali ya hewa, maji, udongo, mimea, tabia nchi, sauti, sehemu ya burudani, dini, yaani ibada, utamaduni au kwa kutishia haki ya mtu mwingine kushindwa kutimiza wajibu wake au jukumu lake ni uchafuzi wa mazingira na mtu huyu anatakiwa kushitakiwa Mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya uchafuzi wa mazingira ya Bunge vinavyotokea humu ndani, kwa mfano, matumizi ya lugha mbaya, zinawaweka Waheshimiwa Wabunge kwenye mazingira yasiyo salama na hatarishi. (*Vicheko/Makofij*)

Kwa bahati mbaya, vitendo hivi hatarishi vinaendelezwa hata kwenye Sekta za Elimu, hasa Vyuo Vikuu, na kwenye Udini. Kuna wimbi la wanasiasa wanaokwenda Vyoni kuharibu mazingira ya elimu kwa kuwafundisha wanafunzi hao udini na ugaidi. Mambo ya kushangaza yanayotokea hapa ndani ni mambo yaliyotokea kwenye Mabunge ya Vyuo Vikuu. Kutokana na uharibifu wa mazingira ya elimu, wanafunzi wengi wameshindwa kusoma na hatimaye kufukuzwa au kuacha masomo.

Kwa mfano, hii ni mifano halisi iliyonipata mimi wakati nikiwa *Dean of Students DUCE*. Kuna Mwanafunzi anaitwa Gwakisa, ameshindwa kuendelea na masomo, yupo Mtaani anahangaika bila msaada wowote na kijana huyu ni yatima.

Mwingine anaitwa Ludovick yupo kwenye mazingira magumu kwa kukutwa na tuhuma nzito za Ugaidi, naye ni kijana yatima. Aidha, kuna wasichana wengi ambao leo hii wanashindwa kuendelea na shughuli za masomo au kazi za maendeleo ya kila siku kwa sababu za vitisho vya kisiasa.

Vilevile maandamano bila kibali ni uchafuzi wa mazingira. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali hii haikubaliki, ni uharibifu wa mazingira Bungeni, Vyuo Vikuu, sehemu za biashara, sehemu za Ibada na sehemu nyingine.

Kwa kifupi, ni uvunjwaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Kwa bahati mbaya wanasiasa wanaokwenda Vyuoni kuharibu mazingira ya elimu Vyuoni wao wenyewe hawajaweza kumaliza vizuri masoma yao na walipata *Division Sifuri*, na wengine walifukuzwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge Iako Tukufu kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Tangazo la Serikali Na. 193, Sehemu ya 20, Kifungu cha 232 linalohusu mgongano wa Sheria ya Mazingira na sekta nyingine. Sheria inasema hivi:

"Pale ambapo masharti ya Sheria hii yatakuwa yanapingana au kuhitilafiana na vifungu vingine vyovvyote vy'a sheria nyingine inayohusu usimamizi wa mazingira, masharti ya Sheria ya Mazingira ndiyo itakayotumika na ndiyo itakayosimama."

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wakati Sheria hii inatungwa mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira, naona wakati huo labda ilikuwa maandamano...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):**  
Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Nadhani wakati huo hiyo *definition* haikuwepo. Haya, ahsante. (*Kicheko*)

Namwita mtoa hoja. Mheshimiwa mtoa hoja, dakika 35.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MUUNGANO):**

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia hoja ya utekelezaji wa malengo ya mwaka huu tulionao wa fedha na maombi ya fedha kwa mwaka ujao na mpango kazi kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 37 kwa maandishi, na 12 kwa kusema. Naomba niwashukuru wote na niwaahidi kwamba tutatoa ufanuzi wa hoja walizoiuliza na zimeshaanza kutolewa na Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, lakini pia kwa yale ambayo tutakuwa hatukuyaeleza hapa, niwaahidi tu kwamba tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza ufanuzi wa hoja kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais na Waziri wa Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais, naomba sasa mimi nijielekeze moja kwa moja kwenye masuala ya Muungano. Naomba nianze na hoja za Kamati ya kudumu ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya kudumu ya Bunge ilitoa maelekezo kadhaa ambayo nitajaribu kuyatolea ufanuzi. La kwanza, ni kuimarishwa kwa Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais, ambapo wametoa ushauri kwamba ili kumwezesha Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yake ipasavyo akiwa Zanzibar, ni vyema kukawa na fedha zinazotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kulifanyia kazi hili, ni kweli kwamba Ofisi ya Tunguu kule Zanzibar imekamilika, na kwa ukubwa wa Ofisi ilivyo ni vyema kwa Ofisi binafsi Zanzibar kuwa na kifungu chake cha fedha. Hatua tuliyochukua hapa ni kwamba, tunakamilisha muundo wa Utumishi ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais, tipeleke kwa Wizara ya Utumishi tupate kibali, na baada ya kibali hicho, *Private Office Zanzibar* itakuwa na fungu lake yenye la fedha.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa matatizo ya Muungano, kama nilivyosema katika hotuba kwamba

tunajitahidi kuyafanyia kazi, katika matatizo 13, tisa tumemaliza, yamebakia manne, ambayo nayo yapo kwenye hatua nzuri, tutayaeleza baadaye au kama nilivyoaeleza katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imetaka kupata mrejesho wa yanayozungumzwa katika vikao vyta za Muungano ili wajue kinachoendelea.

Kuanzia kikao kilichopoita, kilichofanyika tarehe 14 Januari, mwaka huu, Wizara yetu ilitengeneza vitabu vidogo na kuvigawa kwa Wajumbe wa Kamati kama mrejesho wa yaliyozungumzwa katika kikao hicho. Pia vitabu hivyo ni huru kutumika na watu wote. Kwa hiyo, kama vinahitajika tunavyo na tutaweza kuvisambaza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu kwa Umma, ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisemea, na sisi tuko tayari kufanya kazi hii, ila tunakwazwa tu na ufinyu wa Bajeti. Lakini katika hatua nyingine, tunajaribu sana kuandika maandiko ya miradi ambayo tunawaomba washirika wa maendeleo watusaidie katika eneo hilo, lakini bado jithada hazijaza matunda.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilirozungumzwa na Kamati ni kuhusu Tume ya pamoja ya fedha na kuuliza kwa nini mpaka leo haijaanzishwa na yale yanayoendana nayo hayajafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Spika, katika hili ni kwamba, kweli Tume ya Pamoja ya Fedha imetakiwa kuundwa Kikatiba katika Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uanzishwaji wa *Account* ya pamoja ya fedha, unaendana na mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo imetoa mapendekezo kadhaa ya kufanyiwa kazi. Lakini nina furaha kusema kama nilivyosema katika Bunge liliopita la Bajeti kwamba kazi hii imeshafanywa vizuri kwa upande wa *SMT*, ila ilikuwa inakwenda ngazi kwa ngazi ndani ya Serikali kupata maoni tofauti.

Hatua iliyofikia sasa hivi ni kwamba, ripoti hii ya Tume ya Pamoja ya Fedha mapendekezo yake yameshajadiliwa kwa mara ya kwanza ndani ya Baraza la Mawaziri na majadiliano yanaendelea. Kwa hiyo, nimatumaini yangu kwamba mwisho wa mwaka huu wa 2013 au kabla, maamuzi kuhusu suala hili yatakuwa yametoka tayari.

Suala lingine ni utafutaji na uchimbaji wa mafuta. Suala hili tumelifanya kazi na kama nilivyosema kwenye Bajeti ni kwamba, sasa hivi Wanasheria Wakuu wa *SMT* na *SMZ* wanaongoza Kamati ambayo inaangalia Sheria za Kitaifa na za Kimataifa za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na iweze kutoa mapendekezo yake kwa Serikali ili tuweze kubadilisha Sheria zilizopo za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili ziweze kutoa fursa kwa Zanzibar kuweza kujandaa na kazi hii ya uchimbaji wa mafuta wakati tukisubiri mabadiliko ya Katiba kutimiza yale ambayo yaliombwa na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Tunguu. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba jengo hili limemalizika, kulikuwa na makosa ya hapa na pale ambayo Mkandarasi ameyafanya, tumekwenda naye, tumekaa naye, tumezungumza na sasa hivi anajitahidi kurekebisha. Lakini jengo tayari limemalizika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ajira ya Wataalamu wa kumshauri Mheshimiwa Mkamu wa Rais. Katika hili, Makamu wa Rais hasa kwa upande wa Muungano, anashauriwa na Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Muungano na Wakurugenzi Wasaidizi katika masuala ya Muungano. Watu hawa wote wana upeo wa kutosha kuhusu mambo ya Muungano. Kwa hiyo, hatuoni haja ya kusema kwamba tuajiri watu wengine maalum wa kumshauri Makamu wa Rais kwenye mambo haya ya Muungano. Ila tunatoa fursa kwa watu wa nje, ambao wanaleta mawazo yao kumshauri Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili. Hili kama nilivyolisema, na bidhaa kubwa inayosumbua katika suala hili ni bidhaa za magari. Tumewataka *TRA* na *ZRB* na Wizara za Fedha mbili wakae, wafanye tathmini ya mfumo uliowekwa, waone upungufu na faida zilizomo katika mfumo huo, watulettee taarifa na Kamati ya Pamoja itoe maagizo yanayopaswa kutolewa kutokana na taarifa watakayoleta.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufanuzi wa hoja hizo za Kamati, naomba sasa nielekee katika hoja za Kambi ya Upinzani. Katika hoja hizi, Kambi ya Upinzani, hoja ya kwanza walitaka kujua kwa nini Mahakama ya Katiba haipo, na kwamba Kero za Muungano zilipaswa kufanyiwa kazi na Mahakama hiyo badala ya chombo ambacho sasa hivi kinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Ibara 126 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninaomba kuinukuu, inasema hivi: "Kazi pekee ya Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni kusikiliza shauri lilitolewa mbele yake, kutoa uamuzi wa usuluhishi juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba hii."

Naomba nirudie hapo, juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar."

Mheshimiwa Spika, kilichoko mbele yetu ni changamoto au vikwazo vinavyojitokeza katika kutekeleza masuala ya Muungano, ambavyo havina utata wa Kikatiba.

Kwa hiyo, masuala haya hayapaswi kupelekwa kwenye Mahakama ya Kikatiba. Chombo kilichoundwa kushughulikia masuala haya ni chombo halisi ambacho ndicho kilitakiwa kushughulikia masuala haya. Kazi pekee ya Mahakama ya Katiba ni kusikiliza utata wa tafsiri ya Katiba utakaowekwa mezani na Serilikali mbili.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia imetaka Serikali elieleze Bunge, kulikuwa na sababu gani ya kuanzisha utaratibu wa Mahakama Maalum ya Katiba, kwa ajili ya kutatua migogoro ya Muungano kama utaratibu huo haukupaswa kufanya kazi hii. Mahakama ya Katiba imewekwa kwa sababu kwenye Muungano kuna utata ambao huwezi ku-*forecast* au huwezi kuitabiri leo kwamba itatokea. Kwa hiyo, kipengele hiki kimewekwa kama migogoro hiyo itatokea, kama haijatokea, ndiyo maana Mahakama ya Katiba haipo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Katiba siyo jengo kwamba kuna jengo tutaliona limeandikwa Mahakama ya Katiba, kama tunavyoona Mahakama Kuu. Mahakama ya Katiba ni mkusanyiko wa Majaji kama ilivyoelezwa kwenye Katiba, ambao watachaguliwa kushughulikia jambo Fulani. Hii inakaa popote, ikiwa Tanzania Bara au Zanzibar. Hiyo ndiyo Mahakama ya Katiba na siyo jengo maalum kwamba hili linaitwa Mahakama ya Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imetaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu, kama ni kweli au siyo kweli kwamba mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 yameongeza kero kwa kuhoji kama Tanzania bado ni nchi moja ama la

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi nataka niseme hivi, kwamba marekebisho ya Katiba ya Zanzibar yaliyofanywa karibuni hayajaongeza kero katika *list* ya kero tulizonazo, kwa sababu hakuna kero mpya ambayo tumei-*register*.

Mheshimiwa Spika, kero zote ni kero ambazo zimeletwa mwaka 2006 au kwenda nyuma na kero za karibu zaidi zilikuwa ni mwaka 2008 ile ya Mfuko wa Jimbo na ile ya *TANESCO*na *ZECO*. Lakini hakuna kero mpya ambayo tumei-*register* kutokana na kurekebishiwa kwa Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia imetaka Serikali iseme hapa kwamba: Je, kila nchi, yaani Zanzibar na Tanzania Bara, kila nchi ina eneo lake la bahari kuu au la;

kama tuna Wakuu wa Nchi Wawili au la; kama tuna Amiri Jeshi wawili au la na kama masuala ya ulinzi na usalama bado ni masuala ya Muungano.

Sasa kwa niaba ya Serikali nasema hivi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi moja iliyotokana na Muungano wa nchi mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine, nchi hizi mbili zilizoungana kabla ya kuungana kila nchi illikuwa na mipaka yake ya bahari na ardhi, pamoja na mambo mengine. Lakini lingine nililotakiwa kusema ni kwamba, tuna Wakuu wa Nchi wawili au la. Mkuu wa Nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mmoja tu, na mwagine ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Suala lingine, ni kama tuna Amiri Jeshi wawili au la; Amiri Jeshi ni mmoja kutokana na Katiba hii, naye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine, liliulizwa kama masuala ya ulinzi na usalama bado ni masuala ya Muungano; ndiyo, bado ni masuala ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilisema *SMZimeamua kuanzisha Mfuko wake wa Jimbo na Majimbo hayo hayo yanapata fedha kutoka Bungeni*. Sasa wanasema, hii siyo kwamba Zanzibar inafaidi mara mbili mbili?

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba labda kiini cha tatizo hili ni kwamba, wakati umeanzishwa Mfuko wa Jimbo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wabunge, pale Zanzibar kuna Wabunge wa Baraza la Wawakilishi ambao wanahudumia Majimbo hayo hayo, lakini Sheria ile ya *CDCF*, haiwatambui Waheshimiwa Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, pesa ile ilivyoanza kuingia Majimboni, Wawakilishi walihisi kwamba Wabunge wanajengwa zaidi kuliko wao, na kwa hiyo, wakadai pesa

hiyo inayoingia, si inaletwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi wote tuwe humo ndani, hiyo pesa tujilabu nayo wote. Lakini kisheria haiwatambui. Mzozo uliana hapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mjadala mrefu, *SMZ wakasema to cut story short* tuanzishe Mfuko wa Jimbo kwa Waheshimiwa Wawakilishi. Sasa *whether Zanzibar inapata mara mbili au la, mimi hapa nataka kusema, hiki ni choyo; kwa sababu kabla hujaona choyo, jiulize kwanza wanapata nini? Kiasi gani?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Zanzibar na udogo wake kama mnavyojua mifuko hii imetolewa kulingana na idadi ya watu unaowawakilisha. Jimbo linalopata fedha nyingi zaidi kwa Zanzibar ni Shilingi milioni 25, wakati ukija Bara kuna Majimbo yanapata mpaka Shilingi milioni 90 na kitu kama siyo 100. Lakini upande wa Baraza la Wawakilishi ni Shilingi milioni 10 tu. Sasa ongeza kwenye Shilingi milioni 25, ni 35. Haijafika hata nusu ya Jimbo moja la Tanzania Bara. Sasa hivi vyoyo vingine hivi, hebu tuvitazameni; kabla hujafanya choyo, jiulize, kuna nini kinachopatikana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine linasema Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili kuhusu suala la Watanganyika wanaoishi na kufanya kazi Zanzibar kutoruhusiwa kumiliki Ardhi Zanzibar wakati Wazanzibar wanaoishi na kufanya kazi Tanzania Bara wana haki kamili ya kumiliki Ardhi, kwani jambo hili linaonekana kuwa Wazanzibar wanapendeleta, wakati Tanganyika wanabaguliwa.

Haya, mtoha hoja mimi naomba ajiulize, ardhi ya Zanzibar haizidi *square kilomita* 3,000; watu wa Zanzibar ni 1,300,000; gawa, kila mmoja anapata chini ya robo heka. Sasa wewe unayekwenda kule, upewe nini? Yaani omba kitu ambacho kipo, lakini huwezi kupata. Lakini unaomba kitu ambacho hakipo! Sasa upewe nini? Ni ku-*create issues* ambazo zitaleta mjadala usio na mantiki ndani yake. Hakuna ardhi Zanzibar ya kugawa kwa watu wote!

Mheshimiwa Spika, samahani, nataka ni-*declare interest* tu, mimi ni Mzanzibar na nina watoto wanne, lakini

Ardhi watakayorithi watoto wangu ni ile niliyobahatika kupata mimi, heka tatu, watoto wanne wanagawanaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusi-create mambo tukawaambia wananchi kwamba kuna ubaguzi kwa kitu ambacho hakipo!

Mheshimiwa Spika, Zanzibar hakuna ardhi, labda tungawane bahari. Bahari ipo kubwa tu. Sasa kama wapo watu ambao wanataka kukatiwa maeneo ya bahari na sheria zinaruhusu, basi waombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna lingine ambalo linazungumzwa hapa, la kero ya Uwakilishi wa Wazanzibari, kwamba Wazanzibari katika Bunge hili hawapo kwa uwiano. Sijui uwiano wa nini, *population* au nini sijui, lakini hawapo kwa uwiano. Mantiki ni kwamba Wazanzibari wapo wengi zaidi kuliko walivyopaswa wawepo.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui walivyopaswa wawepo, ni kwenye sheria gani au Katiba gani! Kwa sababu Katiba hii tunayojua ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 66, inaeleza Wabunge watakaoingia kwenye Bunge hili, na nadhani 66 (c) au (d) inasema Wajumbe watano kutoka Baraza la Wawakilishi kikatiba wapo hapa.

Mheshimiwa Spika, wanaposema wapo wengi, wamependelewa, nini, marekebisho ya Katiba yapo *on the way*, kama hukuwahi kutoa hilo kwenye mapendekezo ya Katiba, liseme kwenye Bunge la Katiba linalokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa ni kuhusu Muungano kwamba, kwa kuwa watu wengi hawana uelewa wa Muungano, basi Muungano huu ni wa kisiasa zaidi au ni wa uongo. Nataka kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Muungano huu ni wa kweli wala siyo wa uongo, kwa sababu sasa hivi kuna Watanzania wako *all over Tanzania*, wanafanya shughuli zao za kiuchumi na kuendeleza maisha yao bila bughudha na bila kukerwa. Isitoshe, Muungano huu ndiyo unaotupa sauti nje ya kuomba au kueleza kitu tukasikilizwa kwa jina la Muungano, tungekwenda mmojammoja, Tanganyika kivyake na Zanzibar kivyake, pengine tungepata au tungenzikilizwa lakini siyo katika jina la Muungano.

Muungano huu umeweka misingi thabiti ya kuendesha nchi hii inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tukafika mpaka leo tulipofika kwenye miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara na keshokutwa tunaingia miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar ni muungano huu huu. Ingekuwa Muungano wa uongo ungeshavunjika. Tumeshuhudia miungano tele ya uongo hapa Afrika; kwa mfano, Senegal na Gambia ulikuwa wa uongo haukukaa umevunjika na mingine ya aina hiyo. Kwa hiyo, Muungano huu ni wa kweli na wala siyo wa uongo na si kitu cha kubeza au cha kusema kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja katika mchango wake au kitu cha kuvunja, ni kitu cha kurekebisha, lakini twende katika mfumo ambao Watanzania wataukubali na tuendelee nao.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la kufuta Mabaraza ya Katiba, nilitaka kusema kwa bahati mbaya yamepelekwa mahali sipo, kwa sababu sisi Idara ya Muungano hatushughuliki na hilo; naomba mngojee Wizara ya Katiba na Sheria nadhani inaingia tarehe 2 Mei, 2013 watakuja kuli-*address* hili.

Jambo lingine, Wazanzibari hawajui kiasi cha fedha kutoka *East African Currency Board* wala hawajui watarudishiwa lini. Nataka kusema kwamba, katika mijadala inayoendelea, huyu anasema changu katika hapa ni hiki na

huyu anasema hapana siyo kiki ni hiki, lakini bila kuwa na zile nyaraka za siri ambazo zimeweka zile *record*. Nyaraka za siri zilizoweka *record* zipo kwenye Makumbusho ya *East Africa*, *Nairobi*/na nyaraka zile huwezi kuzipata kwa urahisi. Kwa hiyo, nchi imeomba nyaraka zile kule na baada ya kupatikana zimepelekwa kwa Mawaziri wa Fedha wazipitie wakubaliane, kila mtu aone kilichokuwepo ili wakae kitako wakubaliane na watuambie ni ngapi. Kwa hiyo, siyo kwamba hatujui, tunajua watarudishiwa lini na si suala la kurudishiwa tu, kwa sababu hoja iliyokuwa *registered* hapa ni kwamba, mgawo wa *BoT* ni asilimia 4.5 kwa Zanzibar kama ulivyowekwa na *IMF* na ulikuwa ni mgawo wa muda mpaka watakapokubaliana. Kwa bahati mbaya, hatujakubaliana mpaka leo, bado kazi ya kujadiliana inaendelea.

Upande wa pili wanasema asilimia 4.5 siyo *share* yetu, kwa sababu *capital*/illyoingizwa humu ilikuwa kiasi kadhaa, upande wa pili wanasema hapana siyo hicho. Kwa hiyo, walikuwa wanacheza kwenye hapo, watakapokubaliana mgawo wa *BoT* *tuta-take shape* makubaliano yatakayofikiwa.

Jambo lingine ni kwamba, kulikuwa na uwakilishi usio wa uwiano katika mchakato wa Katiba. Hili jambo ni lile lile la ubinafsi kwamba, kwa nini huyu na huyu wamo humu wakati sisi hatumo. Nasema hivi; katika uwakilishi wetu katika vyombo vyovyote vile ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatuangalii watu, tunaangalia ule ushirika, historia yake waliifanya vipi. Kwa sababu wakati tulipoungana Zanzibar walikuwa watu 300,000 tu na Tanzania Bara walikuwa 10,000,000, kwa hiyo, masharti ya wingi wa watu yangewekwa kuanzia pale. Kilichotazamwa ni nchi mbili, moja *im-surrender sovereignty* yake na wakawapa wengine chukueni mtuendeshe. Kwa hiyo, makubaliano ni kwamba, nchi mbili zimeungana ziendeshe mambo yao, siyo wingi wa watu, kama ni wingi wa watu, China ingekuwa na *seats* nne Umoja wa Mataifa kwa sababu ina watu wengi kuliko nchi zote, lakini ina *seat* moja tu sawasawa na Seychelles yenye watu 400,000 na wengine wote au Solomon Irelands huko kwenye watu 200,000. Kwa hiyo, suala la wingi wa watu huku na kule linatumika lakini katika kugawana vigezo vya kiuchumi, siyo

katika haki za kisiasa. Hapa tunazungumzia uwakilishi wa kisiasa, zilizoungana ni nchi mbili zote zilizokuwa Jamhuri; moja imetoa jina la Jamhuri ikachanganya kwa mwenzake.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi wa hoja za Kambi ya Upinzani, naomba sasa niende kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge. Yaliyozungumzwa ni yale yale; kwanza, suala la elimu kwa umma kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais iongeze jitihada. Kama nilivyosema, tunataka sana kufanya hii kazi, lakini tunakwazwa na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ufinyu wa bajeti, kama mlivyouzungumza kwamba, kazi tulizonazo na fedha zinazoingizwahaziendani na hadhi ya ofisi kama jina lake liliyivo. Kwa hiyo, hilo nalo limesikika.

Vilevile jambo lingine ni kuhusu kwa nini Tume ya Mipango hajatoa kibali cha Idara ya Muungano kuruhusiwa kupewa fedha kwa ajili ya kuelimisha Umma. Naomba kusema kwamba, tulitayarisha Mradi kama Mradi wetu wa Maendeleo, tumeuwasilisha Tume ya Mipango ambao wamekubali na kwa kuanzia tukapewa shilingi milioni 250. Baada ya kushuka *cealing* ya Wizara, ikawa imetuathiri tena, lakini siyo kwamba Tume ya Mipango haikukubali, imekubali Mradi wetu na fedha zilikuwa *allocated* mara ya kwanza.

Kuna suala pia la maoni kwamba, fedha inayokwenda Zanzibar, yote inakuwa *imparted* kwenye Fungu la Ofisi ya Makamu ya Rais na Ofisi kuonekana ina Fungu kubwa lakini kumbe zote zinapita tu kwenye bomba na inabakiziwa kidogo. Nalo hili tutajitahidi kulifanyia kazi na Hazina, waone jinsi ya kupambanua fedha zile ziwe na *vote* yake na huku kwetu kuwe na *vote* yake.

Lingine ni masuala yatokanayo na *GFC* ambalo nimeshalisema. Kulikuwa na suala kwamba, kwa kuwa kodi ya ushuru wa bidhaa na mapato yote yanaingia Benki Kuu ya Tanzania, Zanzibar inakosa fursa ya kuelewa kinachopatikana baada ya matumizi. Ni kwamba, makusanyo yote ya mapato yanayokusanywa ni kweli

yanakwenda huko, lakini kuna ufanyaji kazi wa karibu zaidi na kwamba, *BoT* kila mwezi inatoa hali ya fedha na makusanyo na kupeleka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanajua kila kitu kinachoendelea ndani ya *BoT*.

Jambo lingine ni wakati mwafaka wa mgawanyo wa mapato kuangalia idadi ya watu. Nataka niseme kwamba, mgawanyo wa mapato, asilimia 4.5 kwa mfano ilikuwa na vigezo vingi; ilikuwa na kigezo cha idadi ya watu, ilikuwa na kigezo cha *GDP*na uwezo wa kuwekeza. Vyote hivyo pamoja na vigezo vingine viliangaliwa. Kwa hiyo, idadi ya watu siyo kigezo pekee katika mgawanyo wa mapato, kuna vigezo vingi vinaangaliwa, ila kama mnasema kwamba ni wakati sasa *formula* iangaliwe upya, hilo ni jambo lingine.

Pia kulikuwa na suala la kero za Muungano, ambazo nimeshazijibu kwamba, tunashughulikia na hizo nne zilizobaki tutajitahidi zimalizike haraka.

Vilevile kasi ya kutatua matatizo ya Muungano haitoshi; sawa tutaongeza jithada.

Changamoto za Muungano zimeendelea kuongezeka; siyo kweli, kama nilivyosema kwamba, changamoto zimebaki vilevile, zilianza 13 na zimeongezeka mbili katikati, hazijaja nyngine. Kwa hiyo, hazongezeki zinapungua. Zile 13 tumemaliza tisa na ya kumi tumeimaliza juzi, tunangoja kikao kikubwa kukubaliana na hilo, nayo ni ushiriki wa Zanzibar kwenye mambo ya nje. Tulikaa Zanzibar tumelizingumza na tumekubaliana, kwa hiyo, kikao kikubwa SMT na SMZ ni kuja ku-*stamp* kwamba hili nalo limekubalika, linatoka kwenye hizo kero, tunasubiri utekelezaji. Kwa hiyo, kero zilizobaki ni chache sana ambazo naomba mniamini kwamba tutazimaliza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, uandaliwe utaratibu unaoeleweka ili zinapojitokeza kero za Muungano, utaratibu uwepo na ueleweke na *registration*

ya kero utaratibu uwepo. Kila upande unaohisi una kero una-*register* na tunazipokea na tunazifanyia kazi.

Jambo lingine ni ushauri tu kwamba, Serikali zetu mbili kuyafanya kazi mambo ya kiutendaji katika mwaka huu wa fedha, ambayo yanahitaji marekebisho ya Katiba, sawa.

Mahakama ya Katiba, nimeshalitolea ufanuzi. Halafu kuna chokochoko za Muungano, udini na ukabila; jambo hili litafanyiwa kazi na vyombo husika. Muundo wa Muungano ni maoni ya Katiba, yataelezwa huko.

Uwakilishi wa Mabalozi kutoka Zanzibar, Mabalozi waliopo nje uwakilishi wa Zanzibar ni mdogo. Nimesema kwamba, tumeshalizungumza na tumekubaliana na tutakapopata *approval* ya Kamati kubwa basi mtapata taarifa tumekubaliana nini.

Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, tumeshasema, *TRA* na *ZRB*, Wizara za Fedha wanalfanyia kazi, kitakachotokea tutawajulisha.

Akaunti ya Pamoja ya Fedha na masuala ya Katiba, kwa ufupi, hoja za Wajumbe nimemaliza kuzieleza, lakini nichukue nafasi hii kuwashukuru wote ambao walitusikiliza.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya *TASAF*; uwakilishi katika *TASAF* hauingizi Viongozi wa Kisiasa na mfumo huu wameuchukua kwa makusudi ili Wananchi katika ngazi zao kule chini waibue wenyewe Miradi yao. *TASAF I*, Viongozi wa Kisiasa wallingia, *as a result* Miradi iliyoibuliwa ilikuwa ni kwa matakwa ya Wabunge au Wawakilishi na si kwa matakwa ya Wananchi. *TASAF II*/wameondoshwa Viongozi wa Kisiasa, kwa hiyo, Wananchi wanaibua Miradi yao wenyewe kule chini.

Kama Mheshimiwa Mbunge unataka kujuu yanayoendelea ndani ya Jimbo lako kuhusu *TASAF*, tafadhali jitume, tafuta hizi taarifa, ulizia, nenda. Unapoijua kabla, Miradi gani labda kuna fursa zipi zinazoweza kwenda kwenye

Jimbo, unaweza kujidai na hili, unaweza ukatangulia wewe kwa Wananchi ukawaambia kuna fursa hii na ile nakuja nayo, kumbe ni ya TASAF. Sasa jitume tafuta, lakini kwa kusubiri Serikali iandae mpango maalum wa kuchukua Wabunge kuwaingiza, hili halipo, kwa sababu hizi ni fedha za Wananchi kule chini, waibue Miradi yao waitekeleze na ndiyo maana kuna mchango wao; na Waheshimiwa Wabunge, nadhani mnashirikishwa katika michango ya Wananchi, kwa sababu wakati mwagine Wananchi hawawezi kutimiza ule mchango wao, wanajua Wabunge na kwa Zanzibar pamoja na Wawakilishi mnasaidia hilo. Sasa nawaomba mjitume, mtafute hizo taarifa na mjue vipi mtajilabu na Miradi hiyo ambayo iko ndani ya Jimbo lako.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa katika kufanya ufanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge na kama kuna lolote tumeliacha, basi naomba mtuulize wakati wa yifunqu au mtuulize pembeni kwa kupunquza muda.

Mhesimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

### *(Hoja iljamuliwa na Kuafikiwa)*

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

## Fungu 26 – Makamu wa Rais

Kif 1001 - Administration and HR

*Management* ..... Sh. 5,699,642,000

**MWENYEKITI:** Hii ni Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Sigusi mshahara, naangalia *item*.

**MWENYEKITI:** Haya basi endelea.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Vizuri sana, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata ufanuzi wako, niko kwenye *Subvote 1001, Item 221000 – Travel in Country*.

Mwaka jana kulikuwa na shilingi 285,660,000 lakini mwaka huu kuna shilingi 382,700,000, kuna ongezeko la shilingi milioni 97. Naomba kupata ufanuzi kwa nini kuna ongezeko kubwa kiasi hicho?

**MWENYEKITI:** Kwa nini fedha zimeongezeka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mwaka huu wa fedha, tumeepata matatizo sana katika safari za Mheshimiwa Makamu wa Rais, ndiyo sababu ikabidi tuongezee kifungu hiki. Kumbukeni kwamba, hata zile ndege siyo kwamba tunapewa bure, kila Makamu wa Rais anaposafiri, hizo ndege tunakodisha kutoka kwa Wakala wa Ndege wa Serikali.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* ..... Sh. 2,233,261,000

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri hapo. Mheshimiwa Halima Mdee. Kuna tatizo la muda, kwa hiyo, nitawaruka wachache. Mheshimiwa Dkt. Kabwe, Mheshimiwa Engineer Mnyaa na Mheshimiwa Mkosamali. Anaanza Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika Hotuba yetu kwenye suala la mazingira, tulizungumzia juu ya uchimbaji wa madini, *red oxide*, Wilaya ya Same. Suala ambalo lilzungumzwa hata mwaka kwenye Hotuba yetu, lakini pia lilzungumzwa na Mbunge wa Jimbo husika, Mama Anne Kilango Malecela na aliletä *CDna* taarifa hapa zinaonesha *NEMC* ilitoa maagizo lakini Kampuni ya *Will Enterprises Limited* imekiuka na kwamba, uchimbaji bado unaendelea. Katika majibu ya Waziri mwenye dhamana hajazungumza kabisa; kwa hiyo, nilitaka atupe ufanuzi kuhusiana na hili suala ambalo lina athari kubwa sana kwenye mazingira ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea kwanza, mwandike nitawaita baadaye. Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tunashukuru Sera nzuri ya masuala ya mazingira hususan maeneo oevu, ikiwemo maeneo chepechepe Kanda ya Ziwa, Kanda za Bahari pamoja na mito na vyanzo vya maji na ulinzi wa misitu. Tunashukuru kwa kazi nzuri ambayo imeendelea katika Bonde la Ihefu, wafugaji waliovamia Bonde waliondolewa, tunashukuru wanyama ambao walikuwa wametoweka wameanza kurejea pamoja na mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hajajipanga vizuri kwa sababu bado katika Bonde la Ihefu wafugaji wengine wameanza kunyemelea wanarudi polepole na Serikali inaangalia baadaye tena waingie katika *operation*.

Katika Bonde la Mto Mara ambalo kwa bahati mbaya ule mto umeshapoteza mwelekeo, kwa sababu kihistoria mafuriko yanazidi kushamiri. Nawapa pole Wanaserengeti kwa matatizo makubwa ambayo yanatokea ya mafuriko pale katika Mto Mara hususan upande wa Serengeti. Serikali inafanya nini mbali na Miradi mingi ambayo Mheshimiwa Waziri ametamka lakini hatuoni chochote kinachofanyika ikiwemo *LIVEMPO*, ikiwemo Makubaliano ya Nairobi na

masuala ya Bonde la Mto Mara chini ya *East African Community*? Naomba maelezo juu ya tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, *Engineer Mnyaa*.

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufanuzi kuhusu kitu kinachoitwa kero za Muungano. Mheshimiwa Waziri amejitahidi na hizi kero zimetajwa za aina nydingi. Kwa mfano, hii kero ya kwanza ya Akaunti ya Pamoja, jibu lake ni zuri kwamba sasa hivi *process* zinaendelea na ni matumaini kwamba mwishoni mwa mwaka huu itaundwa.

Toka mwaka 1977 mpaka hivi sasa ni miaka 36 na mwishoni mwa mwaka huu inakuja Katiba mpya, pengine ikiundwa Akaunti ya Pamoja ni kipindi kidogo itakavyotumika na hatujaua mfumo wa ushirikiano utakuwa vipi katika Katiba mpya inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna watu walitafsiri kwamba, Katiba ya Zanzibar ni moja katika kero ya Muungano na imevunja Katiba ya Muungano. Kitu ambacho kwa muda wa miaka 36 kimeachwa hivi hivi, inaonekana kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano imejivunja yenye, hili ni tatizo moja kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijumlisha pia kwamba Ibara ya 4(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo inatupelekea kwenye nyongeza, *Item (11)* kwamba, Bandari nalo ni suala la mwanzo la Muungano na miaka yote mpaka sasa miaka 49 haijakwenda Kimuungano hata siku moja. Je, hapo Jamhuri ya Muungano haijavunja Katiba yake yenye kwa kitu ambacho kiliamuliwa toka mwaka 1964 na mpaka leo hakijakwenda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nakubaliana na maneno ya Mheshimiwa Waziri kwamba, Mahakama ya Katiba si jengo, hii ni sahihi kabisa. Nataka nikumbushe kwamba, katika Katiba yetu, sehemu ya (7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara za 125, 126, 127 na 128, ambazo

toka tuasi si Muungano wetu hazijatumika hata siku moja ku-*practise* lbara hizi na zimewekwa kwa Mahakama ya Katiba na ufanuzi wake namna gani ya kufanya kazi. Hiki kitu tunachosema kero ya Muungano, kusema kweli tunatafuta lugha ya kistaarabu ambayo tunaweza kuishi nayo, lakini siyo suala la kero ya Muungano, ni migogoro ya Muungano ambayo tayari ilikuwa iundiwe Mahakama ya Katiba.

Mheshimiwa Waziri utatufafanulia lini kwamba hiki kitu kimefanywa kwa makusudi na Jamhuri ya Muungano na huu siyo uvunjwaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano? Naomba ufanuzi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae na Mheshimiwa Maida Abdallah ajiandae, kwa sababu tumeona vifungu siyo vingi sana.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi naomba kupata ufanuzi kuhusu suala la sera kuhusu mazingira hasa kwenye vyombo vy ya usafiri. Nauliza kwamba; kwa nini Serikali isiweke mwongozo au itunge sheria ambayo itahakikisha kila chombo ambacho kinasafirisha abiria kwa maana ya mabasi yanayokwenda Mkoa hadi Mkoa, daladala zote zinazosafiri kwenye Majiji yote mpaka vijijini zinazobeba abiria ziwe na chombo cha kuwekea takataka (*dustbins*) na iwe wakati trafiki anasimamisha gari moja ya vitu ambavyo anakagua ni *dustbins* ili kuepuka hizi takataka ambazo zimekuwa zinatupwa kwenye mabasi watu wakiwa wanatasafiri ovyo ovyo tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zile fedha ambazo zitakuwa zinakusanywa kupitia watu wanaokiuka kutoweka *dustbins* au vyombo vy ka kuwekea takataka kwenye magari yao ziwe zinatumika katika kupanda miti na kuwagawia watu ambao watakuwa wanagombea hizo tuzo za Mheshimiwa Makamu wa Rais?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii au utaratibu huu uweke utaratibu kwamba, mabasi sasa yatakayokuwa yanaingia nchini kwetu, yawe na vyoo ambavyo watu watakuwa wanajisaidia kuliko kuendelea kwenda kwenye vichaka au maeneo kadhaa. Ningeomba ufafanuzi wa Kisera juu ya jambo hili namna gani linaweza likatusaidia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kigola, atamalizia Mheshimiwa Maida Abdallah.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Duniani kote nchi nyingi sana zimejiunga na biashara ya hewa ukaa; na ukiangalia katika nchi yetu ya Tanzania kuna sehemu nyingi sana zina misitu mikubwa, ambayo kuna watu binafsi wamehamasika na wamepanda miti yao wakiangalia kwamba wanaweza kupata biashara ya hewa ukaa. Kuna makampuni ya watu wengine yameshaingia mikataba na Wananchi na yamechukua hekta nyingi sana na Wananchi wale wanategemea kwamba wanaweza kupata *share* yao katika hewa ukaa.

Je, Serikali ina Sera ipi ambayo inaweza ikamsaidia Mwananchi ambaye ameingia mikataba na makampuni ili isimamie waweze kupata gawio lao; kwa sababu kuna vijiji vingi sana ambavyo vimeshaingia mikataba na Wananchi; kwa mfano, Kampuni ya *Green Resource* ambayo ililingia mkataba na Vijiji vya Idete katika Wilaya ya Mufindi na vijiji vingine?

Namwomba Mheshimiwa Waziri afafanue ili Sera isimamie Wananchi wale waweze kupewa *share* yao bila matatizo yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize  
Mheshimiwa Waziri swali lifuatalo:-

Kwa kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha ilikwishatoa mapendekezo kwa Serikali juu ya namna ya kutatua changamoto zinazohusiana na masuala ya Muungano; lakini kwa habari tulizonazo sasa hivi ni kwamba, upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari ilishatoa maoni kuhusiana na mapendekezo hayo, lakini upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijatoa maoni ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume. Tukiangalia mapendekezo yatakayotolewa kutoka pande zote mbili yatasaidia kwa kiwango kikubwa kutatua changamoto tulizonazo au zinazotukabili za Muungano; kutatua changamoto hizo za mapato yatokanayo na misaada kutoka nje, mgawanyo wa fedha za kodi ya mapato, faida ya Benki Kuu na kadhalika:-

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mapendekezo haya yaliyotolewa na Tume inayafanya kazi ili Wananchi waweze kuwa na imani na Muungano huu kwa mujibu wa Katiba?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dakika zangu 25 bado, Mheshimiwa Ester Bulaya ndiyo awe wa mwisho.

**MHE. ESTER M. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nitahitaji kupata ufanuzi kwa suala zima la nyumba ambazo zimejengwa ambazo zipo kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Naomba niseme kabisa kwamba, nilisiporidhika na majibu, natoa nia yangu ya kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la mwingiliano wa Mhimili kwamba suala hili lipo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilieleza wakati nachangia na nikasema kuna baadhi ya nyumba zilibomolewa wakati kesi zipo Mahakamani. Vilevile nilisema *NEMC* iliweza kuvunja nyumba katika fukwe za Mbezi

ambapo Wananchi walijenga kwenye mikoko huku kesi ikiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba nchi yetu inaongozwa na Mihimili mitatu rasmi, upo mwингine wa Vyombo nya Habari; Dola, Bunge na Mahakama. Bunge tunatunga sheria, Dola kwa maana ya Serikali tunajua inasimamia Sheria. Sasa kama tutaruhusu watu ambao wanataka kutumia Mhimili mwингine kwa ajili ya kufanya Mihimili mingine ambayo inatekeleza Sheria halali ambayo imetungwa na Mhimili wa Bunge kushindwa kufanya kazi yake. Ningependa kupata ufanuzi hili suala la mwингiliano wa Mihimili.

Serikali inapotaka kutekeleza sheria halali, mtu anapokwenda kuweka zuio Mahakamani hapo ni kosa kwamba Mhimili huu unaingilia Mhimili mwингine. Serikali mbali na kwamba kuna zuio Mahakamani, inapotaka kutekeleza sheria halali ambayo imetungwa na Bunge lako Tukufu, hapo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina tatizo na naongea haya kwa uchungu kabisa kwamba, *contradiction* hizi zinafanya ionyeshe kwamba Serikali kuna watu ambao inawaogopa kwa kutumia nguvu zao za kifedha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, natoa shilingi nisipopata maelezo ya kutosha kwa nini nyumba zile zilivunja na kesi ipo Mahakamani na kwa nini nyumba hii inaachwa kwa sababu kesi ipo Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki, Wananchi wanakosa imani ya Serikali kwa Viongozi wachache ambao wanafanya wenzao wengine washindwe kutimiza majukumu yao. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Naomba hilo alijibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunaanza na hili la Mheshimiwa Bulaya kuhusu mambo yapo Mahakamani na watu wakatekeleza vinginevyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu *statements* za Waheshimiwa Wabunge kuhusu watu ambao wanaona haki zao zinavunjwa au zinakaribia kuvunjwa au zimevunjwa kwenda Mahakamani na kupata zuio. Wanafanya hivyo kwa mujibu wa Katiba, hata mimi pamoja na *reservation* zangu nilizonazo, mtu akifanya hivyo sisemi vunja.

Ibara ya 13(6) ya Katiba inawapa watu waliojenga nyumba katika maeneo hayo haki hiyo na ni wajibu wetu sisi sasa kwenda Mahakamani na kusema wamevunja sheria hizo na Mahakama hiyo ambayo imetoa *injunction* inatusikiliza.

Kabla ya hapo, nisingependelea kulishauri Bunge litoe Azimio au Mheshimiwa Ester Bulaya, dada yangu, utoe shilingi kwa Hotuba ya Waziri, kwa sababu hahusiki, kinachohusika hapa ni Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukumbusha kwamba, jambo hili pia linaweza kutokea kwako hata kama hujajenga ufukweni, lakini una jambo na unaona una haki, lakini kuna mtu amekwenda Mahakamani ameweka zuio na Mahakama imemkubalia. Mahakama inafanya hivyo ni kama *temporary relief* upate nafasi uje useme nina haki au yule mwingine hana haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kwamba, tumetunga Sheria, Mahakama inafanya hivyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge na mojawapo ya Sheria hiyo ni ile *Civil Procedure Code*, utaratibu wa uendeshaji wa mashauri ya madai ambayo inaruhusu mtu ye yeyote kufanya hivyo. Kwa hiyo, badala ya kufanya hasira ni vizuri tufuate utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kuna wakati fulani, Marehemu Mzee Kawawa, alisema hatuna haja ya kutumia Mawakili, lakini alipopata kesi kwenye uchaguzi, Mawakili wakamsaidia akasema kumbe nilikuwa nakosea. Kwa hiyo, nashauri kwamba, Mheshimiwa Ester Bulaya, usiondoe shilingi dada yangu, uje tu tuzungumze, kama ni

huyo kigogo amejenga kwenye huo mto, basi tuangalie namna gani. Tusaidieni Mahakama iweze kusema nani ana ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na namshawishi Mheshimiwa Ester Bulaya, arudishe shilingi yake.

**MWENYEKITI:** Katoa alikuwa tu anasema *in case*. Kwa hiyo, nawaita Mawaziri, nani anayejibu masuala ya mazingira; Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kufafanua suala hilo hilo kwamba, nyumba zilizovunjwa hazikuwa na kesi, wameenda baada ya kuvunjiwa. Wakati tunavunja nyumba zote kulikuwa na hakuna kesi na ndiyo maana tuliweza kuzivunja isipokuwa hiyo nyumba moja. Huo ndiyo ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala mengine, Mheshimiwa Halima Mdee ameulizia suala la *red oxide Same*, ni kweli na liliuja hapa na tulitoa ahadi kwamba, tunalishughulikia na tumelishughulikia vizuri. Wakati tunalishughulikia, *NEMC* waliweka katazo, kwa sababu uchimbaji ule *NEMC* ilikuwa haijafanya *Environmental Impact Assessment* na kama Mradi unakuwa umeshaanza, kitu ambacho kinatakiwa kifanywe ni *Environmental Audit*. Kwa hiyo, tuliwasimamisha ili mwekezaji yule aweze kufanya *Environmental Audit* na *NEMC* waweze kumshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifa Bunge lako Tukufu kwamba, mwekezaji yule, *Environmental Audit* aliifanya na *NEMC* walienda kule kuangalia wakamshauri, wakamwelekeza kwamba aendelee na uchimbaji. Tunaendelea na *process* kwa sababu cheti bado hakijatolewa. Kwa hiyo, kuendelea kwake haina maana kwamba, tunahalalisha utoaji wa cheti. Mimi ndiyo ninayetoe cheti, nitaenda kukagua kama sitardhika sitatoa hicho cheti. Kwa hiyo, bado cheti hakijatolewa. Mradi huu ulianza kabla

ya kufanya *Environmental Impact Assessment*, kwa hiyo, sheria inawaelekeza *NEMC* kufanya *Environmental Audit*. Kwa hiyo, tumefikia katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kebwe amezungumzia kuhusu maeneo chepechepe na ulinzi wa misitu na pia akazungumzia lhefu. Kweli kule lhefu tulifanya Mkakati wa Kitaifa wa kuondoa mifugo na wakulima. Vilevile Kilombero mwaka jana tuliweza kuondoa mifugo mingi, *percent* 90 ya mifugo imeondoka na hata zile sehemu ambazo ziliikuwa na wanyama wale, kwa sababu Bonde la Mto Kilombero lina Hifadhi ya Maliasili, lakini pia ipo Hifadhi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mabonde ambayo ni chepechepe.

Kwa hiyo, tulichofanya ni kushirikiana kwa pamoja, kwanza, kuanza kuweka alama ya eneo klini, kwa sababu katika mabonde haya kuna eneo la klini ambalo mtu ye yeyote haruhusiwi kufanya kazi. Pia kuna eneo lingine linalofuatia ambalo linahifadhi hilo eneo kiini. Kwa hiyo, tuliweka mipaka na watu wote kwenye hifadhi ya kiini waliondoka, labda kama wamerudi huko nyuma, lakini baada ya Bunge hili tutaenda tena kuangalia. Bila kufanya hivyo ni kweli mabonde yatazidiwa na udongo na athari zilizotokea; kwa mfano, Mto Mara zitatokea tena Kilombero hata na Mto Pangani, Mto Wami, Mto Ruvuma, Mto Ruvu na mabonde yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kuwatahadharisha Wananchi, tunaposema waondoke siyo kwamba tunataka kuwaonea, tunasema waondoke kwanza tuhifadhi hayo mabonde vizuri ili *segmentation process* na mambo ya kujaza udongo kwenye mto tuweze kuhifadhi yasiwepo. Kwa sababu yakiwemo yanaleta maafa ya mafuriko, mto unashindwa kuhimili wingi wa maji unaopita kwenye mkondo. Kwa hiyo, hilo ni moja. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tufanye hivyo kwa nguvu za pamoja, tunapokuja tuisipinge kwa sababu tunavyopinga maana yake tunaleta maangamizi kwa ajili ya wapiga kura wetu. Kwa hiyo, naomba tushirikiane kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikakati gani inafanywa, tunao Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Mabonde yote na Fukwe zote za Bahari na Mkakati huo tunao hapa Ofisi ya Makamu wa Rais. Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Kwa hiyo, ninaomba mtupitishie hii bajeti kwa sababu tumeshaandaa na mkakati huu tutaanza kuutekeleza kwenye kipindi hiki cha bajeti. Tupo mbioni kutekeleza haya ambayo tumeyaandika na hii itahusu Mito yote Mikuu pamoja na Fukwe, Maziwa Makuu ili kuhakikisha vyanzo veya maji vinawekwa katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyaa, ye ye ameulizia kuhusu kero za Muungano, mwenzangu atajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyombo veya usafiri ni kweli ni kero kubwa na suala la kuchimba dawa nakiri kweli hapo kuna matatizo. Mheshimiwa Makamu wa Rais mwenyewe amekwishatuelekeza cha kufanya, hata ye ye hili suala linamkera binafsi na kila mmoja wetu linamkera, kwa sababu linakiuka maadili yetu sisi wenyewe. Kwa hiyo, tumewasiliana na Waziri wa Uchukuzi, tulishapeleka barua na agizo hilo lilitolewa kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri wa Uchukuzi ameshawapelekea *SUMATRA* na sasa hivi wapo wanaandaa michoro kwa ajili ya vituo maalum veya mahitaji hayo ya kuchimba dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, ameagiza pia vyombo vyote veya usafiri; daladala, mabasi ya mikoani na vyombo vingine, ni lazima viwe na *dustbins* na katika hivyo vituo veya kuchimba dawa tutakuwa pia na sehemu ya *ku-empty* hizo *dustbins* ili angalau haya mabasi wakati fulani wanafika kwenye kituo fulani waweze *ku-empty*. Watatoa tozo kiasi fulani ili waweze kutupa hizo taka kwenye sehemu ambazo tutakuwa tumeweka muhimu za kuchimba dawa.

Hivi sasa tunasubiri ramani ya sehemu hizo na tunawakaribisha wadau mbalimbali, kwenye haya maeneo ambayo *SUMATRA* itakuwa imeyaainisha, waweze nao kutoa mchango wao wa kujenga na nini. Tunaamini katika sehemu

hizo pia kutakuwa na sehemu za biashara, watu watakunywa chai, watakula chakula, kwa hiyo, kutakuwa na shughuli nyingi. Vilevile mabasi yote ambayo yatasafiri zaidi ya kilomita 100 kuanzia sasa, yale yatakayonunuliwa ni lazima tutahakikisha kuna vyoo ndani, kwa sababu hata tukiwa na hivyo vituo, kuna watu wana matatizo ya Ugonjwa wa Kisukari, kuna matatizo mbalimbali, kuna homa na kadhalika, mtu atahitaji kujisaidia, itabidi mabasi hayo yawe na vyoo. Mikakati yote hiyo tunayo na tumeshaanza kuwasiliana na Waziri mwenye dhamana ya Uchukuzi ili kuweka vitu katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna biashara ya hewa ukaa, Wananchi wameingia mkataba na wametoa hekta nyingi sana *green resource*. Ninachoweza kusema ni kwamba, tunaomba Wananchi wasidanganywe, kwa sababu biashara ya hewa ukaa ina taratibu zake Kimatalifa na sheria moja inasema kwamba nchi ile inayofanya hewa ukaa inatakiwa ipate asilimia 51 ya biashara hiyo ya fedha kwa wenye miti, kwa sababu ile miti iko kwenye nchi yenye ardhi. Kwa hiyo, mimi najiuliza hivi vijiji viliingia mkataba huo kwa ruhusa ya nani? Ndiyo maana *green resource* mpaka sasa hivi hawajapata cheti, anayetoa cheti hicho ni Waziri mwenye dhamana ya Mazingira, kwa sababu ya ukiukwaji wa taratibu. Vijiji ambavyo waliweza kuwapa hiyo hewa ukaa walipewa asilimia kumi. Pato hilo ni dogo sana, kwa hiyo, bado tumewapa masharti hayo warekebishe.

Sharti la pili, kuna *Coordinating Unit* ambayo ndiyo inafanya biashara hiyo, ndiyo soko lenyewe, linatakiwa lianzishwe sehemu yenye biashara ukaa hususan Tanzania. Wao wanataka iwe Norway, sasa tatizo la kuifanya iwe Norway maana yake Serikali haitapata mapato. Kwa hiyo, tumewaambia warudi watuletee hiyo *Coordinating Unit* Tanzania ili Serikali iweze kupata mapato. Wakitimiza hayo masharti mawili, basi biashara hiyo ya hewa ukaa itaendelea.

Kwa kifupi, hiyo biashara ni kitu ambacho kimejjificha, hata mimi ukiniuliza sasa hivi hilo soko lilo wapi na iko wapi ninaona tu watu wanakuja kuomba biashara ya hewa ukaa

lakini zinatoka wapi hela, ni ngumu sana kwa sababu hata kwenye Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Doha, bado wenzetu nchi zilizoendelea wanakataa kuchangia Mfuko huu wa Miradi hii ya Hewa Ukaa na Miradi ya *CDM*.

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Waziri, Kilombero ndiyo walianza huko na Ifakara.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Ni kweli lakini wameanza kwa kukiuka masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine, nyumba zilizopo kwenye Hotuba; sawa hili limeshajibwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sijui kama kuna kitu kingine nimekiacha, nadhani nimemaliza yote. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Twende ya Muungano sasa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Muungano, kuna masuala ya Mheshimiwa Mnyaa, ambaye anasema hizi kero zimekaa kwa muda mrefu, miaka 36 sasa na hasa hili la Akaunti ya Pamoja, mkilimaliza sasa hivi na mwakani Katiba inabadilika na hatujajua mambo yatakuwaje; je, *position* ikoje?

Mimi naona ni vizuri tufanye kuliko kutokufanya kabisa, kwa sababu, kwa mfano, kama unamurai mtu, mmekubaliana muda umepita na bado muda uko mbele, utamwambia muda umepita usilipe tena, utasema nipe tu haki yangu. Kwa hiyo, nadhani tuendelee tu sasa kama kuna mabadiliko basi yataendana na mabadiliko ya Katiba inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la bandari, halijawa la Kimuungano, ni kweli na siyo bandari peke yake, kuna masuala ya leseni za viwanda, kuna masuala mawili, matatu, ambayo yaliingizwa lakini hayatekelezeki Kimuungano. Hii inatokana na kwamba, wakati imevunjika

Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, masuala haya mengine yote yalikuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, wakati wa kurudishwa yakarudishwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, yanaonekana kwenye *Listya* Muungano lakini hayatekelezeki na kila upande unatekeleza mambo yake kama unavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Katiba kwa nini hajijatumika miaka yote na ilipoundwa Katiba kipengele hiki kimewekwa? Kipengele hiki kimewekwa sawa na kipengele kilichowekwa katika *Memorandum of Understanding* ya Kampuni. Kuna kipengele kinawekwa kwamba, ukitokea mgogoro, mgogoro huu utakuwa *settled* aina hii. Inawekwa kwa sababu Kampuni pengine ni ushirikiano wa watu kadhaa wameungana kufanya hiyo Kampuni. Kwa hiyo, kwenye masuala ya Muungano, lazima kuweka vipengele vya aina hii, kikitokea utata wa tafsiri ya Kikatiba, basi Mahakama ya Kikatiba ndiyo itakayofanya kazi hiyo. Mpaka sasa utata wa tafsiri ya Kikatiba haujatokea, kilichotokea ni kama unavyosema, unaweza ukaita migogoro ya Muungano, Masuala ya Muungano, Kero za Muungano na unaweza ukaita changamoto za Muungano. Usajili wa vyombo vya moto halina utata wa Kikatiba, labda wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili halina utata wa Kikatiba. Kuweka Akaunti ya Pamoja ya Fedha ni Kamati ya Pamoja ya Fedha kuleta mapendekezo kufanyiwa kazi. Kilichotokea upande mmoja umechelewa kufanya kazi, siyo utata wa Kikatiba. Kwa hiyo, vifungu hivi ulivyovitaja havijatumika kwa sababu hakujatokea mgogoro wa tafsiri ya Kikatiba ya Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, ambalo anaulizia kufanyiwa kazi kwa mapendekezo ya *GFC* ili kuondosha kero nyingine zinazoendana nayo. Kama nilivyotoa ufanuzi kwamba, tayari Baraza la Mawaziri, tumefanya mazungumzo ya kwanza na majadiliano yanaendelea kujadili mapendekezo ya *GFC* kwa upande wa SMT na baada ya kupata maridhiano, basi tutakaa na wenzetu wa SMZ, kuona jinsi

tutakavyoweza kukubaliana mapendekezo yaliyotolewa na kuweza kuendelea na safari ya kuanzisha hii Akaunti ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ni kuondoa shilingi kwa hili hutaruhusiwa kwa sababu tumeshakujibu toka zamani.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu wakati wa Kamati ya Matumizi, hatuna utaratibu wakati wa Matumizi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwanasheria Mkuu, kwa majibu yake. Lakini pla ningependa ...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, kuhusu Kanuni hii kama unatoa shilingi unatoa, lakini huwezi kuzungumza mara ya pili. Kama unatoa shilingi toa, lakini kuzungumza mara ya pili siyo utaratibu. Unatoa shilingi au unasema nini?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mwanasheria Mkuu kama alivyosema kwamba ataongea na mhusika.

**MWENYEKITI:** Ahaa, sasa hiyo tukifanya hivyo kila mtu anataka kuzungumza mara ya pili, aidha utoe shilingi tujue hii hoja tupige kura au basi na kama umeelewana na Mwanasheria siyo vibaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nilikuwa nataka ufanuzi tu kwenye *Subvote 1001, Item 410200*.

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri tumemaliza, Mheshimiwa Esther Matiko, anaendelea na vifungu. Haya endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *Item 410200 - Acquisition of Vehicles and Transportation Equipment.* Mwaka juzi walitengewa shilingi milioni 399.5, mwaka jana hawakutengewa kabisa na mwaka huu kuna shilingi 153,844,000. Sasa nataka ufanuzi; je, hizi *vehicles* ambazo zilikuwa *acquired* mwaka juzi na *transportation equipment* zimeshachakaa au kuna manunuzi mengine?

**MWENYEKITI:** *Comment yake kwamba kulikuwa na zero sasa mmeongeza; what is it?* Ndiyo swali lake.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tuna Naibu Katibu Mkuu na Katibu Mkuu, ambao hawana magari kabisa na mwaka jana kwa sababu ya ufinyu wa bajeti hatukuweza kubajeti. Kwa hiyo, magari haya ni kwa ajili ya Naibu Katibu Mkuu na Katibu Mkuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali ni kifungu na siyo maneno mengine, kama maneno mengine hapana, kama kifungu endelea.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu utaratibu, suala la akidi, tunapitisha vifungu akidi haijatimia.

**MWENYEKITI:** Akidi imetimia Mheshimiwa Machali. Sisi wenyewe tunajua kama akidi imetimia.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuhesabu watu, mimi nimehesabu hata 140 hawazidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, naomba ukae chini tafadhali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... Sh. 300,487,000

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwneyekiti, nina shida na Kifungu Kidogo 410600 - *Acquisition of Office and General Equipment*. Kifungu hiki mwaka wa juzi hakikutengewa kitu, lakini mwaka jana kimetengewa shilingi 2,500,000 na mwaka huu naona kimeongezeka mara mbili. Je, kulikoni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi zetu za Tunguu na Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli, sasa hivi zimekamilika na zinahitaji kuwa *furnished* ndiyo sababu mwaka huu tumeweka bajeti.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning Division* ... .... Sh. 799,545,000

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina tatizo kidogo, naomba kuelewa kwenye *Subvote 1003, Item 220100*, ambayo mwaka jana kulikuwa na shilingi 46,300,000 na mwaka huu kuna shilingi 62,850,000, kuna ongezeko la shilingi 16,000,000. Naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Umekipata? Kifungu gani Mheshimiwa Masoud?

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 220100

**MWENYEKITI:** Kipo pale, *Office and General Supplies and Services*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo hayo tuliyosema kwamba, tuna Ofisi mpya, sasa pale kuna *photocopier, printer*, tunatakiwa tununue kwa Ofisi zote ambazo zinaanza. Kwa hiyo, fedha hizo tumezitawanya kwenye mafungu mbalimbali.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1004 - *Government Communication Unit* ..Sh. 224,472,000  
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* ... .... Sh. 197,588,000

(*Vifungu vilivytajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* ... Sh. 142,170,000

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Subvote 1006, Item 210100, utaona Basic Salary* haikutengewa kitu kabisa na hiki Kitengo cha *Procurement Management Unit* ni muhimu sana. Nataka niulize ina maana hamna mwajiriwa aliywewkwa ambaye ni *permanent?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za waajiriwa hawa ziko katika Utawala.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko pale pale Kifungu 410600 - *Acquisition of Office and General Equipment*. Miaka miwili iliyopita hakuna fedha iliyotengwa na mwaka huu kumetengwa shilingi 13,500,000; je na huku nako kuna shughuli nyingine za kuhamia kwenye ofisi?

**MWENYEKITI:** Jamani hiyo ni Wizara moja, maeneo ni *Department* hii, *Department* hii, kama ni Wizara moja lazima kitakuwa ndiyo hicho hicho tu kila kitu kama ni *supplies* na kadhalika. Mnapoona fedha zimeongezeka zero zero ni hao hao tu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, labda anakewekeaa maneno.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti umeshanisaidia jibu ndiyo hilo hilo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 - *Information and Communication Tech.*  
Unit ..... Sh. 163,835,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Legal Service Unit* ..... Sh. 89,570,000

**MHE. SUSAN A. L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Katika Kifungu 1008, Item 210300, kuhusu mshahara naona mwaka uliopita walipanga shilingi 13,330,000, lakini mwaka huu wanasema shilingi 11,600,000 na hiki ni Kitengo cha Sheria. Naona wazi kwamba, katika Wizara hii hasa ya Mazingira, suala la sheria ni kitu muhimu sana. Mimi ni mmojawapo kwenye Kamati ya Maliasili na kuna taarifa zisizokuwa na shaka kwamba, Wanasheria baadhi yao wanatishwa katika kufuatilia masuala mbalimbali ya kisheria kuhusu masuala ya Mazingira. Sasa nimeona hapa suala la mishahara limepungua; je, wanapunguza Wanasheria katika hii Wizara badala ya kuongeza; kimetokea nini mpaka mishahara imekuwa midogo mwaka huu? Naomba ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Ofisi ya Makamu wa Rais kupata Naibu Waziri mmoja Mwanasheria ndio Msaidizi wa Naibu Waziri, kwa hiyo, amehama kutoka Kitengo hicho na sasa yuko *Administration*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2001 – *Union Secretariat* ... .... ... Sh. 33,375,245,000

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwenye kasma 220800 - *Training Domestic*. Ningependa Mheshimiwa Waziri atupatie ufanuzi, tumebaini hapa masuala ya Muungano watu hawayafahamu na imedhihirika hata Wabunge wenzetu humu ambao wanahoji kwa nini Majimbo yana watu kidogo na *representation* yote kumbe nao hawayafahamu. Shilingi 18,300,000 naziona kidogo, ikiwa wenzetu ambao hawajui hata hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano imekuja vipi na wanahoji ukubwa wa Majimbo ya Zanzibar na wingi wa Wabunge humu; fedha hizi zitahusika kwa *training* ya hawa wenzetu kwa sababu naona ni kidogo. Naomba nipatie ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima ulienda Jeshini, sasa unaenda kusomea Muungano. (*Kicheko/Makof!*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni *training domestic*, ni kwa ajili ya *Staff* wa Wizara na si kwa ajili ya *capacity building* ya shughuli za Muungano.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kupata ufanuzi kwenye kifungu 271100 - *Current Grants to Other Levels of Government*, imetengewa shilingi 32,627,535,000; tunaomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili kama

nilivyosema kwenye Kitabu cha Bajeti kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwa tunapata *General Budget Support* kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na katika fungu lile kuna 4.5 ya Zanzibar. Kwa hiyo, kiasi hiki ulichokiona ni kutoka 4.5 ya ile *General Budget Support* inayokwenda Zanzibar. Kawaida huwa inapitishwa kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais kwenda kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Environment* . . . . . Sh. 5,184,372,000

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye *Subitem 220800 - Training Domestic*. Natambua kwamba, siyo Tanzania tu lakini tuna matatizo makubwa sana ya mabadiliko ya tabia nchi na mazingira kwa ujumla wake. Nilikuwa nategemea kwamba, kasma hii ingekuwa kubwa ili wataalam waweze kusoma hapa ndani kuweza kujua mambo yanayoendena na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mazingira. Naomba kujua ni kwa nini kifungu hiki kimepungua kwa takriban shilingi milioni 30?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Subvote 5001, Item 270800 - Current Grant to Non-Financial Public Units (General)* shilingi 3,164,303,000. Naomba kujua ni za nini?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufanuzi kwenye *Item 221300 - Educational Material, Supplies and Services*. Kifungu hiki tumekuwa tukilalamika kwenye Kamati miaka miwili mfululizo kwamba, tunajua changamoto inayoikabili nchi yetu kuhusiana na elimu kwa mazingira na hapa ndipo ambapo fedha za kununulia vifaa vya kutolea elimu ya mazingira inatakiwa itengwe ya kutosha. Kwenye Kamati tumekuwa tukilalamika miaka miwili mfululizo kuhusiana na Kitengo hiki kutengewa fedha kidogo.

Napenda nipate uafanuzi Serikali hamwoni umuhimu wa kuongeza fedha katika eneo hili ili Watanzania waelimishwe vya kutosha kuhusiana na utunzaji wa mazingira kama kilio cha Kamati kinavyosema?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 220800 - *Training Domestic*. Hizi hela ni za kuwa-*train staff* wa Idara ya Mazingira na siyo Elimu kwa Umma. Kuna *staff* ambao walishaanza masomo, kwa hiyo, ni kwa ajili ya kuwasomesha hao *staff* wa mazingira na ni ukomo wa bajeti tu, hatuna namna ya kuongeza. Kifungu 221300 - *Educational Material*, hapo ndipo tungeweza kuweka hela za kutosha kwa ajili ya *training* kwa umma. Kutokana na ukomo wa bajeti, hela zile tulizoweka mwaka jana na hivi sasa tunaendelea kuweka, kwa hiyo, hatuna uwezo mwengine.

Kifungu 270800 - *Current Grant*, hizo ni hela zinazoenda *NEMC*. Kwa hiyo, lile ni gawio la *NEMC*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – *Administration and HRM Division* ...Sh. 2,800,000,000

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye *Subvote 1001, Item 6389 - Construction and Rehabilitation of Vice President Offices*. Sasa kuna shilingi bilioni 2.3; ukarabati huu ni wa ofisi ya wapi na maeneo gani? Naomba uafanuzi na ofisi hizi zipo ngapi maana naona kila mahali zipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa tuko kwenye *development*; anauliza hizo ofisi ni wapi huko?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwanzo, Ofisi ya Makamu wa Rais ina makazi yake kule Tunguu na Luthuli. Hii ndiyo tunakamilisha malipo ya *certificate* kwa Ofisi za Makamu wa Rais pamoja na *furniture* zake.

**MWENYEKITI:** Sasa mliosimama vi-item viko viwili tu kama kimeshaulizwa haurudii. Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nasimama kwa *Subvote 6309*, ambayo ndiyo iliyofafanua *construction of the Vice President office and residence in Zanzibar*. Ile aliyouliza mwezangu haiko Zanzibar ile aliyouliza mwenzangu haiko Zanzibar. Hii ndiyo *particular* inayofafanua Zanzibar. Sasa nauliza hii ya Zanzibar ambako kumetengwa milioni 500 na mwaka jana ilikuwa bilioni moja; je, hii ofisi imekamilika iko pale na leo tumezitengea hizi pesa?

Mimi sina tatizo kutenga hizi fedha, lakini usoefu tulionao muda uliokamilika ni sawasawa na Ofisi ya Bunge iko pale Zanzibar kwa mambo ya Muungano na hajatumika ipasavyo na hii muda umeshapita bado ofisi hajatumika ipasavyo. Leo tunatenga milioni 500; Waziri atuhakikishie Bunge likiidhinisha hizi fedha hii ofisi itafanya kazi vizuri lini na tuweze kuitumia kwa kuwa shughuli zetu ziko nyangi pamoja na Mfuko wa Jimbo (*CDF*)?

Huo ndiyo ufanuzi ninaoutaka, kwa sababu tukiletewa tena na bajeti ya mwakani ofisi hii tutenge pesa tena, mimi nitakuja kutoa shilingi wakati huo, lakini leo nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie itatumika lini kwa sababu imeshakamilika? Nataka ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipata milioni 500 kwa ajili ya Zanzibar, ofisi hii itakuwa *full operation*. Kwa sasa ofisi inafanya kazi lakini kuna *Private Office* ya Makamu wa Rais na ofisini kwangu Waziri wa Muungano kule juu, hakuna vitendea kazi, ni meza tu na viti. Kwa hiyo, tukipata milioni 500 tuna-*furnish office* na itakuwa *full operation*.

**MWENYEKITI:** Vifungu vyote vimeshakanyaga hapo sasa utauliza nini?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru wameshaliuliza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba ufanuzi kwenye kifungu kidogo cha 6389. Kwanza, maelezo kwamba ni *construction and rehabilitation* nashindwa kuelewa kwa sababu kama ni nyumba ya Vice President pale Dar es Salaam inavyoonekana imekamilika. Mimi swali langu ni kwamba; hizi shilingi bilioni mbili tunazotaka kuzipitisha leo ni kwa ajili ya nini na hii nyumba inakamilika lini?

**MWENYEKITI:** *Actually, siyo nyumba. Soma vizuri hicho kifungu ni construction and rehabilitation of Vice President offices and S/Lod ndiyo hapo nadhani hamkumjibu vizuri. Mheshimiwa Masoud alisema ofisi zingine ziko wapi?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Luthuli hatujakamilisha ile Ofisi lakini kuna *state lodges* za Vice President ndiyo hiyo ilioandikwa S/Lod ni State Lodges.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – Environment. .... . . . . . Sh. 10,171,883,000

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiki, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kifungu cha 5001, Item 5301, ambacho ni *Climate Change Adaptation Programme*. Nilichokuwa napenda kujua na ukiangalia utaona ongezeko ni kubwa la bilioni saba na pointi kadhaa. Ni masuala yapi hasa ambayo Wizara imepanga kuyatekeleza kwa mwaka ujao wa fedha?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, langu lilikuwa katika kifungu hicho hicho, lakini katika *approach* tofauti. Nikwamba, katika taarifa zote inaonekana mabadiliko ya tabia nchi yameenda kasi na hali inakuwa mbaya katika nchi yetu, naona bajeti ya bilioni saba lakini *commitment* yetu kama nchi ni milioni 70 peke yake. Naiomba Serikali itueleze kwa nini katika jambo hili ambalo linaathiri nchi yetu tunategemea misaada toka nje peke yake?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu hichohicho lakini *Item 6569 - Lake Tanganyika Environment Management Project*. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia udhaifu wa kupambana na tatizo la magugumaji kwenye mabwawa na kwenye malambo ambayo tunatumia fedha nyingi kwa ajili ya maji safi na salama kwa Wananchi. Utakuta hapa wameendelea tu kutenga fedha za ku-manage haya mazingira kwenye Ziwa Tanganyika na nikasema Kijiji cha Kabainja bwawa lao limeziba kabisa kutokana na magugumaji hawana maji ya kunywa. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, amegeme shilingi milioni 20 kwenye hicho kifungu ili aweze kwenda kunusuru bwawa la Wananchi wa Kijiji cha Kabainja ili wapate maji, hawana maji kabisa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niulizie kwenye *Item 5303 - National Biosafety Programme*. Mwaka 2012/2013, walitenga shilingi milioni 20, mwaka huu hakuna hata shilingi moja iliyotengwa na tunajua kabisa kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo inashughulikia mambo ya *Biosafety* ambayo inahusisha pia masuala ya *GMO*. Naomba waangalie namna ya kutenga fedha hapo ili angalau kile Kitengo cha Watafiti waruhusiwe kufanya utafiti katika *GMO* na sisi pia Tanzania tuweze kwenda mbele kama wenzetu majirani walivyokuwa wanakwenda. Ni muhimu sana kwa nchi yetu katika kuijendeleza katika suala la utafiti.

**MWENYEKITI:** Swali lako wewe unauliza kwa nini hazikutengwa fedha, ukisema watenge watazitoa wapi sasa!

Ulitakiwa kusema kwa nini fedha hazikutengwa kwa sababu jambo hilo ni muhimu. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tujielekeze kwenye *Subvote 5001* kwenye Kasma Namba 6569 - *Lake Tanganyika Environment Management Project*. Naona fedha zilizotengwa kuna upande wa *local/na* upande *forex*. Sasa ukipita katika vifungu vingine linajitokeza kwamba, fedha hizi za *forex* hasa kuna *SIDA* na *World Bank*, lakini katika fungu hili na kwenye kifungu 5306 hatujaelezwa kwamba fedha hizi zinatoka kwa nani ni *Sida*, *World Bank*, *ADB*, ni *JICA* au ni wapi?

Nina-raise concern hii kwa sababu wakati mwingine tumekuwa tunalalamika kama Taifa kwamba, fedha za nje zinachelewa kuja au haziji. Sasa kwa ajili ya kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuweza kufuatilia, wamefanya *negotiation* na hawa *donors* na fedha hizi zitakuja au haziji, hilo litakuja kuwa suala la baadaye ambalo tunapaswa kujua ni nani ambaye atatoa pesa hizi. Napenda ufanuzi kwa Wizara kwa nini hawajatuonesha fedha hizi zitatolewa na nani kwenye kasma hii ya 6566 lakini pia kwenye kasma 6306?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali moja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipewe ufanuzi na naomba nihitimishe bado akidi hajatimia.

**MWENYEKITI:** Bwana mimi ndiyo naangalia nyumba hii. Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Fungu dogo la 5301, ambalo ni Mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ambayo ina shilingi bilioni saba. Nataka nipate ufanuzi kwa sababu katika Hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani tulizungumzia masuala ya misitu ya asili na misitu ya kupandwa, ni namna gani Serikali itaokoa misitu yetu ya asili tukawa na programu za misitu ya kupandwa ili tuweze kutumia fursa ya kiuchumi ya mikaa na

tunatunza mazingira lakini wakati huohuo tunapanda miti mingine kwa ajili ya shughuli hizi za kibiashara ambazo zinaonekana ni sehemu ya ajira, lakini pia inachangia Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa.

Sasa nataka njue katika hizi fedha ambazo zinatolewa na *UNDP* kuna programu ndani yake na kwa sababu zinahusiana na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na kama hii hoja ambayo sisi tumeipendekeza itakuwa sehemu ya huo mpango ili kuweza kutoa ajira, kuongeza pato, lakini vilevile kutunza mazingira yetu?

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hata mchango wangu kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikemea kabisa bajeti kutegemea asilimia 100 za wafadhili. Mwaka jana hatukupata kitu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy tulipofikia hapa huwa hatusemi hivyo.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Namba 5001, karibu hela zote ni za wafadhili tuna *guarantee* gani kuzipata hizi pesa?

**MWENYEKITI:** 5001 ni kifungu kidogo, sasa tunakwenda kwenye kifungu kidogo zaidi.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kafungu Kadogo 5301, karibu shillingi bilioni saba zote zinatoka kwa wafadhali; *UNDP*, *World Bank* na wapi; tuna *guarantee* gani na hizi fedha tutazipata wapi? Mwaka jana kwenyewe hatukuzipata hizi pesa. Sasa tutakuwa tunazozana hapa tunaanza kuzungumza hatuna *guarantee* ya hizi pesa. Hebu tuangalie kama tuna *guarantee* ya kuangalia hizi pesa. Ndiyo swali langu dogo.

**MWENYEKITI:** Swali hili alishauliza Mheshimiwa Halima Mdee, kwa hiyo, atajibu swali hilo, maana unarudia pale pale. Nimalizie na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nakuja katika Kifungu Kidogo cha 6507 - *NEMC*. Mwaka jana tumeona fedha za ndani zilitengwa shilingi milioni 500 na mwaka huu shilingi milioni 400. Tunajua mwaka huu *NEMC* wana Miradi kama sita na tunajua changamoto ambazo zinawakabili katika suala zima la kushughulikia masuala ya mazingira, wao wenyewe hawana ofisi kama nilivyochangia kwenye mchango yangu, wapo wanaendesha shughuli zao katika kontena. Napenda kujua kwa nini baada ya fedha kuongezeka zimepungua mbali ya changamoto kubwa ambazo zinaikabili *NEMC*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri, majibu kwa kifupi kwa sababu dakika zilizobaki ni chache sana na mtajibu kulingana na *segment* ya maswali yalivyoulizwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na *Item 5301* ambayo inashughulikia *climate change*; labda niseme tu uwezo wa Serikali ni milioni 70 na ni ukomo wa bajeti. Kwa hiyo, hatuna namna nyingine ya kuongeza pesa na hizi pesa tumeziweka kwa ajili ya kutoa elimu ya *climate change*, kwa sababu kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwamba, Wananchi hawaelewi mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hiyo, tumeziweka kwa ajili hiyo na hatuna hela nyingine za kuongeza hapa.

Tukienda kasma ya *National Biosafety Programme*; mwaka jana na mwaka juzi ni kweli ilikuwa inafadhiliwa, lakini *NEMC* imeshafunga huo Mradi. Kwa hiyo, kwa sababu ya ukomo wa bajeti, tumeshindwa kutoa pesa. Tutatoa wapi, kwa sababu tunajua kuna suala muhimu sana la *GMO* na watu wanahitaji elimu lakini ukomo wa bajeti ndiyo umetufanya tusiweze kutenga pesa kwenye kifungu hicho.

*Mainstreaming Environment and Climate* fedha zile zimetoka wapi. Kuna nyingine ambazo zimetoka kwa wafadhili. Kwa mfano, *UNDP*, lakini hawaja-*confirm* ndiyo maana tumeshindwa kuweka ni nani ata-*confirm* kwa sababu ni wafadhili zaidi ya mmoja, kama wawili, watatu,

mpaka watakapo-*confirm* ndipo tutakuwa na uhakika, lakini hatujajua nani ata-*confirm*. Kwa hiyo, kiasi hicho tutakachokipata ndicho tutakitumia kwenye huo Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 6507, ni kweli *NEMC* ina kazi kubwa na hawana sehemu ya kufanya kazi, wana kontena lakini inabidi tufanye hivyo hivyo na ukomo wa bajeti ni huo; kwa hiyo, hatuna namna ya kuongeza pesa pale. Pesa ni hizohizo walizonazo.

*Lake Tanganyika Authority*, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi mwanzoni kwamba, hii ni Jumuuya ya nchi nne; Burundi, DRC Congo, Tanzania na Zambia. Kila mwaka Serikali ya Tanzania na Serikali za kila nchi lazima zitenge dola 303,900 kwa ajili ya kulipia *Lake Tanganyika Authority*. Makao Makuu yapo Burundi na kule kuna wafanyakazi wanaotoka Tanzania, Burundi, DRC Congo na Zambia, kwa hiyo ni lazima tuwapeleke. Siyo hivyo tu, kila Nchi Mwanachama ina ofisi ndogo; kwa mfano, Tanzania tuna ofisi hiyo ipo Kigoma. Kwa hiyo, wale wanalipwa mshahara kwenye hiyo *Lake Tanganyika Authority*. Kwa hiyo, ni lazima tupeleke fedha hizo kwa sababu ni Mkataba wa Kisheria, ndiyo maana tumechanga hizo pesa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Makamu wa Rais; Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila

mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitawahoji muiamue.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja ilihamualiwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa  
Mwaka 2013/2014 Yalipitishwa na Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Watendaji wao, kwa kazi nzuri wanayofanya. Haya waliyoyagusia Waheshimiwa Wabunge, myaangalie katika mwaka unaofuata kusudi muweze kufanya vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mchezo wa kutaka kuchelewesha kazi tu, kwa sababu anayesema akidi imepungua hajajua wagonjwa walioniomba ruhusa wangapi. Hii idadi sisi tunaangalia. Kwa hiyo, tusifanye hivyo, siku nzima tusifanye kazi kwa sababu ya watu wawili ambao wamepungua! Hapana, haiwezekani. (*Makofii*)

Naomba niwatangazie kwamba, tukitoka hapa wenzetu wa *TBL* wana tafrija hapo nje, piteni tu muwape mkono, lakini kesho tuna Semina ya Maadili ya Viongozi kuanzia saa tatu asubuhi. Naomba m jitahidi kuhudhuria kwa sababu ni muhimu sana katika kazi zetu. Mnakuta mnashtakiwa kwenye Mahakama kumbe hamjui Sheria yenyewe inasema nini, inayotuongoza sisi kama Viongozi.

Ninawashukuru sana kwa kazi yote mliyofanya kwa wiki hii, mmefanya kazi nzuri sana, naomba niwatakie *weekend* njema na mpumzike ili tuanze upya Siku ya Jumatatu na Wizara ya Kilimo. Hivyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.24 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 22 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*